14 MEI, 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 14 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 199

**Uendelezaji wa Sekta Binafsi Nchini**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Maelewano na kutegemeana kwa Serikali na Sekta Binafsi huchangia kukua kwa Serikali na Sekta hizo binafsi.

(a) Je, Serikali inaendeleza sekta binafsi kwa kiasi gani?

(b) Je, Serikali inapata mafanikio gani makubwa kutoka Sekta Binafsi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina jukumu la kusimamia, kuwezesha na kauendeleza Sekta Binafsi kwa kuweka sera, sheria, kanuni na kuboresha mifumo ya kitaasisi ili kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua nchini. Hivyo, Serikali inatekeleza mambo yafuatayo ili kuwezesha na kuendeleza Sekta Binafsi:-

(i) Kwanza maandalizi ya Sera ya Maendeleo ya Sekta Binafsi Tanzania.

(ii) Kufanya majadiliano na Sekta Binafsi ili kutatua changamoto za kisera, kisheria na mifumo ya kitaasisi ili kuwa na sauti moja ya Sekta Binafsi nchini.

(iii) Kuandaa taarifa za ushindani wa Sekta Binafsi katika biashara na uwekezaji kuanzia ngazi ya Wilaya mpaka Taifa kwa lengo la kuainisha changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta Binafsi nchini na kuzipatia ufumbuzi.

(iv) Kituo cha kutoa huduma Bandarini Dar es Salaam kimeanzishwa. Hatua hii imepunguza muda wa mizigo kukaa bandarini kutoka siku 25 mwaka 2009 hadi siku 9 mwezi Mei, 2013.

(v) Kuunda Kamati za pamoja kwenye vituo vya mipakani ambazo zimeongeza ufanisi na kupunguza muda na gharama za kuvusha mizigo mipakani.

(vi) Kuweka mkazo kwenye matumizi ya mifumo ya kielekitroniki kwenye maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma kama vile ulipaji wa kodi, ulipaji wa huduma mbalimbali kwenye mabenki, usajili wa makampuni kwa kutumia tovuti ya *BRELA* pamoja na utunzaji wa kumbukumbu.

(vii) Kuondoa urasimu katika umilikishwaji wa ardhi, kupata vibali vya kazi na ukaazi kwa wawekezaji kwa kuweka wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kazi na Ajira na Idara ya Uhamiaji katika Kiuto cha Uwekezaji Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendeleza na kukua kwa Sekta Binafsi, manufaa yaliyopatikana ni kama vile, upatikanaji wa mitaji, ujuzi na teknolojia mpya na ya kisasa, kuongezeka kwa fursa za ajira na masoko nje ya nchi kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini, idadi ya watalii kutoka nje na mapato ya fedha za kigeni, mapato ya Serikali kutokana na makusanyo ya kodi, ushuru na mrabaha na hivyo kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi.

Mathalani, mitaji kutoka nje iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 520 mwaka 2005 hadi Dola za Marekani bilioni 1.1 mwaka 2011, pato la taifa linalotokana na kodi limeongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 25 miaka ya 1980 hadi wastani wa shilingi bilioni 800 kwa sasa. Aidha, katika kipindi cha miaka 12 iliyopita (2000-2012) jumla ya miradi 7,012 iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*) imeweza kupunguza tatizo la ajira kwa kuajiri Watanzania wapatao 1,029,737. *(Makofi)*

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri kifungu namba 1, 2 na 3 yameonyesha kwamba ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa mbali sana na sekta binafsi na hivyo kupelekea kuyumba katika ushiriki wake katika kukuza uchumi na kuongeza tija na ajira katika nchi.

Je, Serikali inaliambia nini Bunge hili na Watanzania katika kuikuza sekta hii binafsi kiukweli kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kuweza kuwawezesha wazawa katika kuwekeza katika sekta binafsi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI)** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kutoka miaka ya 90 sera ya nchi imebadilika kutoka uchumihodhi kuwa uchumi wa masoko.

Kwa hiyo, kama sera imekuwa ni ya uchumi wa soko maana yake ni kwamba sekta binafsi ndiyo imepewa injini ya kuendesha uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, Serikali haina uchaguzi lazima isaidie sekta binafsi ambayo awali ilikuwa imedumaa ili kuweza kukuza na nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba Serikali inafanya kila inaloweza ili sekta binafsi ikue, iwe imara na iendeshe uchumi wan chi yetu.

Lakini naiomba sekta binafsi nayo ichukue nafasi yake pekee na itambue kwamba sasa isipochukua jukumu lake la msingi la kuendesha uchumi maana yake ni uchumi wa nchi yetu utadorora. Kwa hiyo, naahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kisera, kisheria na kitaratibu Serikali itafanya kila litakalowezekana sekta binafsi ichukue nafasi yake.

Sasa mikakati ya makusudi ya kufanya wazawa waweze kuwekeza kwenye nchi yao hadi sasa wawekezaji wa ndani ni wengi na thamani yao ya uwekezaji ni kubwa kuliko wawekezaji wa nje, lakini katika ujumla wake wawekezaji bado ni wachache kwa sababu mahitaji ya ajira na mahitaji ya kukuza uchumi ni makubwa mno.

Ninaomba sekta binafsi iweze kuwa na akiba na kama haina akiba iweze kutafuta vyanzo vingine ili iwekeze na Serikali itawala kipaumbele. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa, tunaelewa vizuri kwamba sekta hii ni muhimu sana katika njia zote mbili yaani njia ya kutoa ajira na kulifanya taifa likwamuke kiuchumi. Lakini kwa kuwa vilevile tunaelewa kwamba bado kuna baadhi ya viwanda vinavyotengeneza vinywaji kuagizia malighafi kutoka nchi za nje badala ya kutumia matunda yaliyopo ndani ya nchi, na ni kitu ambacho kinawakwaza na kuwarejesha nyuma wakulima wa nchi hii.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba kunafunguliwa benki maalumu ya kuwawezesha watu wa ndani ambao wako tayari kujikita katika kufungua viwanda vidogovidogo vya kuongeza thamani ya matunda ili tuweze kutengeneza matunda wenyewe na kusindika juisi badala ya kuagizia kutoka nchi za nje kama Brazil, India na Spain?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya kama ifuatavyo:-

Kwanza nishukuru kujua kwamba tunakubaliana kwamba sekta binafsi ni muhimu katika kukwamua uchumi wa nchi yetu na kwamba sekta binafsi itakuwa inatoa manufaa makubwa kama tutatumia malighafi ya nchini hasa pale ambapo ipo kuliko kuagiza kutoka nje kwa sababu tutakuwa tunaongeza fursa za ajira hasa kwa wakulima wetu. Ni muhimu sana kwamba wawe na chanzo cha fedha za kuweza kununua malighafi hizo. Kwa hiyo, suala la benki kama alivyoeleza ni muhimu sana.

Napenda kumjulisha Mheshimiwa Sanya na Bunge lako Tukufu kwamba Benki ya Raslimali Tanzania ipo kwa madhumuni hayo lakini pengine mtaji wake ni mdogo kwa hiyo katika kuwezesha na kuinua sekta binafsi nchini Serikali itakachofanya ni kuona kwamba benki ile inakuwa na mitaji

zaidi na kufungua taasisi nyingine za fedha ambazo zitawezesha sekta binafsi ili ziweze kutumia malighafi za hapa nchini kuliko kuagiza malighafi na kujenga uchumi wa nchi nyingine. *(Makofi)*

Na. 200

**Kujenga Malambo na Majosho ya Ufugaji Wilayani Tarime**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Wilaya ya Tarime ina wafugaji wengi ambao hufuga mifugo mbalimbali lakini wanakabiliwa na matatizo kadhaa kama vile ukosefu wa malisho, maji, majosho na soko la mazao ya mifugo yao.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haijengi malambo kwa Kata zote za Tarime zenye shida ya maji kama Susuna, Bumera, Mwama, Komaswa, Manga, Kibasuka, Nyarukoba, Gorong'a, Nyangoto, Kamambo, Muriba, Nyamwanga na Nyinginezo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali haijengi majosho ya kuogeshea mifugo hiyo kwa kila Kata?

(c) Je, Serikali inawashauri nini wafugaji wanaotangatanga kutafuta sehemu za malisho Wilaya ya Tarime?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Nyangwine Chacha, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimwa Naibu Spika, Wilaya ya Tarime ina jumla ya Malambo 16 yaliyoko katika Kata ya Susuni, Komaswa, Manga, Kibasuka, Nyarukoba, Gorong'a, Nyanungu, Kemambo, Kore na Binagi. Aidha, ni kweli kwamba yapo maeneo ambayo hayana malambo kabisa kwa ajili ya mifugo. Mkakati wa Wilaya katika kukabiliana na upungufu huo ni kujenga malambo kwa kila Kata zenye mifugo mingi kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Nchini (*ASDP*).

Kwa mwaka 2012/2013, *SENAPA* imepanga kujenga lambo katika kijiji cha Gibaso kwa ajili ya kunyweshea mifugo kwa gharama ya milioni 75.0 ili kupunguza mwingiliano wa mifugo katika hifadhi ya mbuga ya Serengeti. Mkakati huu utakuwa unaendelea kila mwaka katika maneo yote yanayohitaji malambo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ina Majosho 25 yaliyoko katika Kata za Nyandoto, Pemba, Genyange, Nyamaraga, Namwaga, Kibasuka, Binagi, Muriba, Susuni, Gorong'a, Komaswa, Manga, Matongo, Bomani, Bumera, Kiore, Nyarero, Kemambo na Nyamungu. Katika mwaka 2011/2012 zilitengwa shilingi miloni 45.0 ambazo zilitumika kujenga majosho mawili ya Gibaso Kata ya Nyarokoba na Josho la Nyarwana Kata ya Kisabuka.

Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, zimetengwa shilingi milioni 22.5 kwa ajili ya kujenga josho moja katika kijiji cha Mtana Kata ya Manga. Mkakati wa Halmashauri ni kujenga josho moja katika Kijiji cha Mtana Kata ya Manga.

Mkakati wa Halmashauri ni kukarabati majosho mabovu yaliyoko katika Kata za Nyamaranga, Nyarero, Pemba, Kemambo, Nyanungu katika mwaka wa fedha 2012/2013. Josho la Nyamaraga liko kwenye Bajeti ya kukarabatiwa kwa shilingi miloni 10.0. Utaratibu huu utaendelea kwenye maeneo mengine kwa kadiri upatikanaji a fedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

(c) Ili kuhakikisha wafugaji wanapata mahali pa kufugia mifugo yao, Halmashauri imekuwa ikitekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Wilaya ambao unakusudia kuhakikisha kila kundi linakuwa na mahali pa kufanyia kazi zake bila mwingiliano. Hivyo, wafugaji wote na wakulima wanatakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya mwaka 1999 kuheshimu utaratibu huu uliowekwa ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima. Hivyo, Serikali za Vijii kwa kushirikiana na Halmashauri zinatakiwa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji ili wafugaji waotangatanga waweze kupata maeneo ya kufugia mifugo yao. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo kwa kiasi fulani yanatia matumainina kwa kiasi fulani yanakatisha tamaa, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wafugaji wa Tarime na wakulima wapange mkakati wa kutenga maeneo na ambapo mpaka sasa hivi naamini kwamba hayo maeneo hayapo na kuna wakulima na wafugaji. Naomba mwenyewe kama atakuwa tayari kuambatana na mimi au kwa muda wake mwenyewe ahakikishe kwamba anafika Tarime ili aweze kuongea na wafugaji na awashauri mwenyewe ili wamsikie vizuri.

Pili, kwa kuwa malambo mengi yaliyochimbwa katika nchi yetu ikiwemo Wilaya ya Tarime na hata Musoma Vijijini kuna Lambo linaitwa Wegelo ambalo kwa kiasi kikubwa limejaa tope na Serikali ilitumia fedha nyingi sana kulijenga ambapo sasa hivi limekuwa *useless*. Naomba Mheshimiwa Waziri awashauri wananchi wa Tanzania ambao Malambo mengi yalichimbwa lakini sasa hivi yamekuwa *useless*, anawaambia nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyambari Nyangwine Chacha Mbunge wa Tarime kama ifuatavyo:-

Hili eneo la kwanza linalozungumzia mimi kwenda kuzungumza na wafugaji ni muhimu naweza kuliweka kwenye mpango wangu wa kazi ili niweze kwenda Tarime kuona hali hii. Lakini pia niwajulishe Watanzania kwamba Serikali ina mpango mzuri tu ambao umefanywa katika vijiji vingi kwa kuweka matumizi bora ya ardhi katika kila kijiji na vile vijiji mpango ule unabainisha maeneo ya ufugaji, kilimo, makazi na maeneo mengine ambayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji kama ardhi wanayo ya kutosha.

Kwa hiyo, ni vema sasa Serikali za vijiji kwa usimamizi wa Halmashauri zenyewe za Wilaya kuhakikisha kwamba wafugaji walioingia katika vijiji wanapata nafasi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji badala ya kurundikana na kuleta usumbufu ambao si muhimu. Kwa hiyo, pamoja na ujio wangu jambo hili lizingatiwe kwanza ili nitakapokuja niweze kukaa na wafugaji na kushauri maeneo ambayo yanawezekana.

Lakini la pili ni kweli najua upo upungufu kwenye maeneo mengi ya utendaji wa watendaji wetu kwamba malambo yamechimbwa yanaweza kuwa maeneo ambayo si muhimu lakini pia uchimbaji unaweza kuwa siyo bora. Jambo hili tunashirikiana na mamlaka zilizopo kwenye Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba kila fedha iliyotengwa kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kwenye eneo hilo tunataka fedha hizo zitumike kadri ambavyo zimetakiwa kwa thamani halisi ikiwemo na uchimbaji wa malambo, yachimbwe kwenye maeneo ambayo kweli yatatoa uthamini wa fedha na malamboyataendelea kutumika na mifugo ambayo inatakiwa iyatumie kwa kipindi kilichokusudiwa. Kwa hiyo,natoa wito kwa Wakurugenzi kuhakikishia kwamba maeneo haya ambayo yanahitaji kuwa na miundombinu ya aina hii, fedha iliyotengwa itumike kama inavyotakiwa nje ya hapo hatua zinazostahili kwa wahusika zitachukuliwa, Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa; wafugaji wengi hapa nchini wafuga kiutamaduni zaidi na siyo kisasa hali inayosababisha kuwa na mifugo mingi, lakini mifugo hiyo inakuwa haina afya, lakini wafugaji hawa wanakuwa hawana afya njema kwa kuwa wanasafiri mwendo mrefu sana na mifugo.

Lakini kubwa zaidi wamekuwa wakisababisha migogoro mingi pamoja na vifo pale ambapo wanakumbana na wakulima.

Je, Serikali sasa ina mikakati gani kuhakikisha kwamba wafugaji wetu wanafuga kisasa ili kuepusha migogoro hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa kutoka Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ukweli usiopingika kwamba, hapa nchini sasa tuna mifugo mingi sana na wafugaji wetu wanafuga kienyeji zaidi. Nakumbuka nilikuwa Mkuu wa Wilaya pale Urambo, tumeshuhudia hali hii maeneo mengi. Nataka kushauri kwa kuwaambia kwamba, Serikali kwa mipango yake inalenga kumfanya mfugaji wa Tanzania awe na ufugaji ulio bora na endelevu kwa kuwa na mifugo michache itakayozalisha kwa wingi zaidi.

Hili ni jambo ambalo ninaomba Waheshimiwa Wabunge sasa tushirikiane kwa sababu hawa wananchi ni wetu. Tushiriki kwa sababu tuna nafasi ya kuzungumza na wafugaji hawa kama watu wetu wapenda maendeleo.

Ni vyema sasa tukawashauri hili ambalo Serikali imeliweka kwenye mpango wake na kuwashauri, wakubali kukaa kwenye maeneo ambayo kweli yamepimwa na yanatosha kwa mifugo waliyonayo. Tunawaletea usumbufu pia hata Watendaji na Wenyeviti wa vijiji kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo pia tatizo la wafugaji hawa kuomba kibali cha mifugo, ng'ombe 100 lakini baada ya wiki unakuta eneo limejaa ng'ombe zaidi ya 1000. Jambo hili linaleta usumbufu mkubwa sana. Nawasihi tena Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuwaelimisha kupitia mikutano yetu kwenye maeneo yetu ili jambo hili lisiendelee tena kuwa tatizo nchini kwa maeneo ya kulisha, lakini pia kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo mwananchi anakuwa nayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia, swali la mwisho kwenye eneo hili.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia suala la malambo kule Kibasuka, Susuni na jimbo jirani kuna matatizo Kisumwa na sehemu nyinginezo na mkoa mzima wa Mara na maeneo mengine ya Tanzania, na hili liko kwenye lengo la saba la Milenia; *sustainability and environment protection*. Kwa kuwa, inaonekana ni jukumu la Serikali tu kujenga haya malambo, Serikali inatoa elimu gani kwa jamii husika au watanzania ili kuweza kuchimba mabwawa madogo madogo kwa lengo la kuvuna maji ya mvua, kuyahifadhi, kuyasimamia na kuyatumia ili mzunguko uwezo ukafanya kazi yake vizuri ikiwa ni kuokoa uharibifu wa mazingira unaofanyika kutokana na mifugo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Mbatia kama ifuatavyo.

Ni kweli suala la ujenzi wa malambo kwanza ni jukumu la Serikali. Lakini pia wafugaji wenyewe wakikaa mahali vizuri na yeyote ambaye ana nia njema kwa ajili ya kuwafanya wafugaji kukaa mahali pa zuri anayo nafasi pia ya kuchimba mabwawa na malambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikakati hii ya Serikali kwanza, halmashauri yenye idadi hiyo ya mifugo inayojua kwamba kuna mahitaji ya majosho kadhaa ndiyo ambayo inatakiwa kuweka mpango wa awali wa namna ambayo wanaweza kuchimba malambo hata ya majosho. Lakini pia tunayo mifuko kama ile niliyoitamka ya *ASDP,* nao pia katika mpango wake wa fedha wametenga fedha kwa ajili ya malambo kwenye wilaya ambazo malambo yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado halmashauri kupitia Baraza la Madiwani inaweza kutenga Bajeti kwa ajili ya kuongeza malambo kutokana na mahitaji yao. Serikali kwa maana ya ngazi ya Wizara ya TAMISEMI, tunatenga fedha za kilimo katika kila halmashauri kwa kuzingatia mahitaji ambayo yameibuliwa na halmashauri yenyewe. Sisi tunatoa maelekezo kwamba, fedha hii ifanye moja, mbili, tatu, nne, kwa kipaumbele kilichowekwa na Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, bado umihumu wa Serikali kuchukua nafasi yake ya ujenzi wa malambo na majosho, unabaki palepale. Halmashauri zizingatie mipango yao na maagizo ambayo Serikali tunayatoa kwa ajili ya kuboresha au kujenga malambo kwenye maeneo ambayo kweli yanahitaji kuwa na malambo mengi na majosho ya kutosha. *(Makofi)*

Na. 201

**Mradi wa Ufugaji Samaki – Kagera**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa nguvu wafugaji wa samaki katika mabwawa Mkoani Kagera?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa ufugaji wa samaki mkoani Kagera, Serikali iliwapeleka wataalam wawili mahususi katika ufugaji wa samaki ili kutoa elimu na ushauri katika ufugaji bora kwa kushirikiana na wadau wengine. Aidha, Serikali imekuwa ikiwapa nguvu wafugaji wa samaki kwa njia mbalimbali zikiwemo kuwahamasisha kuwapa elimu ya ufugaji bora wa samaki, kutoa miongozo ya kuchimba mabwawa ya mfano, kuzalisha na kusambaza vifaranga vya samaki na kutoa mafunzo kwa wafugaji ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hamasa, elimu na mwongozo walioutoa pamoja na juhudi za wafugaji samaki, jumla ya mabwawa 446 yamechimbwa mkoani Kagera: Wilaya ya Biharamulo ina 37, Bukoba Mjini 81, Karagwe 69, Misenyi 89, Muleba 12) na Ngara 49. Aidha, jumla ya wananchi 999 wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa samaki katika mkoa wa Kagera: Wilaya ya Biharamulo wamefundishwa wafugaji 120, Bukoba Mjini 218, Karagwe 126, Misenyi 180, Muleba 224 na Ngara 131. Vilevile Wizara imechimba na kuweka vifaranga katika mabwawa matatu ya mfano yanayotumika kama shamba darasa. Aidha, vifaranga 4,200 vya samaki aina ya perege na kambale wamezalishwa katika mabwawa haya na kusambazwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2010 – 2012, jumla ya vifaranga 115,700 vya samaki aina ya perege na kambale wamepandikizwa kwenye mabwawa ya samaki mkoani na mfugaji mmoja Bwana Bashiri Hussein Rashid wa Kijiji cha Ruhanga, kupelekwa Vietnam kwa mafunzo zaidi ambapo sasa amekuwa chachu kwa wenzake na anatumika kama shamba darasa. Tunampongeza kwa kuwa mwalimu wa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, imeandaa mpango wa kufufua kituo cha samaki cha Nyamirembe na kuboresha miundombinu iliyoko ili kituo hiki kitumike kutoa mafunzo ya ufugaji samaki kwa wananchi

wanaoishi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, ukiwepo mkoa wa Kagera na kuzalisha vifaranga vitakavyokidhi mahitaji ya wafuga samaki katika mikoa hiyo.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kutokana na takwimu ambazo zimetolewa na Waziri, ufugaji unapendwa na watu wanauendeleza katika mkoa wa Kagera. Moja ya tatizo ambalo lililopo ni bei ya vifaranga ambavyo hununuliwa shilingi 800 kwa kila kifaranga. Pale ambapo mtu ana bwawa la mita 20 kwa 10, anahitaji vifaranga zaidi ya 200 ambavyo gharama yake ni kama shilingi 160,000/=, kwa wafugaji wadogo hiyo ni bei kubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha kifedha hawa wafugaji, hata kwa mkopo waweze kuendeleza miradi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba, kwa kuwa Serikali sasa imesema inayo mabwawa ya darasa, ni kwanini sasa isiweke vifaranga katika mabwawa hayo ili wakulima hao waweze kupata vifaranga kwa bei ndogo na waweze kukidhi mahitaji kutokana na uwezo wao mdogo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kweli bei ya vifaranga iko juu, lakini mkazo umewekwa katika kuandaa vituo ambapo vifaranga bora vinapatikana. Baada ya vifaranga kuwa vingi zaidi ni jambao la uhakika kwamba, bei itashuka kwa sababu ni suala la kiuchumi. Pia tunaomba kwa namna ya kuwawezesha wafugaji wa samaki mkoani

Kagera, wamejipanga katika makundi na kwa njia ya makundi haya wanaweza wakapata mikopo kwa sababu zaidi ruzuku haipo ya kutosha, hivyo itabidi waende katika taasisi na vyombo vya fedha kuweza kupata fedha kwa ajili ya mitaji ya kupata vifaranga.

Mabwawa haya matatu ya mfano yaliyochimbwa na Serikali kule ni Serikali ndiyo iligharamia kuweka vifaranga na vifaranga hivi vimesambazwa katika mkoa mzima wa Kagera. Bado tutajitahidi zaidi kuboresha ili kuwepo na vyanzo ambavyo *restocking* imefanywa na Serikali na humo wafugaji wa samaki waweze kupata mbegu ya samaki watakaokuwa wanawafuga.

**NAIBU SPIKA:** Tumejifunza Kiswahili Waheshimiwa Wabunge kumbe watoto wa samaki wanaitwa vifaranga.

Swali limetoka Ziwa Victoria, swali la nyongeza naomba litoke baharini, Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Maisha ya kamba tangu kuzaliwa hadi kuzeeka ni miezi tisa. Sababu zipi zilizopelekea Serikali kupiga marufuku kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita sasa uvuvi wa kamba usifanyike hasa kule kwenye *delta?*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu ya uvuzi ni endelevu. Kutokana na utafiti uliofanywa na taasisi yetu ya kitaifa inayojishughulisha na utafiti wa samaki - *TAFIRI,* hawa kamba walibainika wamevuliwa kupita kiasi na hivyo kulikuwepo na hatari ya kuwamaliza kabisa, hivyo ikaonekana ni busara kufunga kwa muda ili kuwapa muda wa kuzaana na kuongezeka ili kiasi kitakachovuliwa kisije pia kikatishia kumaliza aina hii ya samaki ambayo ni muhimu sana kwa lishe na uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni sera ndiyo imeelekeza na hatari ya kumalizika kwa aina hii ya samaki, ndiyo ikaonekana kwamba, tufunge kwa muda ili wapate nafasi pia ya kuzaana na kuongezeka.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa Konde.

Na. 202

**Makosa ya Kuyafungia Magazeti**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Je, makosa ya aina gani yanaweza kusababisha Serikali kuyafungia magazeti kama ilivyotokea kwa kufungiwa kwa gazeti la Mwanahalisi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magazeti ni moja ya vyombo vya habari ambavyo hutumika na watu wengi kupata habari, kujielimisha na kujiburudisha. Hapa Tanzania magazeti huendeshwa kwa kuzingatia Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 pamoja na Kanuni zake za mwaka 1977. Hivyo, basi uendeshaji wa shughuli za magazetu ni lazima uzingatie sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, magazeti hupewa adhabu ya kufungiwa, kusimamishwa na hata kufutiwa usajili kwa kukiuka Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na sheria nyingine za nchi kama vile Sheria ya Makosa ya Jinai na Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970.

Mheshimiwa Naibu Spika, magazeti pia hufungiwa iwapo mambo yafuatayo yatatokea:-

Kuchapisha habari zisizo na kweli, kuchapisha habari za uchochezi na kuchapisha picha mbaya zinazokiuka maadili ya Mtanzania na taaluma ya habari. Sababu nyingine ni pamoja na gazeti kutochapishwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo na kufilisika kwa kampuni inayochapisha magazeti husika.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa moja kubwa ya Serikali za kidikteta duniani kote ni kupenda kusifiwa na kutukuzwa, na huwa mbogo sana pale wanapokosolewa kwa kuambiwa maovu ya Serikali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hizo hutumia sheria dhaifu katika kugandamiza uhuru wa kutoa maoni, kama ilivyo sheria dhaifu ya magazeti ya mwaka 1976 hapa nchini ambayo inampa mamlaka Waziri anayehusika na Wizara ya Habari kufungia chombo chochote cha habari kwa kadiri atakavyojisikia yeye mwenyewe.

Je, Serikali haioni kuendelea kutumia sheria hii kandamizi ni kujitafutia nafasi ya kuwa miongoni mwa nchi ambazo haziheshimu haki za uhuru wa kutoa maoni? (*Makofi*)

Swali la pili, pamoja na jibu la Mheshimiwa Waziri kwamba, moja ya sababu zinazopelekea kufungiwa magazeti ni kuchapisha picha mbaya zinazokiuka maadili. Lakini tunashangaa sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa…

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Kuna magazeti ambayo yamegeuza picha za miili ya mama zetu, dada zetu na ndugu zetu wanawake kuwa ni malighafi ya kuuzia magazeti hayo na yamejaa nchini mwetu na hakuna sheria yoyote wala hatua inayochukuliwa na Serikali kudhibiti uchafu ule unaoanikwa katika nchi yetu kote. Naomba jibu sahihi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, kama ifuatavyo.

Kwanza niseme tu kwamba, Serikali ya Tanzania siyo ya kidikteta, ni Serikali ambayo inaheshimu uhuru wa wananchi wake kupata habari.

Nataka niseme kwamba, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache za Afrika zenye magazeti mengi (Magazeti 781. Kuna magazeti 13 yanayotoka kila siku na kuna magazeti 52 yanayotoka kwa wiki. Kwa hiyo, ni Serikali ambayo inajali na siyo Serikali ya kidikteta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, sheria hii tayari tumeishakusudia tutawasilisha Muswada hapa Bungeni wa kusimamia vyombo vya habari, lakini bado sheria hii ndiyo inayotumika na kwamba, maamuzi ya Waziri ni ya kisheria, siyo kwa hisia zake ni kwa kufuata sheria zilizopo sasa; Sheria Na. 3 ya mwaka 1976 kifungu cha 25(1).

Tumepokea changamoto hiyo kwamba, yapo magazeti ambayo yanatumia picha mbaya lakini hawaruhusiwi kwa maana ya kufuata sheria na weledi wa uandishi wa habari. Kama Serikali tunatoa onyo na tutachukua hatua kali pale itakapothibitika.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Pamoja na maelezo ya Waziri, naomba nimwulize swali moja. Hebu atuambie kiukweli kwa sababu tangu enzi za Mawaziri wa Habari waliopita, wamekuwa wakituambia kwamba, tutaleta sheria ya vyombo vya habari.

Sasa hivi pia Waziri amesema italetwa. Ni lini hasa sheria ya vyombo vya habari italetwa humu Bungeni? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba, kumekuwa na ahadi hiyo. Nataka niwahakikishie tu kwamba, mchakato umeishakamilika na tayari imeishafika katika Baraza la Mawaziri. Kuna mihimili mitatu, kuna Serikali na Bunge na hatimaye tutawasilisha hapa Bungeni wakati wowote kuanzia sasa. (*Kicheko*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siulizi swali la nyongeza bali naomba swali langu Na. 203 la kulinda utu wa Mwanamke lijibiwe sasa.

Na. 203

**Sanaa Kudhalilisha Utu wa Mwanamke**

**MHE. JAMES F. MBATIA** aliuliza:-

Baadhi ya sanaa kama vile filamu na muziki huonyesha ukatili dhidi ya Mwanamke kama vile kupigwa kikatili, kutukanwa na kuvalishwa nguo fupi kama chachu ya biashara hizo:-

Je, Serikali inalishughulikia vipi suala hili ambalo linaporomosha maadili na kudhalilisha utu wa Mwanamke? *(Makofi)*

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Ukahaba nchini kama vile ilivyofanyika katika nchi nyingine kama Afrika Kusini kwa kuwa hivi sasa hata makahaba wanapokamatwa na Polisi huachiwa huru kwa kuwa hakuna sheria ya kuwadhibiti?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa makahaba ili waweze kutambua athari za tabia hiyo na wajue thamani waliyo nayo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa mstari wa mbele kukemea na kuchukua hatua katika suala la mmomonyoko wa maadili unaolenga kudhalilisha utu wa mwanamke kama vile kupigwa kikatili, kutukanwa na kuvalishwa nguo zisizofaa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kuchukue hatua za kurekebishwa, kushauri, kuzuia na kukataa filamu ambazo zilionekana kuvunja maadili ya Kitanzania na zile zilizokiuka taratibu na Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza na kanuni zake.

Hii inajumuisha pia filamu zenye matendo yenye mwelekeo wa kudhalilisha wanawake zilizozuiwa kuonyesha hadharani na baadhi zilisitishwa kusambazwa mpaka zilipofanyiwa marekebisho kutokana na kasoro zilizojitokeza.

(ii) Wizara yangu kupitia Bodi ya Filamu imeendelea kukemea na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari, Elimu inayotolewa inahusu masuala yote yanayohusiana na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni ambazo zinaelekeza uzingatiaji wa maadili, weledi na taaluma katika tasnia ya filamu. Aidha, Serikali imekwishaanza utekelezaji wa taratibu za urasimishaji wa tasnia za filamu ya muziki ambao utasaidia kurejesha nidhamu katika tasnia hizi na kuongeza wigo wa usimamizi, udhibiti na ufuataji wa sheria na kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwakumbusha watengenezaji, wasambazaji na wasanii kutotengeneza na kutoshiriki katika filamu zenye udhalilishaji na kukiuka maadili.

Aidha, wakumbuke wanawajibika kuwasilisha Miswada ya filamu zao na filamu kwa ukaguzi kabla ya kuingiza sokoni. Kinyume na hivyo ni ukiukwaji wa sheria na kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu kuhusu suala la maadili, weledi na taaluma katika tasnia za filamu na muziki ili mazao ya kazi hizo yarejee katika hadhi na taswira chanya katika jamii.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa suala la utu ni ubinadamu na lengo la tatu la millennia linazungumzia usawa wa jinsia zote, licha ya kwamba baadhi ya wasanii wetu wanafanya kazi nzuri lakini zaidi ya asilimia 90 wanahamasisha masuala ya mapenzi, ngono, ngono ambayo yanaigwa *copy and paste* na sio maadili ya Kitanzania.

Je, Serikali kupitia Bodi inafanya ukaguzi wa namna gani na kutoa elimu na kuwapatia uwezo wasanii wetu ili waweze kufanya mambo ambayo ni chanya kwa Taifa. Kwa mfano kuhamasisha masuala ambayo yanaendana na mazingira na maadili ya Kitanzania ili kukuza utu zaidi ya Mtanzania hasa mwanamke kwa maadili yaliyo mema ya Kitanzania. Hilo la kwanza.

La pili, wako baadhi ya wafanyabiashara wanatumia watoto zetu, mabinti zetu na hasa akinamama kama bidhaa kuwafanya kama ni chombo cha biashara na kinadhalilisha utu wao kwa ajili ya kujipatia kipato na baadhi ya shughuli nyingi hata sisi viongozi tunaona. Je, Serikali inasema nini, inatoa tamko gani na sisi tunajitambua kiasi gani hasa sisi wanaume kukemea udhalilishaji huu mkubwa wa wanawake katika jamii ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba filamu nyingi unaweza ukazikuta kwa asilimia kubwa labda zinahusu mapenzi.

Lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba Bodi ya Filamu inafanya ukaguzi kuhakikisha kwamba filamu zinazotengenezwa hapa Tanzania na zinazokuja kutoka nje ya Tanzania zinakaguliwa na zile ambazo zinakuwa zimekiuka maadili hayo basi hurekebishwa au kukatazwa kabisa kuonyeshwa na hutenga madaraja mbalimbali ya kuangalia kwa maana ya watoto na watu wazima.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie kwamba kupitia Bodi ya Filamu Serikali inaliona suala hilo na inafanya ukaguzi maalum kabisa kwa suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhusu kwamba wafanyabiashara kuwatumia watoto na wanawake kuwadhalilisha. Nitumie fursa hii tu kusema kwamba wafanyabiashara wote wahakikishe kwamba hawawatumia watoto, kuwalinda watoto hao.

Lakini pia wasiwatumie wasichana na wanawake katika kuwadhalilisha kwa maana ya kufanya biashara zao na Serikali inatoa onyo kwa wafanyabiashara hao ambao watabainika kwamba wakikiuka maadili ya Kitanzania.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda wetu tusaidiane tu tuna maswali 10, maswali 5 yameshachukua robo tatu ya saa, tuna robo tatu saa imebaki kwa maswali matano (5). Kwa hiyo tuendelee na swali la Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto swali la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige.

Na. 204

**Uundwaji wa Sheria ya Kudhibiti Ukahaba Nchini**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Biashara ya ukahaba imeendelea kushamiri hapa nchini na kusababisha mmomonyoko mkubwa wa maadili, maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, ongezeko la Watoto wa Mitaani na kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherina Valentino Magige, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wowote wa Serikali kutunga sheria ya kudhibiti ukahaba nchini kama vile ilivyofanyika katika nchi nyingine itafanyika kama patatokea matokeo ya tathmini ya kuonesha upungufu wa mfumo wa sheria tulionao unavyoshughulikia vitendo vya ukahaba. Kwa sasa, vifungu vya 146, 148, 149 vya Kanuni ya Adhabu (*Penal Code, Cape 16 R.E. 2002*) vinaharamisha kitendo cha mwanamke kuishi kwa kutegemea mapato ya ukahaba na kusaidia kufanyika kwa vitendo vya kikahaba kwa kutoa mahali pa kufanyia vitendo hivyo au kula njama ya kuwezesha kufanyika kwa vitendo hivyo. Adhabu ya mtu anayevunja sheria ni pamoja na kutumikia adhabu ya kifungo jela kisichozidi miaka miwili au kulipa faini na kifungo cha miaka mitatu jela.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hatua zinazochukuliwa na vyombo vya sheria dhidi ya vitendo vya ukahaba, kwa sasa Serikali itaendelea kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali mojawapo likiwa lile la "*Kiota Women and Health and Development*" (KIWOHEDE) kuielemisha jamii wakiwemo wanaume na makahaba ili waweze kutambua athari za tabia hiyo na wajue thamani wakiwemo wanaume na makahaba ili waweze kutambua athari za tabia hiyo na wajue thamani waliyo nayo.

Shirika hilo kwa mfano, limekuwa likiwaondoa wasichana makahaba kwenye maeneo wanayofanyia ukahaba na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukahaba pamoja na kuwapatia stadi mbalimbali ambazo zitawawezesha kujitegemea na kuachana na ukahaba. Stadi wanazopatiwa ni ufumaji, utengenezaji wa batiki, usindikaji wa vyakula ushonaji na kadhalika. Aidha, Shirika hili limekuwa likiwaendeleza ki-elimu na baadhi yao wanajiunga na Vyuo vya Ufundi *(VETA).* Hadi sasa zaidi ya vijana 40,000 wamefaidika na huduma za KIWOHEDE. *(Makofi)*

**MHE. CATHERINA V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kwa mujibu wa Mheshimiwa Naibu Waziri ni dhahiri kuwa adhabu inayotolewa kwa wanaojihusisha na vitendo hivi vya ukahaba ni ndogo sana. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuweka adhabu kali ili kudhibiti vitendo hivi.

Swali la pili, je kwa mujibu wa takwimu hadi sasa ni kesi ngapi ambazo zimeshapelekwa Mahakamani dhidi ya hawa wanaojihusisha na vitendo vya ukahaba?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kuhusiana na kutunga sheria ya kufanya marekebisho ili kuweka adhabu kali ya kuzuia vitendo hivi vya ukahaba. Napenda kusema kwamba suala hili la ukahaba linaenda mbali zaidi ya sheria. Suala hili ni tatizo la kijamii, ni tatizo ambalo tunahitaji tuboreshe zaidi maadili yetu na kila mmoja kwa nafasi yake anatakiwa aweze kukuza maadili.

Sisi wenyewe pia kama ni wanaume tusipoenda huko hawa makahaba watakosa biashara. Lakini kwa upande wa adhabu tutaliangalia kwa makini kwa sababu kwa hali ilivyo sasa imejitokeza kwamba washtakiwa wengi ni wale ambao wanajirudiarudia. Akimaliza kifungo au akimaliza faini yake amekuwa anakuta anarudi kwenye shughuli zake. Kwa hiyo tutaliangalia ili tuone ni kwa namna gani basi tukichanganya na kuboresha maadili yetu na elimu kwa umma tuone ni kwa namna gani tutaboresha sheria hii.

Lakini suala la pili kuhusiana na takwimu za kesi mbalimbali ambazo zimefunguliwa hadi sasa nitoe tu mfano wa Dar es Salaam, kwa miezi mitatu kuanzia Januari mpaka Aprili, mwaka huu katika Mahakama ya Jiji zilifunguliwa kesi takribani 22 zenye washtakiwa 123.

Lakini napenda tu kutoa angalizo kwamba kesi hizi huwa nyingi imekuwa ni taabu sana kama ambavyo nimeeleza tumekuwa tukitumia kifungu cha 146, 149, 149 ya Kanuni ya Adhabu.

Lakini watu wengi wamekuwa hawatoi taarifa. Watu wengi wanajua madanguro mbalimbali yanayotumika lakini hawatoi taarifa na ukiangalia katika kifungu cha 147 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu ukipeleka taarifa Mahakamani Hakimu anaweza akatoa kibali cha kufanya upekuzi kwenye nyumba fulani na mmiliki wa nyumba anaweza akachukuliwa hatua. Ahsante sana.

Na. 205

## Ghala la Kuhifadhia Chakula Kigoma

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga maghala ya kuhifadhi chakula katika Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Gdenzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ulifanya tathmini katika mkoa wa Kigoma kwa lengo la kubaini kiwango cha uzalishaji, miundombinu ya kuhifadhi nafaka na usafirishaji ili kuona uwezekano wa kufungua vituo vya ununuzi wa mahindi katika msimu wa 2013/2014. Tathmini hiyo ilibaini kuwepo kwa uzalishaji wa kutosha katika mkoa huo na uboreshwaji mkubwa wa miundombinu hususan barabara katika miaka ya hivi karibuni. Kufuatia hali hiyo Wakala uliridhika na hivyo kupanga kuanza kununua mahindi mkoani Kigoma katika msimu wa mwaka wa fedha 2013/ 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango huo Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* utaanzisha vituo vya kununua na kuhifadhi mahindi kwa muda (*Transit Sheds*) wakati yakisubiria kusafirishwa kwenda kwenye maghala ya Shinyanga na Musoma kwa ajili ya uhifadhi. Aidha, *NFRA* itaendelea kutumia maghala yaliyopo kwa sasa yaliyojengwa kwa ufadhili wa Programu ya Maendeleo ya Kilimo *(ASDP)* kupitia Mpango wa *DADP's* na mradi wa *DASIP* na yale yaliyofadhiliwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango yake ya muda mrefu *NFRA* itaangalia uwezekano wa kujenga miundombinu zaidi ya kuhifadhi chakula ili kusogeza zaidi huduma kwa wananchi. Aidha, *NFRA* kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi inaandaa mpango wa uwekezaji (*Investment Plan*) ambao pamoja na mambo mengine utabaini maeneo mahsusi ya ujenzi wa maghala kulingana na tathmini za uzalishaji wa mazao yote nchi nzima. Mpango huo utakapokamilika utatumika katika kutafuta fedha za kugharamia uwekezaji kutoka Taasisi mbalimbali za fedha.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda nipongeze majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, lakini vilevile nipongeze kwamba mmetambua kwamba mkoa wa Kigoma sasa unao mahindi ya kutosha.

Kwa kuwa uhaba wa maghala haya ndio umesababisha uzalishaji usiwe wa kiwango kikubwa. Kwa kuwa mna mipango yote hii nilitaka kujua moja ni lini sasa haya maghala yataweza kujengwa ili wananchi waweze kujua wapi wapeleke mazao yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa mipango ambayo tayari imeshakamilika kwa maana ya *feasibility study* ilishafanywa ili kupata nakisi ya tani 160000 ambayo ndiyo nakisi ya hifadhi inayokadiriwa. Fedha zinazohitajiwa ni shilingi bilioni 211. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona hizo fedha kidogo ni nyingi lakini kwa sababu tumegawa maghala haya kwenye maeneo yote pamoja na kwamba tutapata *transit shed* pale Kigoma ambayo yenyewe peke yake yanagharimu karibu shilingi billioni 2. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kigoma kwamba kwa sababu tunatambua kwamba katika miaka 6 iliyopita mkoa wa Kigoma umetoka kwenye uzalishaji wa nafaka tani 200000 hadi karibu tani 500000. Kuna umuhimu wa dharura kabisa kupeleka maghala hayo na Wizara yangu inaifanyia kazi kupitia Bajeti yetu ya mwaka huu ili tuweze japo kuanza na usanifu wa mradi huo kwa upande wa Kigoma.

Na. 206

**Ujenzi wa Barabara ya Ukanda wa Pwani**

**MHE. AMINA M. MWIDAU** aliuliza:-

Wananchi wa Tanga-Pangani-Bagamoyo wana shida kubwa ya barabara ya lami (Barabara ya Ukanda wa Pwani) ambayo ilikuwa inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu ili ianze kujengwa:-

Je, ujenzi wa barabara hiyo utaanza lini hasa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** aljibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tanga-Pangani-Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 178 ni sehemu ya barabara ya Malindi-Mombasa-Lunga Lunga/Tanga – Bagamoyo ambayo inafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na Mhandisi Mshauri aitwaye Aureco wa Afrika Kusini chini ya ushirikiano wa Jumuiya wa Afrika Mashariki kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya usanifu wa barabara hii bado inaendelea. Kazi hii imechelewa kukamilika kutokana na kubadilishwa kwa mwelekeo wa barabara (*realignment)* katkika Hifadhi ya Taifa ya Saadani ili kukwepa athari kubwa za kimazingira ambazo zinaweza kusababishwa na kupitisha barabara hii ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina na kupatikana kwa fedha.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kila tunapotaja barabara hii ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mwaka wa juzi, mwaka jana na mwaka huu pia nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetengewa fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe kauli ya Serikali ni lini hasa upembuzi yakinifu utakamilika na barabara hii kujengwa mara moja?

Swali la pili, kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana na ukamilifu wake utafungua fursa za kiuchumi, za kibiashara na utalii na kukuza uchumi wa watu wa Mwambao wa Pwani na Watanzania kwa ujumla. Na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi amesema ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina na kupatikana kwa fedha. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa haraka na mara tu baada ya upembuzi yakinifu kukamilika au ujenzi huo kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba usanifu wa barabara hii unaendelea. Pia nimekiri kwamba umechelewa kwa sababu tulibadilisha *realignment* ilikuwa imekamilika ikaja hoja kwamba isipite ndani ya hifadhi. Kwa hiyo kidogo ikachelewa. Kwa hiyo nina imani kabisa

kazi ya usanifu itaisha mapema iwezekanavyo. Kuhusu suala la fedha mradi huu wa Tanga-Pangani-Bagamoyo upo katika hii miradi ambayo ni kipaumbele kwa Ushirikiano wetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, tunasema kwamba kwa sababu tunafanya kwa ujumuiya tutakapomaliza *design* tutajua gharama ya fedha ni kiasi gani kinahitajika, basi fedha hizo zitatafutwa na zikishapatikana ujenzi utaanza.

Na. 207

**Askari wa Barabara Kupatiwa Simu za Upepo**

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEHE** aliuliza:-

Polisi wa Usalama Barabarani Zanzibar mara nyingi hutumia simu za Mkononi kwa ajili ya kazi zao kiulinzi na Usalama.

Je, Serikali itawapa lini Askari hao Simu za Upepo (*Radio Call*)?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowaambia kwa sababu ya muda mnaona maswali mawili bado na muda wetu umeisha. Kwa hiyo, tatizo letu kubwa maswali ni mengi kuliko muda ambao unapangwa na ndio maana hampati maswali ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali ya Mheshimiwa Ramadhani Haji Salehe, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya Askari wa Usalama Barabarani Zanzibar walikuwa wanatumia Simu zao za mkononi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Hii ilitokana na ubunifu wao katika kukabiliana na upungufu wa vitendea kazi zikiwemo Radio. Hata hivyo, kwa sasa Serikali imefanikiwa kutatua tatizo hilo kwa kiasi

kikubwa kwani kikosi cha Usalama Barabarani Zanzibar kimepatiwa jumla ya Radio 10 za Upepo (*Radio Call)* ambazo zitatumika kwa ajili ya kazi za ulinzi na usalama. Serikali itaendelea kuboresha hali ya vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi kwa kadiri ya uwezo utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama alivyosema Mheshimiwa NaibuWaziri kwamba tatizo hilo lipo kwa muda mrefu na hadi hivi sasa askari hao wanatumia simu za mkononi katika kazi zao za kawaida. Je, ni lini askari hao watapatiwa hela kwa ajili ya kujikimu hizo simu zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze askari hawa kwa kuonyesha uzalendo na kuwa na moyo wa kufanya kazi hii. Tunawashukuru kwa kitendo hiki na suala la kupatiwa vocha halitatatua tatizo hili la msingi isipokuwa tatizo la msingi ni kuhakikisha kwamba tunawapatia radio, tunawapatia hizi na tutawapatia nyingine ili kazi hii ifanyika kwa misingi inayotakiwa. Simu za mkononi si vyombo rasmi vya kufanya kazi hii na tusingependelea kuendelea kuvitumia kwa kazi hizi kwa namna ambavyo vipo. Unaweza ukamtafuta mtu akawa amezima au anashughuli nyingine. Kwa hiyo, si vyombo ambavyo tunavipa kipaumbele isipokuwa tunashukuru pale ambapo hakuna njia nyingine zikatumika.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge swali la mwisho kwa siku ya leo ni swali la Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa na litaulizwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa niaba yake.

Na. 209

**Kudhibiti Uvunaji Holela wa Miti**

**MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. MHE. MCH. PETER S. MSIGWA**)aliuliza:-

Utafiti wa Shirika la Chakula na Kilimo, Duniani *(FAO)* ni kwamba Tanzania ni moja kati ya nchi kumi zinazozalisha

mkaa kwa wingi duniani; na inatumia tani 2,650 za mkaa kila siku, kiasi ambacho kinahitaji hekta 856.25 za eneo la misitu kwa ajili na tafiti zinaonyesha kuwa ukataji huu wa miti ukiendelea hivi, miti yote Tanzania itakwisha kwa kipindi cha miaka saba mpaka kumi ijayo:-

Je, Serikali in mpango gani wa kudhibiti uvunaji holela wa miti?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala hili hapana shaka ni saula muhimu sana. Niseme ili kudhibiti uvunaji holela wa miti, Wizara ilianzisha mwongozo wa uvunaji endelevu wa mazao ya misitu nchini kwa tangazo la Serikali Na. 69 na 70 la mwaka 2006 ambapo kila Wilaya ina Kamati ya uvunaji ambayo ina wajibu wa kudhibiti uvunaji holela wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mwongozo huo, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu *(TFC)* nchini imeanzisha *program* zifuatazo:-

(i) Kuanzisha teknolojia mbadala ya kutayarisha mkaa kwa kutumia matanuri ya kasamansi kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI).*

(ii) Utengenezaji wa mizinga ya kisasa ili kuondokana na utegemezi wa misitu katika kuongeza kipato cha mwananchi, kwa mwaka 2012/2013 mizinga 10,000 ya kisasa imesambazwa na mwaka 2013/2014 mizinga 70,000 itasambazwa.

(iii) Doria maalum na ukaguzi za kushtukiza ili kudhibiti na kuchunguza mfumo wa biashara ya mazao ya misitu nchini hufanyika.

(iv) Kuongeza kasi ya upandaji miti nchini pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mei 2009 Serikali za Tanzania na Finland kwa kushirikiana na wataalam kutoka Shirika la Kilimo na Chakula *(FAO)* zilianzisha mradi wa Tathmini ya Rasilimali za Misitu Tanzania Bara *(NAFORMA).* Matokeo yatatangazwa rasmi tarehe 24 mwezi huu Jijini Dar es Salaam wakati tutakapokutana na Waziri wa Finland kuhusu matokeo ya kazi hii. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2009 Benki ya Dunia ilifanya *study* inayoitwa *Transforming the Charcoal Sector in Tanzania* ambapo iligundua zaidi ya tani laki tano kwa mwaka zinatumika kama mkaa katika Jiji la Dar es Salaam peke yake. Thamani ya sekta nzima ya mkaa nchini ni zaidi ya dola milioni 650/- ambayo ni kama one trillion na Serikali inapoteza mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 150/- katika mfumo mzima wa biashara ya mkaa. Katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani tulipendekeza kwamba Serikali ichukue mfumo wa Brazil wa kurasimisha biashara hii na kuruhusu watu waweze kulima misitu kwa ajili ya mkaa. Serikali inachukuliaje pendekezo hilo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunaokoa misitu yetu ambayo inakatwa kwa kasi kubwa sana hapa nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi *World Bank* walifanya *study* lakini pia ni sahihi *FAO* walifanya *study* na matokeo hayakupishana sana. Ni kwamba changamoto tulizonazo kwenye eneo hili ni kubwa na Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, Serikali kuu nikiri kabisa kwamba yenyewe peke yake haitaweza kukabiliana na tatizo hili. Ndiyo maana tulianzisha Kamati ngazi ya Wilaya, ndiyo maana kumekuwa na vikao husika lakini pia na Wabunge wanahusika katika kuhamasisha lakini pia katika kutoa mawazo mbadala ili tuweze kuondokana na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango kupitia *TFS* ambayo na ndiyo ilikuwa shabaha kubwa ya kukabiliana na tatizo hili na mengine ambayo yako katika Sekta ya Misitu na niseme tu kwamba tunajiandaa kuwa na kongamano ambalo tutaitisha wadau mbalimbali. Kwa sababu tunataka kutizama mapendekezo mbalimbali ambayo yamekuwepo na *experiences* mbalimbali za nchi tofauti kwa sababu India wanazo *experiences* zao, Malaysia wanazo *experiences* zao, Brazil ndiyo imekuwa juu zaidi ukitizama katika *study* ya *World Bank* na *study FAO.* Tunataka kutizama ni njia ipi katika mwaka huu na tuje na mapendekezo gani.

Lakini kubwa ni la ku-*involve private* sekta na kuwa-involve wananchi wenyewe kuona kama wanaweza waka-take leadership wakati Serikali ikiwa ina-*provide framework* ya *policy* kuhusu sala hili zima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwa kipindi hiki cha maswali. Kwa kweli nawaona jinsi mnavyokereka kwa kutokupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Lakini utaratibu wetu wa kuwa na maswali kumi ndani ya saa moja ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, tunakaribisha maoni ya namna gani nadhani kipindi chetu kinaweza kuwa bora zaidi ili Kamati ya Uongozi na Kamati ya Kanuni mbele ya safari waje kuona namna ya kuboresha kipindi chetu cha maswali tupunguze kukereka huko kama yapo mapendekezo.

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo mawili tu hapa, kwanza kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Margaret Sitta, anawaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane saa saba mchana leo ghorofa ya pili jengo la Utawala ukumbi Namba 227.

Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uchumi Viwanda na Biashara saa saba wakutane Ukumbi wa Pius Msekwa. Katibu tuendelee!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2013/2014 Wizara wa Ujenzi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Deusderius Mipata atafuatia. Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niungane na wenzangu kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri na wenzake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakwenda moja kwa moja kwenye msongamano Dar es Salaam. Msongamano Dar es Salaam umekuwa ni kero lakini nipongeze hata taarifa ya Kamati imesema hivyo na imetoa mawazo yake. Mimi nimwombe tu Waziri alipochaguliwa kwenye Wizara hii kitu cha kwanza alichozungumza ni kuhakikisha msongamano ule wa Dar es Salaam, unapungua au unakwisha.

Kwa hiyo, nikuombe Waziri ile dhamira yako uendelee nayo. Kamati imezungumza mengi tu kwamba msongamano unasababisha uchumi kuwa si mzuri lakini pia msongamano unasababisha mapato mengi ya Serikali yanakosekana. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri na nilete maombi ya Wabunge wa Dar es Salaam wanasema wako tayari kukodi ndege dola 2600 sawa sawa na milioni nne na kitu hivi ili tupate masaa mawili asubuhi na jioni Mheshimiwa Waziri na timu yako muone hali ya Dar es Salaam ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema inawezekana huwa unazungumza tu lakini hujui hali ya Dar es Salaam ilivyo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tukuombe sana. Lakini mwanzo kabla ya Wizara yako kugawanywa ilikuwa ni Wizara moja. Bado tunakuomba ushirikiane na Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kuhakikisha mnashirikiana kupunguza msongamano. Maana yangu kuna gati Namba

13, 14 na reli. Mheshimiwa Dkt. Mwekyembe kaanza utaratibu mzuri tu wa kupunguza msongamano kwa kutumia reli. Kwa hiyo, nina uhakika mkishirikiana itaweza kusaidia sana sana. Lakini Mheshimiwa Waziri J*ICA 2007* waliwahi kufanya *study* wakaoanisha barabara karibu 600. Wakatoa jawabu kwamba kama Dar es Salaam kwa miaka sita kila mwaka ingepata dola milioni 100/- basi kwa kiasi kikubwa msongamano ungeweza kupungua. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri ile *study* uliiona?

Mheshimiwa Naibu Spika, *flyover* ilikuwa tangu mwaka 2010 ianze. Lakini hadi leo kimya. Tumeona umetenga bilioni 3/- sijui zitafanya kazi gani? Kwa hiyo, kubwa Mheshimiwa Waziri tunakuomba sanasana utusaidie Dar es Salaam kuondoa msongamano. Mheshimiwa Waziri barabara ya *Davis Corner - Jet Corner,* barabara ile ilikuwemo kwenye msongamano; ilianza tangu mwaka 2009 lakini hadi leo kuna eneo kubwa kabisa la Sigara – Lumo na darajani imekwama na mkandarasi anasema sababu ni pesa na pesa tunatenga kila mwaka za barabara hiyo. Sasa tunapata maswali mengi sana Mheshimiwa Waziri, sijui hela zinakwenda wapi?

Lakini yako maeneo hebu yachunguze kwa sababu wakandarasi wengi wanakwama kwa ajili ya pesa. Inasemekana kwamba pesa zile kuna mchezo unachezwa kwamba huchukuliwa hela za makandarasi zikawekwa kwenye *fixed deposit* zikazaa hapo kwa miezi mitatu minne zikafanya kazi nyingine. Hebu liangalie hilo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hii barabara ya *Jet Corner – Davis Corne*r tuna barabara pale tumeongeza pale ya mashine ya maji ambayo inakwenda mpaka *Kilwa Road.* Nilikuwa naongea na Meneja wangu anasema kwamba imetengwa hela kidogo ya *moram.* Nikuombe Mheshimiwa Waziri pale ni pafupi tu, tuangalie uwezekano kama tuna dhamira ya kupunguza msongamano Dar es Salaam tuongeze hela ili barabara ya Mashine ya Maji kutoka Azimio kwenda *Kilwa road* iweze kupata pesa iweze kusaidia kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bandari, *BP* pale mpaka Mtoni ni barabara ambayo ilijengwa na Kajima lakini bahati mbaya tuliipokea kabla ya wakati wake barabara imeharibika. Kwa hiyo Kajima hawakuichukua kwenye marekebisho. Wamechukua barabara ya kutoka Mtoni mpaka Mbagala. Kwa hiyo, nimeambiwa zimetengwa fedha kidogo nikuombe tuongeze pesa za kutosha ili barabara ile nayo tuweze kuishughulikia ipasavyo. Kuna pesa tumetenga siku nyingi za taa barabarani, *Nyerere Road – Jet Corner* lakini taa zile hadi leo hazijawekwa. Barabara ya Sokota kwenda Viwandani tuliomba taa ya barabarani hali yake pale si nzuri ajali ni nyingi. Kwa hiyo, tunaomba uliangalie hilo uweze kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameniomba kwa sababu hawachangii, barabara ya Uhuru, Mheshimiwa Zungu amekuwa akiipigia kelele muda mrefu sana lakini hii barabara ni ya kihistoria. Mtu yoyote ambaye anaijua nchi hii lazima atakuwa anaijua Barabara ya Uhuru. Mwalimu Nyerere ndiyo alikuwa anapita wakati tunatafuta uhuru lakini leo imekosa heshima inayostahili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu ipe kipaumbele barabara hiyo. Mheshimiwa Idd Azan kaniomba nizungumzie barabara ya Magomeni. Mabasi yaendayo kwa kasi. Mheshimiwa Waziri eneo la Magomeni limekuwa ni kero, mvua zikinyesha maji yanaingia kwenye majumba ya watu.

Kwa hiyo, tuombe umwambie mkandarasi najua TAMISEMI ndiyo wahusika zaidi lakini kwa kuwa wewe ndiye msimamizi wa barabara zote useme na makandarasi wajaribu kurekebisha maji yawe yanakwenda kwa wakati. Lakini leo kwa kuwa barabara ile inapitika hivyohivyo unaweza ukapita karibu na nguzo za umeme. Sasa sijui tatizo ni nini kama barabara inajengwa, nguzo za umeme mpaka leo hazijatolewa.

Lakini ukifika pale *NSSF Kawawa Road* na *Morogoro Road* kwenda mpaka Samora barabara ile imeshakwisha. Kwanini isifunguliwe watu wakaendelea kutumia wakati tukiwa tunasubiri mabasi yaendayo kwa kasi yaanze kazi

zake. Lakini hii barabara yote ukiiangalia; ni kweli tunataka ijengwe iishe iwe nzuri. Lakini imekua ni kero, imekuwa na foleni kupita kiasi. Kwa hiyo, tuombe zile kero zisizokuwa za lazima ambazo zinaweza kupunguzika tuzipunguze kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana kwa mpango wa kuanzisha boti ya kutoka Dar es Salaam kwenda Bagamoyo lakini pia nipongeze sana daraja la Kigamboni. Nimpongeze Waziri wetu wa Kazi na Ajira mama Kabaka, nipongeze uongozi wa *NSSF* ukisimamiwa na Dkt. Dau lakini niiombe Serikali zile ahadi zake kwenye hii mifuko iwe inatekeleza. Ama sivyo mifuko hii itapata lawama kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambazo kwa kweli imekuwa ikifanya kazi katika nchi hii. Mahala pote kazi zinakwenda vizuri, mipango yake naona inaendelea vizuri kwa kweli wanatakiwa kuwa ni mfano wa kuigwa. Kwa maana hiyo naunga mkono hoja moja kwa moja nisije nikasahau. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara inayojengwa kwenda Sumbawanga kutoka Tunduma. *Speed* ni nzuri lakini eneo la kutoka Tunduma kwenda Ikana, speed yake haina kasi ya Wizara. Wizara ina kasi yake lakini ile sio kasi ya Wizara inatakiwa isukumwe zaidi. Tuna hamu watu wa Sumbawanga kupita kwenye lami. Ikazaniwe.

Lakini pia kuna barabara zinazoendelea Mkoani Rukwa kutoka Sumbawanga kwenda Kanazi, Kanazi kwenda Kibaoni na Kibaoni Mpanda au Kizimpanda. Kasi hapa ni mbaya kabisa, hazieleweki kama zilijengwa au zilishasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu nililisemea hili lakini sikupata majibu. Naomba kufahamu hasa ni kitu gani kinaendelea. Tumekuwa tunatenga fedha kidogo, mwaka jana tumetenga shilingi bilioni sita kwa barabara hizi mbili, bilioni sita, sita. Mwaka huu nimeona zimeongezeka kidogo, zimekuwa shilingi bilioni 8.8, sidhani kama pia ni kiasi cha kutosha kwa sababu barabara hizi ni zaidi ya shilingi bilioni 75 kwa kila barabara. Kwa hiyo, nadhani tutafute changamoto zinazopelekea kusuasua kwa mradi huu. Wananchi wana hamu ya kuona barabara hizi zinakamilika kwa vile ni za muda mrefu. Sasa hivi tunaelekea kwenye mwaka wa mwisho wa kumaliza mradi lakini hazijafikia hata 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa barabara hii, kuna jambo la fidia. Vijiji vyote kutoka Sumbawanga, Kizi mpaka Kibaoni, wamefidiwa vizuri tu wala hakuna malalamiko isipokuwa kijiji kimoja tu cha Chala na Chala ni jirani na ninapotoka mimi. Kijiji changu jirani ni Kasu, tumefidiwa vizuri, Chala imekuwa ni gumzo, hapa Bungeni imesemwa mara mbili na leo ni mara ya tatu. Kwenye Bodi ya Barabara tumekubaliana kimsingi kwamba kwa kweli jambo hili halieleweki kwa nini wasifidiwe. *RCC* pia tuna msimamo wa pamoja kwa sababu ni jambo linalowezekana, ni kama tumewatenga hawa Watanzania. Vijiji vyote zaidi ya ishirini vimefidiwa lakini hapa Chala kuna nini? Mwisho wananchi wanasema labda viongozi wetu hamna uwezo wa kutusemea au Serikali inachuki na sisi, hata haieleweki hasa sababu ni nini. Naiomba Wizara inisikie kwa makini, iwapunguzie umaskini wananchi hawa, iwafidie na kama haiwezekani itakuwa ni jambo la ajabu kwa sababu mmewatenda wananchi walewale namna hii na hawa unataka uwatende tofauti, hizi sababu haziwezi kutosheleza, sidhani kama tutaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema pia kama sababu za kuwalipa hazitoshelezi mnavyoona nyinyi basi muhamishe barabara ipite nje ya mji wa Chala. Hiyo ndiyo itakuwa nafuu kwetu na kwa uongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Haiwezekani kijiji kimoja, cha pili, cha tatu vimelipwa vizuri

tena bila kujali lakini hawa tu ukasubiri na baadaye ukasema huwezi kuwalipa, ni jambo la ajabu sana. Ninaomba sana Serikali iliangalie kuwatenga wananchi wale ni jambo baya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika ujenzi wa barabara kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika mtandao wa Mkoa wa Rukwa, ninaomba tunapofikiria lami tuangalie kutoka Namanyere kwenda Kirando. Kirando ni mpakani na tuna bandari yetu nzuri ya Kipili, itatusaidia kufanya biashara, ndiyo namna nzuri ya kutufungua sisi. Vilevile kutoka Matai kwenda Kasesha iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hakuna mpango wowote unaoendelea sasa hivi. Kwa hiyo, tunaomba mtufungue hapo mtakuwa mmetusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la barabara, *RCC*, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa tumekuwa tukizungumza juu ya kupandisha hadhi ya barabara mbili zilizoko Wilaya ya Nkasi, barabara ya Kana – Kala, kilomita 67 na Barabara ya Kitosi - Wampembe. Barabara hizi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini zimekuwa na changamoto kubwa ambayo Halmashauri haiiwezi. Daima tumekuwa tukisema kuwa zikipandishwa hadhi ndiyo sasa zinaweza zikashughulikiwa kwa vile zinaenda maeneo muhimu kiuchumi na kiusalama na kuna changamoto nyingi sana kule. Viongozi wengi wanakubali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu umekuwa kwetu muda mrefu unazifahamu vizuri, tumezipitisha kwenye Bodi ya Barabara muda mrefu, Kamati ya Kitaifa imekuja ikazipitisha, Dkt. Wanyancha alikuja, Mheshimiwa Mwanri amekuja, wote wameona changamoto za barabara hii kwamba Halmashauri haiwezi kuzimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilishawahi kumwandikia Waziri barua na nimewahi kuzisemea hapa, ninaomba zifikiriwe. Zinaenda mwambao mwa Ziwa Tanganyika, zinaenda mpakani, kunatokea ujambazi mwingi, hakuna mawasiliano ya simu, kuna vifo vingi vya akina mama, kuna wafadhili wengi mfano *JIPYGHON* na *AFRICARE*

wanajenga Kituo cha Afya cha Wampembe. Wanauliza watapitisha wapi vifaa vyao na mwezi wa saba wanatoa gari. Hakuna gari la kusaidia akina mama na watoto, wapi watapita hakuna barabara? Mwisho wanasema Mbunge lisemee hili, gari letu litaharibika na adhma yetu ya kupunguza vifo vya akina mama na watoto katika Mwambao mzima wa Ziwa Tanganyika, itakuwa ni kazi bure kama barabara haiwezi kupitika. Naiomba sana Wizara wafikirie jambo hili kwa vile litatusaidia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwa Wizara, suala la barabara vijijini, ni la msingi sana. Barabara hizi za kuunganisha Mikoa tumepiga hatua kama tunavyowasifu lakini muanze kufikiria ni mpango gani utakaotuwezesha kuboresha barabara hizi za vijijini ambazo ziko kwa wazalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tuwe na mpango wa kuwa na *Rurul Road Agency*, Wakala wa Barabara Vijijini, hili jambo nililisema hata hotuba ya Waziri Mkuu ya mwaka jana. Wakala yule apewe shughuli za kuhangaikahangaika na barabara za vijijini kwa sababu inavyoonekana Halmashauri ina hela ndogo tu. Tulikuwa tunapiga hesabu na Mhandisi wangu wa Wilaya ya Nkasi, anapata chini ya shilingi laki tisa, ukigawanya kwa kilomita kwa barabara zake alizonazo pale, huwezi ukaleta mabadiliko katika hali ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile siyo namna nzuri ya kutumia wataalamu hawa, wanakuwa *under utilized,* hawatumiki sawasawa. Tuje na mpango ambao utawezesha barabara kwenda kwa wazalishaji. Barabara mfano ya kutoka Nkhundi kwenda Kate, kwenda Isale mpaka Namanyele. Barabara ya kutoka Kasu, Katani, Chonga mpaka Miyula, zikiboreshwa hizi maana yake ni uzalishaji mzuri sana, tunategemea kupata mavuno mazuri. Wananchi wa Rukwa shida yao ni kuwaunganisha na barabara, wala hatuwasumbui kwa chakula, hatuwasumbui sana kwa ajira, sanasana vijana wasomi hawa ambao wanataka kazi za kisasa lakini vijana ambao wanajishughulisha na kazi za

kilimo walishatambua, tunachotaka kufanya ni kuwaunganisha kwa barabara, kuwaunganisha kwa miundombinu ya masoko, waunganishwe kwa mawasiliano, utakuwa umewaweza. Mkoa wa Rukwa hauhitaji mambo mengi, tunahitaji uboreshaji wa barabara Mheshimiwa Waziri utakuwa umetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tufungue Mkoa vizuri, ili utufungue vizuri barabara zetu za kuelekea Mpanda, za kuelekea Tabora, za kuelekea Uvinza nazo hizi zifunguke, tumezisema mara nyingi lakini hazijaweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mipata. Sasa ni Mheshimiwa John Mnyika atafuatiwa na Mheshimiwa Cyril Chami. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niungane na Kambi Rasmi ya Upinzani kutaka ufafanuzi kuhusiana na hatua ambazo Wizara ya Ujenzi imechukua juu ya kuanguka kwa jengo katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo kwa sababu taratibu za ukandarasi wa pale pamoja na kituo kiko chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na mimi kama Mjumbe kule nimeshataka hatua vilevile, lakini Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* na Wakala wa Barabara kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu wana wajibu wa kuhakikisha ubora na ufanisi. Kwa hiyo, kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imetaka majibu na mimi niungane kutaka majibu kwenye hilo na kwenye kuanguka kwa jengo la ghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Kambi Rasmi ya Upinzani imetaka ufafanuzi juu ya Kasma ile ya shilingi bilioni 252 ya miradi maalum ambayo kwenye Mkutano wa Bunge mwaka jana tulihoji sana. Pamoja na majibu kutokana na maswali yaliyoulizwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, mimi

ningependa kupata maelezo vilevile kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwa nini Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa pamoja mliamua kutoa taarifa zisizokuwa za kweli kwa Bunge kuhusu mradi ule. Kwa sababu Kifungu kile ni cha shilingi bilioni 252 kililenga kujenga matumani hewa kwa Wabunge kuwa kuna pesa za miradi mipya shilingi bilioni 252 wakati Serikali ikijua wazi kabisa kuwa imeweka kifungu kwa ajili ya kulipa madeni kwa miradi ya zamani. Sasa kwa sababu ilikuwa ni kwa ajili ya kulipa madeni ya miradi ya zamani, tuelezwe na siyo kwa maelezo ya juujuu tu, ni nini kilitokea kwa pesa zilizokuwa zimetengwa awali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya kuilipa ile miradi mpaka pesa shilingi bilioni 252 ziingizwe kwenye bajeti mpya kama vile ni miradi mipya. Katika hili ningependa kupata ufafanuzi wa Wizara na vilevile maelezo ya kwa nini Serikali iliamua kutoa maelezo ya uongo Bungeni na kwenda kutoa maelezo tofauti kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kupata ufafanuzi kwa Serikali, ninashukuru kuwa mwaka huu tofauti na mwaka jana kwenye ile Kasma ya kupunguza foleni kwa Dar es Salaam pesa zimeongezwa kidogo. Mwaka jana jambo hili la kutenga pesa kidogo kwenye miradi ya kupunguza foleni, ilisababisha nikatolewa Bungeni humu wakati ninachangia hotuba ya bajeti. Nilikuwa ninazungumzia udhaifu wa namna tunavyoandaa bajeti yetu. Sasa safari hii kumeongezwa kiwango kidogo cha fedha, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, zimepanda kutoka shilingi bilioni 10.5 mpaka shilingi bilioni 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kupanda huko bado kiwango ambacho kimepangwa hakijaenda kutimiza lengo la Mpango wa Taifa wa maendeleo ambao kwanza ulipita kwenye Baraza la Mawaziri ambalo Rais ni Mwenyekiti wake, ulipita kwenye Tume ya Mipango ambayo Rais ni Mwenyekiti wake, lakini ulifika vilevile hapa Bungeni, ukaidhinishwa na Bunge. Ukurasa wa 131 wa Mpango wa Maendeleo kwenye Kifungu hiki cha barabara za pembezoni mwa Dar es Salaam kulipaswa kutengwa kwa mwaka wa

fedha wa kwanza jumla ya shilingi bilioni 68.6. Nilipotaka ufafanuzi mwaka 2011, Mheshimiwa Waziri na Serikali mlinijibu kwamba ni kipindi cha mpito pesa zitaongezwa mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka unaofuata ambao ulikuwa ni mwaka jana badala ya kutegwa kile kiporo cha shilingi bilioni 68.6 kukatengwa shilingi bilioni 10.5 peke yake. Mwaka jana ambapo zilitengwa shilingi bilioni 10.5 kulipaswa kutengwa jumla ya shilingi bilioni 31.5. Sasa Mheshimiwa Waziri ningependa bado kupata ufafanuzi, hizi barabara kwanza ni sehemu ya mpango wa Taifa wa Mendeleo na ndani ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo hazikuwekwa kwamba zitatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, ziliwekwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili 2011/2012, 2012/ 2013. Ningependa kupata ufafanuzi, ni kwa nini Wizara ya Ujenzi na ni kwa nini vilevile Ofisi ya Rais, kila mnapokaa kutengeneza bajeti kwenye hiki kifungu cha barabara za pembezoni, hamtekelezi Mpango ambao mmeupitisha na umepitishwa na Bunge, umeridhiwa na Serikali. Kama Serikali haitekelezi Mpango uliopitishwa na Baraza la Mawaziri na Tume ya Mipango, uliopitishwa na Bunge, hivi ni kwa vipi tutaamini kuwa itatekeleza maneno ambayo Wabunge tunayasema kama ambayo yamepitishwa na Bunge hayatekelezwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba nyongeza hiyo ya shilingi bilioni 28.6 inakwenda kusaidia baadhi ya barabara. Nilikuwa ninapitia Gazeti la jana la *Daily News,* tangazo la Serikali la tenda ya ujenzi wa baadhi ya hizi barabara kuanza. Napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hii tenda ilitangazwa kwa mara ya kwanza kuwa ingefunguliwa tarehe 22/5, ndiyo ilikuwa mwisho wa kuwasilisha maombi na kufunguliwa lakini ghafla jana Serikali imetoa tangazo la kusogeza mbele hii zabuni mpaka tarehe 5/6. Napenda kupata maelekezo kutoka kwa Serikali sababu za kusogeza mbele hizi zabuni, kwa sababu wananchi wa Dar es Salaam wana historia huko nyuma, kuna wakati tangazo lilitoka la zabuni za barabara kama hizi halafu likapotelea hapo katikati. Sasa kama tangazo limetoka

na muda unaahirishwa, ni kwa vipi wananchi waamini kuwa safari hii hakutakuwa na kuuziwa mbuzi kwenye gunia?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaelewa kuwa barabara zilizotangazwa ni pamoja na barabara ya kutoka *Wazo Hill,* Goba, Mbezi, *Morogoro Road,* barabara ya kutoka Tanki Bovu mpaka Goba Samaki Wabichi, Kimara Baruti, Msewe, barabara ya Kilungule, *External*, Mandela, barabara ya Malamba Mawili, Kifuru, Kinyerezi na barabara ya Tabata Dampo. Hizi barabara zimetangazwa, tatizo langu Mheshimiwa Waziri ni kiwango cha Kilomita. Kama barabara kubwa ya Kilomita 20 ya kutoka Goba ambayo ingesaidia sana kupunguza foleni, inatangazwa kuanza matengenezo kwa kilomita saba peke yake. Tafsiri yake kama kasi ni hii, itahitajika miaka mitatu au minne kwa barabara hii kuweza kukamilika. Hali hii iko vilevile kwa barabara ya muhimu sana ambayo ingepunguza foleni ya kutoka Malamba Mawili, Mbezi, Kinyerezi mapaka Kifuru. Barabara ya kilomita 14, tangazo la sasa ni kilomita nne peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipate ufafanuzi wa Wizara kwa maana ya ahadi za Rais, kwa maana ya mipango ya Serikali, ni lini Serikali itaamua kufumba macho, Dar es Salaam kuna magari yamesajiliwa takribani milioni moja, hizi pesa zinazozungumzwa hapa za mapato ya ushuru wa barabara kwa sehemu kubwa zinatoka kwenye magari ya Dar es Salaam. Ni lini Serikali itaamua kufumba macho imalize hili tatizo la msongamano ambalo kila kukicha inalisababishia hasara Taifa, shilingi bilioni nne kila siku kwa mwezi ni shilingi bilioni 120, kwa mwaka ni shilingi bilioni 1440. Maana yake ni nini? Tukiamua kufumba macho, tukaingiza kiwango hiki cha pesa tutaweza kwa kweli kuokoa nchi yetu na hasara kubwa. Siyo hasara tu ya fedha, wananchi wa Dar es Salaam, jana nilikuwa ninapokea simu, wanatumia muda mwingi kwenye foleni ni kama masaa manne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo foleni tu, hali za barabara zile ni mbaya, mradi wa *DART* ule Mheshimiwa Waziri unaendelea pale. Mwaka 2011 niliwatahadharisha kwamba jamani tufungue hizi barabara za pembeni, tufungue

barabara ya Kilungule, *External* tupate njia ya pembeni, barabara ya Kimara, Baruti, ili tupate njia za pembeni za kupita wakati mradi unaendelea. Napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri, sasa hivi foleni imeongezeka sana barabara ya Morogoro, ni nini kimetokea? Ni kwa nini Desemba foleni haikuwa kali sana kama sasa hivi? Ni kwamba Mkandarasi wa *DART* ameshindwa kusimamiwa vizuri mradi au nini hasa, napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupata majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, mwaka 2011, tuliwashauri kuharakisha matengenezo ya kituo mbadala cha mabasi ya Ubungo pale kwa sababu tuliona tatizo litakuja mbele, ushauri haukusikilizwa wakati ule, mwishowe sasa kuna tatizo pale Ubongo kubwa sana kwenye kituo kile. Sasa Rais alishaelekeza mwezi Septemba, 2012, ujenzi wa kituo mbadala Mbezi lakini mpaka sasa hatua hazijachukuliwa kwa ufanisi, naomba majibu kutoka kwa Serikali, kama hata agizo la Rais halitekelezwi, ni agizo la nani litekelezwe kwenye nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata ufafanuzi vilevile, barabara ya *DART* sasa hivi imegeuka kuwa mabwawa na madimbwi utafikiri ya kufugia samaki. Hivi ni nini kinatokea kwenye ile mitaro kwa kiwango ambacho maji haya yanashindwa kuongozwa kuweza kupata ufumbuzi wa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vilevile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnyika. Katika mchango wa Mheshimiwa Mnyika anauliza kwa nini Desemba foleni ilipungua na sasa hivi imeongezeka, hilo

halihitaji Mheshimiwa Waziri ajibu, hilo ninaweza kukujibu mimi, si wale Wanyamwezi walikwenda kwao! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami atafuatana na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru kwa kupata fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara hii na mimi ninataka niungane na wengine wote waliompongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Kwa hakika Mheshimiwa Waziri ukiona tunalalamika siyo kwamba haufanyi kazi ila mimi ninadhani ni kwa sababu uwezo tuliokupa wa kufanya kazi kubwa uliyonayo ni mdogo. Hakuna mtu yeyote ambaye anasema hufanyi kazi vizuri isipokuwa tunachangia tu kwa sababu kama njaa inauma mtoto atalia tu hata kama mama anajitahidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tulinufaika sana na ushauri wa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti aliposhauri kwamba kumsaidia Mheshimiwa Waziri afanye kazi yake ni lazima tufanye maamuzi magumu ya kutafuta fedha za kumsaidia Mheshimiwa Waziri kufanya kazi. Wote wanaoongea hapa wanasema kazi ni nzuri lakini ukiangalia kilio ni kwa sababu fedha haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nataka niongezee yale maneno mazuri ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa kutoa ushauri mwingine. Nadhani tungewekeza kwenye yale maeneo ambayo tunajua kwamba tukijenga tu barabara tunaongeza mapato mara moja. Eneo mojawapo ambalo nataka nilipendekeze leo ni eneo la barabara zinazoingia Mlima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maneno yalikuja hapa kwamba barabara za Kilimanjaro zinakwenda migombani. Napenda nikanushe suala hilo, zile barabara haziendi migombani, zinaelekea Mlima Kilamanjaro na Mlima Kilimanjaro ni nini? Mlima Kilimanjaro ni mojawapo ya hifadhi 13 muhimu za Tafa letu. Katika hifadhi hizi 13 ambazo

zinamilikiwa na *TANAPA*, Mlima Kilimanjaro unachangia asilimia 38 ya mapato yote ya *TANAPA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba kila shilingi mia moja ya *TANAPA*, shilingi 38 inatoka kwenye hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Hizi shilingi 38 kwa kila shilingi 100 zinaingizwa na barabara mbili tu, barabara ya Marangu na barabara ya Machame.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akijenga barabara ya Kibosho ikakamilika, atafungua Umbwe *gate,* kwa maana hiyo umeongeza fedha nyingi zaidi katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Ukikamilisha barabara ya Uru, ina maana kwamba njia ya Njaru umeifungua, umefungua sasa njia ya nne ya kuingia Mlima Kilimanjaro. Ukikamilisha barabara ya *Old Moshi*, utakuwa umefungua njia ya tano. Ukikamilisha barabara ya Kawawa-Nduoni, utakuwa umekamilisha njia ya sita. Kama utafanya hivyo, mimi sina wasiwasi kwamba baada ya muda mfupi hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ambayo inachangia asilimia 38 ya mapato yote ya *TANAPA* itachangia zaidi ya asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi, kwa nini namwomba Waziri alione kama ni suala la Kitaifa, ni kwa sababu Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro tumekuwa tunaomba Serikali kwa miaka mingi kwamba mapato ya Mlima Kilimanjaro na Halmashauri zile ambazo zinazunguka ule Mlima zipate kiasi chake kidogo lakini majibu ambayo tumejibiwa ni kwamba Mlima Kilimanjaro ni Kimataifa na kwa hiyo mapato yake yote yanaingia kwenye Hazina ya Taifa. Sasa kama Mlima Kilimanjaro mapato yake yote yanaingia kwenye Hazina ya Taifa, ni kwa nini Taifa lisione umuhimu wa kujenga zile barabara ili mapato yaendelee kuongezeka? Kwa sababu zikiongezeka ina maana kwamba Mheshimiwa Waziri utapata fedha nyingi zaidi ambapo utajenga barabara nyingi zaidi, siyo tu Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu barabara zenyewe kwani ni nyingi basi? Ni jumla ya kilomita 92 tu ambazo ukishazikamilisha, umeingiza fedha nyingi pale *KINAPA* na

*TANAPA* imepata fedha nyingi, barabara nyingi zitajengwa na tutakuwa tumechangia katika mawazo mazuri ya Mheshimiwa Chenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu Jimbo langu moja kwa moja. Barabara ya *Old Moshi,* ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nilisikitika kwamba barabara ile imesahauliwa pale Wizarani na Mheshimiwa Waziri nataka niombe, kama Mheshimiwa Rais akishaahidi barabara kwamba itawekwa lami, kama Wizara yako haitachukulia kama agizo, ni nani tena atatekeleza? Mpaka Mbunge aje hapa aombe, akiomba anaambiwa kwamba aandike maombi rasmi, yale maombi yafikiriwe, uchaguzi hauko mbali Mheshimiwa Waziri, baadaye mgombea wa CCM atakwenda palepale *Old Moshi* watamwambia kwamba mgombea mwenzako aliahidi, Chama chako cha Mapinduzi kitapata shida. Kwa hiyo, naomba hizi ahadi za Mheshimiwa Rais siyo tu kwa Moshi, popote pale ambako Mheshimiwa Rais ameahidi barabara zijengwe, naomba barabara zile zijengwe ikiwepo hii ya *Old Moshi* inayoanzia pale Kiboroloni kuelekea Kirarara, Suduni mpaka Kidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri alisaidia sana jana kwa kusema kwamba barabara ikishwekwa lami haipaswi kukarabatiwa kwa kuwekwa kifusi. Barabara ya Rau, Madukani kuelekea Kishumundu ilijengwa miaka ya sabini lakini baada ya kujengwa haikukarabatiwa tena, kila ikiharibika wanaweka kifusi, mpaka jana Mheshimiwa Waziri akadhani kwamba ni kilomita tatu na nusu tu kumbe ni kilomita kumi yote ilikuwa imejengwa kwa kiwango cha lami. Nataka niseme tu kwamba maagizo ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamesikiwa na Watendaji wa Serikali. Kwa hiyo, barabara ile kwa kweli irudishiwe katika kiwango chake, siyo tu barabara hiyo lakini na barabara zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri wa pili wa namna ya kuongeza mapato ya Serikali. Ukiangalia fedha nyingi za kujenga barabara zinatokana na aidha hazina ya Serikali lakini vilevile na *Road Fund* ambayo

inachangiwa kwa kiasi kikubwa na mafuta. Mafuta yanatozwa kodi na fedha ile inatumika katika ujenzi wa barabara lakini *Road Fund* hii kwa wale Wachumi, ukiwauliza watakuambia kwamba ni aina ya kodi ambayo siyo *progressive*. Siyo kodi ambayo inamtoza yule anayetumia kwa jinsi anavyotumia, ni kodi ambayo inampa adhabu mtu mwingine ambaye hatumii, kiuchumi inaitwa *Regressive Tax System*, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu unakuta mtu anayesafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma kwa mfano au mpakani Tunduma pale, analipa sawasawa na mkulima wa miwa ambaye ananunua mafuta, anaweka kwenye trekta, trekta haipiti barabarani, iko shambani inalima. Kwa sababu kodi ya mafuta ni ileile, unakuta huyu mkulima analipa sawasawa na yule mtu ambaye ananufaika na usafirishaji wa mafuta kutoka Dar es Salaam mpaka mpakani au wa mizigo. Kwa hiyo, hiyo inakuwa inamwonea huyo mkulima ambaye mara nyingi ni Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili kwa sababu barabara zetu zinatumiwa na wageni na Watanzania vilevile, ina maana kwamba kwa sababu Watanzania wote tunalipa kodi kwa ajili ya kujenga barabara hizi, Serikali yetu inakopa au tunaomba kwa wafadhili kujenga barabara hizi, sasa inakuwaje wageni wanatozwa sawasawa na sisi tunaposafirisha mizigo katika barabara hizihizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba utafutwe utaratibu wa kuhakikisha kwamba yeyote anayenunua mafuta analipa kodi, lakini yule anayenufaika zaidi na barabara ikiwemo Mtanzania anayefanya biashara ya kupeleka mizigo mpaka mpakani au wageni ambao wanatumia barabara zetu lakini hawalipi kodi, wanatozwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ule utaratibu wa *Road Toll,* naomba urudishwe. Ilishasemwa hapa Bungeni kwamba utaratibu ule unaleta *corruption*, unafanya rushwa inakuwa kubwa, ule utaratibu siyo mzuri kwa sababu hatuna uhakika

kwamba unaweza kukusanya fedha lakini udhaifu katika kutoza kodi usifanye kitu kizuri kiwekwe pembeni. Mimi naamini kwa uwezo wa Mheshimiwa Waziri, akishirikiana na Mheshimiwa Waziri mwenzake wa Fedha, tunaweza kabisa wa kuhakikisha kwamba wanaotumia barabara wanalipa zaidi kuliko wale ambao hawatumii barabara zaidi, namna hii tutaweza kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili siyo kwa Tanzania tu, nchi nyingi ambazo zimeendelea na ambazo zina fedha nyingi, zina *system* hiyo. Sisi ni nchi maskini lakini tunaacha barabara zetu zinatumiwa na wenzetu, majirani zetu bila kuwawekea kiwango cha ziada cha kulipa kodi. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba tuweke utaratibu huo, ni utaratibu mzuri tu ambao unaongeleka hata katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unaongeleka vizuri tu. Wenzetu katika Afrika Mashariki hawatapenda kwa sababu nchi zao ni ndogo, lakini sisi nchi yetu ni kubwa kwa hiyo ni lazima tujenge hoja katika Afrika Mashariki na katika *SADC* ili kuhakikisha kwamba tunaweka utaratibu ambao wanaotumia barabara zetu wanalipa zaidi na namna hiyo peke yake itasaidia kuhakikisha kwamba tuna-*maintain* barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo, namtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema na ninamwomba sana asisahau barabara za Kilimanjaro, akizijenga vizuri mapato ya Kilimanjaro yataongezeka, *TANAPA* itapata fedha nyingi zaidi, Hazina itapata fedha nyingi zaidi na atajenga barabara kwa wepesi zaidi kwa fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami. Baada ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda tutaenda *NCCR* sasa, Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Mkosamali. Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza kama wenzangu waliotangulia Waziri na Watumishi wa Wizara yake na wadau wengine katika sekta ya barabara kwa kutatua changamoto ya msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wametueleza na wengi tunaona jitihada za dhati kabisa na mikakati ambayo inaelekea tatizo hili muda si mrefu tatizo hili litakuwa limepata ufumbuzi. Pamoja na jitihada hizi, bado naishauri Serikali na ninaiomba iongeze jitihada za zaidi ili haya waliyopanga yakamilike katika muda mfupi kwa sababu yanaathari kubwa sana za kiuchumi na kijamii katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati wanaweka jitahada hizi na mikakati hii, nilikuwa na angalizo nafikiri pengine na wao wanaliona kwamba sasa watapunguza msongamano wa magari kuanzia Ubungo, Kimara au maeneo ya Gongo la Mboto kuelekea Dar es Salaam lakini bado huduma nyingi katika Jiji letu zinatolewa katikati ya Jiji. Kwa hiyo, baada ya miaka miwili kutakuwa na msongamano mkubwa sana katikati ya Jiji. Inatakiwa Serikali sasa ijitayarishe kwa kuboresha huduma hizi za biashara na kijamii ili zitolewe nje ya Jiji. Hii ni pamoja na kutengeneza Miji midogo nje ya Jiji lile, Miji midogo hii itoe huduma zile ambazo wananchi wanakwenda kuzifuata kule katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Huduma hizi ni kama za kibiashara, huduma za Serikali, kama hii itafanyika inaweza ikasaidia kutatua hili tatizo la msongamano wa magari katika Jiji letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine ni kwamba utaratibu mwingine uanze kutayarishwa sasa hivi wa *congestion charges,* kwamba kuwekwe tozo ya magari yanayoingia mijini, hii itapunguza magari ambayo hayana ulazima wa kuingia kule mjini. Vilevile naishauri Serikali

wapunguze matumizi ya magari ya Serikali. Si lazima Wakurugenzi wote wa Idara waende na magari kuingia katikati ya Jiji ambako ndiko ofisi nyingi za Serikali zipo kule. Kwa hiyo, watumie usafiri wa jumla ili ikapunguza msongamano wa magari kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye Jimbo langu la Ulanga na ninaomba kwa niaba yangu na kwa niaba ya wakazi wa Ulanga na Kilombero, kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuingia mkataba kuanza ujenzi wa daraja la Mto Kilombero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba ule umesainiwa tarehe 24 mwezi Oktoba 2012 na inatakiwa daraja lile ujenzi ukamilike ndani ya miaka miwili na tayari Serikali imeweka shilingi bilioni tatu ndiyo maana Mkandarasi yupo pale. Katika bajeti hii zimetengwa shilingi bilioni 7.5 lakini thamani ya daraja ile mpaka likamilike ni shilingi bilioni 53.2, muda uliobakia ni karibuni mwaka mmoja na nusu. Wananchi wa Ulanga na Kilombero tuna wasiwasi na tunaanza kuikumbusha Serikali kwa sababu kwa *speed* hiyo kuna mambo mawili tuna wasiwasi kama daraja hili litakamilika ndani ya miezi 24 kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni *speed* ya mjenzi. Huyu mjenzi alitakiwa awepo *site* ndani ya mwezi mmoja baada ya kusaini mkataba lakini imemchukua zaidi ya mwezi mmoja na hadi leo zaidi ya miezi sita bado tu anafanya maandalizi ya magodauni na makazi na sasa muda umeliobakia ni robo tatu ya kipindi chake. Jambo la pili kama nilivyoeleza kwamba mpaka sasa hivi shilingi bilioni karibuni 10.5 ndiyo zimepangwa wakati mradi mzima mpaka ukamilike ni shilingi bilioni 53.2, sasa je, kipindi cha mwaka mmoja na nusu kilichobaki, tunaikumbusha Serikali ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani daraja la Kilombero kwa kweli ni ukombozi wa wakazi wa Ulanga na Kilombero. Daraja hili ndilo mhimili wa uchumi, wakulima wengi wanalitegemea sana daraja hili kupitisha mazao na bidhaa

zao. Wilaya ya Ulanga kwa ujumla tupo kwenye kisiwa kwa hiyo tusipowekewa daraja hili adha za kiuchumi na huduma za kijamii zitatuathiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa pili, athari ambayo kama haitamalizwa ndani ya miaka miwili Serikali itakayoipata ni kwamba riba itaongezeka na adhabu kutegemeana na mkataba unavyosema. Kwa hiyo, maana yake badala kukamilika daraja hili kwa shilingi bilioni 53 litagharimu zaidi ya shilingi bilioni hizo kwa hiyo ni hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa wakazi wa Ulanga na Kilombero bado tutaendelea kuathirika sana kiuchumi, kijamii na mtakumbuka hata kiusalama. Mwaka 2000 tulipoteza wenzetu 100 pale kwa ajali ya *MV Kilombero One*. Kama Serikali haitajipanga vizuri zaidi hasa kuwekeza fedha katika awamu hii ya pili ili Mkandarasi huyu atakapoanza kujenga daraja ziwepo. Tunaisisitiza Serikali kwa kipindi kilichobaki wamalize malipo ya zile fedha zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa zaidi ni kisiasa. Daraja lile ni ahadi ya Mheshimiwa Rais mwaka 2005 na ninashukuru Serikali imesikiliza imeanza kujenga daraja lile. Tayari tuliahidi kwamba kabla ya mwaka 2015 wananchi wa Ulanga wataachana kabisa na adha ya kuvuka kwa kutumia vivuko vile. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri hili alikamilishe kwa sababu lina athari ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri tena kwa jitihada zake kwa kuanza upembuzi yakinifu kwa barabara ya Lupilo, Londo, Lumecha mpaka Songea. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu katika mazungumzo yangu mengi katika Bunge hili nazungumzia suala la FAMOGATA kwamba Fanya Mkoa wa Morogoro Gala la Taifa. Kwa hiyo, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ndiyo inapita kwenye ukanda ule wa kuzalisha miwa na mpunga. Vilevile kuna *program* ya *SAGCOT*. Hii programu ya *SAGCOT* kama barabara hii haitaendelezwa haitaweza kutekelezwa kwa ufanisi kwa kiasi kikubwa. Lingine barabara

hii ni kiunganishi kati ya Mkoa wa Ruvuma na Mikoa ya Kaskazini na Mikoa ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba wakati upembuzi yakinifu ukiendelea kufanyika, tunaomba basi zile kilomita zilizobaki kama 20 hivi zitobolewe ili tukutane na wenzetu wa Londo - Lumecha tuanze kuitumia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie la mwisho ni barabara ya Malinyi, *Juction to* Malinyi. Hii barabara ipo chini ya Mkoa na *TANROAD* lakini mara kwa mara inaathirika sana na mafuriko ya mto ambao upo jirani yake, Mto Furuwa. Wananchi wa Wilaya ya Ulanga mwaka huu hasa Tarafa ya Malinyi, tumejitahidi kuweka angalau tuta dogo kuzuia mafuriko ya Mto Furuwa lakini jitihada hizi tunaomba ziungwe mkono na Serikali kwa sababu Halmashauri peke yake uwezo mdogo na wananchi peke yao uwezo ni mdogo. Kwa hiyo, kama tuta hili likiwekwa pale litatusaidia kuondoa tatizo la mafuriko katika Mji mdogo wa Malinyi lakini vilevile litaifanya barabara hii ambayo inatumia hela za Serikali, hela za wavuja jasho iwe ya kudumu maana mara kwa mara inatengenezwa baada ya miezi mitatu inaathirika na mafuriko. Kwa hiyo, tukipata tuta katika Mto Furuwa litaweza kutoa jibu la athari ambazo tunapata mara kwa mara ya barabara hii ambayo inakarabatiwa ndani ya miezi mitatu inaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kama wenzangu wengi walivyojadili, tumeridhia, tumeridhika na utendaji wa Wizara hii, kwa hiyo, mimi mwenyewe binafsi naungana mkono na Wabunge wenzangu waliokubali kupitisha bajeti na ninaomba wale ambao wamebaki, tukubaliane tupitishe bajeti hii, tuwape hizi hela. Hili kundi kweli limekamilika, kundi la wafanyakazi, tuna hakika wataweza kutimiza ahadi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda. Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Mkosamali dakika tano tano. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa mara ya pili napenda kumshukuru Waziri wa Ujenzi, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kukubali walau kuiona ile barabara ya Kidahwe, Kasulu, Kibondo, Nyakanazi kuitengea fedha kiasi cha shilingi bilioni kumi ili kusudi walau iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa kwa taarifa ambazo pengine zipo sasa kwamba wameshatangaza kandarasi, ni imani yangu ujenzi wa barabara ile kuanzia Kidawe, Kasulu, Kibondo na Nyakanazi utaanza kama dhamira ya Serikali ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi ni moja tu pengine na angalizo ambalo ningependa Wizara ya Ujenzi waweze kuangalia. Ile rekodi ambayo ilijengeka kuanzia mwaka wa fedha wa 2010/2011, hali kadhalika mwaka 2011/2012 kutenga fedha halafu fedha hazitolewi, naomba kwa kweli Wizara mhakikishe kwamba hizi fedha ambazo mmetenga ziende kwa wakati na tuone sasa Mkandarasi yuko *site* akifanya kazi. Ni imani yangu kwamba fedha hizi ambazo zimetengwa mwaka huu na zile fedha za mwaka jana kiasi cha shilingi bilioni tatu na milioni mia tano, hazitakuwa changa la macho. Ni imani yangu kwamba utekelezaji wake utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawashukuru kwa hilo na niseme kwamba wakazi wa Mkoa wa Kigoma ambao wamekuwa wanalilia sana barabara hii, watafarajika walau kwa kuona fedha zimeanza kutengwa kwa kiwango kikubwa. Mwakani pia muangalie ili kusudi sasa pengine tuweze kuharakisha ujenzi wake

ukamilike mapema inavyowezekana. Barabara hii itakuwa ni ukombozi kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma lakini pia hata kwa Mikoa ambayo ni jirani zetu, jirani zetu wa Mikoa ya Kagera, hali kadhalika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na ni barabara ambayo tumekuwa tunatumia hata sisi Waheshimiwa Wabunge tunapokuwa tunakuja kwenye shughuli zetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimshukuru Mheshimiwa Magufuli. Sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza kuhusiana na hoja hii, japo usiseme hizi ni fedha za CCM, ni fedha za Watanzania wote, sote tunalipa kodi. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na nampigia saluti kwa sababu ameonyesha kutukumbuka watu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia *TEMESA. TEMESA* wakati mwingine hawafanyi kazi yao vizuri. Kwa mfano Chuo cha Ualimu Kabanga pale walikuwa wanataka waingiziwe umeme wa *TANESCO* ambao Wilaya ya Kasulu tuliupata majuzi. Sasa ukiangalia zile *costs* walizokwenda kufanya tathmini, kwanza walikuwa wana umeme, tayari walisha-*install system* nzima imekuwa inafanya kazi na wamekuwa na umeme ambao walikuwa wanapewa na Mzungu mmoja Brother Tell, hawa Wakatoliki walikuwa wanawapatia umeme pale. Sasa *TEMESA* wamewaambia kwamba inatakiwa wawe takriban zaidi ya shilingi milioni 100 ili kusudi waweze kuingiziwa umeme. Sasa unajiuliza hii *system* ambayo ipo na wamekuwa wanaitumia siku nyingi, hivi imeharibika kwa kiwango hicho kiasi kwamba hawawezi wakaingiziwa umeme ili wanachuo ambao wanasoma pale, ni Chuo cha Ualimu cha Serikali, ili kusudi waweze kuondokana na adha ya kukosa umeme, tatizo ambalo linawakabili hivi sasa. Kwa hiyo, ninakuwa na mashaka

wakati mwingine na *feasibility study* ambayo imekuwa inafanywa na *TEMESA*. Imani yangu katika hili, Mheshimiwa Magufuli ataweza kutupatia majibu, ni kwa nini wanatupa viwango hivyo, kwa sababu wote tunajenga nyumba, ukijenga nyumba sidhani kwamba huwa tunafikia viwango vya namna hiyo, kwa nini kwenye fedha za Serikali, gharama zinakuwa kubwa? Naomba hili tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni magari ya Serikali. Nampongeza Waziri wakati fulani aliweza kutangaza *operation* ya kukamata magari ambayo yana usajili wa namba za Serikali, kwa mfano STK na kadhalika. Lipo gari moja ambalo ni la Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, lina namba ya STK bila shaka litakuwa kwenye Wizara yako. Gari lile lilinunuliwa halikumaliza hata miezi miwili. Likagonga pikipiki, wakalipeleka Mwanza kutengenezwa kule lakini kumekuwa na hulka na silka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wanapeleka magari bila kupata kibali cha *TEMESA* kutoka Kigoma, wanakimbilia Mwanza. Sasa inaonekana kama vile *TEMESA* Mwanza ni kama genge la watu kupitishia mambo yao. Naomba ucheki hiyo Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wapinzani tunapongeza kama Mheshimiwa Machali alivyosema leo na wengine kwa Mawaziri ambao wanafanya kazi. Mtu anayefanya kazi sisi tunampongeza na wale ambao wanakaakaa tu,

wanashangaashangaa sisi hatuwapongezi. Waziri wa Ujenzi na baadhi ya Mawaziri wengine, wachache, *they are doing very nice job,* kazi nzuri sana. Tunaomba na wale ambao hawafanyi hivyo wawaige. Wanafanya kazi nzuri, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niulize machache. Mwaka jana barabara ya Kibondo, Mabamba kwenda mpaka wa Burundi ilitengewa fedha *feasibility study* shilingi milioni 144. Naomba kufahamu, fedha zile zimefanya kazi gani mpaka sasa hivi? Kwa sababu ile ni kiu ya kuunganisha Tanzania na nchi ya Burundi ukizingatia wao kule pia wameishapitisha bajeti ya kuunganisha Burundi kupitia Kibondo. Kwa hiyo, naomba kujua *feasibility study* ile imefikia wapi na ujenzi wa barabara ile ya Kibondo, Mabamba hadi mpaka wa Burundi ambao ni kilometa chache tu kama 30, umefikia wapi na itatengewa fedha lini sasa za kuanza kujengwa kwa sababu *feasibility study* tayari fedha zilishajengwa mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda pia kuchangia kuhusu hii barabara ya Nyakanazi – Kigoma. Wakati Mheshimiwa Rais amefanya ziara Mkoa wa Kigoma, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba lazima barabara ianzie Kidahwe. Nataka tu kuifahamisha Wizara kwamba hakuna Mbunge anayewasemea Wabunge wengine wa Kigoma. Kila Mbunge wa Kigoma anawakilisha Jimbo lake na hatujawahi kukubaliana hata siku moja kwamba barabara ile inaanzia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuifahamisha Wizara kwamba hakuna kikao chochote cha Wabunge wa Kigoma ambacho kilikubaliana kwamba barabara ianzie Kidahwe au ianzie Nyakanazi, yalikuwa tu ni maoni ya Mbunge huyo aliyezungumza kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais. Sisi Wabunge wa Kibondo na Kakonko Mheshimiwa Chiza, barabara hii ilipangwa na Serikali kuanzia Nyakanazi watu wa Kigoma barabara kule zilishaanza lakini kuanza kuchakachua chakachua mambo, huo ni ubinafsi wa namna fulani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiambie tu Wizara kwamba hakuna kikao, yalikuwa tu ni maoni ya mtu wala hata Mheshimiwa Rais asije akadanganyika mwisho wake akifika Kibondo pale watu wakamwambia eeeh vipi bwana mbona unageukageuka ahadi uliyoahidi. Kwa hiyo, yalikuwa tu ni maoni ya mtu, hakuna Msemaji wa Mkoa wa Kigoma, kila Mbunge anajiamini hapa, anaweza kuchangia Jimbo lake *very nice,* vizuri sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia kuhusu Kigoma, jambo la mwisho nakumbushia ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo imo kwenye kitabu chake kwa sababu ahadi ni deni. Kwenye kitabu cha barabara za Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya Kibondo Mjini kilometa mbili. Naomba mjitahidi mjenge zile barabara. Nimeuliza swali hapa, Naibu waziri wa Ujenzi akaniambia niende kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ambayo inakusanya mapato yake ya jumla ya shilingi bilioni moja, itaweza kweli kujenga barabara hizi alizoahidi Mheshimiwa Rais pale Kibondo? Tunaomba mjitahidi, Wizara hii tunajua nyie ni wachapakazi, mnafanya kazi nzuri, tunaomba mjitahidi muendelee kujenga barabara. Watu wa Kibondo wana kiu hawajawahi kuona barabara ya lami kama alivyoeleza Mheshimiwa Buyogera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekuwa wanatuona sisi Wabunge wao tunapambana kila mwaka. Mwaka jana nilikuwa *so hash,* nilikuwa *so radical* kuhusu barabara hii. Kwa hiyo, naomba hizi fedha ambazo zimetengwa shilingi bilioni 10 kwa kweli zianze ujenzi na hakuna msimamo kama nilivyosema wa barabara kuanzia wapi. Naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Huyo ni Mheshimiwa Felix Mkosamali, alikuwa anaweka msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mhandisi Athumani Mfutakamba, akimaliza tutaelekea *CUF* sasa, Mheshimiwa Moza na Mheshimiwa Rajab. Mheshimiwa Mfutakamba!

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niendelee palepale alipomalizia Mheshimiwa Mkosamali kwamba naunga mkono hoja hii asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Lwenge pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wake kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nitoe rambirambi kidogo kwa Jimbo la Igalula tulipata ajali pale, kijana mmoja wa timu ya mpira amefariki, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi, Bwana Juma Omari Ramadhani lakini pia Abdallah Famba anatibiwa Muhimbili. Nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Profesa Mcharo pamoja na Dkt. Njelekela wanaendelea kumtibu vizuri ameumia uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwenye mada, barabara ya Chaye-Nyahua. Mheshimiwa kwa Jimbo la Igalula hizi kilometa 90, niishukuru sana Wizara katika kilomita 700 kutoka Kigoma mpaka Manyoni, hili ni eneo ambalo halikuwa na lami lakini nimshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika ziara yake ya Kuwait nimeona Amir Alsabaha anasema hii barabara itapata fedha za *Kuwait Fund*, kwa hiyo, naomba zije haraka zile fedha ili hizi shilingi bilioni 2.2 zilizotengwa kwa ajili ya Chaya-Nyahua barabara iweze kujengwa mapema iwezekanavyo ili wananchi wote wa Kata 10 za Igalula wafaidike. Barabara hii ni kama mshipa mkubwa, hizi nyingine ni mishipa midogomidogo kutoka kwenye Kata zote 10 na barabara ya lami hii inahitajika sana kuunganisha Dar es Salaam mpaka Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la barabara nyingine zinazokuja Mkoa wa Tabora, najua Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameziongelea lakini nilitaka kusisitiza tu kwamba tunavyochelewa kukamilisha

hizi barabara na hususan barabara ya Chanya - Nyahua ambayo ingeweza kupunguza kilomita 200 za usafiri kwenda Kigoma, kwenda DRC Congo, kwenda Rwanda na Burundi, kuna kilomita 200 tutaokoa kwa magari kama tutapita hii barabara ya Chanya – Nyahua, lita karibu 400 za mafuta zitaokolewa na muda wa masaa manne kwa usafiri kuokolewa. Kwa hiyo, hiki kiungo cha kilomita 90 ni muhimu sana lakini wakandarasi wote wa barabara zote zinazoingia Mkoa wa Tabora kila tunapochelewesha kuwalipa, kuna shilingi milioni 154 kwa mwezi ambayo ni riba ambayo ni lazima tuwalipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini ninashauri, baada ya kuliiona tatizo hilo ngoja niende haraka haraka. Ziko njia mbalimbali ambazo Wizara ya Ujenzi inaweza kushirikiana na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Gavana wa Benki Kuu ili kutafuta hii mikopo ambayo itakuwa na riba nafuu badala ya kuendelea kuwalipa riba kubwa wakandarasi. Kuna niongee tu lugha ya Kinyamwezi, kuna *sovereign bonds,* kuna *municipal bonds*, kuna *debenture*, kuna *infrastructure bonds,* kuna *Euro bonds,* kuna *Hedge Funds,* kuna *structured finance*, kuna *syndication,* kuna *financial engineering* haya mambo kidogo ni ya Kinyamwezi Nyamwezi, lakini wakiyafanyia kazi wataalam wa fedha katika hizi Wizara mbili mikopo inaweza kupatikana, barabara hizi zikamilike haraka kwa mikopo na hii itatusaidia sana kuanza kupata faida kubwa kwa sababu magari yatakuwa yanapita kwenye barabara za lami na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ninaamini kabisa itatekelezeka ifikapo mwaka 2015 kwa lami katika kila sehemu. Naipongeza sana Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko barabara hizi, lakini tusisahau pia barabara ya Tabora, Ipole, Sikonge, Koga mpaka Mpanda. Hii barabara ni muhimu sana kiuchumi. Kuna usafirishaji wa mahindi, mpunga, asali, mbao na pia wananchi ambao mtandao wa reli hauwafikii, wanaitumia sana barabara hii, nayo pia iwekwe lami haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee suala la Kitaifa, mradi wa *DARTs*, Dar es Salaam, msongamano wa magari katika Majiji yetu kwa ujumla. Huu mradi wa mabasi ni muhimu sana tukajifunza uzoefu wa maeneo mbalimbali, maathalan Kuala Lumpur, Bogota, Singapore, San Francisco, Pretoria, je, iko nafasi ya ujenzi wa reli kati ya hii *DART* maana yake *design* ile sina uhakika kama ina-*incooperate* reli nyepesi, *light rail.* Hili nalo ni muhimu, naomba litazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia apatikane Mshauri Mwelekezi mzuri (*transaction advisor)* kwa sababu hii *concession* kama haitazamwi vizuri, iko *risk factor* ambayo inaweza kusababisha ikawa gharama kwetu tukishampata yule mwekezaji. Kwa hiyo, kuna *transaction risk* ambayo ningeomba Wizara itazame kwa kina na kuwa na wataalam watakaotumia uzoefu wa sehemu mbalimbali kuweza kufanya huu mradi ukawa na manufaa kwa Dar es Salaam na kwa Taifa kwa ujumla badala ya kuwa wa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua ni utaratibu wa *PPP* lakini nivuke sasa kwenye suala la barabara ya kulipia *Toll Road* kutoka Dar es Salaam-Mlandizi-Chalinze kutoka *lane* sita kwenda *lane* nne. Mimi ningeshauri sana Wizara ya Ujenzi ishirikiane na Wizara ya Uchukuzi kwa sababu ya kupiga hesabu ya zile *traffic volumes.* Reli ikishaimarika, bandari inaimarika, baadhi ya mizigo mingi itakwenda kwenye upande wa reli, barabara pia itakuwa inatumika, sasa kama hesabu hazipigwi vizuri kwenye *PPP* tunaweza kujikuta yule mwekezaji anasema bwana hapa kuna upungufu wa *volume,* kwa hiyo, inabidi Serikali ilipe. Naomba tuwe waangalifu katika kumpata pia *transaction advisor* kwenye hizi *Toll Roads. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo la riba, nafikiri nimelizungumza, lakini matatizo katika barabara zetu ni kwamba kila malipo yanapochelewa kuna riba, gharama inaongezeka na kuna madai kucheleweshwa. Pia kuna suala la mkandarasi anaweza kusitisha ujenzi au kupunguza kasi. Kuna kazi zilizokamilika, zinaanza kuharibika na mradi inabidi kurudiwarudiwa tena kwa gharama ya Serikali. Kuna ukosefu

wa fedha kutoka kwa wakati na pia kuchelewa kulipa fidia wananchi katika maeneo yanayojengwa miundombinu hivyo kuna manung'uniko. Pia kama tunachelewa kumlipa mkandarasi, kuna *construction risk, contractors risk* na miradi mingine inaweza kuwa ina gharama kubwa zaidi tunapowaleta wale wakandarasi kushindana katika miradi hii. Kwa hiyo, tujitahidi sana, fedha zipatikane ili miradi hii ikamilike kwa wakati na mimi naunga mkono hoja asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa machache hayo niliyozungumza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Athumani Mfutakamba. Mheshimiwa Moza na Mheshimiwa Rajab dakika tano tano, watafuatiwa na Mheshimiwa Saleh Pamba na Mheshimiwa John Cheyo ajiandae.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Ujenzi. Waswahili wanasema aisifiaye mvua imemnyeshea lakini siwezi kuisifiwa mvua wakati haijaninyeshea wala siwezi kujisifu Kidigo wakati kwetu bado kuna makundi ya fisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumzie kwenye kuporomoka majengo. Niungane na Watanzania wenzangu wote wale waliopoteza ndugu zao niweze kuwapa pole. Suala la kuporomoka majengo, ni suala linaloitia dowa Serikali na Taifa kwa ujumla. Najiuliza maswali, Mheshimiwa Magufuli ukali wako wote umeuweka wapi kwa watu hawa waliohusika katika uporomoshaji wa majengo haya, umepitiwa au unawaogopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba chondechonde, tuondoke kwenye kadhia hii ambayo inajirudia ya majengo kuporomoka. Naomba katika majumuisho yake atueleze ana wakandarasi wangapi ambao wana utaalam uliokithiri au uliokubuhu katika ujenzi wa magorofa na barabara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihame katika suala hilo, nije katika barabara ya Dodoma - Mayamaya. Mheshimiwa Waziri, nataka nikukumbushe kwamba, niliwahi kukueleza kabla bajeti hii haijaja hapa mbele yetu, ndani ya wiki mbili zilizopita, kwamba barabara hii ijengwayo ya Mayamaya – Dodoma, kiwango cha lami kilichoanza kujengwa sio sahihi; tayari kiwango kile kinaonesha dalili asubuhi na mapema sio sahihi, kinayumba na kinaonesha dalili kwamba baadaye itakuja kuwa ni majuto katika utengenezaji wa barabara ile. Nilikuomba kwamba ufuatilie bado mapema na tayari huku pembeni wameanza kufukia michanga kupoteza malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninukuu katika bajeti hii, Wizara hii mwaka 2012/2013, ukurasa wa 44, Waziri alisema kuwa, kipande hiki kingekuwa kimekamilika Oktoba 2012, lakini si hivyo, tatizo ni nini na imefikia wapi mpaka sasa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pamoja na kutengewa kukamilika mapema, bado haijawa hivyo, licha ya mkataba kusainiwa mwaka 2010. Mwaka 2008 katika Bunge hilihili Wabunge, walisusia na walikataa mpaka bajeti hii iweze kuongezwa ili barabara hii iweze kukamilika; nini tatizo Mheshimiwa Waziri? Kama mnataka kuturudishia barabara hii iwe katika Ilani ya Uchaguzi ya kipindi kijacho, naomba muwaeleze wananchi waweze kutambua kabisa; wananchi wa Wilaya ya Kondoa, Dodoma na wananchi wote kwa ujumla wanaopita katika ile barabara wanahitaji kupata lami kwa kuwa, wanalipa pia kodi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atambue kwamba, Wilaya ya Kondoa ina pande nne za barabara ambazo ziko katikati ambazo zote ni barabara kuu. Pamoja na kwamba haziko katika kiwango cha lami lakini ahakikishe kwamba walipa kodi wale wanaondokana na adha kubwa ya barabara na ni wakulima na wafanyabiashara wazuri. Naomba kile kipande kilichobaki pale cha Bonga – Babati, angalau basi muendelee kukimalizia ili sehemu ile iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika ujenzi wa mizani. Ni vyema ukawepo mpangilio mzuri ili kuondoa usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji. Imekuwa ni kero kubwa na ni msongamano katika mizani, hasa barabara itokayo Dar-es-Salaam – Dodoma hadi Mwanza. Ukianzia Dar-es-Salaam hadi Dodoma ziko mizani nne, zilizojengwa ni Kibaha, Mikese, Kihonda na Nala-Dodoma. Ukiangalia kwa umakini mizani nne kwa sehemu ndogo kiasi hiki, inaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara. Kuna tatizo gani mizani zinakuwa nyingi namna hiyo? Angalau basi ingetengenezwa kwa kuleta manufaa badala ya kuleta kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Mheshimiwa Waziri, naomba utuambie kwamba, hizi mizani pamoja na kwamba zina faida na manufaa, lakini sisi tunataka tutambue manufaa ya barabara zetu zinazoharibika, kila sehemu mizani na zinatozwa *fine.* Sasa niambie hizi *fine* mnazotoza katika hizi barabara, mmetengeneza barabara ngapi na wakati bado kuna barabara zinazoleta ajali, barabara hizihizi za kutoka Dar-es-Salaam mpaka Morogoro mpaka hapa Dodoma? Naomba utuambie na mapato yenu mnayokusanya ni kiasi gani yanayoweza kutengeneza barabara hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuongezea suala la ujenzi wa kiwanja cha ndege kilichopo hapa Dodoma. Ni lini basi Mheshimiwa Waziri wangu, kiwanja kile kinaweza kikajengwa na kikawa tayari kimeshakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, mimi sitaunga mkono Hoja hii ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu, mimi nahitaji barabara ya kutoka Dodoma mpaka Arusha kwa sababu ndio barabara kuu ambayo tunaihitaji kwa umuhimu zaidi wananchi wa Kondoa na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Moza na Waheshimiwa Wabunge wengine.

Waheshimiwa Wabunge, katika kuchangia kwenu ni vizuri sana kuifahamu Serikali inavyofanya kazi. Kwa mfano limejirudia sana jambo la maghorofa, kwa asilimia tisini na kitu, jambo la maghorofa halimhusu kabisa, wala haliihusu Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, ni vizuri kujua tu jambo fulani linahusu watu gani vinginevyo tutakuwa tunawaonea watu wengine hapa ambao wala hawahusiki sana na kinachoendelea.

Mheshimiwa Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Saleh pamba na Mheshimiwa John Cheyo ajiandae. Mheshimiwa Rajab?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu muda ulioutumia sasa hivi sijui ni huu wa kwangu ama?

**NAIBU SPIKA:** Hauhusiani Mheshimiwa Rajab. Nikikupa nafasi ndio unaanza na mimi Meza nina muda wangu Mheshimiwa Rajab. Wewe Mwenyekiti wa Kamati bwana, namna gani? *(Kicheko)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka ufafanuzi wa hilo tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kwamba Mheshimiwa Waziri ameshapewa sifa nyingi hata hivyo na mimi ninataka nimpongeze. Nianzie katika suala la Mfuko wa Barabara. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Wanyancha, Mwenyekiti wa huu Mfuko, kwa kweli anajitahidi na anafanya kazi nzuri na kila mwaka huu mfuko unazidi kuongezeka mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nizungumzie changamoto ambayo wanaipata watu wa Mfuko wa Barabara. Mheshimiwa Waziri, mwaka jana nililiongea hili na mwaka huu ninataka niliongee; hata katika Taarifa ya Mheshimiwa Arfi, nimeona kaliongelea. Makampuni matano

makubwa ambayo ni ya wachimbaji madini katika nchi hii bado wanaendelea kukaidi kutoa tozo ile ya barabara. Je, ni kwa nini hadi leo Makampuni haya yanaendelea kukaidi amri hii wakati hii ni Sheria ambayo imepitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Serikali inapoteza zaidi ya shilingi bilioni 26 kwa makampuni haya kukwepa kutoa tozo hii. Kama Mheshimiwa Waziri, hawa jamaa wamekuweka mfukoni, vilevile twambie tu, ni jambo la kawaida lakini kwa kweli, hatupendi kuona kwamba, sisi wananchi wa kawaida tunalipia shilingi 200/= katika kila lita ya mafuta, haya makampuni makubwa hayataki kulipia ni kwa nini? Hawahawa ndio ambao wanatuharibia barabara zetu, ndio ambao wanasafirisha mitambo katika barabara zetu, ndio ambao wanatumia mafuta mengi zaidi ambayo yanaingizwa hapa nchini. Hili tunaomba Mheshimiwa Waziri, utupe ufafanuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimwombe Mheshimiwa Wanyancha pamoja na Injinia Muhegi, wajaribu kupeleka elimu zaidi katika Halmashauri zetu. Fedha hizi nyingi za Mfuko zinapelekwa katika Halmashauri, kwa hiyo, wajaribu kwenda zaidi. Najua Mheshimiwa Muhegi anapeleka timu zake kwa ajili ya kusaidia Halmashauri, kutoa semina kwa Halmashauri; naomba waendelee kwa kasi zaidi kuliko wanavyofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende *TANROAD.* Bado tuna tatizo, barabara zetu nyingi zinachelewa kukamilika lakini mbali ya kukamilika ni kwamba baadhi yake ziko chini ya kiwango. Hii inatokana na Mameneja wetu wa *TANROAD* wa Mikoa kutokusimamia shughuli zao kikamilifu. Baadhi ya Mameneja hawa wamewekwa mifukoni na Wakandarasi, wamedhibitiwa na Wakandarasi; tunakuomba Mheshimiwa Waziri, hili ulifanyie kazi, haiwezekani barabara kuharibika katika kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuchelewa huku muda mwingine kuna sababu, kuna wizi unafanyika.

Kazungumza Mbunge mmoja wa Dar-es-Salaam hapa kwamba kuna mtindo wa kwamba, *certificate* za kuwalipa Wakandarasi zinacheleweshwa kwa makusudi. Zile fedha zinawekwa katika *Fixed Account,* zinazaa *interest,* baadaye wanacheza mchezo baina ya hawa Watendaji wa *TANROAD* na watu wa Benki; hadi zile fedha zimeshazaa *interest,* ndio zinakwenda kutolewa wanalipwa wakandarasi. Huu ni mchezo wa makusudi ambao unachezwa. Tunaomba hili uliangalie na utupe ufafanuzi kwa nini bado suala hili linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri, nataka niseme kwamba bajeti yako hii yote imetupa matumaini lakini matumaini yaliyoko humu yana mashaka kwa sababu asilimia kubwa ya bajeti yako hii inaenda kulipia madeni. Tunataka uwe mkweli, hii bajeti yako asilimia kubwa inaenda kulipia madeni. Umejaribu kutoa tu fedha kidogokidogo kila Mkoa, ili kuwaridhisha kwa kweli, sio vizuri. Ni vema alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, hebu chagua miradi ambayo inaonekana kwamba hii ni muhimu, ikopee fedha, tuikamilishe mara moja, tuachane na hili suala la kugawa vipesa kidogokidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo barabara ya Nyakanazi, umeitengea *10 billion,* barabara ya *200 kilometres,* ifanye nini? Unawapiga change la macho tu wale, hamna kitu mle. Mwaka jana mmetengewa shilingi bilioni mbili, kimefanyika nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia barabara ya Ndundu – Somanga; hebu Mheshimiwa Waziri, tuambie ukweli. Tatizo la barabara ya Ndundu – Somanga, tunavyolijua sisi ni kwamba hapa Serikali inadaiwa katika Daraja la Mkapa. Lipeni zile fedha ili hawa jamaa wamalizie kujenga hii barabara. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saleh Pamba, atafutiwa na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Kapt. John Komba ajiandae.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii. Napenda nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, Naibu Waziri na Wataalamu wote wa *TANROADS* wanavyofanya kazi vizuri sana katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kitabu hiki cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kitu kimoja ambacho utakiona ni kwamba miradi ipo karibu nchi nzima. Kama kuna barabara basi barabara inaanza, kama kuna barabara basi kuna barabara ambayo upembuzi yakinifu unafanyika na *details design* inafanyika na kama kuna barabara basi kuna barabara nyingine ambazo zimekwishafunguliwa. Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa upande wake inafanya kazi nzuri sana katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na mtandao wa barabara unaoweza kufikika katika sehemu zote. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa sababu nayo pia imeongeza bajeti ya Wizara hii katika kipindi cha miaka miwili. Kwa mfano, mwaka huu unaomalizika wa 2012/2013, fedha za barabara peke yake ni shilingi bilioni 700 ambazo ni 4% ya bajeti yote ya shilingi trilioni 15. Mwaka tunaoanza mwezi Julai, fedha za barabara ambazo zitatolewa na ninaomba ndugu zangu Wabunge tumpitishie Waziri Magufuli bajeti yake ili aende akafanye kazi; shilingi trilioni moja na milioni mia mbili ambayo ni 7% ya bajeti ya shilingi trilioni 17. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kama tukimpa Mheshimiwa Magufuli fedha hizi wakati tutakapopitisha vifungu, basi barabara zile ambazo zilikuwa zinasuasua, barabara zile ambazo ziko

katika upembuzi yakinifu na barabara nyingine zote, basi zitatekelezwa kwa haraka kama ilivyo katika ahadi na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya madeni yaliyopo katika ujenzi wa barabara. Madeni haya huwezi kuyaepuka kutokana na jinsi fedha zinavyotoka Hazina lakini ili kuepukana na madeni haya wakati tumefanya *commitment* kwa sababu, Wizara hii inayo mikataba na mikataba nayo ni *binding* kwa pande zote mbili kwa Mkandarasi vilevile kwa Serikali. Kwa hiyo, naiomba Wizara pia kwa wale Wakandarasi ambao wanachelewesha kazi nao pia wapigwe tozo kama jinsi ambavyo wao wanaipiga tozo Serikali. Kwa upande wa Serikali, tunaiomba Serikali, iweze kutoa fedha kwa haraka na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Rage alipokuwa anachangia, nilikuwa nimekaa karibu naye. Alikuwa analalamika juu ya kucheleweshwa malipo kwa barabara zake zile za Tabora. Kwa bahati nilipata nafasi ya kuona *penalties* zile ambazo zipo, zinakuja karibu shilingi bilioni 10 ukichanganya *penalties* za nchi nzima, zinaweza kufika hata shilingi bilioni 50 shilingi bilioni 60. Nachoiomba Serikali, ni kuhakikisha kwamba tunajitahidi zile *certificate* zinapotolewa basi zinalipwa kwa wakati. Kwa sababu ukilipa *penalty* ya shilingi bilioni 50 maana yake ukiitafsiri ile *penalty* ni sawasawa na kujenga barabara ya kilometa 50 ya lami iliyokamilika. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, itoe fedha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie juu ya barabara ya Tanga – Pangani – Saadani. Nataka niishukuru Serikali na kupitia Bunge lako, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutoa maamuzi kwamba sasa barabara hii ipite kama ilivyopangwa. Ipite pale katika Hifadhi ya Saadani na tusiwacheleweshe Watendaji wetu katika kuhakikisha barabara hii inajengwa. Napenda nichukue nafasi hii nimshukuru sana Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa maamuzi

aliyoyatoa ambayo nina uhakika kabisa yataharakisha barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa watu wa Pangani na ni muhimu sana katika kuetekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa *Africa Development Bank* pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, wako tayari. Kwa hiyo, ule uchelewesho ambao ulikuwepo zamani, natumaini kwamba sasa hautakuwepo kwa sababu Mheshimiwa Kiongozi wetu ameshatoa amri, kwa hiyo, amri hiyo ni kuweza kuitekeleza, ili kusudi barabara hii ianze. Tunapokwenda huko kupambana na wenzetu tayari CCM tutakuwa kifua mbele kwamba barabara hii imeanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ambalo ninataka kulizungumzia ni suala la utaratibu wa kujenga barabara kwa kitu ambacho kinaitwa *Performance Best Management and Maintenance of Roads.* Mpango huu ni mzuri, umeanza kwa majaribio katika Mkoa wa Tanga lakini majaribio haya kwa upande wa Tanga, hayakuzaa matunda vizuri. Barabara ya Tanga – Pangani, barabara ya Muheza – *Boza Junction,* zote zilikuwa chini ya utaratibu huu. Mkandarasi hakuwa mzuri, tumemwondoa katika barabara ya Muheza tukamwachia barabara ya Tanga – Pangani, lakini bado hajafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, sisi katika *Road Board* na katika *RCC,* Mkoa mzima wameamua na taarifa hiyo iko kwako Mheshimiwa Waziri kwamba barabara ya Tanga – Pangani kwa wakati huu irudi kwa *TANROADS,* ili iweze kutengenezwa vizuri. Nina tumaini kwamba hilo utalishughulikia na mimi ninazungumza hapa kwa niaba ya Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga. Hilo ndio ombi letu na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri, utalishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, ni vivuko. Napenda nichukue nafasi hii nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa suala la vivuko. Nimeona picha ya Kivuko hapa cha Dar-es-Salaam – Bagamoyo, ni jambo zuri. Miji yote iliyoendelea, miji yote ya kisasa, ina njia mbalimbali za usafiri;

usafiri wa ndege, usafiri wa meli, usafiri wa barabara. Kwa hiyo, nasema endelea katika mradi huu mzuri, mradi huu ni *very positive.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri, nimeona katika ukurasa wa 69 wa bajeti yako kwamba, utanunua vivuko vingi kwa ajili ya mradi huu na vivuko vingine kwa nchi yetu. Nimekuandikia barua kuhusu kivuko cha *Pangani One,* nimezungumza na wewe mara kadhaa na umeniahidi kwamba utanipatia kivuko kipya kwa ajili ya wananchi wa Pangani, kivuko cha *Pangani One.* Natumaini Mheshimiwa Waziri ni mchapa kazi, Mheshimiwa Waziri ni msikivu na nina uhakika kabisa katika shilingi bilioni zile 12 za kununua vivuko kwa mwaka huu, utanitengea angalau fedha kidogo ili tununue kivuko cha Pangani, ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Pangani, ili waondokane na adha ya kuvuka katika ule Mto Pangani ambao una mamba sana, wananchi wanapata matatizo sana. Kivuko kimoja naishukuru Serikali kipo, lakini hakitoshi ni lazima tuwe na kivuko cha pili, ili vivuko vyote viwili viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane tena niseme kwamba naunga mkono Hoja asilimia mia kwa mia, lakini namwomba ndugu yangu, namwomba mtani wangu kwamba atakapo-*wind up* anieleze kuhusu kivuko cha Pangani. Ahsante sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamishna Saleh Pamba, Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kapt. John Komba.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake umpe. Mimi kwa niaba ya watu wa Jimbo langu, nashukuru sana tumepata Daraja la Bukingwaminzi na Daraja la Gamaroha linafanya kazi na watu wa Mwasware na wenyewe nitawaombea hapo baadaye, kwa hiyo, kazi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona pamoja na sifa tulizompa ndugu yangu lakini lazima pia tutambue kwamba, nyuma yake kuna Makatibu Wakuu, kuna watu wa *TANROADS* na kuna watu wa Mfuko wa Barabara. Mimi naona wote wale wanastahili kupewa pia pongezi kwa kazi zao wanazofanya na pia kwa sisi ambao tunatoka Simiyu, tunaomba Mheshimiwa uharakishe kupata Ofisi mara moja kwa ajili ya *TANROADS*, kwa sababu ukiwaona wahandisi walivyosongamana katika chumba kimoja, siyo staili ambayo ningefurahi kuona inatumika katika Idara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika tano hapo umenichakachua ndiyo naanza, ahsante sana. Nataka kusema, pamoja na mafanikio mengi, lazima tuseme changamoto ambayo Wizara hii inayo. Naona changamoto ya kwanza kabisa ni jinsi tunavyoipa pesa, kila mwaka ni kama vile tuna *deficit budget,* yaani unasema umetenga na kweli kitabu hiki ukikisoma kimetengewa fedha nyingi. Changamoto; hizi pesa zitapatikana lini na kwa wakati gani? Mimi naona hili ndiyo tatizo kubwa tulilonalo na kama tusipolitatua hili tatizo, najua Waziri hapendi kujisema vibaya hata siku moja, lakini ukweli ni kwamba, angeweza akajenga barabara nyingi zaidi kama pesa na mtiririko wake ungeenda kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtindo wa hivi sasa, ukiangalia ufanisi, *cost effectiveness* ya Miradi hii, lazima uweke alama ya kujiuliza. Tunapoteza pesa nyingi sana kwa sababu Wakandarasi wanaacha kazi halafu wanaanza tena kazi, wanaacha tena kazi, haiwezekani. Pia huwezi ukawaahidi watu kwamba utajenga barabara; kwa mfano, Lamadi mpaka Bariadi, ikaendelea kujengwa kwa muda wa miaka minne, mitano, huu huwezi ukauita ni ufanisi.

Nafikiri lazima tujielekeze katika kutafuta njia mbadala. Natumaini lililosemwa na Mwenyekiti wetu wa Bajeti ni jambo zuri la kuangalia, lakini pia na mimi naongezea, kama kila mwaka tunatenga mabilioni kama tulivyotenga, basi hizo pesa zipatikane na kama kazi hazijamalizika, basi zihamishiwe kwenye Mfuko Maalum, *Project Fund Deposit*

*Account* ili zikae huko, siyo kila mwaka tunaanza tena A, kila mwaka unapanga tena, mara unaanza kuisahau hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hiyo *area* ni lazima tuikalie sisi sote, kuhakikisha barabara zetu zinajengwa kwa wakati na kwa ufanisi ambao unastahili. Si hivyo tu, kusema kweli mojawapo ya changamoto ambayo Wizara hii inayo ni Dar es Salaam; kwa mfano, pale *TAZARA* inachelewesha watu kwenda *Airport,* lakini pia inachelewesha watu kutoka *Port.* Kwa hiyo, kule *port* ipo *congested,* huwezi ukatoa mizigo kwa sababu ya *TAZARA.* Mimi nafikiri kama uamuzi ni *flyover,* basi tungependa kuona hiyo *flyover* inafanyika mwaka huu. *Flyover* haiwezi ikachukua miaka mitano inazungumzwa, rafiki zetu wa Nairobi wamezungumza *flyover* wengine wamekuja hapa wamechukua mipango ambayo tulikuwa nayo, badala ya wao kuzungumza wametenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hapo lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri, tuhakikishe anapata njia ya kuweza kuondosha msongamano wa Dar es Salaam. Lazima pia nichukue nafasi hii kuunga mkono barabara zote ambazo ni za Kitaifa na zimewekewa fedha zijengwe. Barabara za Mkoa wa Tabora zijengwe, Barabara za Mkoa wa Simiyu ambayo tumekueleza kama Mheshimiwa Chenge alivyosema zijengwe, kwa sababu tunapotengeneza haya mambo ndiyo tunapanua uchumi wetu na kufungua njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kumaliza kuzungumza juu ya mambo haya bila kuzungumzia barabara za vijijini. Barabara vijijini ndiyo maendeleo ya Wananchi wetu waliotuleta hapa. Mimi nimeona tangu tumepata Mfuko huu wa Jimbo, nimefungua mahali ambapo watu walikuwa hawatembei zaidi ya kilomita 200; greda tu linapita pale barabara imepatikana. Sasa hivi rafiki zangu Waluguru kwenda Mahaha kwa ndugu yangu Mheshimiwa Limbu, kule sasa wataanza kupata barabara na nataka nione basi linapita kutoka Luguru linaenda Mahaha mpaka Magu. Mimi naona tuweke umuhimu kabisa katika barabara hizi za vijijini. Barabara hizi za vijijini zina changamoto moja; vidaraja vidogo

vidogo, ndiyo maana mimi nimekunwa sana na ile zana ya *bailey bridges*, yaani haya madaraja ya chuma kama Daraja la Magu kwenda Ngaya, lile ni daraja la chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja haya yanatumika sana kwa Vyombo vya Ulinzi, wanaweka pale tena ni rahisi kuyaweka mara moja na hayahitaji pesa nyingi sana. Kama umeniambia kweli ni milioni 50 kwa kila daraja, basi mimi ningeshauri kwamba, Serikali inunue madaraja mengi ili iweze kutusaidia vijito vidogo vidogo ambavyo unajenga barabara, lakini huwezi kupita kwa sababu ya mto mdogo. Mimi naona hiyo dhana ya *bailey bridge* iwekwe nguvu zaidi na ikiwezekana siyo lazima zitengenezwe Ulaya, sisi pia tunaweza, kuna wahandisi wa kutosha, watengeneze *bailey bridges* za hapa hapa nyumbani ili kuhakikisha kwamba hizi *bailey bridges* zinaweza zikatumika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi za vijijini nyingi zinahitaji makalvati. Makalvati haya yanatengenezwa kwa ufanisi mbalimbali. Mimi ningeshauri kama ikiwezekana makalvati yatengenezwe na watu maalum na pia yakaguliwe ubora wake ili Mkandarasi akanunue mahali ambapo yametengenezwa kwa ufanisi na viwango ambavyo vinakubalika. Hakuna sababu mtu ajenge kalvati, ukipitisha gari moja tayari kalvati limeshabonyea. Sambamba na hilo, lazima iendane pia na Sheria, tumezungumza sana juu ya Sheria ya Barabarani na tumeweka mizani kila mahali, lakini kuna *point* gani ya kujenga barabara vijijini, unaweka kalvati, halafu unakubali lori la tani 40 linapita siku moja na makalvati yote yanakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito, Sheria ile ile ambayo ina mkazo kwenye Barabara Kuu, pia iwekwe kwenye Barabara ya Vijijini na anayevunja kalvati aliweke yeye mwenyewe alilipie pale pale. Zamani barabara hizo za pamba zilikuwa za magari madogo madogo tani kumi, tani kumi na tano *maximum.* Leo tunaona watu wanaenda kusomba mahindi tani 40 akipita pale barabara inakwenda tunaanza tena kutengeneza kila siku. Mtindohuu hauwezekani. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri,

pamoja na watu wa TAMISEMI, kama ni Sheria ndogo ndogo, tuweke Sheria ndogo ndogo kuhakikisha mtindo huu tunaumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia jinsi ulivyotaka kujenga nyumba za Serikali. Katika Mikoa mipya na Wilaya mpya kama vile Itirima, Lagangaviriri tuwapeleke *TBA* watujengee hizo nyumba. Nimesikiliza hapa Wilaya mpya hata hakuna mmoja anazungumzia hizi Halmashauri zetu zinajengwa na nani? Naomba wito siyo tu kwa Simiyu, lakini kwa Mikoa mipya yote ambayo imetengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, mimi ni mmoja wa wazee katika nchi hii na katika Bunge hili. Nataka kusema moja nje ya hili; amani ya nchi hii ni lazima ipatikane kwa bei yoyote ile. Hatuwezi, mtu unakwenda kanisani unawaza hutatoka salama na mke wako na wajukuu wako. Haiwezekani; kama kweli sisi tuliochaguliwa na wananchi kuhakikisha nchi hii inaendeshwa kwa amani na tumeshindwa, tunaona watu wanamtukana hata Rais wa nchi hii bila kujali atafanya kitu gani; kama tumefikia hatua hiyo, basi afadhali tumwombe Mheshimiwa Rais avunje Bunge hili twende tukaombe uchaguzi mpya, tupate Viongozi wenye ujasiri na uwezo wa kutuhakikishia amani makanisani, amani misikitini na amani wakati wowote ambao tunatembea katika Taifa hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mzee Cheyo, tunakushukuru kwa busara zako. Mheshimiwa Kapteni John Komba, atafuatiwa na Mheshimiwa Machemli na Mheshimiwa Mngodo; dakika tano tano.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuchangia Wizara hii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cheyo, naona unakatiza.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Apewe adhabu sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, pamoja na Naibu Waziri wake, kwa kutekeleza Sera za Ilani ya Chama cha Mapinduzi vizuri, kwa utiifu, kwa upendo na kwa mshikamano mkubwa sana. Nimekaa hapa na Rais wa Simba, sasa anasema niseme na hawa wote ni Wanasimba; ni kweli? Mnafanya kazi nzuri, nchi inawapenda, John Magufuli heri maziwa uliyoyanyonya maana yanakubariki sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ambayo natoka ipo pembezoni sana mwa nchi yetu na ni Wilaya ambayo ilikuwa huwezi kupita, wale ambao wanakumbuka wakati naingia Ubunge hapa kwa mara ya kwanza, ulikuwa huwezi kupita kutoka kijiji hadi kijiji. Leo hii ninaweza kutoka Mbamba Bay kwenda Lituhi, nikitoka Lituhi naenda Kitai, Kitai - Songea, Songea - Mbinga, Mbinga - Mbamba Bay, kwa siku moja mara mbili, mara tatu; hii yote ni kazi ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli; nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Rais wa Jamhuri ya Muungano; nchi hii leo hatuwezi kuona wema na uzuri wa Rais huyu, lakini kizazi hiki kitakuja kutokea baadaye kitakumbuka mema makubwa sana ambayo Rais Jakaya Kikwete amekifanyia. Anafikiria watu zaidi kuliko kujifikiria yeye mwenyewe. Hebu angalia, alikuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze, pale Chalinze ukipaangalia panafaa kuwa Makao Makuu ya Mkoa palivyokuwa, lakini amepaacha katupa sisi wa pembezoni ili tupate Wilaya yeye hajatoa hata Wilaya hiyo. Unaweza kuona namna gani mwenyewe hajipendi, anapenda watu wengine. Kwa hiyo, nampongeza sana Rais huyu, tuombe Mungu tupate Rais mwingine mzuri kama yeye na Rais mzuri Mwalimu alishasema atatoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kule kwangu, barabara zote ni nzuri, kwa sababu kutoka Songea kuja Mbinga, Wachina wale wametengeneza barabara nzuri ya lami, inapitika vizuri, sasa hivi kutoka Songea mpaka Mbinga dakika 45 umefika. Kutoka Mbinga kwenda Mbamba Bay

nimeona hapa tumetengewa pesa na karibu mnaanza ujenzi. Naomba hizi ahadi ziwe za kweli na sisi tuendelee kujiona kama watu wengine ambao wanafaidi keki ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Mbamba Bay na Lituhi hatujawahi kuona lami kama watu wa Tabora walivyokuwa hawajawahi kuona lami. Jana nilikuwa naona Mwenyekiti wa Simba akilalamika habari ya barabara zake, mimi nina hakika kwa juhudi ambayo Mzee Magufuli anayo, barabara zile zitatengenezwa haraka na watu wa Tabora nao wataona lami kama ambavyo na sisi tunaona lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara inatoka Mbamba Bay kwenda Lituhi, barabara ile sasa hivi ni nzuri, imetengenezwa vizuri na nampongeza *Engineer* wa kule, Bwana Kisimbo, amesimamia vizuri barabara ile. Tatizo kubwa barabara ile madaraja yamebana na ni madaraja ya chuma. Naomba kama inawezekana, kwa sababu ipo chini ya *TANROAD* basi barabara ile itengenezewe madaraja ya kudumu ya saruji itakuwa imara zaidi.

Lingine ni Kivuko cha Mto Ruhuhu, ambacho kimewekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwamba, ifikapo 2015 daraja lile litakuwa limejengwa. Sasa daraja lile halijajengwa, bado miaka miwili na daraja lile linaunganisha Mikoa mitatu; Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa. Utakuta bila daraja lile watu wa maeneo haya hawawezi kufanya biashara wala kutembeleana na wala hawawezi kufanya mambo mengine ya maendeleo. Ninashukuru Naibu Waziri wa Ujenzi alifika hapo akaona ninachokizungumza. Kwa hiyo, ni vizuri sasa tukatilia maanani ujenzi wa Daraja la Mto Ruhuhu ili tukamilishe mambo yaliyoko ndani ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Nyoni kwenda Liparamba hadi Mitomoni, barabara hii imepandishwa hadhi kuwa ya Mkoa chini ya *TANROAD.* Namshukuru sana sana Mwenyekiti wa Mfuko wa Barabara, Dokta Wanyancha na yeye ameenda kule ameiangalia na

ameahidi kutusaidia kupata fedha. Ninaomba sana ahadi zenu zitusaidie kujenga barabara hii, ambayo ni kero ya muda mrefu sana ya Wananchi wa kule kwa sababu ni barabara ambayo iko mpakani kati ya Tanzania na Msumbiji; kwa hiyo, watu wale wanaonekana kama wametengwa hivi. Naomba muisimamie barabara hii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye Kitabu cha Hotuba kuwa, kuna mfuko wa kujenga nyumba. Naunga mkono kauli ya Mzee John Cheyo kwamba, hizi nyumba badala ya kwenda kuzibandika Dar es Salaam, kuzibandika sijui Morogoro, pelekeni kwenye Wilaya Mpya ambazo hazijajengewa nyumba kabisa na moja ya Wilaya hizo ni Wilaya ya Nyasa; mkajenge kule *beach,* nyumba zikae vizuri na sisi tuonekane watu kama watu wengine. Ukipeleka Dar es Salaam ni kama tone kwenye bahari, *impact* yake haitaonekana. Ukipeleka mahali kama Mbamba Bay, Lituhi, Mbinga au Songea, Mfuko huo utaonekana unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sikuwa na mengi ya kuzungumza zaidi ya kupongeza. Nina hakika hivi sasa watu wa nyumbani kwangu hawawezi kunisikia, kwa sababu kwanza hawapati mawasiliano ya redio, wao wanasikia Redio Malawi tu. Eeh, wanasikia Radio Malawi tu na TV Malawi, kwa hiyo, wataambiwa kwamba nimewasemea vizuri. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Kepteni John Komba, nakushukuru sana; sasa sijui uko upande gani wewe; Mheshimiwa ni huku au ni kule, tuambiane mapema!

Mheshimiwa Machemli, Mheshimiwa Mngodo, dakika tano tano atafuatiwa na Mheshimiwa Kepteni John Chiligati.

**MHE. SALVATORY M. MACHEMLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Nasema uchumi wa Nchi yoyote hutegemea umadhubuti wa miundombinu ya nchi husika na umadhubuti huo, hutegemea zaidi mfumo wa udhibiti wa ubora wa kazi na ubora wa kazi una miiko yake

katika kazi husika. Miiko ya kazi ya ujenzi ni kiwango cha kazi, yaani thamani ya pesa ya mradi husika, kukamilika kwa wakati na adhabu zilizoainishwa katika kazi kutekelezwa kwa wakati, hiyo ndiyo miiko ya kazi ya ujenzi. Tutapiga kelele sana katika Bunge hili kwamba, miradi haitekelezwi kwa sababu miiko ya kazi inaepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda mchache, naomba sasa nijikite kwenye Jimbo langu. Nina mkanganyiko, katika bajeti ya 2011/12 na 2012/13 kulikuwa na Mradi wa Barabara wa kutoka Nansio – Lugezi - Kisorya hadi Bunda. Huu Mradi ulifanyiwa *feasibility study* na sasa umetangazwa kwa wakandarasi. Cha ajabu, mwaka huu wa fedha, Mradi huu unataka kuyeyuka na umebadilishwa jina. Sasa ningemwomba Waziri husika, atupe ufafanuzi wa kina, atupe maelezo ni Mradi upi unatekelezwa kati ya Mradi wa Nansio – Lugezi – Kisorya hadi Bunda au Mradi wa Nyamuswa hadi Kisorya, huo ndiyo utata wetu. Ningependa kupata maelezo ili Wananchi wa Ukerewe wajue kabisa kwamba, imekula kwao au huu Mradi unatekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri Mkuu anatembelea Wilaya ya Ukerewe mwaka jana, alitoa kauli. Kauli ya Waziri Mkuu ni Kauli ya Serikali. Kwamba, kwa kuwa Ukerewe ni Kisiwa na barabara hii niliyoitaja ya Bunda - Kisorya hadi Lugezi kwenda Masonga kupitia Nansio, inaishia Ukerewe, haiendi tena zaidi kwa sababu ni kisiwa, angewaomba sasa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu wake, wasivunje majumba yaliyoko kandokando kwa sababu ile barabara ni kubwa na sasa hivi ina upana karibu wa mita 12, angalau Wananchi walioko pembezoni mwa barabara wasivunjiwe kwa sababu hii barabara haiendelei zaidi. *TANROAD* wametangaza mwaka huu wanawaambia Wananchi wavunje. Nini kauli ya Serikali; hao Wananchi waondoe mabanda yao au waendelee kuyaendeleza? Naomba kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jiografia ya Kisiwa cha Ukerewe imezungukwa na maji na wakandarasi wengi

wanaogopa sana kutenda zile kazi katika kile Kisiwa. Tuliomba ombi maalum kwa Wizara ya Ujenzi kwamba, tupelekewe greda na *roller* ili wale Wakandarasi wanaoomba kazi wavikute vifaa vya ujenzi vikiwa pale pale. Ombi liko ofisini kwa Waziri.

Namshukuru sana Eng. Kadashi, Meneja wa *TANROAD* Mkoa, ametusaidia sana kufuatilia na hatujui sasa hili ombi limefikia wapi? Tulikuwa na wenzetu wa Mafia, nadhani wao wametekelezewa. Tunaomba sasa tupate kauli ya Serikali kwamba ombi letu limefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vivuko, tulikuwa na Kivuko cha MV Ukara, nimezaliwa nimekikuta kinafanya safari zake kati ya Kwelu kuja Ukerewe mpaka Kisiwa cha Ilugwa ni Kata hii. Kivuko kile kilikwenda kufanyiwa ukarabati na kilipokamilika kikabadilishwa jina leo kinaitwa MV Chato. Mheshimiwa Magufuli, samahani sana, sijui Chato ndiyo kwako hata sielewi, lakini kimebatizwa MV Chato! Sasa kwa kuwa kimemwagiwa maji ya utukufu kikaitwa MV Chato na MV Chato iliyokuwepo leo imekamilika, tunaiomba sasa ibadilike nayo ibatizwe MV Ukara irudi Ukara ije ifanye kazi zake kati ya Ukerewe na Ilugwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jiografia ya Ukerewe tunahitaji zaidi vivuko, leo tunasafiri kupitia *Ferry* ya Nyahunge na *Summer Three.* Nimeona kivuko kizuri sana hapa na hawa watu leo hawahitaji zaidi kivuko wanahitaji barabara. Nimwombe Waziri wa Ujenzi, wawasiliane na Waziri wa Uchukuzi hiki kivuko kibadilishwe kiitwe MV Ukerewe, angalau ifanye *route* zake kuanzia Mwanza kuja Ukerewe ili kuondoa adha ya watu wa Ukerewe wanaosafiri kwa kutumia mashua na kupunguza vifo kwani kila siku watu wanazama.

Kumekuwa na maafa pale, watu wanazama kwa sababu wanasafiri kwa kutumia boti. Hiki kivuko ni kizuri, kila mtu akikiona kinapendeza, kibadilishwe jina tu kiitwe MV Ukerewe halafu kiletwe Ukerewe kifanye *route* eneo hilo. Ukifanya hivyo utakuwa umetusaidia sana Mheshimiwa

Magufuli na tutakuwa tumekuongezea uhai katika maisha yako. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Machemli, Mbunge wa Ukara. Mheshimiwa Rebecca Mngodo, baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Capt. John Chiligati.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazofanyika kujenga barabara zinazounganisha Miji yetu mikubwa katika Mikoa yetu, zimepelekea barabara za vijijini kuonekana ni nchi mbili tofauti na hivyo umaskini wa Watanzania Vijijini kuonekana zaidi mahali ambako ndiko chakula kinakotoka cha kuwalisha watu wanaoishi mijini. Hata hivyo, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mkuu wa Hesabu za Serikali, imeonesha upungufu uliopo katika baadhi ya Miradi ya Barabara, ambapo wakandarasi wameshindwa kufanya kazi zao katika viwango vinavyotakiwa. Mara nyingi tumemwona Mheshimiwa Waziri akisema kwamba, wanafukuzwa, lakini ningependa kujua, wale wanaowapa kazi Makandarasi ambao wako chini ya viwango wanachukuliwa hatua gani za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo pia na ucheleweshaji wa malipo kwa Wakandarasi. Nazungumzia Barabara inayotoka Kigogo kwenda Jangwani; Mkandarasi wa barabara ile alicheleweshewa fedha zake kwa miezi saba, hadi ikabidi aombe fidia kwa Serikali kudai shilingi milioni 174.5 na Wananchi wa Jangwani waligoma kuondoka mahali pale kwa sababu ya kucheleweshewa fidia. Leo hii nimesikia mzungumzaji mmoja akisema kumbe fedha zile huenda zinapelekwa katika masoko ya hisa. Ningependa kujua wale ambao wanachelewesha kuwapa fedha wakandarasi wanafanywa nini?

Hilo liwe somo kwa Serikali kwa sababu ni kweli Wananchi wa pale Jangwani wameishi pale kwa miaka mingi na hakuna utaratibu wowote uliofuatwa wa kuwashirikisha na kuwaelewesha kwa nini fedha zile zilikuwa

zinacheleweshwa. Fidia waliyoambiwa watapewa haikuwa kamili.

Zoezi zima la bomoa bomoa hapa Tanzania, napenda kusema kwamba, huwa halifanyiki kistaarabu. Wenye nyumba wengine ni wazee na wengine ni wanawake wajawazito na watoto. Pale bomoa, bomoa inapofanyika kwa mtu ambaye ni mzee au mstaafu, Serikali inategemea kwamba, huyu mtu ambaye ni mzee mstaafu, atapata wapi fedha nyingine za kujenga nyumba na fidia anayopewa huenda isiwe kiwango cha kumwezesha kujenga nyumba nyingine.

Pia, zoezi zima la fidia halifanywi kwa usawa; kwa mfano, Wananchi wanaoishi hapa Msalato, wameamka wakakuta greda limepita katika mashamba yao, mazao yao yameondolewa kwa sababu ya kupanua barabara. Kupanua barabara ni jambo zuri, lakini wapo ambao wamelipwa fidia zaidi, wengine wamelipwa pungufu na wengine hawakulipwa kabisa. Utaratibu huu wa kutoa fidia uangaliwe vizuri na kutekelezwa katika hali ya usawa ili Wananchi wetu wasiendelee kuumia kwa sababu tukiwaangalia Wananchi hawa wamepewa fidia ambayo hailingani na mazao yao. Wengine waliopewa fidia zaidi sijui ni vigezo gani vilivyotumiwa mpaka wao wakapewa viwango zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kwamba, inawaangalia Wananchi wake. Watanzania wengi wanaoishi katika hali ya umaskini wanaiona Serikali kama mzazi, wakiamini kuwa Serikali inaweza kuwasaidia. Serikali inapokuwa haiwasaidii ndiyo maana tunaona hakuna amani na tunasema tunataka amani kumbe sisi wenyewe ndiyo sababu ya kutokuwepo kwa amani.

Barabara kutoka Arusha kwenda Makuyuni, kila baada ya mita 200 kuna tuta, matuta yanaleta athari.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Rebecca Mngodo, dakika tano ni chache sana. Mheshimiwa Capt. John Chiligati, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. David Mwakusya.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, niseme kwamba, naunga mkono hoja hii. Pili, ukisoma magazeti hasa kwenye mitandao, picha unayoipata ni kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Nne hakuna inachokifanya, kiasi kwamba, Watanzania ambao wako nchi za nje wanaofuatilia maendeleo yetu kupitia magazeti na mitandao, wanapata picha kwamba, Serikali iko likizo, hakuna kinachofanyika, Ilani ya Uchaguzi haitekelezwi. Ukweli ni kwamba, kazi inafanyika.

Ajenda iliyopo mbele yetu leo ni mfano wa kuonesha kwamba, kazi inafanyika na Serikali Awamu ya Nne iko kazini na mambo yanaonekana. Mimi nataka nitoe ushuhuda, Mkoa wa Singida ambako ninatokea, miaka michache iliyopita ulikuwa haufikiki, *not reachable*, leo hii ninapozungumza, kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi, Mkoa wa Singida unafikika. Barabara ya lami kila upande Mkoa wa Singida. Unapotoka Dodoma - Singida mpaka Igunga – Mwanza, barabara ya lami; ni ushuhuda kwamba, kazi imefanyika na Ilani imetekelezwa. Kutoka Singida – Kateshi - Babati mpaka Arusha, lami imekamilika na kazi imefanyika.

Tunapozungumza hivi sasa kazi inaendelea kufanyika kutoka Manyoni – Itigi - Chaya mpaka Tabora. Sasa anayesema Serikali iko likizo, likizo ya wapi? Kazi inafanyika na sisi tunashukuru. Muungwana ni lazima ushukuru kwa kazi ambayo Serikali inafanya. *(Makofi)*

Vilevile katika bajeti ya sasa tumeona kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa barabara kutoka Makongorosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa, tunaomba upembuzi ukamilike ili kazi ya lami ianze na Serikali iko kazini.

Katika bajeti hii kuna hela za Daraja la Sibiti ambalo linaunganisha Mikoa ya Singida, Simiyu na Arusha, kazi imeanza kufanyika. Kwa hiyo, wale wanaosema Serikali haitekelezi Ilani ya Uchaguzi, ijiandae kuondoka mwaka 2015, kwa mtaji huu haondoki mtu hapa na Magufuli chapa kazi na timu yako mzidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani kwa ajili ya Barabara ya Mchepuo pale Manyoni Mjini. Jana waliposikia Wizara yako ndiyo iko kwenye bajeti, nimepigiwa simu nyingi; wanasema hivi, Waziri aliahidi mbele ya Rais tarehe 5 Novemba, 2012 kwamba, Barabara ya Mchepuo wa Manyoni Mjini katikati pale je imo? Nimepigiwa simu nyingi, sasa nataka niwajibu wale walionipigia simu, najua wanasikiliza saa hizi kwamba, Waziri amekuwa muungwana hii barabara imo kwenye bajeti yake, itaanza kutekelezwa mwaka huu na itatekelezwa kama alivyosema pale Manyoni Mjini. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, watu wa Manyoni Mjini majibu wameyapata kwamba, ahadi ambayo uliahidi mbele ya Mheshimiwa Rais, umeitekeleza na barabara imo kwenye bajeti ya sasa. Ahsante sana, Mungu akubariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado changamoto kubwa iliyopo kwenye sekta sasa hivi ni barabara za vijijini. Tumepata mafanikio makubwa katika Barabara za Mikoa na Barabara za *TANROADS*. Mafanikio ni makubwa lakini barabara za vijijini bado ni changamoto. Ili tuondokane na utaratibu wa sasa, ambao barabara za vijijini zimeachiwa Halmashauri. Jamani Halmashauri zetu haziwezi kutengeneza barabara za vijijini. Uwezo wa kifedha katika Halmashauri haupo hivyo, tutafute utaratibu mwingine. Barabara za vijijini tuziwekee Mfuko Maalum kabisa kwa sababu ya umuhimu wake, hizi barabara zinahudumia asilimia 75 ya Watanzania na ndiyo zinabeba kilimo chetu na ndizo zitakazoondoa umaskini kule vijijini.

Tungekuwa na Mfuko Maalum kabisa tunauchangia wa barabara za vijijini, chombo kingine kiuundwe na siyo Halmashauri; tuwe na kitu kama *TANROAD,* lakini kwa ajili ya

barabara za vijijini tu, ili tuweze kujiondoa katika tatizo la barabara za vijijini ambalo ni tatizo letu kubwa sana hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Jimbo langu. Pale Jimboni kwangu kila siku nasema, tuna upande wa mwinuko *(plateau)* na upande wa Bode la Ufa. Huku kwenye Bonde la Ufa hatuna barabara ya uhakika. Tuna Kata tano ambazo hazina barabara za uhakika, lakini huko ndiko kuna kilimo kingi na ufugaji mwingi, pia kuna viwanda vidogo vidogo vya chumvi katika eneo hilo. Tunaomba tupandishe daraja barabara ambayo inatoka kwenye lami Chukuyu kwenda Majiri – Ikasi – Chaligogo na inakutana na barabara za *TANROAD* za Dodoma na Singida.

Tumeshapitisha katika vikao vyote vinavyohusika kuanzia *Regional Road Board* mpaka kwenye *RCC* na ombi liko Wizarani kwa Mheshimiwa Waziri, naomba utukubalie ombi letu ili Kata tano zilizoko katika Bonde la Ufa zichukuliwe na *TANROAD* ili kuwe na barabara ya uhakika. Naomba ombi hili likufikie, najua wewe ni muungwana sana, naamini safari hii barabara itachukuliwa iwe ya *TANROAD*.

Vilevile nashukuru kwa Barabara ya Manyoni - Ikasi - Chaligongo, hii ni Barabara ya *TANROAD* na *Regional Manager* wa *TANROAD* anajitahidi sana kuitengeneza; namshukuru sana anachapa kazi vizuri. Ninachoomba katika ile barabara ni daraja. Pale Sanza ambako ndiyo mpakani mwa Mkoa wa Singida na Dodoma, lile daraja ndiyo linalounganisha Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida. Kwa hiyo, naomba fedha za kutosha kwani huo mto ni mkubwa na daraja linalojengwa pale ni kubwa. Mwaka huu halipo kwenye bajeti, lakini mwaka kesho naomba hili daraja liwemo katika bajeti ili kuweza kuunganisha Mkoa wa Dodoma na Singida, kwa sababu wakati wa mvua mawasiliano yanakatika kabisa.

Kwa sababu bado nina muda kidogo, nizungumzie kidogo juu ya Wakala wa Nyumba. Nashukuru juhudi zinazofanywa na Wakala wa Nyumba, kwa kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi na nyingine za kukodisha katika Mikoa

mbalimbali. Katika bajeti hii, tunaona kuna mpango wa kuwa na nyumba 2500; hili ni jambo zuri. Hata hivyo, naomba tuzisambaze hizi nyumba zisirundikwe sehemu moja, sehemu ambayo mnadhani ndiyo kuna hela nyingi. Hili siyo suala la hela peke yake, ni suala la kutatua shida za Watanzania popote pale walipo.

Kwa hiyo, tunaomba mtawanyiko wa nyumba hizi zifike katika Wilaya mbalimbali. Kweli kuna Wilaya mpya zinahitaji nyumba, hiyo ni sawa na naunga mkono kabisa, lakini hata Wilaya za zamani kama Manyoni nazo zinahitaji nyumba. Naomba mtawanyiko wa hizi nyumba ziguse sehemu mbalimbali zenye matatizo mbalimbali katika mikoa mbalimbali. Hapa Dodoma, kwanza, ni-*declare interest,* mimi ni mpangaji katika nyumba za *TBA.* Sasa tatizo lililopo ni kwamba, hatulipi kodi, hata baadhi ya Watendaji Waandamizi Serikalini hawalipi kodi, Wabunge hatulipi kodi katika hizi nyumba.

Nataka kutoa wito, tulipe kodi ili *TBA* wapate pesa za kujenga nyumba kwa Watanzania wengine, kwa sababu kama hatulipi kodi tunawanyima uwezo wa kujenga nyumba nyingine na hawawezi kukarabati. Zile nyumba za Kisasa, ukipita leo zipo katika hali mbaya, lakini sasa hatuwezi kuwalaumu *TBA*, kwa sababu baadhi yetu hatulipi kodi. Hivyo, natoa wito kwamba, tulipe kodi ili *TBA* wapate uwezo wa kukarabati nyumba ambazo zipo sasa hivi na wapate uwezo wa kujenga nyumba nyingine kwa Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Capt. Chiligati. Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKUSYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Ujenzi. Jana Jumatatu kulitokea ajali katika Kijiji kinaitwa Igula, Kata ya Kiwira katika Barabara Kuu

inayotoka Mbeya kwenda Malawi kupitia Tukuyu, mtu mmoja alipoteza maisha na tunamwombea Mungu roho yake aiweke mahali pema na wengine waliojeruhiwa wako hospitali na wao tunawaombea wapone haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hiyo niliyoitaja, ajali zinatokea mara kwa mara, kuna mteremko na kona kali na magari huwa yanaacha njia na kutumbukia kule chini mpaka panaitwa Uwanja wa Ndege.

Niliwahi kuleta ombi hapa katika Bunge kwa njia ya swali na ninalileta tena; tunaomba tuwekewe kinga ili maisha ya Wananchi yasiendelee kupotea bila sababu. *(Makofi)*

Tumefanikiwa katika Milima ya Kitonga na milima mingine na kule kuna binadamu wanaomba hizo kinga ili tusiendelee kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rungwe inapata mvua takribani miezi minane kwa mwaka. Hii ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, tunapata mazao ya chakula, ya biashara na imetuepushia baa la njaa. Kama wote tunavyojua, mvua siyo rafiki wa barabara hususan Barabara za Rungwe ambazo ni za udongo kwa asilimia karibu 99.

Halmashauri inatumia fedha nyingi sana kila wakati kutengeneza sehemu korofi na kila wakati vifusi ndiyo vinapelekwa kule. Kwa hiyo, fedha zinazopelekwa Rungwe ni za kutengeneza sehemu korofi. Nimewahi kuomba hapa na ninaomba tena, baada ya kutumwa na Halmashauri yangu kwamba, wakati mgao wa fedha unapofanyika Wizarani, tunaomba hili, tuko tofauti kidogo, tuwe tunapata ziada kwa sababu fedha zote tunazopata zinakwenda kwenye sehemu korofi, kwa hiyo, hatuwezi kuendeleza barabara sehemu zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya kongwe ya Rungwe, huko tulikotoka iligawanywa karibu miaka 40 iliyopita ikazaa Wilaya ya Kyela, Ileje na Rungwe yenyewe ya sasa hivi. Haishangazi kwamba, kuna mahusiano mengi kati ya hizi

Wilaya, mambo ya kijamii, uchumi, biashara na maendeleo kwa ujumla, lakini kwa bahati mbaya hakuna barabara za kuaminika zinazowaunganisha hawa watu. Barabara zilizopo ni duni na ipo haja kusema kweli umoja huu na mshikamano uendelee. Kwa nyakati tofauti, nimeuliza maswali hapa Bungeni kwa niaba ya Wananchi wa Rungwe, nikiwa nazipigia debe barabara zifuatazo:-

Kuna barabara inayotoka Kyemo, inapita Ikuti katika Jimbo langu na kwenda Luswiswi mpaka Isongole, ambalo ni Jimbo la Ileje. Nyingine inatoka Kiwira - Kipande - Isangati mpaka Mbalizi; hii ni barabara muhimu sana, kwa sababu ndiyo inakupeleka Uwanja wa Songwe, inaondoa ulazima wa kupitia Mbeya Mjini ambako ukipita njia hii kama ni imara utakuwa umepunguza kilomita karibu 50.

Niliuliza katika maswali yangu ni lini Wananchi watawekewa lami katika hizi barabara, lakini majibu yalikuwa ya kukatisha tamaa. Vilevile kuna barabara inayotoka Tukuyu inapita Mbambo, Lwangwa na Katumba; mwaka 2005 na tena mwaka 2010, wakati wa Kampeni za Urais, Mheshimiwa Rais alipofika Tukuyu alitoa ahadi moja tu, nayo ni kuhusu hii barabara; aliahidi hii barabara itawekewa lami. Tumefuatilia, tumeambiwa upembuzi umekamilika, usanifu umekamilika. Sasa mimi nadhani na wenzangu hapa tunaelewa mambo ya upembuzi, usanifu na kwamba lazima hiyo hatua ifanyike kabla ujenzi haujaanza, lakini kwa bahati mbaya, Wananchi wangu hawaelewi huo Msamiati, wanachotaka ni barabara waliyoahidiwa na Rais wao mpendwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri, mwaka 2010, barabara hii iliingia kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Mwaka wa Fedha uliofuata (2011/2012), zilitengwa shilingi milioni 600 ili zikaanze kujenga madaraja mawili, lakini hadi leo hakuna daraja lililojengwa na hatujui hatima ya hizo fedha. Mwaka uliofuata ambao ndiyo huu tunaoumalizia sasa hivi, hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa. Fedha tunazoziomba sasa hivi nashukuru kwamba, shilingi milioni 110 zimetengwa kwa ajili ya madaraja

mawili na shilingi bilioni 1.27, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siyo Mhandisi kama unavyojua, lakini Mheshimiwa Magufuli na Makamu wake ni Wahandisi, wanajua kwamba, shilingi milioni 110 haziwezi kujenga hata asilimia kumi ya daraja moja na hii bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara, wao wenyewe wametuambia ni kilomita moja. Urefu wa barabara tunayoizungumzia ni kilomita 83. Sasa kwa mwendo huo, ina maana tutachukua miaka 83 kuikamilisha hii barabara ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Rais ni agizo, nilitaka kukumbusha tu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli imesemwa hapa mnyonge mnyongeni, mimi sijaona kama Rais wangu ni mnyonge au Waziri ni mnyonge, wote ni watu wakakamavu na imara kabisa. (*Makofi*)

Huko tunakokwenda, moja ya mambo ambayo tutayakumbuka kuhusu Awamu hii ya Nne ni mtandao wa barabara mpya. Historia hii ya mafanikio huwezi kuitenganisha na utendaji binafsi wa Waziri Magufuli, napenda nikupongeze Waziri na timu yako. *(Makofi)*

Watanzania tumevutiwa na jinsi unavyozijua barabara hapa nchini, utatuambia umbali mpaka nukta, Makandarasi wamepewa upande gani, lakini kumbukumbu zangu zinaniambia kwamba, sijawahi kukusikia Mheshimiwa Magufuli ukizungumzia barabara za Rungwe. Hujawahi kufika huko, kama nakumbuka sawasawa na nikumbushe tu kwamba, Rungwe ni sehemu ya eneo lako la kujidai kwa barabara, jirani yangu anasema na Kilolo pia hujawahi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi hasa siku za Jumapili, kuna kipindi maalum, ambapo utamwona Mheshimiwa Rais anaweka Jiwe la Msingi au anafungua

barabara au madaraja, Wanarungwe wanaona wivu, tunapoona hizi kazi zinafanyika kwingine tu, kwetu hata siku moja haijawahi kutendeka. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba, tuibue Miradi ya Barabara mikubwa ambayo tunaweza tukamshawishi Rais aweze kuja kutufungulia. Isionekane tu wenzetu ndiyo wanafaidi matunda ya Uhuru na ya Chama chao wanachokipenda. Hata katika majedwali ambayo tumeletewa, mimi nikipewa bilioni 1.27 za kujenga barabara, wengine wamepewa bilioni kumi, lakini sisi tunaishi kwa matumaini.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anajua kwamba milioni 110 haiwezi kujenga daraja au bilioni 1.27 haiwezi kujenga barabara ya kilomita 83, najua hakuweka hapo kwa mzaha. Ningeomba tupitishe, kwa sababu hizo najua ni za kuanzia halafu atatembeza kibakuli ili apate fedha za kuweza kutukamilishia hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo kwa kukushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Said Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kama Mbunge wa Mpanda Mjini. Nianze kwa kusema kwamba, neno baya hujibiwa kwa neno jema na unapotaka kusema ni lazima uangalie mwanzo, katikati na mwisho, ukiona ni jema basi liseme na ukiona ni baya basi ni afadhali unyamaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuna tatizo kama Wabunge, ama la kutokufanya rejea kwenye Katiba; niwakumbushe tu Wabunge wenzangu kwa unyenyekevu na adabu, turejee kusoma Katiba, Kifungu cha 63(2) na kifungu cha 3(b); zimeainishwa waziwazi kabisa nini kazi za Mbunge. Moja ni pamoja na kuishauri Serikali, lakini si kazi ya Mbunge kuijibia Serikali. *(Makofi)*

Jana baada ya kuwasilisha kama Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Wizara hii ya Ujenzi, msemaji wa kwanza kutoka Chama cha Mapinduzi, amejaribu kuupotosha Umma wa Watanzania. Ninaomba nichukue fursa hii kuwaambia Watanzania kwamba, sisi siku zote hatuko kungojea fadhila na hisani kutoka kwa mtu yeyote. Kinachofanywa tu, ni Watanzania wamewapa dhamana ya kuongoza na kukusanya fedha kutoka kwa Watanzania wote na yote yanayofanywa yanatokana na fedha ya Watanzania wenyewe. Hivyo basi, mafanikio au kutokuwepo mafanikio ni ya ujumla wa Watanzania. *(Makofi)*

Siyo kosa hata kidogo na leo siyo mara yangu ya kwanza, nimewahi kumpongeza Mheshimiwa Magufuli, katika Hotuba yake ya Bajeti ya mwaka uliopita, kwa mambo mazuri ambayo alikuwa ameyafanya. Pale ninapoona kwamba, pamekosewa, isionekane kwamba ni dhambi kumtaka tu ndugu yetu Mheshimiwa Magufuli katika kazi nzuri anazozifanya, aweze kusahihisha huo upungufu, ni kwa nia njema kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maoni yetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani, ni kutaka kujenga Taifa ambalo ni la mshikamano, lenye umoja, lenye maendeleo na hasa tukizingatia Sekta hii ya Ujenzi na hasa Barabara, ina sehemu kubwa katika kuchochea maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa Mjumbe katika Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa mfululizo toka nimekuwa Mbunge siijui Kamati nyingine yoyote ya Bunge. Kama mtu alikuwa ana miaka mitano, sasa mimi nina mwaka wa saba na nusu katika Kamati hii na ninaamini kwamba, nitamaliza miaka kumi bila kutoka kwenye Kamati ya Miundombinu. Kwa hiyo, naifahamu vya kutosha na ninayoyasema, ninasema kwa sababu nina uhakika nayo, kwa sababu nimekuwa Mjumbe katika Kamati ya Miundombinu kwa kipindi kirefu. *(Makofi)*

Kwa nia njema pamoja na ndugu yangu, namheshimu sana Mheshimiwa Mbunge wa Chama cha

Mapinduzi, tena *senior*, nimemkuta humu Bungeni. Sikuwa nimebahatisha, nilikuwa na yakini na nina hakika na kile ninachokisema na siku zote ndiyo maana najivunia kwamba, sijapata hata siku moja ndani ya Bunge hili toka nimekuwa Mbunge, kuambiwa futa kauli au kupewa taarifa; kwa sababu najiamini na ninachokisema nakuwa nina uhakika nacho. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, mimi ninazo Hotuba mbili hapa za Mheshimiwa Magufuli ya mwaka 2012/13 na 2013/14, aende akarejee, akasome Bajeti ya mwaka 2012/13, ukurasa wa 159 - 160 na Bajeti ya mwaka huu, ukurasa wa 72 - 73. Halafu asome katikati ya mistari, kisha aje kulaumu haya niliyokuwa nimeyasema. *(Makofi)*

Nimeyasema kwa nia njema sana, kutaka kueleza tu kwamba ni vizuri Serikali ikasema kile ambacho inakiweza na wala sikutaka kwenda mbali sana na kufikia mahala pa kunyosheana vidole au kutamka lugha ambazo mimi binafsi siwezi kusema, lakini inasikitisha wakati mwingine unaweza ukasukumwa ukasema hayo ambayo hayapendezi. Tunapozungumzia ujenzi wa nyumba, *TBA*, kwa maelezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri, kwamba nyumba nne tayari zimeshajengwa Katavi na wana mpango wa kujenga nyumba 50. Nasikitika sana kusema kwamba, taarifa hii siyo sahihi, lakini sitaki kumlaumu Mheshimiwa Waziri, pengine amepotoshwa na Watendaji wake. Uhakika ni kwamba, wameomba viwanja viwili na wamelipia na hakuna nyumba hata moja iliyojengwa. *(Makofi)*

Sasa tusifikishane huko, tunaposema tunasema vitu ambavyo tuna uhakika navyo. Nilikuwa napenda kulisahihisha hilo tu. Tunajua yale mazuri ambayo mwenzetu Mheshimiwa Magufuli ameyafanya pamoja na wasaidizi wake na Wizara, lakini pia upo upungufu ambao tunadhani ukiachiwa kama hautachukuliwa hatua sasa, utaliongezea mzigo wa deni Taifa hili. *(Makofi)*

Sasa hivi Taifa hili linadaiwa zaidi ya shilingi trioni 22 na deni linaendelea kuongezeka na riba katika Miradi ya Barabara inaongezeka. Kwa hiyo, tulikuwa tunashauri kwa nia njema kwamba, ni namna gani tunaweza tukapunguza

huu mzigo ambao utalipwa na vizazi vinavyokuja vya Watanzania maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika eneo hilohilo, ukiangalia hiyo ndoto ya kujenga nyumba 50 ambayo unawapa matumaini Watanzania na hususan Wakazi wa Mpanda, haiwezi kutimia kama Bajeti iliyopita ulikuwa umetenga shilingi bilioni tano na ya mwaka huu umetenga shilingi bilioni mbili. Ndiyo maana tukasema tusilete zile hotuba za kuwapa matumaini, wakati huku ukijua kabisa huna fedha na wala hujui utazipata wapi hizo fedha, ndiyo maana ya msingi wa kusema hayo ambayo tumeyasema.

Nipende kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Chiligati, ni Mbunge pekee ambaye ameona umuhimu wa kuwa na Wakala wa Barabara Vijijni. *(Makofi)*

Jambo hili sisi tumelipendekeza katika hotuba yetu na ninamshukuru sana Mheshimiwa Chiligati kwa kulisemea hilo. Kuna umuhimu mkubwa na kama alivyoeleza Mheshimiwa Chiligati ndivyo na sisi tulivyoeleza katika maelezo yetu kama Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba, Halmashauri zetu hazina uwezo wa kifedha na hazina Wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, nampongeza sana Mheshimwa Mbarouk, katika hili ambalo amelisema kuhusu tozo, inasikitisha kabisa watu wanakereka na maneno tu, lakini yale ambayo Taifa linapoteza, hawataki kuyasemea. *(Makofi)*

Taifa letu linapoteza zaidi ya shilingi bilioni 26 kama alivyosema Mheshimiwa Mbarouk kwenye tozo, wakati Mfanyakazi maskini, Mbunge, Mfanyabiashara na yeyote mwenye kumiliki chombo cha usafiri, analipia shilingi 200 kwa ajili ya lita moja ya mafuta kama tozo. *(Makofi)*

Mfuko wa Barabara, unakusanya zaidi ya shilingi bilioni 504 kutokana na tozo itokanayo na mafuta, lakini Wazungu wanasamehewa! Hakuna yeyote ambaye anaona kwamba

Taifa hili linapoteza fedha na akasimama akasema, wamenyamaza, wameridhika. Pengine inaweza ikatulazimisha, tukadhani kwamba, fedha hii labda Wazungu wanalipa katika Mfuko mwingine siyo wa Serikali ambao sisi hatuujui na hii ni hatari, kama sheria basi iwahusu wote na hata kama msamaha uwe na kikomo. Huwezi kuendelea kuwasamehe wenye migodi ya madini, leo wana zaidi ya miaka 12, mnaendelea kuwasamehe! *(Makofi)*

Nzega pale wanafunga mgodi, hawakulipa hata senti tano kwenye tozo ya mafuta na wengine watafunga bila kulipa. Tunaendelea kunyamaza na tunaendelea kupiga makofi na kuishangilia Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, bila kumhimiza na kusisitiza kwamba, sasa Watanzania tumechoka, tunataka Makampuni haya yalipe hii tozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, katika Jimbo langu nina kilomita zisizofika kumi za barabara kuu, lakini nasikitika sana jirani yangu pale Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye ana tatizo kubwa. Juzi alikuja Mheshimiwa Makamu wa Rais, ilibidi wampeleke kwa Helikopta Inyonga, Makao Makuu ya Wilaya ya Mlele, kwa sababu ya barabara mbaya. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, hebu angalieni hii Barabara ya Ipole – Inyonga – Mpanda. Kadhalika, magari yamekaa katika msimu huu wa mvua ulioisha siku 21 barabarani yakingoja kuvuka barabara ya kati ya Mpanda kwenda Uvinza, hadi Kigoma, hali hii ni hatari. Katika miaka 50 ya Uhuru, leo hii mtu anashindwa kusafiri kutoka Mpanda kwenda Kigoma, analazimika kukaa wiki tatu barabarani. Hebu chukueni hatua za haraka katika kurekebisha dosari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Arfi. Sisi tunaokaa kuwasikilizeni wakati mwingine Bungeni pagumu, maana aliyepata bilioni mbili za nyumba analalamika, sasa asiyepata sijui atasemaje!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nisije nikasahau, siiungi mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sababu ninazo. Sababu kubwa kabisa Barabara ya kutoka Sumbawanga – Kanazi, Kanazi – Mpanda – Kibaoni, muda wake umekwisha mwezi wa tatu 2013. Barabara hiyo mpaka sasa ina asilimia 28. Nimezungumza kila mara hapa, Wachina kule wanauza kokoto. Amepewa leo Mchina barabara ya kutoka Sumbawanga – Kibaoni, shilingi bilioni 17. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wa Rukwa na Katavi, waniunge mkono ikiwa ni pamoja na Waziri Mkuu, ambaye Jimbo lake ninapakana naye na ndiyo barabara inayokwenda kwenye Mkoa wake mpya wa Katavi. Hakuna kinachofanyika, Wachina wameweka silaha chini, wanakaa wanauza kokoto; nitaungaje mkono hoja. Anayeunga mkono hoja ndugu yangu mvua imemnyeshea kwake. Mimi siwezi kuiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Rais aliwahi kutoa ahadi alipotembelea mara ya kwanza kabisa, wakati wa kampeni mwaka 2010; Barabara ya Chala – Miombo – Londokazi – Mashete pale inapitia, Mtenga – Mwai mpaka Paramawe kuwekwa lami; lakini siaona upembuzi yakinifu wala chochote kwenye vitabu vya bajeti. Kwa vipi nikuunge hoja mkono. Siwezi kuunga mkono hoja. Nimepiga kelele sana hapa kuhusu Barabara ya Kirando – Namanyere, akanijibu majibu ya ajabu kabisa, hakuna hela wala haiwezekani. Hajafika kuangalia umuhimu wa ile barabara, watu wanakwenda Congo kila siku kwa magari, ni muhimu kwa uchumi wa nchi hii, lakini ananiambia wala haiwezekani. Barabara nyingine nimetembelea lami mpaka majumbani. Kwa nini niunge mkono hoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwambao wa Ziwa Tanganyika, nimezungumza toka nilipoingia Bungeni, kuna vijiji zaidi ya 30 havijaona hata bajaji. Halmashauri hazina uwezo kabisa wa kutengeneza zile barabara. Tulitaka barabara kutoka Simbo – Kigoma kupitia Kalya, kupitia Mgambo, Karema mpaka Kasanga, barabara ni mbovu. Sasa labda tuombe Congo iingie pale ndiyo tupeleke barabara. Wananchi hawana barabara. Mpaka msikie Congo imeingia kule, Kabila ameingia na Majeshi, ndipo

mtakapopeleka barabara; itawezekana nchi namna hii? Mbona katika Mwambao wa Ziwa Victoria kuna barabara kwenye kila kijiji? Ziwa Tanganyika ni Tanganyika bado siyo Tanzania? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siuingi mkono hoja ya Waziri, hata Wabunge wa Mkoa wa Rukwa wakiiunga mkono hoja hii, ndugu zangu mtakuwa mnaangamiza watu wengi. Asilimia 28 barabara ya lami, wametupiga changa la jicho hapa, changa la macho, sijui wanawaleta wataalam, hakuna kitu kinachofanyika kule Rukwa, tumedanganywa mpaka tumechoka. Tumenyanyaswa tumechoka. Leo barabara inakuwa ya kutazama tu, hamwoni hata aibu, hata Waziri Mkuu yuko kule, kwa sababu hazungumzi hapa Bungeni; ni aibu Mheshimiwa Magufuli. Hatutaiunga mkono kabisa Wizara yako hii. Nimezungumza mwanzoni kabisa hapa, barabara ya Kipili kwenda bandarini, kilomita saba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, ongea na mimi hapa.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Ninakushuru sana Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kipili kwenda bandarini inaishia Kipili kwa kilomita saba hamna barabara. Hiyo bandari itakuwa bandari kweli? Kwa hiyo, ninatamka kabisa sitaunga mkono hoja mpaka nipate majibu sahihi ya Barabara ya Sumbawanga – Kanazi, Kanazi – Kibaoni, iko asilimia 28 na muda wake umekwisha mwezi wa Machi, 2013. Sasa sijui tunafanyaje? Mmetuahidi barabara, tukizungumza hapa, tunaambiwa mmependelewa barabara; ni barabara gani tuliyopendelewa?

Leo hii watu wanaomba barabara zao kufukiwa mashimo, madaraja yamejengwa makubwa makubwa, vivuko mbalimbali, lakini sisi hamna cha kivuko, wala chochote. Tumekaa tunatazama vumbi linapita kwenye nyumba za watu. Kwa hiyo, Mheshimiwa ni hayo ninakueleza kabisa kuna barabara ya ahadi ya Waziri Mkuu, Itindi –

Kibaoni, inakwenda nyumbani kwa Waziri Mkuu hata hamwogopi. Ninazungumza kila siku hapa, Itindi – Kibaoni, ni ahadi yake Waziri Mkuu, wakampigia na makofi watu wa Itindi, imekuwa kama ka-*appendix.* Halmashauri haina uwezo wa kutengeneza barabara zozote, Halmashauri kule Wilaya ya Nkasi haina uwezo. Barabara zake kutoka Kitosi – Wampembe tumeomba siku nyingi, Nkana - Kala zichukuliwe na Serikali Kuu mmekataa moja kwa moja, hata kwenye kitabu hakuna na maombi yalikwishafika kwenu. Ili Serikali ya Halmashauri ipunguziwe uzito wa hizo barabara ziingie Serikali Kuu ipate kutengeneza barabara zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa watu kule wamekosa nini kwa Mwenyezi Mungu? Nenda kaangalie Wampembe – Kitosi, Nkana - Kala, huwezi. Zinaitwa ni barabara, lakini hakuna barabara kule. Tuna uhuru kwa kipindi cha miaka 50, nimekwambia vijiji kule katika Ziwa Tanganyika hawajaona gari, kama unabisha twende kwa miguu. Wanakwenda kwa miguu.

Walimu mnapowapeleka kule ndiyo maana wanagoma, wanakuja kuchukua mshahara kwa miguu, atakubali nani mtoto wa mtu. Nani atakubali kwenda kufanya kazi Kazovu, Isaba, Chongo, kwa nini wafanye kazi namna hiyo, anatembea kwa miguu kwa saa sita kufuata mshahara; kwa nini? Ana laana?

Hakuna miundombinu, leo mnawalaumu walimu hawaendi, waganga hawaendi, mtawapeleka kwa nguvu, wamekosa nini kwa Mwenyezi Mungu, anafuata mshahara siku tatu njiani. Siku tatu! Ninyi mmekaa mnatengeneza mabarabara ya kwenu, kwani hatuyaoni hayo mabarabara kule kwenu, lami mpaka milangoni. Nchi hii imegaanyika kwenye Kanda, tunazijua wazi. Kanda zingine zina upendeleo, Kanda zingine tumebaki kama vile tuko, basi tumetelekezwa tunaitwa Wananchi wa Tanzania, lakini siyo Tanzania; wamekosa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maneno mengi, sitaunga mkono hoja mpaka nipate majibu ya barabara nilizozitaja hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed umemaliza? Ahsante sana. Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa ndiye atakayekuwa mwongeaji wetu wa mwisho kwa mchana wa leo.

**MHE. MAHAMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nikushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninawapongeza kaka zangu, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika nchi yetu. Kwa hali halisi ya Bajeti ya nchi yetu, hawezi kutekeleza maeneo yote kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipenda kuzungumzia katika maeneo yafuatayo: Eneo la kwanza, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 kuhusu Barabara ya kutoka Mafinga kupitia Saadani – Madibira – Igawa. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 ilikuwepo, kilomita 151, lakini hakuna hata kitu kimoja kilichofanyika kuhusu hili. Ninataka niwakumbushe kaka zangu, hili lilikuwa changa la macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Mwaka 2010 – 2015 imejirudia tena kwamba, tutawajengea barabara ya kilomita 151 katika eneo hilo. Ninataka niseme, mpaka ninapozungumza leo hii, hakuna jambo lolote lililofanyika katika hizo kilomita 151. Kwa hiyo, nina wasiwasi kwamba, mchanga wa macho unaweza kujirudia tena. Kwa hiyo, kwa sababu kaka zangu ninawapenda na mimi nitawaunga mkono kwenye Bajeti hii, ninaomba mliangalie jambo hili. Mwakani mtakapokuja kuleta Bajeti yenu, naamini kabisa mtatufikiria kilomita 151 zitakuwepo.

Kutokana na kutokuingiza katika Mpango wao, wamewaweka Wananchi wanaotoka katika maeneo yale kwenye mashaka. Wamepiga alama ya (X) maeneo yao, Wananchi hawajui nini cha kufanya, lini Serikali itawalipa fidia na wapi watajenga. Ninaomba jambo hili lifanyike mapema

kusudi Wananchi waondokane na hofu walizonazo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninataka kuchangia ni ahadi ya Rais. Mheshimiwa Rais, wakati wa kampeni mwaka 2010 aliahidi kuweka kilomita mbili za lami katika Mji wa Mafinga Mjini, lakini mpaka sasa kilomita za lami zilizowekwa Mafinga Mjini ni 1.6, ambayo ilifanyika mwaka 2011. Kwa hiyo, miaka miwili mizima Wizara ya Ujenzi imeshindwa kukamilisha kilomita 0.4. Hii ni aibu kubwa, kama wameweza kufanya jambo kubwa kwa nini wanashindwa kumalizia eneo dogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni Barabara ya John’s Corner kwenda Mtili mpaka Mgololo. Eneo hili ni nyeti, lina viwanda vikubwa sana ambavyo vinachangia uchumi mkubwa sana katika nchi hii na Barabara hii ni ya *TANROAD*. Cha kusikitisha, kila siku wanatengeneza kwa matengenezo makubwa sana, lakini kama wangelikuwa wameamua hata kwa kuweka kilomita tano tano kwa kiwango cha lami, nina hakika leo hili wangelikuwa wamemaliza, lakini zile gharama zinazotumika ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba ndugu zangu waliangalie jambo hili na waachane na huu utaratibu wa kuwa wanatengeneza barabara kila siku. Waanze kuanzia sasa kutengeneza kilomita tano tano za lami, baada ya miaka mitano tutakuwa tumefika kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninataka kulizungumza ni Barabara ya Mtili kwenda Ifwagi – Mdabulo – Ibwanzi – Lulanda mpaka *TAZARA.* Eneo hili lina kilomita 130, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi haina uwezo wa kutengeneza eneo hili. Ninawaomba ndugu zangu barabara hii waichukue na tumeshaiombea, lakini hawajatupa majibu mpaka leo hii. Barabara hii inapitika kwa tabu sana na eneo hili ni *very sensitive* katika uchumi wa nchi

hii, kwani ni eneo ambalo chai inapatikana kwa wingi na eneo ambalo linapatikana misitu na miti kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni Barabara ya *Ruaha National Park. Ruaha National Park,* ni moja ya Mbunga kubwa kuliko Mbunga zote hapa nchini. Inasikitisha sana, unapoona sehemu ambapo tunategemea tungelipata uchumi wa kutosha, wenzetu hawataki kuliangalia jambo hili. Ninaomba wawekeze katika eneo hili tupate barabara ya lami kusudi tupate Watalii wengi ambao wataingiza kipato katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowapongeza kaka zangu hawa wawili. Kwanza, wamechukua Barabara ya Mufundi ya Kijanambo (C) mpaka Kisusa, imechukuliwa na *TANROAD,* ambayo ilikuwa haipitiki mwaka mzima. Ninaomba niwashukuru sana kwa jambo hili. Sasa hivi kuna uhakika wa usaifiri wa moja kwa moja. *(Makofi)*

Eneo la pili, ambalo ninataka niwapongeze ni ile barabara ya kutoka Iringa Mjini mpaka Mafinga, ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami. Ninaomba niwapongeze kwa hilo. *(Makofi)*

Eneo la tatu, ambalo ninataka niwapongeze ni barabara ya kutoka Dodoma – Mtera mpaka Iringa, ambayo inajengwa sasa hivi. Huu ni ukombozi mkubwa sana kwa Wananchi wa Iringa na mikoa jirani. Ninawaomba ndugu zangu waweke *diversion* ile barabara isipite katikati ya Mji wa Iringa, kwa sababu kesi ambayo tunalalamikia msongamano wa magari ikipita pale mjini itakuwa ni tatizo, kwa hiyo, ninaomba waingize *diversion* ipite nje ya Mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia kwa ujumla ni suala la mizani. Kumekuwa kuna mizani mingi sana hapa nchini. Mizani hii badala ya kuleta tija, imekuwa inaongeza msongamano. Mizani badala ya kuwekwa nje ya mji, inawekwa katikati ya

miji. Ukiangalia mzani kama ule wa Kibaha, unaleta msongamano mkubwa sana pale mjini. Kwa hiyo, misongamano mingine tunaitengeneza wenyewe. Ninaomba Wizara iliangalie suala hili na mzani ule uondolewe. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja, ninataka niwape nguvu wenzangu waendelee kututengenezea barabara zetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wahehimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Ninazo dakika kama sita, Mheshimiwa Margareth Sitta, kama unaweza ukatumia dakika hizo sita. Karibu mama jitahidi.

**MHE. MARGARETH S. SITTA:** Mheshimiwiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu.

Kwanza, ninaipongeza Serikali ya CCM, kwa kazi nzuri inayofanya, hongereni sana, msivunjike moyo, mwendelee. Ninashukuru sana kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumzie kwa kifupi sana kuhusu Barabara za Tabora. Tupeni pole watu wa Tabora, hatuna hata barabara moja inayoingia Makao Makuu ya Mkoa katika miaka yote hii ya Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mkoa wa Tabora wamechangia sana maendeleo ya nchi hii. Ninaishukuru Serikali kwa kuja na wazo la kusema sasa tuanze kujenga barabara, ni wazo zuri na kama nilivyosema, ninaipongeza Serikali. Ukifikiria jinsi Mkoa wa Tabora ulivyochangia mapato ya nchi hii, kwa kweli inasikitisha sana mpaka sasa hatuna hata barabara moja ya lami inayoingia mkoani.

Tunaongea kwa uchungu, Mheshimiwa Rage, ameongea, Mheshimiwa Zedi ameongea, lakini bado Mheshimiwa kuna haja ya kuikumbusha Serikali, kitu kikubwa

hapa ni kasi. Kweli barabara zimeanza, lakini zimesimama, tunaomba kasi iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninasema kuhusu kuchangia, asilimia 65 ya tumbaku yote inayolimwa katika nchi hii inatoka Mkoa wa Tabora na inaiingizia nchi hii kila mwaka zaidi ya dola milioni 240 za Kimarekani. Ukibadilisha kwa fedha za Tanzania, maana yeke ni shilingi bilioni 400, kila mwaka na tungeliweza kutokana na Taarifa ya Wachumi tungeweza kufikisha hata bilioni 600 kwa mwaka. Kinachochangia kimojawapo ni ubaya wa miundombinu. Tunaomba, Serikali iongeze kasi, ndiyo ombi letu, Barabara zote zinazotoka Nzega kuingia Tabora, zinazotoka Itigi kuingia Tabora zote zimesimama. Kazi imesimama kwa sababu ya malipo, tunajua Serikali yetu inajitahidi sana, inatumia fedha za ndani. Pamoja na juhudi zote za Serikali, tunaomba hata ikibidi wakope barabara hizi zikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya kutoka Ndono - Urambo ilikuwa iishe mwaka 2012, imesimama hakuna kinachoendelea. Mheshimiwa Rais, alipokuja Urambo, tarehe 9 Januari, mimi mwenyewe nilisimama mbele ya mkutano wa hadhara nikasema Watu wa Urambo wana swali moja tu, Mheshimiwa Rais wetu, tunakuheshimu na tunakupenda; lini Barabara ya Urambo itaisha?

Ninamwomba kwa heshima Mheshimiwa Magufuli, utujibu leo Watu wa Urambo walale usingizi. Wanashindwa kupata fedha za kutosha kutokana na Tumbaku.

Mheshimwia Naibu Spika, tumbaku inatesa watu, tunaingiza dola milioni 240 za Kimarekani kila mwaka, kutokana na jasho la wakulima. Kuchoma tumbaku siyo rahisi, afya za watu zimeathirika, lakini pia hata hawa wanaonunua tumbaku wanaongezea bei ya pembejeo kwa sababu ya kutumia barabara, reli haifanyi kazi, treni inakwenda mara mbili kwa wiki, ndege hakuna, wanategemea barabara tu. Sisi wenzenu tukifikiria kwenda Tabora, la kwanza unafikiria nitaendaje, ndege hakuna, reli

inafanya kazi mara mbili kwa wiki na barabara zote ni za udongo.

Mpaka ninakumbuka maneno ya Mheshimiwa Said Nkumba, aliyoyaongea humu kwa niaba ya Wabunge wote kwamba, mtoto anazaliwa kwenye udongo, anakua kwenye udongo, anakufa na kuzikwa katika udongo, mpaka lini? Mheshimiwa Magufuli, ninakuheshimu, kazi yako ni nzuri sana, lakini Mkoa wa Tabora tumechoka kuteseka, miaka 50 baada ya Uhuru barabara zote ni za vumbi. Nani hapa asimame ambaye barabara zote zinazoingia Makao Makuu ya Mkoa wake ni udongo, asimame Mbunge aseme. Atakayesema ni wa mikoa mipya tu, lakini kwa mikoa ya zamani nani hapa ana barabara ya vumbi inayoingia kwenye Makao Makuu ya Mkoa wake?

Wewe hapa mkoa wako ni mpya, kaa. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wetu umechangia maendeleo ya elimu ya viongozi wakubwa wengi kama Marehemu Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Jaji Ramadhani, Mheshimiwa Jaji Samatta, ambao wamesoma Tabora. Tumechangia elimu, tumechangia uchumi, lakini bado hatuna hata barabara moja ya lami. Mheshimiwa, ninakushukuru umegeuka unaniona ninaongea kwa uchungu, Tabora hatuna hata barabara moja inayoingia Makao Makuu ya lami, ni sawa na ninyi?

Watoto wetu hawajaona lami. Mheshimwia Magufuli, ninakusihi, ninakuomba, Mkoa wa Tabora, Wabunge wote ni CCM, lakini hatuna hata barabara moja inayoingia Makao Makuu. Ninyi wenzetu upande wa Upinzani muwe mnashukuru, Serikali yetu hii haibagui, mnapata barabara za lami, mnafurahi halafu mnakashifu, shukuruni, sisi wenzenu hapa hatuna hata barabara moja muwe mnashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusisitiza kuwa, Tabora hatuna barabara hata moja ya lami, baada ya miaka 50 ya Uhuru, licha ya kuchangia uchumi wa nchii hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mama. Kwa kweli Tabora wamesikia na kilio cha Tabora Mheshimiwa Magufuli amekisikia, hata kule Kongwa Wapinzani walikuwa huko wiki iliyopita, walisema hii ndiyo barabara ya Naibu Spika hii, vumbi tupu. Wamenichapa kweli huko. Ndugu yangu barabara ya Naibu Spika ndiyo ile, namna ile vumbi tupu, sina hata pa kupitia maana hoja nzito ipo shingoni hapa, kwamba ndiyo Barabara ya Naibu Spika hii. *(Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba nzuri, lakini sijaona Barabara ya Arusha – Usa River *(Nelson Mandela Institute of Science and Technology).* Siku ya ufunguzi, Mheshimiwa Rais alisema, itakuwa kwenye Bajeti ya mwaka 2013/2014 na ile ya Tengeru kushuka mpaka Nelson Mandela – Arumeru – Arusha.

Tafadhali, je, Kitabu kimekuwa kikubwa?

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Ujenzi. Sambamba na pongezi hizo, zipo changamoto katika baadhi ya barabara zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa, naelewa ni fedha nyingi sana zinatumika kujenga barabara hizi, isipokuwa wasiwasi wangu ni juu ya baadhi ya barabara ambazo mara tu baada ya ujenzi, kabla hata ya mwaka mmoja, barabara zimeshabomoka. Je, Wizara inawachukulia hatua gani makandarasi wanaosababisha hasara kama hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Arusha zipo baadhi ya barabara ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa Kampeni mwaka 2010; Wilayani Arumeru aliahidi kujengwa barabara ya lami toka Njia Panda ya Ngaramtoni hadi *Selian DDH* na barabara za Wilaya hizo zingetengenezwa kwa kiwango cha changarawe ili zipitike mwaka mzima. Akiwa anazindua Hospitali ya Wilaya ya Olturumet aliahidi kuwa atasaidia ujenzi wa barabara ya lami toka Redio Habari Maalum hadi Olturument; mpaka sasa hakuna mradi hata mmoja ulioanza. Wananchi wanateseka sana na hasa wanawake wanapata tabu nyingi sana, wanatembea kwa miguu; je, ni lini sasa Serikali itatekeleza miradi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Barabara ya Arusha – Losinyai – Simanjiro – Kibaya – Kongwa (Dar es Salaam – *Dodoma Road Junction*), ipo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano; ni lini barabara hizo zitaanza kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SLYVESTER M. MABUMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa mizani za barabarani, kwani panakuwepo usumbufu kwa wasafiri wanaotumia mabasi. Vilevile bado kuna watumishi kwenye mizani ambao siyo waadilifu, mapato mengi ya Serikali yanapotea kutokana na kukosekana kwa uadilifu kwa baadhi ya watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Serikali kupitia Wizara hii ya Ujenzi, kuhakikisha inakamilisha kwa wakati ujenzi wa barabara ambazo ujenzi wake umekwishaanza. Kukamilisha ujenzi wa barabara hizi, una manufaa mengi; kwanza, utasaidia kuwaondelea Wananchi kero ya usafiri; pili, itaokoa fedha nyingi za umma kutokana na riba zinazodaiwa na wakandarasi; na tatu, itawezesha Serikali kuanza Miradi mingine mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilete Muswada tutunge Sheria kali dhidi ya watu wanaoiba alama za usalama barabarani kwa ajili ya biashara ya vyuma chakavu, hali ambayo imechangia kuwepo kwa ajali nyingi na kugharimu maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iiangalie kwa moyo wa huruma Barabara ya Nzega – Kahama kupitia Tarafa ya Itobo – Mwamala – Igusule – Kagongwa. Barabara hii ni muhimu sana, kwani Wananchi wa Kahama hulazimika kupitia Tinde na hivyo kuwalazimisha kuzunguka pasipo sababu yoyote kutokana na barabara kuwa mbaya na haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kahama ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kahama inayo migodi mikubwa miwili ya dhahabu lakini barabara zake zote ni za vumbi, hali ambayo ni kuwanyima fursa Wananchi kufurahia matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akija kufanya majumuisho, awaambie Wananchi wa Wilaya ya Kahama, barabara zao zitafanyiwa upembuzi lini ili kazi ya ujenzi ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Wizara ituangalie kwa huruma kwa kutoa ushirikiano kwa Barabara za Zanzibar kwani Zanzibar ina eneo dogo na hivyo kuisaidia kutaimarisha zaidi Muungano wetu.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi inafanya kazi nzuri sana inayoonekana na watu wote kote Tanzania, Mungu awatie nguvu mwendelee na kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na mengi nilizungumza ndani ya Kamati, naomba nikumbushe machache ambayo niliyasema kwenye

Kamati kwenye Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ya ziada kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano barabara za Dar es Salaam, Daraja ya *Salender,* Reli Gerezani nilieleza kwa kina sana juu ya umuhimu wa madaraja hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya boti toka Bagamoyo mpaka Dar es Salaam hayataondoa msongamano uliopo sasa. Kazi nzuri sana imefanyika na *TANROAD* baada ya Wizara kukubali kuchukua Barabara za Dar es salaam ambazo kwa kweli Manispaa haziwezi kuzihudumia, lakini pia ikitiliwa maanani kuwa Dar es Salaam ni kwa kila mtu. Kazi hii nzuri ya barabara zote za Wilayani inachafuliwa na hali ilivyo kwenye madaraja hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *flyover* haiendi Mjini katikati. Ninafahamu kutakuwa na *flyover page* Daraja la Gerezani, lakini watu wengi wanakwenda katikati ya Mji na si *TAZARA.* Ninaomba Wizara ilichukue hili na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara zinatakiwa kufanyiwa kazi ili kubaini sababu ya kuharibika mara kwa mara. Hizi ni barabara za Morogoro – Dodoma – Chalinze – Dar es Salaam, zimetengenezwa hivi karibuni lakini sasa hivi hali yake ni mbaya na zinaweza kuleta ajali mbaya sana. Je, sababu ni lami hafifu, ubovu wa wakandarasi au magari makubwa yaliyozidi ama hali ya ardhi haikutiliwa maanani wakati wa ujenzi? Suala hili ni muhimu, lazima lipatiwe ufumbuzi kunusuru fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kunduchi – Ununio – Boko ni mbovu hasa mwanzoni Kunduchi ni ya kiwango cha chini sana. Imeharibika hata kabla ya kumalizika. Niliona mkandarasi karudia lakini amefanya vibaya sana kuliko ilivyokuwa mwanzo. Ninaomba Wizara kupitia *TANROADS* Dar es Salaam, kuifanyia kazi sehemu hii maana inaendelea kuharibika kwa kuendelea kumegeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kujenga nyumba na *Canadian Village* ili kutoa makazi ya Wananchi na hususan Wafanyakazi wa Serikali na wengine kwa ujumla. Ninaomba nyumba hizo ziwe za bei zinazoweza kumudiwa na wafanyakazi hasa vijana wanaoanza kazi baada ya kumaliza vyuo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipewa kijiji kilichokuwa Makazi ya Canada, *Canadian Village* pale Masaki. Kijiji kile sasa hivi ni pori, nyumba zimehujumiwa na imekuwa vichaka na makazi ya wezi, walevi na wahalifu wengi. Nimesikia kuna kesi; hivi kesi hii kwa mali yetu ikoje? Nani atalipa fidia ya uvamizi na hujuma ya kung'oa vitu vyote vya nyumba hizo? Ninajua kwa utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri, ana uwezo wa kuokoa mali hii ya Serikali. Ninaomba aingilie kati ili lifike mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara za Dar es Salaam umesimama, hivi sasa ukipita katika barabara karibu nyingi ni kama vile kazi zimesimama. Naomba tujue je, ni kwa ajili ya malipo au ni nini? Nina wasiwasi kama watamaliza kama ilivyo kwenye ratiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote na naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya Bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba nitoe maombi yangu ya ujenzi wa barabara kama ifuatavyo:-

(a) Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Serikali imekuwa ikiahidi kuanza kujenga barabara kwa kiwango cha lami baada ya kukamilisha hatua zote lakini kazi hii haijaanza kutekelezwa hadi sasa. Ieleweke kwamba, barabara hii ina

umuhimu mkubwa kutokana na vitega uchumi muhimu sana vilivyoko katika maeneo ya Katumba, Mwakaleli, Ikama na Kyejo, kwa viwanda vya chai na viwanda vya gesi. Pia ieleweke kwamba, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kukarabati barabara hiyo kutokana na wingi wa mvua na udongo wake ni wa *volcano.* Dawa yake na suluhisho lake ni kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, tunaipongeza Wizara kwa kukamilisha hatua za awali mapema sana, hivyo kilichobaki ni kuanza kujenga tu.

(b) Jiji la Mbeya kama ilivyo kwa Majiji mengi, msongamano wa magari mengi makubwa ya mizigo unaleta adha kubwa kwa watumiaji wa barabara hii. Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mbeya kilipendekeza kuwa na barabara ya nyongeza kutokea Mlima Nyoka kupitia Uyole ya zamani Iyunga na kuendelea hadi Mbalizi. Mapendekezo haya yatarahisisha usafiri, kuokoa muda na fedha, vinavyopotea wakati wa safari zinazopitia Jiji la Mbeya. Tunaomba Serikali ilione ombi hili kuwa ni la muhimu.

(c) Pamoja na juhudi kubwa ya ujenzi wa barabara mpya, kiwango cha ubora wa barabara hizo nyingi siyo nzuri sana. Nina shaka kama viwango vya vifaa vinavyotumika katika ujenzi huo ni imara vya kutosha. Kwa ujumla, tunaomba wataalam wasimamizi (*consultants*) wa barabara zinazojengwa wasimamie ujenzi kwa makini sana. Mfano ni Barabara ya Morogoro – Dodoma karibu na Gairo, maeneo ya Ruvu karibu na Daraja la Ruvu katika Barabara ya Dar es Salaam – Morogoro. Kutozingatia ubora wa barabara hizo ni kupoteza fedha za umma kwa kujenga barabara mara kwa mara. Uharibifu mwingine unatokana na matawi ya miti magogo na kadhalika ambayo huachwa barabarani na madereva wanaoharibikiwa na magari yao. Nashauri Wizara ya Ujenzi iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Ndani (Usalama Barabarani), kuwachukulia hatua madereva wote wanaotupa matawi au miti na majani ambayo yanaharibu barabara. Hakuna nchi yoyote hapa Duniani wanaotumia majani, matawi, magogo na matuta, kama alama za barabarani. Naomba hatua za haraka za kuchafua na

kuharibu barabara na kupiga marufuku kabisa matumizi ya alama za barabara zisizoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo mfupi, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Ujenzi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kupanua barabara ili kurahisisha mawasiliano na kupunguza msongomano katika Miji mikubwa hasa Dar es Salaam, jitihada hizo zinakwenda taratibu sana; hivyo, kupelekea usumbufu mkubwa sana kwa Wakazi wa Dar es salaam. Je, ni lini sasa Mradi huo utakamilika haraka na kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini barabara kwa kiwango cha lami kati ya Njiapanda – Mangola Karatu itajengwa kwa kuwa pia ujenzi huo kwa kiwango cha lami ni ahadi ya Rais wakati wa kampeni ya uchaguzi 2010? Je, ahadi hii ilikuwa ni lengo tu la kuwahadaa Wananchi ili wamchague Rais? Naomba kufahamu ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa? Naomba majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inajaribu kuangalia na kuweka nguvu kubwa kwa upanuzi wa barabara Jijini Dar es Salaam, ni jambo jema, lakini kwa jinsi Miji mikubwa inavyopanuka na kukua, ndivyo ambavyo msongamano unavyozidi. Miji kama Arusha, Mwanza na Mbeya ni Miji inayokuwa sana hivyo tutaraji miaka kumi ijayo hali katika Miji hiyo itakuwa kama ilivyo sasa Dar es Salaam. Je, Wizara inajipanga vipi kuwa na mipango endelevu inayodhibiti msongamano mkubwa unaotarajiwa miaka ijayo? Wizara ituambie nini mkakati wake iliyojiwekea?

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007 inatamka bayana ni kwa namna gani Serikali italipa fidia kwa ardhi iliyoichukua toka kwa Wananchi. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana toka kwa

Wananchi kwamba, hawatendewi haki pale ambapo wanakuwa wanastahili. Kama ambavyo Kamati ya Miundombinu pia imeona, Sheria hii ya 2007 ina mikanganyiko kwani haitekelezwi ipasavyo, maana inachukua yale yaliyopo kwenye Sheria ya Ardhi ya 2002 na hivyo kuchelewesha ulipaji wa fidia unaoitaka Serikali ilipe na ndani ya Mikoa sita baada ya kutoa *notice* ya kuchukua ardhi, pande mbili ziwe zimekubaliana na kiwango cha fidia kilichokubaliwa kutolewa. Sheria hii kwa kumkataza mmiliki wa ardhi kuitumia baada ya kutoa *notice* ni adhabu kwa mmiliki huyu. Kwa kuwa tathmini huweza kuchukua muda mrefu baada ya kutoa *notice* na pia fidia kuchukua muda mrefu, hii inapelekea thamani ya fedha kushuka pindi fidia inapotolewa na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa Wananchi. Naishauri Serikali kuzingatia umuhimu wa kuwasaidia Wananchi na si kuzidi kuwafanya wawe maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wakandarasi wa kigeni pamoja na wa ndani (wazawa), wameonesha udhaifu mkubwa katika utendaji kazi wao na hivyo kulipelekea Taifa hasara na usumbufu mkubwa kwa Wananchi. Si wakandarasi tu, bali pamoja na wahandisi washauri, ambao wamekuwa wakifumbia macho udhaifu wa wakandarasi, aidha kwa makusudi au kwa kutokuijua kazi yao vizuri na hivyo kusubiri mpaka uharibifu utokee baada ya kazi kukamilika na mkandarasi kukabidhi kazi na kupewa malipo yake. Mfano mzuri ni mkandarasi aliyekuwa anajenga Barabara ya Sekenke – Shelui, yenye urefu wa kilomita 33.3, Kampuni ya *CHICO Limited* chini ya Mhandisi Mshauri *BCEOM* (Ufaransa), akisaidiana na Mhandisi Mshauri - *M-Konsult Limited* (Mtanzania). Pamoja na kwamba barabara hii ilikamilika mwezi Januari, 2008, barabara hii iliharibika muda mfupi tu baada ya kukabidhiwa. Mbaya zaidi, pamoja na mkandarasi huyo kupewa adhabu ya kurudia kazi hiyo kwa gharama yake mwenyewe, cha kusikitisha mwezi Januari, 2013 Daraja la Msisi lilisombwa na mvua na hivyo kuleta hasara kubwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi na wasafiri.

Daraja hili kabla ya kujengwa upya, lilidumu kwa takribani miaka 15 tangu lilipojengwa mwanzo. Sasa ni kwa

vipi huyu *CHICO* ajenge daraja kwa miaka minne tu na lisombwe lote kama si udhaifu na kutokuwa na utaalam wa kutosha wa kazi yake? Kwa nini watu hawa pamoja na wahandisi washauri wasifutiwe vibali vyao hasa Mtanzania na hawa wageni wasipewe *tender* nyingine tena ya kujenga barabara zetu? Kwa kuwaacha waendelee kubaki pale hata kama ni kwa gharama zao si ni kuendelea kuharibu zaidi? Kwa nini wasingelipa fidia na kurudisha fedha ili mkandarasi mwingine atafutwe kufanya kazi hiyo?

Inasikitisha sana kuona kwamba, Serikali inakuwa ina nia njema ya kuwaletea watu wake maendeleo, lakini inakwamishwa na wachache wasioitakia mema nchi yetu. Zaidi ya hayo, naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kutujengea barabara Mkoa wetu wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa iliyofanya katika ujenzi wa barabara nyingi kwa kiwango cha lami na kufungua njia za Mikoa mbalimbali nchini, ambapo imefungua milango ya kiuchumi kwa Taifa letu. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, kuna tatizo la foleni kuanzia Chalinze – Dar es Salaam. Kama mpango huo wa kujenga *express way* utafanyika haraka, itasaidia kwani sote mashuhuda muda wa Dodoma – Chalinze haulingani na muda wa safari Chalinze – Dar es Salaam, pia itapunguza foleni ya Kibaha mizani.

Je, daraja linalokatisha Mto Ruvu kwenye barabara itokayo Msata – Bagamoyo litajengwa lini kwani hata wakati wa uwekaji Jiwe la Msingi wa barabara hiyo ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alishauri daraja hilo lijengwe haraka na mvua za msimu huu palijaa

maji? Naomba nielezwe lini daraja litajengwa ili lilingane na hadhi ya barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufungua barabara nyingi kwenye Mikoa, naomba Serikali ifikirie kufungua njia nyingine ambayo itakuwa mbadala wa Barabara ya Morogoro endapo (kitu ambacho hatuombei), Daraja la Ruvu litakuwa lina matatizo yoyote, barabara hiyo inaweza kupitia Vigwaza – Kwala – Mzenga – Kisarawe.

Ukarabati wa mara kwa mara wa Barabara ya Mpuyani – Vikumburu (Wilaya ya Kisarawe) ni kuiingizia gharama zaidi Serikali. Tunaomba ujenzi wa lami uanze haraka sana. Hali kadhalika, Nyamwage – Utete. Je, ujenzi au ukarabati wa daraja linalounganisha Barabara ya Kilindoni – Kigamboni Wilaya ya Mafia utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Chanika Wilaya ya Ilala – Msimbu Wilaya ya Kisarawe ni kiunganishi kizuri cha mawasiliano, tatizo upande wa Chanika barabara ni mbovu sana; je, itajengwa lini? Naomba jibu.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi, kwa Hotuba yake nzuri. Napenda pia kushukuru kwa kuhakikisha kuwa, Barabara ya Dumila hadi Rudewa inakamilika katika mwaka wa 2013/2014. Hata hivyo, ningependa kupata ufafanuzi ufuatao:-

Ukurasa wa 16 unaeleza kuwa, urefu wa Barabara ya Dumila – Kilosa ni kilomita 63 (45 Dumila – Rudewa na 18 Rudewa – Kilosa).

Ukurasa wa 81 unaonesha urefu wa Barabara hiyo hiyo (Dumila – Kilosa) kuwa kilomita 78. Dumila – Rudewa bado ni kilomita 45. Umbali wa Rudewa Darajani hadi Kilosa Mjini ni kilomita 23; hizi kilomita 33 barabara hii itapitia wapi? Naomba mtafakari ili kupata gharama halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango kazi wa takribani miaka mitatu iliyopita, kuna barabara inayotoka Usagara hadi Kisesa, imepangiwa ujenzi kwa kiwango cha lami. Je, mpango huo utatekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pia pongezi kwa Wizara hii kwa kupokea kilio cha Wananchi wa Mabatini Mwanza cha ombi la daraja la juu *(fly over bridge);* nasema wanashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero kubwa sana katika maeneo yaitwayo "Katika Mzani." Maeneo hayo yangejengwa kutoa kipaumbele usafiri wa mabasi. Kinachotendeka ni ushindani wa gari gani iliwahi mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES F. MBATIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo ya kina kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa Barabara ya Kawawa – Pakula – Nduoni (Vunjo), kwa zaidi ya miaka mitatu sasa na kusababisha usumbufu na adha kubwa kwa watumiaji wa barabara hii.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya Wizara hii nyeti ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayofanywa katika Wizara hii ni nzuri na inapaswa kuigwa na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuelekeza mchango wangu kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ahadi na Ilani ya CCM ya 2005 – 2010 na 2010 – 2015, juu ya Ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami

ya kilometa 15 kutoka Igawa – Madibira –Mafinga, Kinyanambo A.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ipo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini kwa masikitiko makubwa, Serikali haijaonesha nia ya kutaka kutekeleza ahadi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni pigo kubwa hasa kwa Wabunge wanaotoka Majimbo ya Mufindi Kaskazini na Jimbo la Mbarali – Mkoa wa Mbeya. Ni vyema Serikali ikatekeleza ahadi zake ambazo ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ninalotaka kupata majibu ni juu ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais, juu ya uwekaji wa lami kilomita mbili pale Mafinga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mpaka sasa kilomita 1.6 imeshajengwa kwa kiwango cha lami, bado kilomita 0.4 na ni miaka miwili imepita; ni vyema Mheshimiwa Waziri akamaliza jukumu hili la ahadi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ninalotaka kuchangia ni suala la kuwalipa fidia Wananchi wanaopaswa kulipwa fidia katika Barabara ya Kinyanambo A – Madibira. Wananchi hawa wanaishi kama wakimbizi katika nchi yao wenyewe, Serikali imewataka Wananchi hawa wasiendeleze maeneo haya na fidia hawapewi, kwa hiyo, hawaijui hatima ya maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba kaka zangu; Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Eng. Lwenge, wajitahidi kadiri ya uwezo wao, kuhakikisha Serikali inalipa fidia za Wananchi hawa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ninalopenda kuchangia ni barabara ya John’s Corner - Mtili – Mgololo, ambalo ndipo vinapopatikana viwanda vikubwa na vinavyochagia pato kubwa katika uchumi wa nchi yetu; kuna Viwanda vya Karatasi *(MPM),* pamoja na viwanda vingi vya

chai. Ni vyema sasa Serikali ikajenga barabara kwa kiwango cha lami.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa kujenga barabara za lami kwa kiwango cha juu na nyingi zinaonekana. Pamoja na pongezi, nakumbusha mwaka jana tulihakikishiwa kwamba, fedha zimepatikana na Barabara ya Babati - Kondoa hadi Dodoma itakamilika mapema. Sasa naomba kujua ni kitu gani kilichotokea mpaka barabara isiendelee kujengwa?

Sasa kilichobaki ni kuulizwa maswali na Wananchi hatuna cha kujibu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake ni wachapa kazi, tuna uhakika mwaka huu itakamilika, tunawaamini. Tunaomba maelezo ya Barabara ya Babati - Kodoa - Dodoma - Iringa

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunaomba vilevile Barabara ya Mbande kwenda Kongwa msiisahau.

Barabara ya kutoka Gaira mbele kidogo ilifanyiwa ukarabati muda mrefu sasa inaanza kubonyea, tunaomba mpaangalie.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Natoa shukrani na kuipongeza Wizara, kwa juhudi za kuanza ujenzi wa Daraja la Sibiti. Kimekuwa kilio cha Wananchi cha muda mrefu, hatimaye Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetimiza, Wananchi wanatoa shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri binafsi na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Wizara na Watendaji wote, kwa juhudi wanazozifanya kuhakikisha barabara za nchi nzima zinapitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais anaomba kura, aliwaahidi Wananchi wa Iramba Mashariki, Wilaya mpya ya

Mkalama, kuwa barabara inayoingia Makao Makuu ya Wilaya Nduguti inawekwa lami nyepesi toka Iguguno hadi Nduguti. Vilevile kipande cha barabara cha Iguguno - Shamba pia kitawekwa lami. Katika Bajeti ya mwaka jana, kipande hiki Mheshimiwa Waziri aliahidi kuweka lami, lakini hadi sasa tamko hili halijatekelezwa. Je, ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa? Ikumbukwe imekuwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuunga mkono hoja iliyotolewa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Ujenzi, ikiongozwa na Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali, naomba ihakikishe kwamba, inamsukuma mkandarasi wa kipande cha Barabara ya Tunduma – Sumbawanga. Eneo la Tunduma - Ikone kasi yake ni ndogo sana, haijulikani tatizo ni nini na umegharamiwa na pesa kutoka Mfuko wa *MCC*. Hivyo, kutokana na tatizo la pesa, tofauti na vyanzo vingine vya pesa, naomba Serikali ihakikishe kwamba, Mkandalasi anahimizwa akamilishe kazi na inakamilika kwa wakati kwa mujibu wa Mkataba na si kutoa visingizio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, naomba niongelee msongamano mkubwa wa Mpaka wa Tanzania na Zambia Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linaweza kupunguzwa na kuondoshwa na kuongeza mzunguko wa kibiashara kwa kuhakikisha Vituo vya Kasesha na Mosi

Customs vinafanya kazi na hivyo kupunguza msongomano kwa kutomlazimisha msafirishaji anaeenda Zambia maeneo ya Mbala, Mpulungu na yale wa Congo kupitia Mpaka wa mwisho wa Ziwa Tanzania kulazimika kupita Mpaka wa Tunduma badala ya njia fupi kwa kupitia Mpaka wa Kasesha na Mosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ihakikishe njia fupi kabisa maarufu kama Barabara ya Zamani ya Myevumani, ambayo imeunganisha Mkoa wa Mbeya na Rukwa na pia kuunganisha Bandari ya Kasanga, kiungo cha Nchi ya Burundi na Congo DRC. Naomba Wizara ichukue kipande kilichobakia upande wa Mbeya kwa kuchukuliwa na *TANROADS.*

**MHE. MCH. DKT. GERTUDE P. RWAKATARE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Pongezi nyingi kwa Wizara na Watendaji wote kwa kazi na juhudi tunaziona.

Mimi ninotoa shukrani kwa Daraja la Mto Kilombelo. Pia nashukuru kwa Barabara ya Kidatu – Ifakara – Londo. Nashukuru mara mia moja. Ujenzi Oyee!

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kigoma – Nyakanazi kilometa 310.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua kutangazwa kwa Barabara ya Kidahwe – Kasulu ili hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, kipande hicho kimeshatangazwa, lakini bado mnahoji ni lini barabara yote ya Kigoma – Kidahwe – Kibondo –Nyakanazi itajengwa kwa kiwango cha Lami? Serikali imekuwa ikitenga fedha za bajeti hazitolewi. Mfano, 2010/2011 zilitengwa shilingi bilioni sita lakini hazikutolewa. Mwaka 2011/2012 zilitengwa shilingi bilioni 12.3 hazikutolewa. Mwaka 2012/2013 zilitengwa shilingi bilioni 3.5, lakini pia hazikutolewa. Mwaka 2013/2014 imetengwa shilingi bilioni kumi; je, zitatolewa? Hali hiyo inatia

hofu kama kweli kipande kilichotangzwa kitapewa fedha ili kikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kidahwe – Kasulu hadi Kibondo – Nyakamazi ni muhimu sana, inatuuganisha Wilaya zetu za Mkoa, lakini inatuunganisha na Mkoa wa Kagera na ni rahisi kufika Kahama, Shinyaga. Hivyo, ninashauri Serikali iifikirie barabara hii. Huo mpango wa kutengea pesa kidogo kidogo lakini hamzitoi muuache na mtekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Kigoma – Kidahwa – Nyakanazi ni ya 1932, muda mrefu kabla Sheria Mpya ya Barabara haijaanza. Hivyo basi, Wananchi walio pembezoni mwa barabara hii walipwe fidia, kwani Sheria hiyo mpya imewakuta Wananchi. Naomba Serikali itoe ufafanuzi juu ya ulipaji fidia nyumba zote zilizowekwa X. Vijiji vingi vinavyoambaa ambaa katika ile barabara ni Vijiji vya Ujamaa, vilipangwa vizuri ingawa Sheria ya sasa inahitaji watu wajenge umbali wa mita 30 kutoka barabarani kwa pande zote mbili. Hivyo, nasisitiza kwa kuwa Sheria imetungwa wakati Wananchi wanakaa hapo kabla ya Sheria hiyo, tafadhali walipwe stahiki zao kabla ya barabaraa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulikuwepo mpango wa kupata pesa za ujenzi wa barabara hiyo ya Kigoma – kidahwe – Kibondo – Nyakanazi, kwa kiwango cha lami kwa fedha za *ADB (Africa Development) Bank.*

Mheshimiwa Naibu Spika naomba Waziri akitujibu atueleze huo mango wa kupata fedha za *ADB* upo au la? Je, kuna mpango gani sasa wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? Kwa kuwa Serikali ya CCM inasema ni sikivu, basi itusikie na sisi Wananchi wa Kigoma tunahitaji barabara hiyo ni muhimu sana kwetu. Bado miaka miwili ya Serikali ya Awamu Nne imalizike muda wake. Hivyo, ahadi itimie, ni ya Rais kabla muda wake kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Barabara ya Mwandiga – Mwangongo – Kagunga, pesa za *feasibility study*

tayari na tumeshaomba ipandishwe hadhi, tayari ni barabara ya *TANROAD* na Mheshimiwa Waziri alishakubali kwenye Kamati ya Miundombinu. Nasikitika katika Hotuba haijatajwa na wala haijawekewa makadirio yoyote. Je, nia ipo kweli? Barabara hii itakuwa kiungo kati ya nchi yetu na nchi jirani ya Burundi, eneo la Nyanza na Rumonge. Itasaidia Wananchi kuepuka adha ya maboti yanayochukua muda mrefu kutoka Kagunga hadi Kigoma Mjini. Vilevile itasaidia watalii kutoka nchi jirani kuingia kwetu pale Gombe kirahisi, kwani wapo wasioamini usafiri wa majini kwani maboti hayaaminiki.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 20, ukurasa wa 11 wa Hotuba ya Waziri wa Ujenzi kuhusu Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014; ni lini uchambuzi wa mapendekezo ya makampuni 19 kuhusu utaratibu wa ubia wa ujenzi wa Dar es Salaam - Chalinze Express Way utakamil*i*ka; na je, ni lini ujenzi utaanza?

Kwa upande wa Wakala wa Majengo *(TBA)* na utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi, aya ya 67 ukurasa wa 45 na 110 ukurasa wa 72. Kuhusu ujenzi wa nyumba za Makazi ya Viongozi na Watumishi wa Umma; je, kuna viwanja vingapi viko ndani ya Jimbo la Ubungo? Kutokana na viwanja hivyo, ujenzi umepangwa kuanza lini? Aidha, katika nyumba hizo *(TBA)* iongeze idadi ya nyumba ambazo Wabunge wanaweza kupanga wakati wa Mikutano ya Bunge Dodoma. Toka mwaka 2011, mimi ni kati ya Wabunge tulioomba nyumba kwa ajili ya kupanga, lakini mpaka mwaka huu wa 2013 sijapatiwa. Wabunge kupanga kwenye Nyumba za Umma ni muhimu kwa usalama, ufanisi na pia kuchangia katika mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 81 – 82, ukurasa wa 54 – 70, juu ya Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA);* ni vizuri ukajikita katika majukumu ya ufundi. Wizara ya Ujenzi ishirikiane na Wizara ya Uchukuzi kuweka mfumo bora zaidi wa uendeshaji wa vivuko ikiwemo boti zinazotarajiwa kuanza kufanya kazi za kupunguza msongamano kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo. Kwenye aya ya 186, ukurasa wa 117,

kuhusu mpango wa matengenezo ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara sanjali na viambatisho Na. 5A hadi 5E, kwa barabara ambayo ilikasimiwa na Wizara kuhudumiwa na *TANROADS* na Mfuko wa Barabara, lakini haijatajwa popote hata katika randama na Kitabu kizima cha Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara hiyo ni ahadi ya Rais ya Mei, 2010 ya Kimara – Mavurunza – Bonyokwa mpaka Segerea, ambayo inaunganisha Wilaya mbili za Ilala na Kinondoni na ipo katika hali mbaya sana, pamoja na umuhimu wake katika kupunguza msongamano. Wizara ya Ujenzi ishirikiane na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kupanua wigo wa mapato maalum ya ndani na vyanzo mbadala kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Mfano, Mkoa wa Dar es Salaam tuliunda Kamati ya Halmashauri zote kuhusu kodi ya majengo *(Property Tax),* ambayo na mimi nilikuwa Mjumbe. Katika mapendekezo niliyotoa ni pamoja na mfuko wa sasa wa makusanyo unaofanywa na *TRA* ubadilishwe na hatua hizo zilichukuliwa, Halmashauri ziweke kipaumbele kwenye ujenzi wa barabara. Kwa uhakika wa vyanzo hivyo, Halmashauri ziwezeshe kujidhamini kukopa, kujenga na kulipa baadaye.

**MHE. MARGARET S. SITTA**: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza kwa uchungu Barabara ya Urambo kutoka Ndono itaisha lini? Imekwama ilikuwa iishe mwaka 2012. Tupeni matumaini lini inakwisha? Kopeni fedha mmalize.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko kadhaa kuhusiana na Wizara hii, ambapo malipo ya fidia kwa Wananchi hawa yanacheleweshwa ama kutolipwa fidia Wananchi hao kabisa. Wizara hii imeshawahi kutoa maelekezo kuwa, Wananchi waliojenga pembezoni mwa barabara ambapo wao wameikuta barabara hawatolipwa fidia na wale ambao barabara imewakuta watalipwa fidia. Naomba Mheshimiwa

Waziri atakapofanya majumuisho yake, anieleze mambo yafuatayo:-

(i) Barabara ya Ngongo hadi Milola iliyopo upande mmoja wa Jimbo la Lindi Mjini na upande wa pili wa Jimbo la Mchinga inamilikwa na nani?

(ii) Kumekuwepo na taarifa kuwa baadhi ya Wananchi hasa katika Jimbo la Mchinga watalipwa fidia ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo ilihali Wananchi wa Jimbo la Lindi Mjini hasa maeneo ya Ng'apa, Narumu na Tandangongoro hawatalipwa fidia. Hivyo ni vigezo gani vimetumika katika ulipaji wa fidia hizo?

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake aeleze hatua zilizochukuliwa kwa wakandarasi ambao wameitelekeza Miradi mbalimbali ya Ujenzi kama mkdandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa barabara za Lindi Mjini *(VRB CONSTRUCTION),* ambapo amelipwa malipo yote na hajamaliza kazi yake. Sambamba na kufukuza kazi wafanyakazi wote walioonekana kufuatilia mafao yao. Mkandarasi huyo alipewa zabuni za ujenzi wa barabara za Jamhuri, Eliet, Baraza na Sheikhbad kwa kiwango cha lami, sambamba na kujenga mifereji katika barabara hizo.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake awaeleze Wananchi wa Kusini kuhusiana na kucheleweshwa kwa ujenzi wa Barabara ya Ndundu – Somanga, kilometa 60, ambapo Waziri alimtaka Mkandarasi huyo awe amekabidhi Barabara hiyo mwezi Oktoba, 2011. Tatizo ni nini na lini barabara hiyo itakamilika?

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alieleze Bunge lako Tukufu juu ya kazi ya umaliziaji lami pembeni mwa Barabara ya Mbwemkuru – Mingoyo, ambapo ilielezwa kuwa kazi hiyo ingemaliziwa na Wakala wa Barabara Mkoa, lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. Je, hakukuwa na ukweli

kuhusiana na hilo na kwamba mkandarasi alikwishamaliza kazi yake? Naomba maelezo.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI**: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo Wizara hii inafanya, Mheshimiwa Waziri na Timu yake ya Wataalam wanapaswa kuanza kutafakari suala la udumifu *(durability)* wa barabara za lami zinazojengwa. Suala hili linahusisha mambo mawili makubwa:-

(i) Viwango vya ujenzi wa barabara; barabara nyingi zimejengwa kwa kiwango cha chini cha ubora. Mbinu zipo sasa zitumike kuhakikisha kuwa barabara zinajengwa kwa ubora wa mfano kuanzia sasa.

(ii) Mpango wa matengenezo; barabara zenye urefu zaidi ya kilomita 11,000 zikishakamilika, zitahitaji mpango makini wa matengenezo. Wizara ianzishe Timu za Matengenezo za Kimkoa au za Kikanda ili pindi barabara inapoharibika, itengenezwe mara moja, badala ya kusubiri hadi ikalazimu barabara kujengwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitajielekeza Jimboni kwangu**.** Nitaanza na Barabara ya Uyovu – Bwanga, ambayo ni sehemu ya Barabara ya Uyovu – Biharamulo. Je, sehemu ya Uyovu – Bwanga itaanza kujengwa lini? Na mchakato wa kulipa fidia utaanza lini? Wananchi wanauliza sasa maswali haya na inafaa Serikali itoe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie madaraja ambayo hayawezi kujengwa kwa fedha ndogo inayopelekwa Halmashauri. Maeneo mengi hayafikiki kwa sababu kuna mito isiyo na madaraja. Wananchi wanapolima mazao na kuvuna, hawawezi kusafirisha mazao yao kwa magari; wanahangaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwasaidie Wananchi wa maeneo hayo ili nao wafaidi matunda ya Uhuru, wanachohitaji ni barabara za uhakika zinazopitika mwaka mzima. Kwa hatua ya kwanza, wakijengewa madaraja wao

wapo tayari kusesa njia ya barabara ili wapitishe mazao yao. Madaraja yanayohitajika ni haya yafuatayo: Daraja linalounganisha Namonge na Ilyamchele (kwenye Mto Mlele); Daraja la Busonzo – Nakayenze; Daraja la Msonga – Ludeba (Geita); Daraja la Namalandula; na Daraja la Nyikonga – Ipalamasa (Geita).

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja haya yakijengwa, yataleta mapinduzi makubwa katika uchumi wa maeneo haya, kwani kikwazo cha usafirishaji kitakuwa kimeondoshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamalizia kwa kuzungumzia tatizo lililotokea katika Kijiji cha Busonzo, linahusisha Shule ya Msingi ya Busonzo iliyo karibu na Mgodi wa Kokoto za kujengea barabara wa Kampuni ya Strabag, inayojenga Barabara ya Ushirombo – Lusahunga. Shughuli za krasha za Strabag zilisababisha jengo la darasa kupata nyufa. Shule na Serikali ya Kijiji wamfuatilia lakini mpaka sasa hawajafanikiwa kupata suluhisho la tatizo hili. Wizara inasema nini kuhusu jambo hili?

**MHE. RICHARD M. NDASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza sana Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Mto Simiyu, Barabara ya Musoma linacheza, limekatika kwa chini. Naomba hatua za dharura zichukuliwe ili kunusuru hali na mali za watumia barabara (Daraja hilo). Nashauri ikiwezekana kabla kazi hiyo ya dharura kuanza, wakati wa usiku kuanzia saa 12.00 jioni magari mazito yasiruhusiwe kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mara nyingine kwa kutenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya Daraja la Maligizu (Simiyu). Katika kitabu imesemwa kazi iliyofanyika ni asilimia 90, siyo kweli ni asilimia 70. Daraja hilo lina urefu wa mita 105 zilizokamilika, ni mita 60 bado mita 45. Kandarasi yuko *site* kukamilisha kazi iliyobaki, tatizo fedha

zinachelewa sana ndiyo maana kazi hiyo hadi sasa haijakamilika.

Ili Daraja hilo lidumu, naomba Mheshimiwa Waziri anapo-*approach* Daraja mita 50 na mita 50 kwa upande mwingine, ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuimarisha Daraja hilo; vinginevyo, kwa kasi ya maji ya Mto Simiyu yatasomba makalvati yaliyoko pembezoni.

Barabara ya Fullo – Nyambiti inayojumuisha Wilaya tatu ni ya muhimu sana kiuchumi, ni barabara ya siku nyingi, ni njia fupi ukitokea Mwanza kuelekea Sumve, Nyambiti, Malya, Malampaka au Maswa, Shinyanga na kadhalika. Naomba katika bajeti ya 2014/2015, zitengwe fedha za upembuzi yakinifu (usanifu), ili ijengwe kwa kiwango cha Lami. Kwa kufanya hivyo, utaunganisha barabara ya lami ya Usagara – Kisesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikuombe utekeleze ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais, wakati wa Kampeni 2010, Mjini Ngudu, alipoahidi kujenga kwa lami Barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Jojinzo – Hungumalwa ili kuungana na Barabara ya Mwanza – Shinyanga. Naomba Barabara hii itengewe fedha za usanifu mwaka 2014/2015 ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maombi yangu matatu makuu; barabara ya lami Fullo – Nyambiti, Magu – Hungumalwa na lami katika Daraja la Maligisu (Daraja la Ndassa).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu hawakutaja chochote kuhusu *PPP (Triple P)*, sisi wenyewe hatuwezi kujenga barabara zetu, uwezo ni mdogo, tunataka tujenge barabara za hewani *(flyovers).* Naomba Serikali itafute wawekezaji binafsi ili waweze kujenga barabara za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana *TANROAD* kwa kazi nzuri sana ya kusimamia fedha wanazopata, kwa kusimamia kazi ya ujenzi wa Barabara zote

Mikoani. Kipekee, nimpongeze Mhandisi wa Mkoa wa Mwanza, Eng. Kadashi, kwa usimamizi uliotukuka katika kusimamia Barabara za Mkoa wa Mwanza. Huwa anatoa maamuzi magumu kwa Makandarasi wasiofanya kazi kwa viwango, namtakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mwanza – Shinyanga Boarder na Nyanguge - Musoma zimetangewa fedha nyingi na zimekuwa zikitengewa kila bajeti, lakini hujengwa au hukarabatiwa kwa kiwango cha chini; nashauri wasimamizi wawe makini katika usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono pesa zilizoombwa za maendeleo, shilingi bilioni 845.2 zikatekeleze shughuli zilizoko mbele ya Wizara ikiwemo na shilingi milioni 200 za Daraja la Simiyu (Malipisu). Pamoja na fedha za maendeleo, nakubali zipitishwe pesa zote shilingi trilioni 1.226 ili Watumishi na Taasisi zilizo chini ya Wizara ziweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono.

**MHE. OMARI R. NUNDU**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, kwa sababu Serikali imefanya kazi nzuri na inaendelea kufanya hivyo kwenye ujenzi wa barabara. Hata hivyo, inabidi tuzitundulie barabara hizo, nami natoa ushauri ufuatao:-

Magari yanayozidisha uzito ambayo yamefikia asilimia 26 ya magari yaliyopimwa ambapo faini za bilioni nne zilipatikana, lakini huenda zisirudishe gharama za kutunza barabara hizo. Ushauri wangu, faini za kuzidisha uzito ziwe kubwa za kufanya wahalifu wasizidishe uzito na pia zipatikane pesa za kutosha kuzitunza barabara.

Matuta hayafai yanaharibu barabara na magari; hivyo, yaondolewe badala yake alama za spidi za magari ziimarishwe kwa kuwekwa kila panapostahili. Pia alama hizo ziwekwe katika hali ya kumuwezesha dereva kupunguza spidi

kiusalama badala ya kuweka alama ya 50 ghafla, ni vizuri kuanzia kama ifuatavyo kwa mfano 70 – 60 – 50.

Kumekuwa na matatizo ya malipo ya fidia ambayo imekuwa ni kero. Ninaishauri Serikali katika hifadhi ya barabara, iangalie miaka hamsini kutoka sasa na ipange jinsi barabara zitakavyokuwa wakati huo ili yajulikane yafuatayo na kupangiwa utekelezaji mapema:-

(a) Barabara zitakazohitaji lami nyingi hadi nane kama zile zinazounganisha Miji ya Wilaya kama Tanga – Pangani, Tanga – Korogwe na Tanga – Horohoro, zipangwe *road reserve* zinazokidhi mahitaji hayo sasa hivi ili kuepuka fidia kubwa miaka ijayo.

(b) Barabara za *highway* ambazo haziingii mijini zijulikane na *by pass* za kuingia mijini zijulikane, pamoja na kuwepo *flyovers* kwenye mipango. Barabara zinazojengwa sasa kama ile ya Tanga - Pangani - Bagamoyo ni vizuri zipangiwe taratibu hizo.

Katika mantiki hiyo, kwa Wilaya ya Tanga, kwanza, nashukuru kukamilika Barabara ya Tanga – Horohoro, pamoja na kuwalipa Wananchi fidia ambazo zilikuwa ni kero kubwa. Barabara hii haitakidhi haja baada ya miaka 50 ijayo; hivyo, tangu sasa ingewekewa *road reserve* inayohitaji lami nane na pia iwe ni *highway* ambayo baadaye lami nane hizo hazitaingia Jijini Tanga bali itaunganishwa moja kwa moja na barabara ya Tanga Korogwe. Haya pia yafanyike kwa barabara ambazo Wizara inashughulikia ujenzi wake kama vile Tanga – Pangani – Sadani – Bagamoyo. Barabara hii imekuwa inatajwa miaka mingi; hivyo, kusiwe na longolongo bali itekelezwe kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania alipozindua Barabara ya Tanga – Horohoro kwa kusema kuwa, barabara hiyo ipite Sadani kama ilivyopangwa awali, badala ya kutafuta njia mpya.

Nikitumia Wilaya ya Tanga kama mfano, badala ya kuingia Tanga, Barabara za Horohoro – Tanga, Muheza – Tanga na Pangani – Tanga zipite pembezoni ya Jiji

zikiunganishwa na kuwe na *by pass* za kuingia jijini. *By pass* hizo zitahusisha; kwa Tanga – Muheza zipitie Pongwe – Geza – Marungu ili kuiunganisha na Tanga – Pangani. Hali kadhalika, Majani Mapana, utoofu iiunganishe Tanga – Muheza na Tanga – Horohoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuunga mkono hoja kama nilivyoanzia.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mianya ya wizi wa fedha bado haijazibwa yote. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inayoishia Juni, 2013, inaonesha kwamba, Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam *(DARTS)*, wakala alitumia vibaya kiasi cha shilingi 169,381,739 kulipa posho ambazo hazikuwa na kibali cha Bodi ya Ushauri na kiwango hicho cha fedha hakikuoneshwa kwenye Bajeti ya Wakala kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni hatua gani za Kisheria zilichukuliwa dhidi ya ubadhirifu huo wa fedha kwa waliofanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayoishia Juni, 2012 kuna maelezo kwamba, Barabara ya Kigogo – Jangwani, kwa sababu ya ucheleweshaji wa kazi za mkataba kwa miezi saba, Mkandarasi - China *Civil Engineering,* ameleta madai ya fidia ya kiasi cha shilingi 174,573,138 na kwamba, Serikali haikupata manufaa na Mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara inayopatikana kutokana na ucheleweshwaji wa kazi za Mkataba; nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, kwa kazi nzuri katika mazingira magumu ya kukosa fedha, lakini

vilevile kwa Hotuba nzuri. Aidha, nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Kilindi, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa kutuangalia kwa jicho la huruma na kuzingatia changamoto kubwa za barabara Kilindi, ambayo hadi leo hakuna hata robo kilomita ya lami, lakini tumepewa nguvu ya kukarabati barabara zetu karibu zote. Tunasema ahsante sana, hapa kipekee, ninatambua pamoja na nguvu kubwa uliyonayo, pia nashukuru mchango mkubwa wa Bwana Mfugale wa *TANROADS,* mchapakazi mkubwa, Bwana Ndumbaro – Meneja *TANROADS* Tanga na Ofisi yake nzima. Mheshimiwa Wanyancha na Mrs Mmanga (Hajat), Bwana Matei, Katibu Mkuu na Mainjinia, kwa ushirikiano mkubwa kila ninapowafuata. Wananchi wa Kilindi wanakukaribisha wewe Waziri na Naibu Waziri wako, mfike Kilindi wawashukuru tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nikumbushe tu ahadi ya Rais ya mwaka 2010, ambayo aliirudia tena wiki chache zilizopita, alipokuja kufungua Barabara ya Horohoro kuhusu kipande cha lami kutoka Kibirashi hadi Songe, kilomita tatu. Ilikwishafanyiwa *assessment* na tunasubiri fedha. Ahsante.

**MHE. EZEKIEL MAIGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba kuchangia hoja nataka kusema barabara za Kahama na hasa Kahama – Geita. Nitakuwa mkali kidogo ili kukupa nguvu na ujasiri ili utakapoamua kutupa fedha watu wasiseme unatupendelea.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naomba kuuliza kwenye Kamati niliona wamepitisha Barabara ya Nongwe - Gairo lakini kwenye Kitabu cha leo sijaona; je, iko wapi?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba mwanangu Mheshimiwa Waziri ajenge Barabara

ya Iringa – Kalenga – Ruaha NP tuongeze uchumi wa Nchi na Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na Mungu ampe nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo moja tu ambalo naomba Wizara inisaidie; katika kipindi hiki cha mvua barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba hivi sasa haipitiki hasa sehemu ya Kisegese, Mgeta, magari yamelala hapo tangu juzi, simu nyingi nazipata; je, kwa hilo nitasaidiwaje kimawazo na kiutendaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru tena sana kwa kutenga hizo shilingi bilioni kumi. Ni imani yangu *next year* tutatengewa zaidi na zaidi ili kuharakisha kukamilisha hizo kilomita 310. *Nothing else than saying thank you*.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Butengo – Lumasa – Masumbwe imepangiwa milioni hamsini tu, naomba Mheshimiwa Waziri aikumbuke barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maishani mwangu nitamkumbuka Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya barabara hii na ninaomba kabla ya mwaka 2015 iwekwe kwenye mpango wa kuwekewa lami kwani na kwetu lami ni muhimu sana.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa afya aliyotujalia na kunipa fursa ya kuchangia kwa maandishi na kutoa kero, ushauri na mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vivuko, kwanza nitoe pongezi kwa Serikali kwa kuonesha nia ya kujenga vivuko vingi hapa nchini na hasa maeneo ambayo kumekuwa na matatizo. Kwa utafiti nilioufanya, gharama za ujenzi wa vivuko hivi ni kubwa sana na hasa kazi ya ujenzi ikifanywa na wakandarasi binafsi na wakati mwingine bei huwa zaidi ya mara moja na nusu hadi mara mbili kwa bei za kawaida. Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kikosi cha Wanamaji (*Navy),* wanao uwezo mkubwa sana katika ujenzi na ukarabati wa vivuko vyote vya ukubwa wowote na vyenye uwezo wowote na pia wanao Wahandisi waliobobea katika ujenzi wa aina hii ya vivuko, kwa kuwa Serikali ni moja, kwa nini wasiongeze uwezo katika Jeshi letu ili kazi hiyo iwe inafanyika kwa nidhamu huku gharama zikiwa za chini na kivuko chenye viwango vinavyokidhi ubora? Kama hili litafanyika kwa kuwapa Wanajeshi wetu uwezo mkubwa na jukumu la kujenga vivuko basi kitakuwa ni kitendo cha uzalendo wa hali ya juu sana ambao ninao uhakika kuwa hakuna Mbunge au mwananchi yeyote anayeweza kupinga hatua hiyo. Napenda kuyasikia majibu ya Wizara kutokana na haya niliyoshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mara. Mbali na ahadi nyingi sana za Serikali kuhusu barabara, Mara imekuwa ikitajwa tu lakini utekelezaji wake umekuwa tofauti na inavyotajwa. Mfano, barabara ya Nyanguge – Musoma, ujenzi wake umekuwa wa taratibu sana kiasi cha kuanza kuwafanya wananchi kupoteza kabisa imani na ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo kimsingi ni ukarabati mkubwa kuwa ni wa taratibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo ahadi za ujenzi wa barabara ya Musoma-Majita ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, tangu mwaka 2010 wakati akihitimisha kampeni zake za uchaguzi, pia ikumbukwe muda unaelekea kwisha na ahadi hiyo bado haijatekelezwa. Itakuwa fedhea sana kama tutaingia kwenye uchaguzi tena wakati bado ahadi ya uchaguzi uliopita haijatekelezwa. Napenda sana kuishauri Serikali ipitie upya baadhi ya ahadi za Rais kuhusu

ujenzi wa barabara hizi ili zifanyiwe kazi hasa ikizingatiwa hatuna muda wa kutosha kuelekea uchaguzi mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea pia kupata majibu ya kutosha yenye ufumbuzi kwa haya machache niliyoomba ufafanuzi hapa na yale niliyoshauri.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Ujenzi kwa Hotuba nzuri. Nimpongeze Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba na utendaji mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi ni mhimili mkubwa sana katika maendeleo. Bila ya barabara haiwezekani kufikia maendeleo endelevu. Hivyo, Wizara hii ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya kiuchumi. Pamoja na umuhimu wa barabara, maeneo mengi hasa ya vijijini hayapitiki kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Geita, changamoto ni kubwa sana kutokana na bajeti ndogo za Halmashauri. Hivyo, naomba baadhi ya barabara za Halmashauri zipandishwe hadhi kuwa za Mkoa. Ninaomba kuzitaja barabara hizi kama ifuatavyo:-

(1) Katoro – Nyakamwaga – Kamena – Mwingiro – Karumwa – Nyugwa.

(2) Bugulula - Senga – Sungusila - Mkolani – Lubanga – Mwamititu.

(3) Ilogero – Ugerenga – Iponya – Masumbwe.

(4) Masumbwe-Nyasato – Bwelwa – Ilolangulu – Kasero.

(5) Nyikonga – Iparamasa.

(6) Kerezia - Mnekezi – Nampalahara – Magota.

(7) Kasenga – Kachwamba – Ilemela.

(8) Kachwamba –Chabulongo – Nyamire – Nyabilezi.

(9) Mkungurusi – Kibumba – Buseresere.

(10) Butengurumasa – Ipalamasa – Murukezi.

(11) Muganza – Kasenda – Mwembeni.

(12) Kibehe - Kikumbaitale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni barabara za Mkoa mpya wa Geita zinazoombewa kupandishwa hadhi. Ninaomba mapendekezo yetu yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo juu ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Geita – Bukoli - Kahama umefikia hatua gani katika utekelezaji wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, machache naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2013/2014 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli (Waziri) kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pili, nampongeza kwa utendaji makini wa majukumu yake. Nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge kwa utendaji mzuri na ameonyesha ni jinsi gani yupo makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wimbi kubwa sana la ujenzi holela bila kuzingatia viwango stahiki. Wananchi

wanapoteza maisha kwa kuangukiwa na majengo. Hivyo naishauri Serikali ianzishe utaratibu kwa wajenzi wote wawawekee bima wafanyakazi pamoja na kuongeza udhibiti wa viwango vya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la bomoabomoa limekuwa ni kero ya kwanza na ni la kipaumbele kabisa kwa nchi nzima na malalamiko ni makubwa. Naiomba Serikali isikie kilio hiki kwa kuzingatia haki. Katika eneo la Jimbo la Kilwa Kaskazini mathalani, wananchi wamejenga kabla hata ya Sheria iliyotajwa haijatungwa na Bunge ama kuidhinishwa na Mamlaka husika na hili linathibitishwa na historia ya nchi yetu kwamba Wakoloni wamekuwapo kuanzia karne ya 18 na kabla ya hapo walikuwapo Waarabu na Washirazi katika maeneo ya Kilwa. Hivyo sikubaliani kabisa kuwa uwepo wa wananchi hawa katika maeneo hayo ni kuvunja Sheria kwa sababu wamekuwapo kabla. Aidha, itakuwa pia Katiba inakiukwa kama Ibara ya 13(1) ambayo inatamka watu wote ni sawa mbele ya Sheria na pia Ibara ya 24(1) inayosema kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya kuhifadhi mali yake aliyonayo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la mwezi Februari, 2011 tumejadili na kuridhia Hotuba ya Rais ambayo aliisoma wakati wa uzinduzi wa Bunge la kumi. Katika vipaumbele kumi na tatu (13) ameainisha kuwa Serikali itafanya kila iwezalo kuwawezesha wananchi. Je, wananchi wanawezeshwaje kwa kuwavunjia nyumba zao na kupoteza mali zao? Naiomba Serikali katika hili utumie busara zake na usikivu wake na kuwasaidia wananchi na kuokoa mali zao ambazo wamezipata kwa jitihada kubwa na za muda mrefu ili tusiwakatishe tamaa na kuwaweka katika hali tata. Ifikiriwe namna hata kwa kuwapa kifuta machozi kwani upande wa Serikali pia umechangia wao kuingia katika tatizo kwa maana ya uongozi na watendaji wa nchi hawasimamii ipasavyo Sheria husika na kuruhusu wananchi kujenga ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujenzi wa barabara gharama zinaongezeka kila siku. Ifike wakati sasa tuwe na mpango mkakati kuhakikisha tunamaliza ujenzi wake haraka

na kuepuka gharama ambazo zinaongezeka kwa kasi sana. Vilevile tuhakikishe makampuni ya Kitanzania yanapewa (yanajengwa) uwezo ili yaweze kushiriki kikamilifu katika miradi, kwa maana kuwa tunaposhirikisha kampuni za nje, tunatoa pesa zetu nyingi na tunaimarisha uchumi wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo katika matumizi ya madaraja, haswa daraja la Mkapa ambapo sasa wafugaji wamekuwa wanapitisha mifugo juu yake, licha ya kuhatarisha usalama kwa watumiaji wengine, pia ni matumizi mabaya kwa nini wasitumie magari?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya kampeni, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwa wananchi wa Kilwa Kaskazini, kuwa barabara ya Kipatimu - Nyamwage itajengwa. Naiomba Serikali itekeleze ahadi hii haraka ili kuwaondolea kero wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufuatiliaji mzuri wa viongozi wa Wizara hizi, naishauri Serikali ihimize na kuhakikisha barabara ya Ndundu-Somanga inakamilika kwa wakati, ili iwe ni pumziko kwa wananchi wa Kilwa na Mikoa ya Kusini kwa ujumla ambao kwa kipindi kirefu wameteseka na kutotumia vema fursa za kiuchumi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zimefanyika kwa barabara ya Nangurukuru – Njinjo - Liwale, tunaishukuru sana Serikali kwa jitihada zake ila sehemu korofi bado zinahitaji jitihada zaidi kurekebishwa na kuimarishwa ili barabara ipitike wakati wote na haswa ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nafuatilia kwa makini jitihada za Serikali katika kuondoa kero za msongamano wa magari haswa katika Jiji la Dar es Salaam, ila kwa sasa sikubaliani na wazo la kujenga *"fly overs*". Mpango ni mzuri ila haufai kwa sasa. Ni vema tukaimarisha barabara ya Kilwa na kujenga barabara ambayo itaanzia Mbagala hadi Kisarawe na kutokea Mlandizi au Chalinze. Hii itapunguza sana *traffic volume* na kuongeza uwepesi zaidi

kwa watumiaji wa pembezoni mwa mji kama Mbagala, Chamazi, Kisarawe, Ukonga, Pugu, Segerea na kadhalika kutolazimika kufika maeneo ya mjini ili kuweza kuipata *Morogoro Road*, lakini pia itasaidia kuboresha maeneo ya pembezoni mwa mji na kupunguza magereji ya mtaani. Halmashauri za Wilaya husika zinaweza kunufaika kwa kujenga maeneo ya maegesho (*truck ports)* ambazo zitaondoa kabisa tatizo la maegesho mijini au katika maeneo yasiyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo la msongamano kwa haraka ni vema kuweka muda maalum (saa mbili usiku) wa maroli kutoka bandarini au nje ya mji kwa maana yenyewe ndio husababisha sana msongamano. Pamoja na yote haya, nashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani (Askari Polisi) kuhakikisha madereva (haswa wa daladala) kuwa wanazingatia Sheria zilizowekwa na wanaokiuka wanapewa adhabu kali ili iwe funzo na mfano kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia pesa nyingi sana katika ujenzi wa barabara, lakini kwa masikitiko makubwa zinaharibiwa na uzito mkubwa wa magari ya mizigo. Naishauri Serikali ihimize matumizi ya reli kwa mizigo mizito. Pia uzito upimwe toka bandari ili atakayezidisha mzigo, gari itaifishwe na Sheria iwe kali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara hii. Naomba jitihada hizo nzuri ziendelee kwa kasi ili Wapinzani wakose hoja mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ahadi za Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi za ujenzi

wa barabara katika maeneo mbalimbali nchini, ukiwemo Mkoa wa Mbeya. Baadhi ya barabara hizo ni Mpemba-Isongole, Kikusya-Matemba, Katumba-Mbambo-Tukuyu, Mbeya - Chunya na kadhalika. Ni imani yangu kwamba Wizara itahakikisha kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa na kukamilishwa kabla ya mwaka 2015, kinyume chake wananchi na hasa Wapinzani watapata mwanya wa kuilaumu Serikali kwa kuahidi mambo ambayo hayawezi kutekelezwa. Namwomba Waziri awaeleze Watanzania kama ahadi hizi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa na kukamilishwa au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naipongeza *TBA*-Wakala wa Majengo kwa kazi ya kujenga nyumba na nyingi kati ya nyumba hizo kuwauzia wafanyakazi wa Serikali. Tatizo langu hapa ni bei kubwa ya nyumba hizo. Tunajua viwango vya mishahara kwa watumishi wa Serikali, ni vidogo sana, nashauri Wakala ujipange kujenga nyumba kwa kutumia teknolojia rahisi ili ziweze pia kuuzwa kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni dhahiri kabisa kwamba baadhi ya makandarasi wa ujenzi wamekosa sifa za kufanya kazi za ujenzi wa majengo na barabara. Nasema hivyo kwa sababu hivi karibuni jengo moja la ghorofa lilianguka Mkoani Dar es Salaam na kuua watu kadhaa, aidha majengo mengine yamewahi kuanguka Mkoani Dar es Salaam na kuleta madhara kwa watu na mali zao, baadhi ya barabara pia zimekuwa zikijengwa kwa viwango vya chini sana na hivyo kuharibika mapema sana. Ushauri wangu, makandarasi wote wanaohusika katika kazi mbovu kama hizo wafutiwe usajili mara moja na Wahandisi wa Makampuni hayo wasiruhusiwe kuanzisha Makampuni mengine ambayo yataishia kufanya kazi za hovyo nchini mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ziko habari kwamba viko viwanda ambavyo vinatengeneza nondo *fake*. Kama habari hizi ni za kweli basi ni hatari sana. Nondo hizi kama zitaingia sokoni basi sekta ya ujenzi itakuwa imeingiliwa. Naomba Wizara ifanye uchunguzi wa jambo hili bila kupuuza hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara nyingi zimekuwa hazipitiki wakati wa mvua. Barabara kama vile toka Koga mpaka Mpanda nyakati za mvua ni mbaya mno, kiasi cha kufanya wananchi wanaoishi Mpanda kupitia barabara ya Sumbawanga ama kutegemea treni isiyokuwa na uhakika na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Je, Serikali inasema nini kuhusu ukarabati wa mara kwa mara wa barabara hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Koga - Mpanda imekuwa ikitajwa na kutengewa pesa toka bajeti ya 2012/2013 yaani bajeti ya mwaka jana hadi bajeti hii ya makadirio ya 2013/2014. Je, ni lini barabara hiyo itaanza kutengenezwa ama kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi hasa ukizingatiwa kwamba Mkoa wa Katavi ni moja ya Mikoa inayozalisha chakula na biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Wizara hii imekuwa na mpango wa kujenga daraja la watembea kwa miguu jijini Mwanza eneo la Mabatini, hili ni wazo zuri lakini ninapenda kushauri kwamba kwa kuwa Jiji la Mwanza linakuwa kwa kasi na litahitaji upanuzi wa barabara kama ilivyo Dar es Salaam, je, Serikali kupitia Wizara husika haioni kwamba ni vyema kuachana na mpango wa kujenga daraja ambalo baada ya muda mfupi tu linaweza kubomolewa kwa ajili ya kuboresha barabara na hivyo kupoteza pesa kwa maendeleo ambazo zingefanya shughuli nyingine ya maendeleo? Napendekeza pesa itafutwe kwa ajili ya upanuzi wa barabara hiyo, kwa mwaka huu wa fedha na ujenzi huo wa barabara uanze katika kipindi hiki cha mwaka huu, katika eneo husika yaani Serikali iangalie namna itakavyoweza kupanua barabara hiyo angalau toka eneo husika yaani Mabatini angalau mpaka Nyakato, jambo

ambalo litakuwa limepunguza tatizo na usumbufu kwa watumia barabara maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Napenda zaidi kujikita katika mambo matatu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kuishauri Serikali iwe na umakini wa hali ya juu katika kusajili makandarasi hapa nchini, kwani matukio yanayojitokeza katika sekta ya ujenzi hapa nchini, matokeo kama ya kuporomoka kwa majengo katika baadhi ya maeneo hapa nchini na ujenzi wa barabara zisizo na kiwango ni baadhi ya mambo ambayo kwa kiasi kukubwa hakiashirii kama huko tunakoelekea tutaishia kuzuri. Hivyo ni wajibu wa Serikali kutueleza hatua inazoendelea kuzichukua kukabiliana na wimbi hili baya linalogharimu maisha ya watu wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kukabiliana na msongamano katika Miji mikubwa katika nchi yetu hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Kuna tatizo la msongamano wa magari pale eneo la Kurasini kwa magari makubwa yanayosubiri kupakia ama kushusha makontena pale bandarini, ni bahati mbaya sana hapana eneo maalum la kuegesha magari yale yanayosubiri kuingia bandarini. Hivyo hulazimika kuegesha kandokando ya barabara, jambo ambalo ukiacha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara lakini pia kuna malalamiko yenye ukweli, kwamba wamiliki wamekuwa wakikamatwa na magari yao kwa kosa la uegeshaji sehemu zisizoruhusiwa na kulazimishwa kutozwa faini kubwa jambo ambalo ni dhuluma na uonevu wa wazi kwani, dereva wa gari husika anakuwa tayari kupakia au kupakua lakini hatua mbalimbali na taratibu za bandari huwalazimisha wakae kwa sababu zilizo nje ya uwezo wao. Hivyo, naishauri Serikali iliangalie tatizo hili ambalo limekuwa likilalamikiwa sana na

wasafirishaji hapa nchini, naiomba Serikali ifuatilie ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali inipatie majibu kuhusu muda ambao muathirika wa Sheria mpya za Barabara pale ambapo barabara inamfuata mwananchi na akawekewa alama kwamba amefikiwa na hifadhi ya barabara na alikuwepo kisheria ni muda gani mwananchi huyo anatakiwa awe amelipwa na kutakiwa kuvunja nyumba yake? Malalamiko mengi yamekuwepo kwamba kwa mujibu wa Sheria za Hifadhi ya Barabara mtu hatakiwi kuendeleza eneo ambalo tayari limeainishwa kwa matumizi ya hifadhi ya barabara. Watu wetu wengi nyumba zao huhitaji ukarabati mara kwa mara na kwa mujibu wa Sheria hairuhusiwi na pia muda wa kulipwa akavunja, haujulikani! Je, Serikali haioni inawaweka katika sintofahamu watu hawa? Naomba jibu rasmi la Serikali ni muda gani stahiki wananchi wanaopitiwa na barabara na hifadhi zake anatakiwa awe amelipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la barabara ya Namanyere – Kirando. Hii barabara ni muhimu sana kiuchumi na ni barabara ambayo inatumika sana haswa kwa mizigo iendayo DRC – Congo. Tafadhali naomba Wizara yako iione kwa ukaribu kwa kuiwekea lami kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara Kipili kwenda bandarini Kipili, hakuna barabara, ni Km.8 au 7 tu. Mamlaka ya Bandari inajenga bandari lakini hakuna barabara. Nilizungumza katika Bunge kuhusu barabara hiyo ya kwenda bandari ya Kipili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara ya L‘yazumbi-Kabwe imetengewa pesa kidogo sana kutokana na hali ya barabara ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Sumbawanga – Kanazi – Kibaoni, pesa wanazopewa wakandarasi wa Kichina hazitoshi kabisa maana barabara ya hiyo mkataba wake unasomeka kwisha mwaka 2013, barabara iwe tayari, leo hii wanapewa pesa ambazo zinawafanya Wachina wakae na kuuza kokoto ili wapate kuishi na leo hii mwaka 2013 kazi iliyofanyika labda ni asilimia 20-30% tu. Nategemea Wizara yako itoe tamko hapa Bungeni lini barabara hiyo ya Sumbawanga – Kanazi - Kibaoni itamalizika rasmi.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kazi nzuri inayofanyika katika ujenzi wa barabara. Barabara ya kutoka Makutano – Natta – Mugumu - Loliondo-Mto wa Mbu (km 452 ) haijaanza kulimwa muda mrefu sasa tangu 2009 upembuzi yakinifu na usanifu kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inayotengwa kwa kila mwaka ni kidogo sana. Je, itachukua muda gani kukamilika kwa barabara hiyo? Hela zinazotengwa ni ndogo mfano mwaka 2010/2011- 1.0 bilioni, mwaka 2011/2012 – 1.9 bilioni, mwaka 2012/2013 - 3.8 bilioni, mwaka 2013/2014 – 8.6 bilioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Mji wa Mugumu hauonyeshwi kuwekewa lami wakati ramani ya barabara imepita nje ya Mji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini hadi sasa wananchi walioguswa na ramani ya barabara hawajalipwa fidia wakati Mkandarasi anajiandaa kuanza kulima barabara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini barabara za Manchimworu-Ring'wani (km37) na Majimoto – Nyansurura (km.36) ambazo zimeingizwa *TANROAD* tangu mwaka 2011/ 2012 hadi leo hakuna hela iliyotengwa na sijui zitafunguliwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa nini ahadi ya Serikali ya kufungua barabara ya kupitia Serengeti – sehemu ya Mugumu-Ikoma gate (km 41) haijawekwa katika mpango? Serikali ilitoa majibu Bungeni kuwa wakati wa kujenga barabara ya Magumu - Loliondo – Mto wa Mbu ni vyema sehemu hiyo fupi (km 41) akajengwa ili kurahisisha usafiri kwenda Hifadhi ya Taifa Serengeti (Ikoma gate).

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi uimarishwe ili ujenzi wa barabara na majengo viende vizuri.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi kwa kuwasilisha hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini ya maendeleo kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa masikitiko yangu kwa fedha kidogo sana inayopewa *TANROARDS* na hivyo kushindwa kufanya kazi zake kikamilifu. Barabara nyingi kwenye Halmashauri ambazo ziko chini ya *TANROADS* zina hali mbaya sana. Kwa mfano, barabara ya Ilula-Mlatu-Wotalisoli-Ipalamwa-Kising'a – Lulanzi – Kilolo haipitiki kabisa wakati wa masika na kwa shida wakati wa kiangazi. *TANROADS* iongezewe bajeti ili itekeleze majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kujenga barabara kwa kiwango cha lami kufikia Makao Makuu ya kila Wilaya. Kutokana na hilo, je, lini sasa barabara ya Iringa-Kilolo na Ilula – Kilolo zitajengwa kwa kiwango cha lami? Katika mwaka 2009/2010 ni kilometa mbili tu zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Iringa - Kilolo na baada ya hapo hakuna lolote linaloendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri mwenye

dhamana ya Wizara hii na wataalamu wake kuandaa hotuba hii na kutuletea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mkoa wa Tabora zote zinatakiwa kujengwa kwa kiwango cha lami kazi inakwenda taratibu sana kiasi cha kukatisha tamaa na kusababisha Mkoa na wananchi wake kuendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inajibu hapa Bungeni kwamba barabara hizo Itigi-Tabora, Mega-Tabora, Tabora – Ndono na Ndono – Urambo zitakamilika ndani ya mikataba. Mikataba yote ilishakwisha muda wake wakati hakuna hata barabara iliyofikia nusu ya kazi tarajiwa. Kwanza, Bunge lielezwe ni mikataba ipi inakamilisha barabara hizo na ni lini barabara hizi zinakamilika kwa viwango vinavyokubalika?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wananchi wa Kaliua Mjini – Mkoa wa Tabora walibomolewa nyumba zao tangu mwaka 2003 kwa madai kwamba wanapisha upanuzi wa barabara mpaka leo hakuna fidia yoyote iliyotolewa kwa wananchi hao na hakuna upanuzi uliyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2012 wataalam wa *TANROADS* Mkoa walifika Kaliua na kueleza wananchi kwamba upanuzi wa barabara hiyo ya Urambo – Kaliua hautapita katikati ya mji eneo ambalo wananchi walibomolewa nyumba zao na badala yake itapita pembezoni kuelekea Kazilambwa. Serikali ieleze wananchi waliobomolewa nyumba zao Kaliua tangu mwaka 2003 nini hatma ya madai ya fidia ya nyumba zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maombi ya Mkoa mwaka 2007/2008, Serikali ilikubali kuingiza barabara ya Urambo – Ulyankuru na ile ya Kaliua – km 60 – Mpanda kuwa za *TANROADS.* Barabara hizo haswa ya Kaliua – km 60 – Mpanda iko kwenye hali mbaya sana. Wakati wa mvua mawasiliano yanakatika kabisa, huduma za afya zinashindikana, kina mama wanajifungulia njiani na hata

mazao hayawezi kutoka kwenda sokoni. Serikali inaonaje kuhusu matengenezo ya uhakika ya barabara hii kwa kiwango cha changarawe au lami tofauti na kuinua tuta kila leo linabomoka?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya barabara inayokwenda kwenye Halmashauri za Wilaya zinaingia kwenye mifuko ya watumishi wachache wakishirikiana na Madiwani, ubora na viwango vya matengenezo, ujenzi, ukarabati vinakuwa chini sana *(no value for money)* na ndio maana kila leo ubovu unaendelea na wananchi wanateseka. Ni chombo gani kinasimamia matengenezo ya barabara kwa ngazi ya Halmashauri za Wilaya kuhakikisha fedha inakwenda kwenye kazi iliyokusudiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kuu kutoka Chalinze hadi Vigwaza ina migongo mikubwa, magari yanayumba barabarani na ajali nyingi zimekuwa zikitokea eneo hili na kuteketeza maisha ya wananchi wengi. Serikali inasubiri roho ngapi zipotee pale ndio wachukue hatua? Je, viongozi na hata Dkt. Magufuli hawapaoni pale wakiwa wanapita?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Majengo TBA, ni chombo ambacho kina wataalam wenye ujuzi na uzoefu wa hali ya juu. Chombo hiki kingeweza sana kusaidia wananchi kujenga nyumba bora kwa gharama nafuu kwa kutumia mbinu za kisasa, tatizo kubwa haiwezeshwi kwa kupewa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yao. Wanatengeneza matofali ya kisasa ya *interlock* ya gharama nafuu. Mahitaji ya tofali hizi ni makubwa lakini hayapatikani kwa wakati.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuipongeza hotuba ya Waziri na kuiunga mkono hoja yake moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja moja tu, nayo ni ujenzi wa barabara ya lami kuanzia Masasi,

Nachingwea hadi Nanganga. Barabara hii ni muhimu sana kwa wakulima wa korosho, ufuta, mbaazi na mazao ya chakula wa Nachingwea. Kwa sasa barabara hii inapitika lakini ni ya *gravel.* Mheshimiwa Rais alipokuja Nachingwea mwezi Januari mwaka huu, aliahidiwa na uongozi wa *TANROADS* kuwa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia 2014. Napenda kupewa *update,* je, mchakato huu umefikia wapi? Wananchi wa Nachingwea wangependa kujua hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara ya Ujenzi ni Wizara ambayo ni ngumu sana na wengi waliopewa Wizara hiyo hukwama lakini namshukuru Mungu kwamba wanafanya kazi nzuri pamoja na wasaidizi wake. Mpinzani yeyote hata ukimwambia kwamba hii ni barabara tumejenga atasema hiyo sio barabara isipokuwa ni nyumba, kwa hiyo, msikatishwe tama, Mungu awasaidie kutekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kufikiria kujenga barabara ya Isyonje – Makete kwa kiwango cha lami kwa sababu, kwanza, ni barabara inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Njombe. Ni barabara inayopita katika eneo muhimu kwa utalii (*Kitulo National Park*). Ni barabara ambayo inaharibika mara kwa mara kwa sababu inapita eneo la milima ya Mporoto na *Livingstone* ambako kuna wastani wa mvua nyingi kwa mwaka. Fedha inayotengwa kwa ajili ya matengenezo ni ndogo na hivyo kuifanya barabara isipitike kwa wakati wa mvua maana mvua inanyesha kwa miezi mingi kwa mwaka kuliko maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambayo naiomba Serikali ni barabara ya Kikondo - Ifupa hadi Mswasi. Barabara hii hata ikitengewa fedha kwa kiwango cha changarawe ingewasaidia sana wananchi ambao wanalima sana viazi. Hii ni barabara iliyoko *TANROADS* lakini sijaona fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Ulaya barabara nyingi zimejengwa na *PPP, sector* binafsi, je, hapa kwetu Tanzania mpango huo ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada inazochukua katika ujenzi wa barabara, ukusanyaji wa tozo (*Road Fund)* na Wakala wa Nyumba za Serikali. Mheshimiwa Waziri na Naibu wanajitahidi kusimamia Wizara hii na kwa kweli "*Value for Money*" inaonekana ijapokuwa bajeti ya Wizara hii ni kubwa kulinganisha na Wizara nyingine bali hata majukumu yake katika suala zima la kuimarisha uchumi wetu ni kubwa kwa upande wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya kupimia magari (mizani). Ni ukweli usiofichika kwamba barabara zetu zinaendelea kuharibika sana kutokana na baadhi ya malori hasa ya mizigo kubeba uzito mkubwa kuliko kiwango kilichowekwa kisheria na idadi ya magari ambayo yamepatikana na kosa hilo yameongezeka na yanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka. Ni vyema sasa Wizara ikaangalia aina nyingine ya adhabu kwa madereva, wenye mzigo na wamiliki wa magari hayo ambayo yatakamatwa kwa kosa la kuzidisha uzito. Adhabu ambayo ipo kwa sasa ni ndogo na ni rahisi kuchezewa hata na baadhi ya watendaji waliopo katika vituo vya mizani ambao si waaminifu. Ni vyema pia Watendaji hawa ambao si waaminifu kusakwa kwa njia moja ama nyingine na watakapopatikana hatua

kali za uharibifu wa uchumi zichukuliwe dhidi yao. Pia ni vyema Wizara kuwahamisha watendaji hawa kila baada ya kipindi fulani ili watendaji hawa wasiwe wanakaa katika kituo kimoja kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuongelea Bodi ya Mfuko wa Barabara. Bodi inafanya kazi zake vizuri na tumeshuhudia makusanyo yao yanavyoongezeka mwaka hadi mwaka. Nashauri kwa kuwa fedha nyingi za Mfuko huu huenda katika Halmashauri zetu nchini kusaidia ujenzi wa barabara aina za changarawe au za lami, Bodi iingize ratiba yake ya kwenda katika Halmashauri hizi kukagua miradi ambayo imeifadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kati ya changamoto inazopata Mfuko huu ni ukosekanaji wa tozo kutoka katika baadhi ya Makampuni ambayo yanachimba madini hapa nchini. Makampuni haya yanaikosesha mapato ya tozo bodi hii si chini ya billioni 26 kwa mwaka, ambapo makampuni haya ndio yanayoharibu barabara zetu kwani magari yao hubeba uzito mkubwa zaidi na usafirishaji wa mitambo yao. Makampuni matano nchini yamebainika kutokulipa tozo hiyo ambayo ipo kisheria. Ni vyema Wizara ikatupatia jibu sahihi juu ya kadhia hii ambayo kwa njia moja ama nyingine inaenda kinyume na sheria tulizozipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROAD,* bado tuna wimbi kubwa la miradi yetu ya barabara ama kuchelewa kukamilika au kujengwa chini ya kiwango. Tatizo hili pia huchangiwa na Mameneja wetu walioko Mikoani kwa kununuliwa na Wakandarasi. Uhusiano huu usio halali, ni hujuma kwa Wizara na uchumi wa nchi. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri uweke adhabu kali kwa Mameneja wote ambao watagundulika kuzembea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ni kuwepo kwa madeni mengi ya Wakandarasi nchini, bado Wizara kupitia *TANROAD* haijatuonyesha njia muafaka ya kupunguza tatizo hili bali tunachoshuhudia ni kuongezeka kwa miradi mipya ama ya upembuzi au ujenzi. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri

tueleze njia mbadala utakazozichukua kukabiliana na madeni haya. Bajeti ambayo leo hii tunaipitisha kiasi kikubwa kinaenda kulipia madeni tu, jambo ambalo linasababisha miradi mingi kusimama kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba maelezo juu ya tuhuma za wizi wa fedha unaofanyika baina ya Mabenki na *TANROAD,* pale wanapoamua kuzichelewesha fedha za malipo ya Wakandarasi na fedha hizo kuziweka katika *fixed account* ili ziweze kuzaa *interest* kwanza ndio baadaye wakalipie Wakandarasi. Huu ni wizi ambao upo.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya Waziri Magufuli, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya kupitisha barabara. Kuna mgogoro mkubwa wa kisiasa kwa wananchi wa Mandawa, Mputwa na Milola wanadai barabara yao ya asili ambayo ikitoka Milola ipitayo Mputwa kwenda Mandawa kilomita 27 kuliko ile ambayo inatoka Mandawa kupitia Nahoro. Ugomvi huo ni mkubwa hadi Rais alienda huko. Serikali ituambie mgogoro huu utakwishaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kibiti na Lindi, kauli ya Serikali iseme lini itaisha? Bado kilometa 22 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa barabara za Mikoa. Barabara za hizi huachwa bila kukarabatiwa. Tunashauri barabara ya Nanganga, Ruangwa, Namchiga, Nanjilinji Nangurukulu, tunaomba sana zikarabatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandishwa hadhi barabara. Sheria ya *Road, No 2007,* barabara zifuatazo, tunaomba zipande hadhi. Nyengedi – Rondo – Mandawa, Mchinga- Kijiweni - Jiwe la Mzungu, Liwale - Kilimarondo – Tunduru, Nachingwea - Chiola - Ruangwa. Tunaomba zipandishwe hadhi kutoka Wilaya kwenda Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa ahadi kuwa Makao Makuu ya Wilaya barabara zake angalau kilomita mbili ziwekwe lami. Tunaomba Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Lindi Mjini hizi ziwekwe lami, ni ahadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ahadi ilitolewa kwa barabara ya Nachingwea kwenda Nanganga hadi Masasi kuwekwa lami, ni lini ahadi hiyo itaisha?

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwani inakusudia kuwakomboa Watanzania ikiwa ni kiuchumi na kiustaarabu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, ninaomba Wizara ya Ujenzi kuifikiria kwa makini barabara ya Butengo-Lumasa – Nyikonga - Masumbwe ambayo mwaka jana ilitengewa jumla ya shilingi milioni arobaini (40m) na katika mwaka huu wa fedha mwaka 2013/2014 jumla ya fedha kwa ajili ya maendeleo (kasma 4132) zimetengwa jumla ya shilingi milioni (50m). Fedha hizi hazitoshi kabisa katika kuiboresha barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninaipongeza sana *TANROAD* Mkoani Geita kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuifungua barabara hii kati ya Iparamasa na Nyikanga kwani ilikuwa ni uchochoro wa watembea kwa mguu tu. Kwa sasa barabara hii imefunguka na kuruhusu magari sasa kupita bila matatizo nyakati zote za mwaka masika na kiangazi, pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Butengo-Lumasa- Nyikonga- Masumbwe haijatengewa fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka 2013/2014. (Angalia kiambatisho Na. 3). Naomba siku zijazo zitengwe fedha kuimarisha barabara hii, ni barabara muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua barabara hii iko katika mchakato wa kupandishwa daraja kuwa barabara ya Mkoa na kusimamiwa na Wakala wa Barabara *(TANROAD)*.

Naomba mchakato wa kuipandisha daraja barabara hii ufanyike ili iweze kuingizwa kwenye utaratibu wa kuongezewa fedha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo na Wilaya ya Mbongwe ni Wilaya mpya ambayo miundombinu ya barabara ni duni sana. Katika mazingira haya basi tutaendelea kwa kupitia vikao halali kuleta maombi kwenye Wizara kwa ajili ya kuzipandisha madaraja barabara zingine ambazo katika Wilaya jirani na Wilaya mpya ya Mbogwe zinahudumiwa na TANROADS lakini ndani ya Wilaya ya Mbogwe barabara hizi ziko chini ya Mamlaka ya Halmashauri. Mfano wa barabara hizo na Wilaya zilizomo ni kama ifuatavyo. Katika Wilaya ya Kahama, kuna barabara kutoka Kahama – Masabi - Mega iko *TANROAD,* kutoka hapo hadi mpakani mwa Jimbo langu la Mbongwe iko katika usimamizi wa Halmashauri. Nashauri barabara hii kutoka Mega – Nyanhanga - Maguta - Mpakali - Lugunga kuunganishwa na barabara ya Butengo - Lumasa na Masumbwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni ile ya Mwalo- Iyogelo iko *TANROADS* katika Wilaya ya Bukombe mpaka Mpakani na Wilaya yangu ya Mbongwe, naomba iungwe kupitia Iyogelo – Bugelenga – Bunyihuna – Ipinya – Masumbwe nayo iwe *TANROADS*. Barabara ya Ushirombo – Kalome – Buguba – Kiseke – Isebya – Lwamgasa – Busanda – Kilombero II hadi Gengetano (Bafunda), barabara hii ombi letu ipandishwe kuwa ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ushirombo – Kalome - Nyang'hologe – Kisumo - Nanda - Bwelwa – Iboya – Bwendamwizo – Nyitundu - Ivumwa hadi Wigo kuunganishwa na barabara ya Geita - Nyangusa - Bukoli hadi Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, yeye na timu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kujua juu ya utatuzi wa tatizo la Mji wa Dodoma la magari makubwa ya mizigo na mabasi kupita katikati ya Mji na kusababisha usumbufu na hatari zingine za ajali na hofu juu ya magari yanayobeba vitu vya hatari kama petrol, dizel, sumu mbalimbali na vitu vizito. Je, kuna mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kutatua tatizo hili. Nawatakia kazi njema.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue fursa hii niipongeze Wizara na Serikali katika jitihada za kujenga mtandao wa barabara za lami nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, bado tuna kazi kubwa ya kufanya katika eneo hili la barabara, hali ya barabara zetu hasa maeneo ya vijijini bado hairidhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni uchumi, huwezi kuwa na tija kwenye shughuli za uchumi hasa kilimo kama hakuna barabara itakayobeba hayo mazao na kuyafikisha sokoni kwenye bei yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuiomba Wizara kugawa fedha za Mfuko wa Barabara kwa Halmashauri kulingana na mtandao wa barabara kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yangu ya Nzega ina mtandao wa kilometa 760 za barabara. Hapa kuna hoja mbili, hoja ya kwanza ni ufinyu wa fedha za Mfuko wa barabara zinazotengwa mfano katika mwaka 2012/2013 Nzega iliidhinishwa shilingi 772 milioni. Fedha hizi zinaweza kutosha kuhudumia nusu tu ya mtandao wa barabara za Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine hapa ni upatikanaji wa fedha hizi zilizoidhinishwa mfano katika shilingi 772 milioni zilizoidhinishwa kwa mwaka 2012/2013 ni

shilingi 344 tu ambazo Wilaya ya Nzega imepokea hadi Aprili, 2013 ambayo ni sawa na 45% tu ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010, tumeahidi kufanya upembezi yakinifu katika barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo - Kahama lakini ni miaka mitatu sasa tangu 2010 lakini sijaona mpango wowote wa makusudi wa kutenga fedha za kufanyia barabara hii upembezi yakinifu. Naomba Wizara ya Ujenzi ifanye upembuzi yakinifu katika barabara hii ikiwa ni maandalizi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nyingine hapa ni Wizara kufanya lolote liwezekanalo ili barabara ya Nzega - Tabora ikamilike haraka iwezekanavyo. Wananchi wa Nzega wamepata matumaini sana Mheshimiwa Rais alipokwenda Nzega na kuwahakikishia kuwa barabara hii itakamilika kama ilivyopangwa lakini barabara hii mpaka sasa imekamilika kwa asilimia 15% kwa sehemu ya Nzega-Puge na asilimia 29% kwa sehemu ya Puge Tabora. Barabara hii iko nyuma kwa miezi 22 sasa, tunaomba ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Daraja la Kigamboni, ni jambo jema lakini hata hivyo ni vyema Serikali ikasimamia malipo ya fidia ya wananchi, bado wananchi wanalalamika, naomba suala hili limalizwe tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuondoa msongamano wa magari Dar es Salaam, japo Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza msongamano huo lakini bado *speed* ni ndogo sana. Wananchi wanapata shida sana, ujenzi wa barabara zinazokusudiwa unakwenda kwa kasi ndogo sana na wakati wa mvua ndio kero zinazidi, utatamani uruke kwa juu. Hivyo nashauri Wizara kusimamia

utekelezaji wa barabara zote ili kuona zinamalizika kwa wakati hasahasa barabara ya Morogoro.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuifahamisha Wizara kwamba bado vituo vya kupima uzito wa magari (*weigh bridge*), kuna wizi mkubwa unaoendelea na bado kuna magari mengi ya mizigo yanayopakia uzito zaidi na kuruhusiwa kuendelea na safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kupima *(calibration*) ya magari ya mafuta, kuna msongamano mkubwa sana wa magari kutaka kupimwa na uwezo wa kupima ni mdogo kufuatana na magari yaliyopo ukienda kiuhalali unaweza kupewa nafasi ya kupimwa baada ya miezi mitatu lakini kwa kuwa mmewatengenezea mwanya wa rushwa, ukitoa rushwa utapimiwa haraka. Hii sio haki na kwa nini kuna sheria ya kupima hayo magari ya mafuta kila mwaka? Kama gari la mafuta likipata ajali ni sahihi kupima lakini kupima kila mwaka, sheria hii haiko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora una miradi mitano ya barabara kuanzia mwaka 2010 sambamba na wenzetu wa Peramiho – Mbinga ambapo wao wamekamilisha kilomita 78 za tuta la barabara kwa kiwango cha lami lakini sisi Tabora tuko katika hatua kama ifuatayo:-

| NA. | MIKOA | MUDA WA KUKAMILIKA | MAENDELEO YA KAZI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | NZEGA - TABORA | 2/5/2013 | 15% | AIBU |
| 2 | PUGE - TABORA | 2/4/2013 | 29.6% | AIBU |
| 3 | TABORA-NYAHUA | 26/1/2014 | 21.5% | AIBU |
| 4 | TABORA - NDONO | 3/9/2012 | 31.3% | AIBU |
| 5 | NDONO-URAMBO | 4/1/2013 | 35% | AIBU |

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mradi umechelewa kukamilika, hii ni aibu na hasara kubwa kwani kila mwezi Serikali inaingia hasara ya riba ya shilingi bilioni moja. Fedha za Watanzania za kodi zinapotea, huu uzembe ni wa nani? Nani awajibike? Nani alaumiwe? Wakandarasi hawa

wanadai 25 bilioni na hazijalipwa. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kuridhisha kuhusiana na hilo deni la shilingi 25 bilioni na mpango mkakati wa kulipa deni hilo na pia utaratibu wa kuendelea kulipa ili kazi ya barabara isikwame tena mpaka itakapokamilika? Tofauti na hilo, nitatoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makutano - Magumu - Loliondo - Mto wa Mbu, ni vizuri iitwe *Serengeti Road.* Hii itasaidia kutangaza utalii na pia itawezesha barabara hiyo kueleweka vizuri kwa kila mtu hapa nchini na Kimataifa. Hakuna sababu ya kuiita kwa vipande vipande. Naitaka Serikali itamke rasmi jina la barabara hiyo kuwa ni *Serengeti Road.*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Waziri wa Ujenzi na Naibu wake, kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Hakika barabara za lami zinazojengwa katika nchi hii ni kielelezo cha utumishi uliotukuka wa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kuona kwenye bajeti ya ujenzi wa barabara mwaka huu barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami. Barabara za Vunjo ni hizi zifuatazo:-

(i) Arusha – Moshi – Himo – Holili.
(ii) Kawawa – Nduoni.
(iii) Marangu Mtoni – Kilema Sokoni
(iv) Mwika - Marangu Mtoni.
(v) Mwika - Kilacha Himo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazofanyika katika barabara hizo ni nzuri na Serikali inapaswa kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kilema Pofo - Kilema Hospitali, barabara hii inaunganisha wananchi wa Himo na Hospitali ya Wilaya ya Kilema. Barabara hii inayoanzia katika Kijiji cha Kilema Pofo inapitia katika taasisi

nyeti za Serikali, kipo Chuo cha Ualimu Mandaka, shule kadhaa za sekondari na ufundi pia yako Makanisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inajengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi lakini inaonekana aidha haina fedha au fedha zinazotengwa ni ndogo, wakati wa mvua kama wakati huu barabara hii haipitiki. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo yatakayowezesha barabara hii kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za awali.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Oljoro, Orkesumet, Kibaya, Kongwa *(NARCO),* ifanyiwe maandalizi ya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi iongezwe ya ujenzi wa barabara ya Dodoma, Kondoa hadi Babati ili ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Korogwe, Handeni, Kibaya, Kondoa hadi Singida ikamilishwe maandalizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya *TANROAD* ya Babati, Kimotorok, Engopito hadi Kibaya ikamilishwe na iwe inapitika kwa misimu yote ya mvua na kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za mazingira magumu zinazojengwa kwenye Wilaya zilizopo pembezoni zijengwe na Wizara ili kuondoa uchakachuaji unaofaywa na Halmashauri na wakandarasi.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri inayoonekana. Aidha, ni wazi *TANROAD* chini ya uongozi wa Mkurugenzi wake Mkuu mpya aliyesimikwa na Mheshimiwa Waziri Magufuli anafanya kazi nzuri sana.

Hongera. Katika hali hiyo, ni dhahiri kwamba ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia maboresho, naomba kuainisha yafuatayo. Kwanza, Wilaya ya Muleba ni mojawapo ya Wilaya kubwa sana Tanzania, ina kilometa za mraba 10000 na kati ya hizi kilometa za mraba 3500 ndiyo nchi kavu tu nyingine ni maji na visima. Jografia hii inafanya usafiri wa barabara uwe mgumu. Barabara ya Kigoma - Rusahunga inakaribia kumalizika. Tunashukuru sana lakini kuna matatizo yaliyotokana na maendeleo haya. *Environmental Impact Assessment* haikuzingatia maji ya mvua na mifereji yake Muleba Mjini. Maafa ya mafuriko ndiyo matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi angeshughulikia kero hii na kuboresha barabara za lami kilomita mbili. Kwa kuwa wakandarasi wa *TANROAD* wa barabara ya Kigoma - Rusahungo bado hajaondoa vifaa vyake, tunaomba Mheshimiwa Waziri afanye kila awezalo kuwapa kufanya kazi hii. Kwa kushirikiana na Halmashauri, kandarasi amefanya *BOQ* inayoonesha gharama itakuwa tu asilimia 36% ya gharama ya kawaida. Hapohapo mkandarasi huyo yuko tayari kutengeneza barabara ya kutoka Muleba kwenda Hospitali Teule ya Rubya. Njia hii ina Mlima mkubwa wa Kanyambogo ambao husababisha magari ya wagonjwa kukwama, wajawazito wanataabika sana sehemu hiyo. Mkandarasi wa *TANROADS* pia yuko tayari kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa gharama powa ya shilingi 233,333,000 kwa kilometa ukilinganishwa na viwango vikubwa vya kawaida ambavyo ni shilingi 600 – 800 milioni. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye kila awezalo kuwakomboa wananchi wa Muleba katika jambo hili la kukosa barabara inayokwenda kwenye Hospital Teule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukubwa wa Wilaya ya Muleba na jografia yake barabara zifuatazo zipandishwe hadhi kuwa barabara za *TANROADS*. Barabara ya Kanyambogo – Ibura – Kamachumu na Nshambu – Mushabogo – Rutoro. Eneo hili lina mashamba ya Ranchi za

*NARCO* ambayo yamekuwa na migogoro kwa muda mrefu, bila barabara ya kudumu hatuwezi kuendeleza eneo hili muhimu. Aidha, hivi majuzi wananchi wanne wameuawa, nyumba 20 kuchomwa moto na watu watano kujeruhiwa. Uhasama kati ya wakulima na wafugaji unaongezeka kwa sababu barabara mbovu zinawafanya Polisi kutowajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni Kasharunga – Kitewe- Burigi. Ziwa Burigi ni eneo jipya la uchumi Wilayani Muleba lakini hadi leo hakuna barabara ya kufika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni barabara ya Kasharunga – Karumbi – Kyebitembe – Kosindonga na Kiziromuyaza – Kyota – Kogurumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi zikiwa chini ya *TANROAD,* tutaiwezesha Halmashauri kushughulikia barabara nyingine zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri na kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kwa kujikita zaidi katika eneo la Wilaya ya Biharamulo au Jimbo la Biharamulo Magharibi. Hakika hali ya ujenzi wa barabara unatia moyo na unaridhisha hakika japokuwa kuna baadhi ya mapungufu hasa kwa baadhi ya mazingira au mikataba ya ujenzi wa barabara hizi kutokuwa rafiki kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika suala la mazingira halipewi usimamizi wa kutosha sehemu ambazo ujenzi wa barabara umefanyika, kuna mashimo makubwa yameachwa bila kufukiwa. Aidha, sehemu za mchepuko kwenda kwenye makazi ya watu hazitengenezwi vizuri, hakuna madaraja au vivukio vinavyotoka barabarani kuelekea kwenye makazi ya watu. Naiomba Serikali kuangalia au kupitia upya mikataba yake hususan suala la uharibifu wa mazingira, maeneo mengi mifereji ya

kuchepusha maji haiwekwi na kufanya uharibifu wa barabara kutokana na maji kutengeneza mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabara ya Kagoma – Lusahunga, kilometa 154, ujenzi huu unaendelea vizuri japo bado eneo kidogo ujenzi ukamilike. Niombe Wizara sasa ifanye hima kukamilisha barabara hii kwani sasa tunaona hakika umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia maeneo mengi ujenzi wa barabara hii kuna sehemu bado watu wana madai madogo madogo ya fidia. Naishauri Serikali na Wizara kufanya tathmini mapema kabla ya kufanya milipuko na baada ya ulipuaji wa miamba. Hapa tutaondoa tatizo la watu kudai fidia pasipo na uhakika wa madai.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudi zinazoendelea za ujenzi wa barabara ya Biharamulo - Kalebezo hadi Bwaga – Unyovu, mpaka sasa mkandarasi yupo kazini na kazi inaendelea. Kubwa tu niombe na nisisitize yale niliyokwisha shauri hapa mwanzoni. Naomba kazi hii ifanyike haraka kwa vile ni sehemu ya barabara muhimu ambayo imesahaulika kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa hoja ya ujenzi wa barabara za eneo la Mijini kilomita nne kama sehemu ya ahadi ya Rais lakini mpaka sasa hakuna dalili za wazi za kufanyika kwa shughulli hii eneo la hapo Biharamulo Mjini tofauti na upembuzi wa barabara toka *junction* ya Ng'ambo hadi Makao Makuu ya Boma la Wilaya. Naiomba Wizara kufanya juhudi hizo za makusudi ili jambo hili lifanyike kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, naipongeza Wizara na kwa njia ya pekee, Dkt. John Pombe Maghufuli kwa jitihada anazozifanya kuhakikisha barabara hizi zinapitika kwa kipindi chote.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza wizara kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya

katika majukumu ya wizara bila shaka ni matokeo ya usimamizi mzuri wa viongozi wake kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Magufuli na Mheshimiwa Naibu wake Ndugu Lwenje. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Sumbawanga – Kanazi na Kanazi – kizi – Kibaoni.:-

(i) Kazi inayoendelea katika Barabara hizi haina kasi inayofanana na kasi ya wizara, kulikoni?

(ii) Wananchi wangependa kupata matokeo ya haraka ya thamani ya fedha inayowekezwa.

(iii) Lakini pia tupo mwishoni mwa muda wa kumalizika mradi lakini bado mradi uko chini ya 50% ya utekelezaji. Naomba dosari zilizopo zibainishwe na kumalizwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia; katika ujenzi wa barabara hii katika miradi yake ya Sumbawanga – Kanazi na Kanazi – Kizi – Kibaoni wananchi katika vijiji vyote wamefidiwa vizuri isipokuwa Kijiji cha Chala peke yake. Tunaomba wizara iliangalie jambo hili kwa namna walivyowatendea wananchi wengine. Kama fedha haitoshi hata waahidiwe walipwe kidogo kidogo kulingana na fedha itakavyopatikana. Kutowalipa kabisa sio sahihi kwa kuwa wananchi wote katika vijiji vyote wamelipwa Serikali yetu haina utamaduni wa kuwabagua wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa maana ya RCC na Board ya barabara mtazamo umeonyesha kuitaka Serikali itazame uwezekano wa kuwalipa fidia kama ilivyofanya kwa wananchi wa vijiji zaidi ya ishirini vikiwemo vya Kanondo, Fyengelezya, Nkundi, Kipande, Kantawa, Milundikwa, Kasu, Mkole Lyazumbi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kupandisha hadhi ya Barabara za Nkana – Kala km 67 na Kitosi – Wampembe km 68. Tumeomba kupitia RCC, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa na pia Kamati ya Kitaifa ilikuja na kuthibitisha umuhimu na sifa za barabara hizo lakini wizara haijaridhia bado. Naiomba wizara kulipa umuhimu mkubwa jambo hili. Halmashauri ya Wilaya Kanwe haizimudu barabara hizi na ni muhimu kiuchumi, kijamii na kiusalama maana zinaenda mpakani.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa wizara hii kwa uchapaji kazi mzuri. Pongezi za pekee nazitoa kwa Waziri wa wizara hii Mheshimiwa John Pombe Magufuli (Mb) kwa ufuatiliaji wa kazi kwa makini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la barabara Wilayani Tarime: Napenda kutumia nafasi hii kueleza kwa masikitiko makubwa kuhusu suala la barabara wilayani Tarime. Kijiografia Wilaya ya Tarime ina barabara nyingi lakini zinazohudumiwa na Tanroads ni hizi zifuatazo:-

Barabara ya Nyamwaga Road itokayo Tarime Mjini – Kibumaye – Kemakorere – Nyamwaga – Nyamongo hadi Mto Mara umbali wa kilometa 53. Barabara hii ndiyo inayounganisha Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Serengeti. Ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami tangu mwaka 2008 hadi sasa ni kilometa tatu tu zimejengwa. Ni aibu. Namshauri Waziri angalau kupitia Serikali hii ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aache kumbukumbu ya kudumu wilayani Tarime kwa kuikamilisha barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa wakazi wa Tarime kwani ndiyo njia pekee ya kusafirisha watalii toka mpaka wa Sirari hadi Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Naishauri Serikali ishirikiane na Mwekezaji wa Mgodi wa North Mara ambaye alishawahi kuonesha nia ya kuchangia katika ujenzi wa barabara hii ili barabara hii ikamilike haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, *Security Road* itokayo Rorya kupitia Susuni – Remagwe – Sirari – Gwitiryo – Nyabisaga – Borega – Kimusi – Nyantira – Muriba hadi Kegonga. Hii barabara inapakana na nchi ya Kenya. Cha kushangaza ni kwamba nchini Kenya barabara hii inapitika muda wote (upande wa Kenya) kwani imejengwa kwa kiwango cha changarawe lakini nchini Tanzania ni aibu kwani mvua zikinyesha siku mbili tu barabara hii haipitiki – TUTAFAKARI NA KUFIKIRI ZAIDI. Je, Mheshimiwa Waziri umeshindwa nini kuhakikisha kuwa barabara hii inawekewa changarawe au kama si lami?

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyamwaga – Muriba. Kipande hiki cha barabara ni muhimu kwa uchumi wa WanaTarime kwani ndiyo barabara pekee inayosafirisha mazao ya chakula/biashara toka ukanda wa juu hadi Mjini Tarime. Namshauri Waziri aiwekee lami barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyamwigura – Gwitiryo. Barabara hii ni muhimu sana katika kuharakisha suala la maendeleo wilayani Tarime. Naishauri Serikali ijenge barabara hii kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa muda wote.

Mheshimiwa Spika, maombi ya barabara za kupandisha Hadhi: napenda kutumia nafasi hii kufikisha maombi ya barabara mbili ambazo Waziri Mkuu alipofanya ziara mkoani Mara aliwaahidi wananchi wa Tarime kuzipandisha hadhi kwani ni mzigo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Barabara hizo ni:-

(i) Barabara ya Mangucha – Masanga – Masurura – Gibaso – Mrito

(ii) Barabara ya German Road – Nyamongo – Kibasuka – Manga – Komaswa.

Naamini taratibu zote zimefuatwa na sasa kilichobaki ni utekelezaji. Hivyo namsihi Waziri apokee maombi ya WanaTarime kuhusu hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara zingine za Mkoa wa Mara:-

(i) Barabara ya Nyamuswa – Bunda

(ii) Barabara ya Bunda – Kisorya

(iii) Barabara ya Makutano – Butiama – Nyamuswa – Mugumu Loliondo – Mto wa Umbu.

Hizi barabara zote ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Mara na sehemu nyinginezo za jirani. Hivyo naishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete kupitia wizara hii ya ujenzi kuhakikisha kuwa barabara hizo zinajengwa na kukamilishwa haraka iwezekanavyo ili kuharakisha suala la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu wakala wa majengo, ambapo napenda kuikumbusha Serikali kuwa ilitoa ahadi kupitia wizara hii kujenga nyumba za Serikali wilayani Tarime ili kuwawezesha wafanyakazi na watumishi wa Serikali kupata makazi ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza barabara za Tarime zijengwe kwa lami (Barabara ya Nyamwaga Road) na barabara zinazobaki zijengwe kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwa niaba ya wananchi wa Rombo, kuendelea kutoa shukrani za dhati kwa Serikali, kwa kutimiza ahadi yake ya kujenga barabara ya Kamwanga – Tarakea; Tarakea – Mkuu na Mkuu – Marangu – Mwika – Kilacha kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tunampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara kwa kazi

nzuri ambayo wizara inafanya hapa nchini. Pamoja na hayo ningependa kuleta maombi yafuatayo ili kuboresha barabara yetu na kuifanya idumu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Malori makubwa yanayobeba mahindi kutoka Soko la Himo na Pozolana kutoka machimbo ya Makanga yanapita kwa ujanja kwa kupunguza mzigo kabla ya mizani ya Himo na baadae kuipakia tena eneo la Kilacha na kuanza safari kupitia Mwika Tarakea na kuingia Kenya.

Hivyo basi mizani hata ya kamba inahitajika eneo la Rombo ili kudhibiti uharibifu huu. Vilevile barabara imekatika eneo la Mamba Kisambo kuelekea kwa makundi. Mkandarasi ameziba kwa kupaka lami juu yake lakini ufa bado unaonekana.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka jana na katika maswali niliiomba wizara kurejesha nyumba za wananchi wa Kijiji cha Makiidi eneo la Maureni ambazo ziliuzwa na Serikali kwa makosa.

Wananchi walichangishana na kujenga nyumba hizo kwa nguvu zao ili wataalam kama wageni, *veterinary officer* na kadhalika wapate makazi. Baada ya kuuza nyumba hizi tumepeleka malalamiko katika ngazi zote na hata wizarani lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Tunaomba mwaka huu hatua au kauli itolewe kwani hatutaki kuvutana na Serikali mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika kata ya Ubetu – Kahe eneo la Mashiwa, kuna kambi ya ujenzi ambayo ilikuwa inatumika wakati wa ujenzi wa barabara. Jirani na kambi hiyo kuna kituo cha watoto walemavu na yatima. Tunaomba kambi hiyo yenye majengo madogo matatu, yatolewe kwa chama cha walemavu wilayani Rombo ili yatumike kama kituo kwa ajili ya kulelea watoto hao yatima na walemavu wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naendelea kuipongeza wizara na naunga mkono hoja.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ukurasa wa 90 ameelezea juu ya fedha takribani Shilingi 5,287.74 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Barabara ya NDUNDU – SOMANGA (60 km).

Mheshimiwa Spika, ahadi kama hii ya wizara ilitolewa mwaka wa fedha 2011/2012 lakini barabara haijakamilika. 2012/2013 pia zilitengwa 4,077.25 lakini hazikutoka zote na barabara haijakamilika na Mheshimiwa Rais kwenye ziara yake mwaka huu (2013) aliahidi barabara ingekamilika mwezi July 2013. Kipande cha kilometa 29.5 kilichobaki na sasa Mheshimiwa Waziri anakuja na ahadi ya kukamilisha barabara hii 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, je, Ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi ya mikoa ya Kusini kwamba barabara ingekamilika mwezi July 2013 imekwamishwa na jambo gani? Je, Mheshimiwa Waziri ni nini hasa kinakwamisha kukamilika kwa barabara hii takribani miaka 8 sasa?

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa barabara ya Vikumburu Mloka kupitia Mkongo Ruwe hadi Ikwiriri inahudumiwa na mkoa lakini Mheshimiwa Spika matengenezo ya barabara hii hayaendani kabisa na pesa zinazotengwa. Je ni nini kinasababisha barabara hii kutengenezwa chini ya kiwango na matengenezo yake yanakuwa ya kusuasua wakati pesa zake zinaonekana tunapokutana kwenye vikao vya mfuko wa barabara Mkoa wa Pwani?

Mheshimiwa Spika, Barabara inayoenda katika Halmashauri ya Wilaya Rufiji imekuwa ikifanyiwa matengenezo chini ya usimamizi wa mkoa lakini inaharibika mara kwa mara kutokana na matengenezo yake kuwa chini ya kiwango. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza

barabara hii ya Nyamwage – Utete kwa kiwango cha lami ili kuondoa kabisa usumbufu wanaopata wakazi wa wilaya ya Rufiji hasa wagonjwa wanaopelekwa Hospitali ya Wilaya (UTETE) kipindi cha masika (Mvua).

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, matuta ya barabarani hasa katika maeneo ya *Highways* yanaleta kero kubwa kwa watumiaji wa barabara. Mara nyingine hakuna alama yoyote inayoonyesha kwamba mbele kuna tuta na hivyo kusababisha mshtuko mkubwa kwa wasafiri wakiwemo wanawake wajawazito na watoto. Njia mbadala itafutwe ya kuwakamata madereva wanaozidisha mwendo katika maeneo ambayo si ruhusa.

Mheshimiwa Spika, uharibifu unaotokea kwa magari ni mkubwa, kuvunjika na wasafiri kuumia pale wanapoparamia tuta ghafla. Ziwekwe Cameras barabarani ili kuwabaini madereva ambao hawafuati sheria za uendeshaji hasa katika kuongeza /kuzidisha mwendo. *Automatic Cameras* zitarahisisha kazi na wavunja sheria wataongeza pato la Taifa kwa kulipa faini kwani hawataweza kukwepa kosa walilolitenda barabarani.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Matumizi Stahiki ya nguvukazi ni chuo cha namna gani na chuo hicho kimejengwa wapi?

Mheshimiwa Spika, hali ya Dar es Salaam inakuwa mbaya kila siku kutokana na msongamano wa magari. Shughuli za maendeleo kwa Taifa zinafanyika kwa muda mchache sana kwani baadhi ya watu hufunga ofisi mapema ili kuwahi kurudi nyumbani.

Watu hufika ofisini saa 4 asubuhi na kuanzia saa 8 mchana huanza kugeuza. Wapo wachache wanaowahi zaidi ya hapo na pia wapo wanaokawia kuondoka. Hata hivyo msongamano unakera na unapunguza sana muda wa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, jitihada zifanyike kuwa na mfuko maalum wa kuendeleza majiji (barabara) yakiwemo Dar es Salaam, Arusha na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, suala zima la fidia liangaliwe vizuri. Wananchi wengi wanaumizwa pasipo kutendewa haki pale inapobidi kuwalipa fidia ili wahame kupisha ujenzi/upanuzi wa barabara. Wapo watu wanaolipwa fidia pungufu kulingana na uhalisia wa mali zake, wapo wanaozidishiwa na wengine kutolipwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka husika itekeleze zoezi la ulipaji fidia kwa makini na kwa wakati ili kupunguza changamoto zilizopo ambazo mara nyingine watu hasa wazee wastaafu na wanawake wajane wamepoteza maisha kwa mshtuko wa moyo wanapobomolewa nyumba zao na kutopewa fidia stahiki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na salaam za pongezi kwa wizara hii kwa kukabiliana na changamoto nyingi na usimamizi wa ujenzi wa barabara naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mosi, Mkoani Mtwara tunayo barabara ya ulinzi ambayo ni muhimu sana kwa kilimo, lakini mpango wake wa kuikarabati au niseme kuifufua ni mdogo. Naishauri Serikali kuitengea fedha za kutosha ili iweze kufungulia yote na hivyo kutumika kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ipo haja ya kusimamia kwa dhati mradi wa barabara ya Masasi – Songea hadi Mbambabay. Ikumbukwe kuwa ugunduzi wa Gesi kwa mikoa ya mtwara na Lindi utatupeleka Tanzania kwenye nchi za uchumi wa kati lakini matumizi au mauzo ya gesi hiyo yatategemea pia urahisi wa kibiashara na mawasiliano kusini kwa nchi ya Tanzania. Nchi kama Malawi, Zambia na kadhalika watavutika kibiashara kutumia bandari ya Mtwara na ununuzi wa gesi kama miundombinu ya barabara hiyo

itakuwa imekamilika na kupitika kirahisi. Hivyo, nashauri mkakati mahususi uwekwe ili kwa muda usio mrefu barabara hiyo ikamilike na kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wapo wafanyakazi wa Wakala wa Meli inayoitwa CMA LGM TANZANIA LTD wanaofanyia shughuli zao kwenye jengo la HARBOUR VIEW TOWER lililopo mtaa wa Samora karibu na PPF HOUSE ambao wamekuwa wakilalamika kutingishika kwa mara kwa mara kwa jengo hilo. Je, ni lini wataalam wa majengo watakagua jengo hilo na hivyo kutoa ushauri wa kitaalam ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kuathiri Watanzania kupata ulemavu, magonjwa na hata vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kabisa kuunga mkono hotuba ya wizara hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa utendaji wake mzuri pia nampongeza Naibu wake Mheshimiwa Lwenje kwa kumsaidia vizuri Waziri wake ikiwa ni pamoja na watendaji wote waliopo katika wizara hii kwa kweli hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nielezee kuhusu umuhimu wa barabara ya KIBAONI – MUZE – MTOWISA – ILEMBA – KAOZE hadi KILYAMATUNDU. Serikali ifikirie namna ya kujenga barabara hii kwa LAMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii yenye kilometa 234.58 ni barabara muhimu sana katika ukanda wa Ziwa Rukwa, ni barabara yenye changamoto nyingi kutokana na kuwa karibu na mlima hivyo ina mito mingi inayosababisha kuwa na;

| | |
|---|---|
| MADARAJA | – 14 |
| KALVATI | – 9 |
| MADRIFTI | – 34 |

Hivyo kutokana na barabara kujengwa kwa udongo, barabara hii hubomoka mara kwa mara na kusababisha Makorongo makubwa. Vilevile udongo uliopo katika ukanda huo ni laini mno mvua ikishaulowanisha hubomoka na kusafirishwa na maji ya mvua hivyo udhibiti na suluhu katika barabara hii ni kuiwekea LAMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, KIUCHUMI barabara hii ni muhimu sana kutokana na ardhi yake kuwa na rutuba nyingi inayostawisha mazao mengi, Mpunga, Mahindi, Ufuta, Ulezi, Mtama, Mbaazi, Karanga na kadhalika pia zao la Samaki linalotokana na Ziwa Rukwa na pia mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukanda huu pia unastawisha karibu aina zote za matunda kama Machungwa, Ndizi, Parachichi, Minazi, Michikichi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba viongozi wa wizara hii kutembelea katika eneo hili ili kujionea umuhimu uliopo katika barabara hiyo Mheshimiwa Naibu Spika, ukanda huu ni tegemeo la Mkoa wa Rukwa. Hivyo ni muhimu kulipa kipaumbele kuwa na barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea pia kuiombea barabara ya KALAMBANZITE ILEMBA, ichukuliwe na Wakala wa barabara TANROAD, kama ilivyokwishapendekeza Ziwa na BODI YA BARABARA Mkoa wa Rukwa na kupitishwa na kikao cha RCC Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kwa kumpongeza Meneja wa Tanroad Mkoa wa Rukwa. Kwa namna anavyojitahidi kujituma kwa kutumia uwezo wake, kusimamia vizuri matengenezo ya barabara za Mkoa wa Rukwa ziendelee kupitika wakati wote na hasa kipindi cha Mvua japo fedha tunazopangiwa ni kidogo sana. Ukilinganisha Mkoa wa Rukwa ni mkoa wenye mvua nyingi hivyo barabara na madaraja hubomoka kila wakati.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, licha ya juhudi kubwa za kujenga barabara nchini, juhudi ambazo atakaezibeba atakuwa mpumbavu, bado ubora wa barabara ni mdogo sana. Kuagiza makandarasi kurudia kujenga sio ufahari, ni ishara ya ufuatiliaji mdogo wakati wa kujenga. Serikali isimamie ujenzi wakati wa ujenzi na kuachana na kusubiri barabara zisizo na ubora kuisha.

Mheshimiwa Spika, kamati ya ushauri Mkoa wa Kigoma (RCC) iliomba TANROADS wasaidiane na Halmashauri ya Wilaya Kigoma katika kufungua barabara ya ufukweni mwa Ziwa Tanganyika (Mwandiga – Mwamgongo – Kapunga) yenye urefu wa kilometa 28. Naomba wizara itusaidie ili kufikiwa malengo haya na kuwapa wananchi usafiri mbadala.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuanza mchakato wa kujenga kipande cha Kidahwe – Kasulu. Juhudi za kujenga Nyakanazi – Kasulu ziongezwe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) ina jukumu la kujenga miundombinu kwa ajili ya mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT) kwa ukubwa wa gharama za mradi huu yaani shilingi bilioni 289.9 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ni muhimu hatua za haraka zikachukuliwa kurekebisha kasoro zinazoendelea katika awamu ya kwanza ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mosi, kumekuwepo na msongamano mkubwa katika ujenzi unaoendelea katika barabara ya Morogoro (Kimara Kivukoni). Wizara ikumbuke kwamba kabla ya kuanza kwa ujenzi huo mwanzoni mwa mwaka 2011 nilitahadharisha kupitia kikao cha bodi ya barabara kwamba ipo haja ya kujenga barabara za pembezoni ili zitumike kama mbadala. Pia, nilipendekeza usimamizi wa karibu kwa upande wa mkandarasi kuhakikisha anafungua njia mbadala kwa kadri ya masharti ya mkataba. Kwa kuwa matatizo hayo yameongezeka sana toka mwanzoni mwa mwaka 2013; Wizara ya Ujenzi ieleze ni hatua

zipi zimechukuliwa kurekebisha hali hiyo na ni kwanini njia zinaendelea kufungwa katika maeneo ambayo kwa sasa hakuna ujenzi unaoendelea. Aidha Mfuko wa Barabara uongeze ruzuku kwa upande wa Manispaa ya Kinondoni ili barabara ya Mburahati – Mabibo ambayo kwa sasa inajengwa nusu kwa kiwango cha lami nyepesi iweze kumaliziwa. Barabara hii inasaidia kupunguza foleni kama njia mbadala ya kipande toka Magomeni mpaka Manzese wakati huu ambapo ujenzi unaendelea. Kwa upande mwingine ili kupunguza foleni kubwa itakayojitokeza eneo la Ubungo mataa wakati ujenzi utakapoanza zabuni ya Barabara ya Kimara – Korogwe – Kilungule External (Mandela) ihusishe kilometa zote 9 badala ya 3 pekee na ujenzi wake uharakishwe kwa kuwa ni njia mbadala ya malori kwenda Bandarini.

Mheshimiwa Spika, pili, pamoja na kuwa TANROADS ina jukumu la ujenzi wa vituo vya mabasi ya BRI, ishirikiane pia na DARY na jiji kuharakisha ujenzi wa kituo mbadala cha mabasi ya mikoani badala ya kituo cha mabasi cha Ubungo. Ikumbukwe kwamba kwenye mikataba ya awali ya 2008 kazi hiyo ilikuwa sehemu ya *"Addentum."*
Mwaka 2011 kupitia bodi ya barabara nilipendekeza fidia ya eneo la nyuma ya UBI itolewe kituo kipanuliwe hata hivyo hatua hazikuchukuliwa. Wizara ya ujenzi imechukua hatua gani kwa kushirikiana na mamlaka zingine kuhakikisha agizo la Rais la Septemba 2012 la ujenzi wa kituo mbadala cha kudumu limetekelezwa? Mpaka sasa hakuna kazi ya haraka inayotekelezwa katika eneo la Mbezi Luis lililopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kwakuwa toka mwaka 2003 miaka kumi imepita mradi huu awamu ya kwanza umecheleweshwa, awali ulipaswa kukamilika 2010; ukasogezwa 2012 sasa unatajwa kukamilika Machi 2015. Wizara ya ujenzi itoe mrejesho wa hali halisi kwa wizara ya uchukuzi na SUMATRA. Hii itawezesha mapitio kufanyika kuhusu uamuzi wa kusitisha utoaji wa leseni mpya kwa daladala kwenye mti zitakazoathiriwa na awamu ya kwanza. Tayari kuna upungufu na usumbufu kwa wananchi ikizingatiwa daladala 1500 zinatarajiwa kuondolewa kwa

awamu ya kwanza pekee. Mfumo jumuishi *(integration)* na mti mbadala *(alternative route)* unahitajika hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2012/2013, naomba awali ya yote kupewa majibu juu ya masuala niliyoyahoji katika michango yangu ya tarehe 6 Julai 2012. Kitabu cha majibu ya Wizara ya Ujenzi hakikufika kwa wakati na hakikutoa majibu kwa ukamilifu kama Waziri wa Ujenzi alivyoahidi kwenye majumuisho ikiwemo kuhusu utekelezaji wa mwaka wa fedha 2011/2012. Waziri wa Ujenzi arejee kumbukumbu rasmi za Bunge za Mkutano wa nane kikao cha kumi na nane ukurasa wa 106, 107, 108 na 109 na pamoja na mambo mengine kunieleza hatua alizochukua kuhusu masuala yafuatayo:

Mosi, juu ya usanifu wa *Fly over* ya makutano ya Mandela na Morogoro katika eneo la Ubungo na lini ujenzi utaanza.

Pili, kupatiwa ripoti ya mpango wa awali wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze mpaka Morogoro kwa utaratibu wa PPP na lini ujenzi utaanza.

Tatu; kutokutengwa kwa fedha za barabara za mzunguko na za pembezoni za kupunguza msongamano kwa miaka miwili mfululizo kwa kuzingatia mpango wa Taifa wa maendeleo, ni hatua zipi zilichukuliwa katika mwaka 2012/ 2013 kurekebisha hali hiyo?

Nne; kujirudiarudia kwa mgawanyo wa fedha zilizoitwa za kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam bilioni 899 kwa miaka mitatu mfululizo kwa miradi ile ile. Hali hiyo inajenga picha ya Dar es Salaam kuwa na fedha nyingi katika mwaka wa fedha unaojadiliwa kinyume na hali halisi. Hivyo naomba kupatiwa orodha ya fedha zilizotolewa kwa matumizi halisi ya miradi mikubwa ya Jiji la Dar es Salaam kwa miaka ya fedha 2010/2011, 2011/2012 na 2012/2013.

Tano; Waziri wa Ujenzi kumshauri Rais ili kiwango cha fedha kwa ajili ya barabara za mzunguko na za pembezoni

kuweza kuongezwa kwa kurejea mpango wa maendeleo. Je, ushauri huo ulifikishwa?

Sita; aidha Bunge lilipokaa kama Kamati kwa kurejea kumbukumbu rasmi za Bunge ukurasa wa 266, 267, 282 na 283 kuna masuala ambayo niliyaombea ufafanuzi ambayo sasa naomba mrejesho wa utekelezaji. Waziri wa Ujenzi alitaja kwamba katika Kasma 4138 fedha zilikuwa ni pamoja na za matengenezo ya barabara za Kimara – Kilungule (bilioni 1), Mbezi – Malamba mawili – Kinyerezi – Banana (bilioni 2), Tegeta – Kibaoni – Wazo – Goba – Mbezi (bilioni 2.1), Tangi Bovu – Goba (bilioni 1) na Kimara Baruti (Milioni 577). Hata hivyo, pamoja na kutengewa fedha hizo sehemu kubwa ya matengenezo hayajafanyika na barabara ziko katika hali mbaya. Ni kwanini hali hiyo ilijitokeza na nini hatma ya fedha zilizotengwa wakati ambapo wizara katika taarifa yake ya utekelezaji imeeleza kuwa fedha zilizotolewa kwa wakati?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kwa niaba ya watu wa Jimbo langu na nchi yangu kushauri Serikali haswa katika Wizara ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi katika nchi yetu ambayo ni muhimu kwa maana ya makazi lakini wakati wa uendelezwaji wake huko nyuma maeneo haya hayakupimwa na badala yake hivyo kufanya maeneo hayo kuwa yamejengwa kiholela.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yaliyojengwa kiholela mengi yapo maeneo nyeti tena muhimu katika mitaa ya miji mbalimbali, hivyo ningependa kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kununua maeneo hayo kwa njia ya kujenga nyumba na kushawishi wananchi wanaoishi maeneo haya kuhama kwa utaratibu ambao ni matumaini yangu kwamba wananchi wakiona nyumba nzuri na za maana zinajengwa kwa ajili yao sina shaka kuwa watakubali kuhama na huku Serikali sasa ikitafakari kuuza au kuboresha maeneo ambayo wamehamisha watu kwani maeneo mengi

yako sehemu muhimu kibiashara isipokuwa makazi holela yaliondoa hadhi ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu utaratibu huu ukazingatiwa kwani kwa hali ilivyo sasa makazi holela yamezunguka karibu maeneo muhimu katika miji yetu mfano Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na kwingineko ambayo ni muhimu kuendelezwa kwa ufasaha ili pia kuondoa msongamano wa makazi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Serikali inapaswa kutunga sheria kali kuhusu uuzwaji wa ardhi unaofanywa kienyeji katika miji mbalimbali, uwekwe utaratibu wa kila mtu anayeuza shamba au kiwanja kuwepo na ramani ya barabara na kwa ukubwa gani mtu anapaswa kukata shamba lake kuwa viwanja anapotaka kuuza, ni muhimu kuwepo na sheria itakayolazimisha kiwango cha mwisho cha ukubwa wa kiwanja, tofauti na sasa kwani kuna maeneo unakuta mtu anapimiwa kiwanja cha ukubwa wa chumba kimoja.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unaonekana ungekuwa muhimu katika Wizara ya Ardhi lakini msongamano wa magari katika miji yetu unasababishwa sana na makazi duni yasiokuwa na barabara hivyo kuleta tafrani na msongamano mkubwa wa magari na watu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri mnazofanya za kusimamia ujenzi wa miundombinu ya barabara Tanzania. Nawapongezeni sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe Makete; naishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga fedha za matengenezo ya barabara za mkoa za Makete. Barabara ya Njombe – Makete ipo kwenye mpango wa miaka mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 – 2015 kujengwa kwa

kiwango cha lami. Utekelezaji wa mpango/ilani unasuasua. Tunaomba Serikali itoe kipaumbele cha kutenga fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya barabara ya Makete – Mbeya kujengwa kwa kiwango cha lami; Barabara hii ni kiunganishi cha Mkoa mpya wa Njombe na Mkoa wa Mbeya (Isyonje). Barabara hii ni muhimu sana katika uchumi wa nyanda za juu kusini. Inapita kwenye Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Shamba la Ng'ombe wa Maziwa Kitulo. Hii barabara itafungua fursa za uchumi zilizopo Makete, Ludewa na Njombe na hasa kuuwezesha uwanja wa Songwe – Mbeya kuliingizia Taifa pato kubwa. Tunaomba barabara hii iingizwe kwenye miradi ya barabara ya MCC ya awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuendelea kujenga barabara za lami katika nchi yetu.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na wizara hiyo, naomba sana kumwomba Mheshimiwa Waziri kuhusu kutoa kipaumbele kwa barabara mbili muhimu. Nazo ni barabara za kutoka njia panda ya barabara za kutoka Dodoma kuelekea Wilaya ya Kongwa na Kiteto. Barabara hizo ni fupi tu na hazitakuwa mzigo kwa Serikali lakini ni barabara zenye umuhimu mkubwa sana kujengwa kwa lami kwa maendeleo ya wilaya hizo. Kongwa na Kiteto ni wilaya zinazozalisha sana Mahindi na kusafirishwa kwenda maeneo mengine ya nchi yetu. Hivyo kuunganisha wilaya hizo mbili na barabara ya Dodoma – Dar es Salaam – Dodoma kwa lami itachochea, siyo tu kilimo kwa manufaa ya nchi yetu, bali itahamasisha miji hii miwili, Kibaya, Kongwa (na Kibaigwa) kuendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana sana barabara hii hasa ya kuelekea Kibaya – Kiteto tuonee huruma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe – Lupembe naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za upembuzi yakinifu. Naomba Serikali itenge fedha haraka za kujenga kwa kiwango cha lami mara tu baada ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe – Makete; Rejea maombi yangu kwako kwamba barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi 2010/2015 lakini utekelezaji unachelewa. Tunaomba sana, barabara hii inaunganisha Njombe na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%. Kutokana na kazi nyingi na kubwa kubwa zinazofanywa na Serikali katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam sina sababu ya kutounga mkono hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, natambua miradi mingi ya ujenzi wa barabara inaendelea katika jiji la Dar es Salaam. Ombi langu jitihada zifanyike miradi hii imalizike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo mpaka sasa naomba ifanyiwe kazi kwa haraka ni ile ya Nzasa – Kilungule – Buza. Barabara hii itasaidia sana kupunguza msongamano Kilwa road. Magari yanayoenda Uwanja wa Ndege yatapitia barabara hii badala ya Kilwa road na Mandela.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha mabasi Mbagala Rangitatu pamoja na juhudi za Serikali kutujengea barabara nzuri Kilwa road lakini kunakuwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha hata misafara ya viongozi ipite kwa shida. Hali hiyo inasababishwa na mabus

kuegeshwa ovyo ovyo barabarani. Stendi ile ni kubwa na idadi ya watu Mbagala ni kubwa.

Ushauri wangu kwa Serikali tujengewe stendi kubwa kama ya Mbezi itasaidia kupunguza vurugu barabarani.

Mheshimiwa Spika, Nyumba za Wakala – zitolewe pia kwa wafanyakazi wa Serikali na ikiwezekana na kada za chini pia uelewa wa wananchi nyumba zile ni za Maafisa Wakuu wa Serikali tu. Si kwa watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais – Barabara za Zakhem – Mbagala kuu sasa nayo itekelezwe pale ni uwanja wetu wa safari kuelekea 2015 ni vyema mazingira ya barabara ile yakaboreshwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nikumbushie fidia kwa waathirika wa barabara ya Kilwa road. Wananchi hawa wanafanyiwa tafiti na kuundiwa kamati za matumaini kila siku ni vyema sasa Serikali ikatoe elimu kwa wananchi wake twende vizuri.

Mheshimiwa Spika, nasema kwa sababu mpaka sasa wananchi hawaelewi lakini mimi kama Kiongozi naelewa ndio sababu niko kimya.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu, Makatibu Wakuu. Endeleeni hivyo. Naunga mkono hoja 100%.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

(1) Ni lini Serikali itashughulikia barabara ya Ilagala – Kigoma kwa sababu barabara hii ni muhimu kwa kuwa inapita maeneo ya Kambi ya Jeshi ya Bulombola na vijiji vingi vya mwambao wa Ziwa Tanganyika, hivyo ni vyema barabara hii ikakarabatiwa ili iweze kupitika bila shida kwakuwa barabara hii inapita mpaka Kalia hadi Mgambo, lakini barabara hii inasuasua sana.

(2) Ni lini kipande cha Chaya – Nyahwa na Ilunde – Kaliua havina wakandarasi ili hii barabara ikamilike, je ni lini vipande hivi vitapewa wakandarasi?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya ya utekelezaji ya ilani ya uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana tena sana kumalizia kipande cha Ndundu – Somanga na utueleze lini sasa hiyo kazi itaisha na la pili Mheshimiwa "OMBI MAALUM". Mheshimiwa Waziri jimboni kwangu Mtwara mjini baada ya kugundulika kwa Gas ongezeko la watu limekuwa kubwa sana pamoja na magari makubwa na madogo yameongezeka sana Mheshimiwa kuna eneo linaitwa BIMA na hiyo barabara ni ya TANROAD katika eneo hilo la Bima kuna ajali nyingi sana zinatokea hapo. Mheshimiwa Spika, naomba sana tena sana Mheshimiwa kutusaidia kutuwekea Traffic Light katika eneo hilo na mwisho ni FERY ya Msanga Mkuu lini sasa itafika Mtwara.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie bajeti hii kwa kujielekeza katika changamoto zilizopo jimboni kwangu Mvomero.

(1) Ujenzi wa barabara Magole – Turiani – Mziha – Korogwe. Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hii unasuasua sana na moja ya sababu ni Serikali kutomlipa fedha Mkandarasi. Wiki iliyopita tarehe 10/5/2013 nilifanya ziara kama Mbunge wa jimbo husika kufuatilia na kujua sababu za kusuasua kwa ujenzi wa barabara hii na hasa kipande cha barabara ya Magole- Turiani – Mziha. Nilikutana na wasimamizi (TANROAD) na TIMU YA WAKANDARASI na wamenieleza kuwa wanadai Serikali fedha nyingi. Mathalani mkataba wa ujenzi baina ya Serikali na Kampuni ya China (CCECC) ni Shilingi 41,890,858,200.52 takribani 42 bilioni lakini mwaka huu wa fedha 2013/2014 mmetenga bilioni sita tu. Mpaka sasa mmewalipa fedha Shilingi 13.2 bilioni tu kati ya 18.175,672,168 ya kazi iliyokaguliwa na kuthibitishwa. Fedha

iliyotengwa mwaka huu 6 bilioni ni kulipa deni tu maana yake Mkandarasi atashindwa kuendelea na kazi. Naomba Serikali itoe tamko ili ahadi ya Rais Kikwete itekelezwe barabara hii ikamilike 2014.

(2) mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia kwa wananchi waliofuatwa na barabara. Nashukuru Serikali kuwalipa fidia wananchi wa Kijiji cha Kichangani baada ya kunisikiliza kilio chao nilichokiwasilisha hapa Bungeni na kikao cha RCC mwaka 2011. Naomba sasa Serikali itazame kulipa fidia wananchi wa vijiji vya Kigugu na Mbogo. Nimeshawasilisha malalamiko ya wananchi wangu Tanroad mkoa na Taifa. Nimefika na kuongea na wananchi hawa na Meneja TANROAD mkoa ameahidi atafika eneo hili. Naomba wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri utamke lini utafika usikilize kilio cha wananchi wa vijiji hivi kinyume na hivyo wananchi hawa watakuwa hawajatendewa haki na zoezi la ujenzi linaweza kukwama.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, Upandishaji hadhi barabara; Dakawa – Mkindo; Mhonda – Mafuta – Ubiki – Pemba; na Langali – Nyandira – Luale. Hizi barabara tulishazipitisha katika kikao cha Bodi ya barabara. Kwa hali ilivyo Halmashauri ya Mvomero haiwezi kuzihudumia na ni barabara zinakidhi vigezo vyote vya kupandishwa hadhi ya kuwa barabara za mkoa. Je, tatizo lipo wapi? Mwaka jana ulinijibu vikao vya mkoa vipitishe sasa mbona wizara haijatujulisha kuhusu mapendekezo ya kikao cha Bodi ya barabara na RCC.

(4) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha kwa ajili ya barabara za Mvomero – Ndole – Kibati – Lupanga na Sangasanga - Langali. Pamoja na jitihada za TANROAD Mkoa kuendelea kufanya matengenezo ya barabara hizi bado fedha zinazolengwa ni kidogo sana kuweza kukidhi matengenezo ya barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali kutenga fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri wangu kwa wizara hii kuhusu pale ambapo inadhamiria kutekeleza mradi mkubwa wowote wa ujenzi wa barabara. Pamoja na makisio ya gharama zote za ujenzi, mara nyingi imekuwa haizingatiwi gharama za kulipa fidia kwa waathirika kihalali wanaopitiwa na *Road Reserve*.

Mheshimiwa Spika, kuacha kuwalipa katika muda muafaka wale waathirika kunaipelekea Serikali kulipa gharama kubwa kutokana na kuongezeka thamani ya fedha ya maeneo husika. Na pia husababisha usumbufu kwa raia ambao kwa mujibu wa sheria ya barabara hawaruhusiwi kuendeleza kwa vyovyote maeneo yanayopitiwa na Hifadhi ya barabara.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, elimu shirikishi kwa watumiaji wote wa barabara ni muhimu sana kwa matumizi endelevu ya barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, mipango shirikishi kati ya Wizara za Ujenzi, Uchukuzi, TAMISEMI, Mambo ya Ndani na kadhalika hasa umuhimu wa kuunganisha bandari na mifumo ya Reli (na hasa reli ya kati ambalo ni lango kuu la kufungulia kwa mapana uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uaminifu /uadilifu na uwajibikaji kwa viwango vinavyostahili /vinavyokubalika kitaalam kwa wakandarasi na wahandisi wetu vitiliwe mkazo na wanaokiuka hatua stahiki za kisheria zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kitengo cha *Risk Management* kiimarishwe/kianzishwe kwenye kila idara katika Wizara ya Ujenzi. Wizara ishirikiane na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuandaa/ kuelimisha vijana wa kitanzania katika taaluma hii ya *Risk Management* katika uhandisi ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya usimamizi (Wakala wa Majengo) iangaliwe upya iweze kuendana na ukuaji /kasi

ya ujenzi wa nyumba na hasa za ghorofa. Mfano; nyumba ya ghorofa 17 – katikati ya jiji (Indiragandi – Street) hatua zichukuliwe mapema kabla maafa/janga makubwa kutokea kama ilivyotokea tarehe 29/03/2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Ulinzi zishirikiane kwa kutumia wataalam ndani ya wizara hizi kujenga "gati" (vituo) maeneo ya Bagamoyo, Mbweni, Kunduchi, Mbezi Beach, Msasani kwa ajili ya kuanzisha usafiri wa Boti kutoka Bagamoyo hadi katikati ya Jiji ili kupunguza msongamano wa magari katikati ya jiji.

Mheshimiwa Spika, adui mkubwa wa barabara ni maji, maji, maji, …………maji. Mikataba yote ya ujenzi wa barabara isisitize sana suala la *drainage system*.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa watanzania ni muhimu sana kwa kushirikiana na TAMISEMI kuhusu kutupa takataka ovyo ovyo (mifumo ya kuhifadhi takataka); husababisha kuziba kwa mifereji ya maji iliyopo na hasa mijini (mfano Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, malori makubwa na hasa yanayobeba mafuta ni marufuku kupita katikati ya Jiji la Dar es Salaam wakati wa mchana. Nashauri barabara ya Mandela ifungwe kwa upande mmoja kuanzia saa 3 usiku hadi saa 11 alfajiri ili iwe rahisi kwa malori yote yatokayo bandarini kutumia barabara hiyo kwa wakati huo. (Wizara za Ujenzi, Uchukuzi na Mambo ya Ndani zishirikiane).

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Wizara na *TANROADS*.

Pamoja na kazi nzuri zinazoendelea naomba kupata maelezo katika maeneo ya barabara za Mkoa Muheza – Amani na Boza Janction (Pangani) – Muheza.

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja Mjini Muheza – Barabara – Muheza – Amani. Baadhi ya wananchi Mjini Muheza wamekuwa wakilalamika kwamba daraja sio imara na lina ufa. Nilitembelea daraja hilo wakati wa ujenzi ila sikuona hali hiyo inayolalamikiwa. Kwa kuwa kuna shughuli za uchaguzi wa madiwani eneo la mjini Muheza, "NAOMBA KAULI YA HALI HALISI YA UBORA WA DARAJA HILO" na kama upo udhaifu ni lini marekebisho hayo yatafanyika.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, hali mbaya sana ya barabara ya Muheza – Amani. Mkandarasi aliyekuwepo *Y. N. INVESTMENTS & LUCKY CONTRACTOR* chini ya mpango wa PMMR aliondolewa kutokana na ukweli wa kushindwa utendaji. Baada ya *TANROADS* kuchukua jukumu wakandarasi wawili waliopewa barabara hiyo pamoja na ile ya Boza JCT – Muheza bado utendaji wao hauridhishi. Kuanzia wiki iliyopita 5/5/2013 – 14/5/2013 (leo 14/5/2013) barabara hiyo haipitiki kabisa kutoka eneo la Kisiwani lililo Gate la maliasili kuelekea (juu) – Amani Police – Kibaoni – Malaria – Mwamkoro. Kwa hali hiyo ni wazi kwamba sasa magari ya kubeba CHAI kutoka mashamba makubwa mawili ya Mashamba 15 ya wakulima wadogo Tarafa ya Amani yamekwama!

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, Fedha za Mradi 2012/2013 na 2013/2014. Fedha zinazotengwa ni za barabara mbili kwa kandarasi wawili na mmoja ana barabara ya Boza *JCT* – Muheza na sehemu kubwa ya Muheza – Amani, na wa pili ana sehemu ndogo ya Muheza – Amani kiasi hakitoshelezi na kasi hairidhishi. Je, fedha zilizotengwa 2012/2013 zimetumika vipi hadi kufikia mwisho wa mwaka.

(4) Barabara – Muheza – Amani kutembelewa na Mheshimiwa Waziri – Ujenzi 2013/2014. Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa naizungumzia kila mwaka tangu 2000 barabara hii Muheza – Amani.

Nilifupisha ziara ya aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Mwakyembe kwa hofu ya usalama wa msafara

katika eneo baya zaidi la barabara hiyo "kutoka" "Gate la Maliasili Kisiwani – Amani Police – Kibaoni".

Naomba rasmi sasa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi utembelee barabara hii uone hilo eneo husika! "kwa usalama pia usiende mwezi huu MEI 2013 au June 2013 kipindi hiki ni cha mvua! Utaweza kushuhudia "DHAMIRA YA MHESHIMIWA RAIS KUAHIDI KUJENGA BARABARA HII KWA KIWANGO CHA LAMI" AHADI YA 2005 NA 2010.

Nafahamu fedha za ujenzi hazikutengwa 2013/2014! Hata hivyo upo mpango wa fedha za MCC (Z). Naomba sana Serikali itumie fursa hiyo kuondoa kero hii ya barabara ya Muheza – Amani (34 km); 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote "NAUNGA MKONO HOJA".

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa Luaege. Kazi inaonekana, usimamizi ni wa uhakika. Nadiriki kusema tungekuwa na mawaziri kumi (10) kama Mheshimiwa Magufuli Tanzania tungekuwa tumepiga hatua. Anatumia kanuni na Sheria zilizoko na anasimamia.

Mheshimiwa Spika, napenda nishauri ujenzi wa majengo usimamiwe vizuri zaidi. *Experience* inaonyesha mameneja wa *TANROADS (almost all over the country)* ni watu mahiri na wanaofanya kazi *with a commitment*. Nashauri *Engineers* kama wa TANROADS wasimamie ujenzi wa majengo *Building Permits* ikiwezekana zitolewe zikiambatana na majina ya wasimamizi *(Consultants, Structural, Engineers etc)* ambao watateuliwa/watakuwa chini ya uangalizi wa Wizara hii. Majengo ya urefu fulani iwekwe Sheria/Kanuni ni mjenzi daraja gani atajenga, nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, nyumba zinazojengwa na TBA ikiwezekana zijengwe na kuuzwa kwa bei nafuu kwa

wananchi. Napongeza kuanza kikosi cha ujenzi naamini kitafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga magari ya Serikali yatumike tu mpaka jioni then yapack. Sasa hivi STK nyingi zina *plate numbers 2*, ya Serikali na ya *Private*. Ninaomba Wizara ilichunguze hili na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa ujenzi wa barabara mkoani Kilimanjaro. Kiasi kilichotengwa kwa barabara hizo ni kidogo, mfano barabara za Moshi vijijini ambazo ulishaanza. Mfano barabara za Mkoa kilometa 131.02 tu, wakati idadi ya barabara ni kilometa nyingi.

Mheshimiwa Spika, liko daraja lililoko kata ya Kikavo chini mto Kikavo linaitwa la mhepo, maeneo ya TPC. Daraja hili ni la kamba zilizounga mataruma ya reli. Daraja hili ni refu na mto una kina kirefu kila leo watu wanaanguka huko na kufa. Uongozi wa Mkoa, mimi mwenyewe na uongozi wengine wote. Wanawake wajawazito wanateseka wakati inapobidi waende Hospitali katika kiwanda cha sukari cha TPC. Watoto wadogo nao wanaanguka ndani ya mto, wanavunjika na wengine kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iwahurumie wanawake na wananchi wa eneo hilo ijenge daraja la uhakika. Naelewa daraja liko katika Jimbo la Hai, lakini Serikali ya CCM ni Serikali inayojali wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ni Wizara inayosimamia kikamilifu tasnia ya uchukuzi, usafirishaji na upatikanaji wa maendeleo kupitia barabara zetu mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa uchapakazi wake mzuri na wa uhodari hasa pale nilipolalamika katika Bunge la Bajeti la mwaka 2011 kuhusu daraja la Nzaga lililopo

bararaba ya kutoka Msaginya kwenda Urwila ambayo ni Mpanda – Tabora (Koga) yenye urefu wa (kilometa 192.96) daraja ambalo lilihatarisha maisha ya watu, lakini mpaka mwaka jana 2012 daraja lilikamilika na maroli yanapita bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi azidi kusimamia vyema utengenezaji wa barabara ya Sumbawanga – Mpanda kupitia Kibaoni kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Mikoa hii Rukwa na Katavi tuondokane na adha ya usafiri kama ilivyo sasa hivi. Pia barabara ya Mpanda Tabora kupitia Koga na Mpanda Kigoma kupitia Uvinza. Mazao yetu wananchi wasafirishe bila usumbufu ili uchumi ukue katika mikoa hii ambayo bado iko nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Wizara iridhie mikakati iliyowekwa ili barabara hizi ziishe kuendana na wakati uliyopangwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali itoe fedha kwa wakati kwa wakandarasi ili kazi isisimae kama ilivyo sasa na kusababisha kusubiri msimu wa masika, ambao mvua kali zikianza, kazi husimama kwa uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la uwekezaji vibao katika njia za kuchepukia wakati barabara zinatengenezwa. Wakandarasi waweke vibao vya kuonyesha madereva njia ya kupita ya ziada watengenezapo barabara kubwa, ili kuepusha uharibifu wa barabara zinazotengenezwa. Kutokana na kukosa vibao vya maelekezo madereva wamekuwa wakipita sehemu ambazo zipo kwenye matengenezo na hivyo kurudisha kazi nyuma na kulaumiwa na watengenezaji wa barabara. Hivyo, vibao ni muhimu vya muelekezi.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ili kuepusha ajali pia kwa utunzaji wa barabara zetu. Serikali inachukua hatua gani kwa wale madereva wanaotengeneza magari yao barabarani na kuacha matawi ya miti barabarani yakizagaa hovyo?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho anijibu hili.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, aidha naipongeza Wizara kwa kutimiza majukumu yake kwa ukamilifu kulingana na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihadi zinazoendelea Serikali katika kukabiliana na changamoto ya msongomano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, jitihafa hizo zikiwemo ujenzi wa *fly over's* mradi wa DART (mabasi ya kasi), uboreshaji wa barabara zingine na usafiri wa mjini kwa reli na maji (*town board*).

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yafutayo kwa kupunguza foleni:-

(i) Tozo ya magari yaingiayo mjini *(congestion charge).*

(ii) Kupunguza matumizi ya magari ya Serikali (maofisa wawe wanatumia magari kwa kuchangia).

(iii) Ujenzi wa miji midogo ya kibiashara pamoja na huduma za kijamii. Hakuna ulazima watu wote waende katikati ya mji kufuata huduma za biashara na kijamii zikiwamo za Serikali, nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja la Kilombero (kwa miaka miwili kwa mujibu wa Mkataba) unaleta mashaka!!

(a) Fedha ndogo zilizotengwa yaani shilingi bilioni tatu (3 billion) (Oktoba, 2012) na shilingi bilioni 7.5 (June, 2013) ni kidogo sana kuweza kukamilisha ujenzi wa daraja zima ambalo linatakiwa kukamilika hapo Januari, 2015.

(b) Aidha, *speed* ya mjenzi inatia wasiwasi kwani sasa imeshapita miezi sita (6) hivi (¼ *of the contract period*) mkandarasi bado yuko katika hatua za kujenga kambi na ghala ya kuhifadhia vifaa vyao.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Lupiro/Kilosa, Mpepo/Londo, Lumecha/Songea tunaiomba Serikali katika Bajeti hii basi iweke pesa ya kutosha kutoboa kati ya Kilosa Mpepo hadi Londo ili ianze kutumika katika hali ya changarawe au udongo.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Lupiro – Londo ni muhimu sana kwa ukanda wote ambapo itapita kwani kuna programme kubwa za kitaifa (i) FAMOGATA (fanya Morogoro kuwa Ghala la Chakula la Taifa) (ii) SAGOT (iii) Aidha, kwa barabara hii ni kiunganishi mikoa ya Ruvuma, Njombe, Morogoro, Tanga na mikoa ya nyanda za juu Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Ahsante.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa kazi kubwa mnayofanya. Naomba sana barabara zilizopendekezwa kupandishwa hadhi katika Mkoa wa Simiyu hususani ile ya Bariadi – Kisesa – Mwandoya – Mwanhuzi hadi Sibiti ili iwe *trunk road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara ya kiuchumi ya Bubinza/Musoma *Road Junction* hadi Nyaluhande – Badugu – Nyangili – Mkula iwe ya Mkoa. Naomba pia sasa ile kazi inayoendelea sasa ya Bariadi – Lamadi na iliyotangazwa ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi ikamilike hasa katika kipindi hiki cha kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya uchakavu wa reli takribani mizigo yote inasafirishwa kwa kupitia barabara. Hali hii imesababisha barabara zetu kutodumu kwa muda mrefu. Aidha, ubovu huo

unasababishwa na uzito mkubwa wa mizigo na barabara kujengwa kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti uzito usio wa kawaida wa mizigo nashauri kama hakipo kianzishwe kikosi maalum cha kukagua magari kwa mtindo wa kushtukiza. Mfano, kwa magari yanayotoka Dar es Salaam kwa ghafla wanaweza wakakaa kituo cha kupimia Mikese. Katika kituo hicho wanaweza wakakagua magari na kujua uzito wake na watajua kama kuna uzito wa ziada watajua vituo vyote walivyopita magari hayo kutoka Dar es Salaam wamevunja Sheria na pengine kutokana na rushwa. Hapo hatua itabidi zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ujenzi wa barabara hapa nchini katika maeneo mengi. Kwa sababu ni kawaida ya Bajeti ya Serikali hii, Wizara kutopata fedha kwa mujibu wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge. Je, suala hili haliko katika Wizara ya Ujenzi. Kwani kukosa fedha kwa wakati kunasababisha gharama za ujenzi wa barabara kuwa kubwa, kuliko mikataba ya awali ilivyosainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mheshimiwa Waziri atapojumuisha au hitimisha hoja yake naomba anieleze kwa nini baadhi ya barabara kama Manispaa ya Itigi – Tabora ujenzi umekwisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa mwaka 2013/2014, imekusudia kuendelea kujenga nyumba za Majaji katika mikoa mbalimbali. Wacha Wizara iendelee na mpango huo kwa mwaka 2013/2014, lakini naishauri Wizara kwa mwaka 2014/2015 waangalie uwezekano wa kujenga nyumba za Walimu walioko kwenye maeneo ya pembezoni ili iwe motisha kwa Walimu kwenda kufanya kazi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya kupunguza msongamano Dar es Salaam Wizara imejipanga vipi kwenye maeneo yenye mataa (penye makutano ya barabara). Maeneo haya ndio yanayosababisha msongamano wa magari Dar es Salaam.

Bila ya barabara za juu *(fly over)* katika maeneo hayo bado msongamano wa magari utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanZa kutoa pongezi nyingi sana kwa Wizara ya Ujenzi na viongozi wa Wizara hii Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Naibu Waziri kwa uongozi thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Juhudi za Serikali ya CCM kupitia ahadi ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwenye mkutano tena wa miaka 36 ya CCM Kitaifa Mkoani Kigoma, wananchi wa Jimbo la Manyovu tunaomba barabara ya kutoka Manyovu mpaka Kasulu. Sababu za barabara hii kuombwa zinafahamika ndani ya Wizara. Ni heshima kubwa kunitengea kilomita 42 kati ya hizo kilomita 100 zilizopangiwa nami nipate toka Nyakanazi mpaka Kidahwe. Naomba uokoe CCM Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Magufuli juu ya fidia za wafanyabiashara wa Kijiji cha Mnamila (100). Naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri awaambie kitu wapiga kura wangu, bado wanahangaika bila kujua cha kufanya, wanaomba hisani yako. (Hivi ni vibanda vya biashara 100 vilivyobomolewa).

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuungana na Waheshimiwa Wabunge kwa kukubali kazi nzuri inayofanywa na Wizara lakini angalizo kubwa ni uwiano wa ujenzi wa barabara kwa viwango mbalimbali hasa kiwango cha lami uangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mikoa inazo barabara nyingi nzuri na za lami. Mikoa mingine si hivyo. Napenda kushukuru Serikali kwa kujenga barabara ya kutoka Peramiho *Junction* na Mbinga. Nampongeza pia Mkandarasi na

waliotoa fedha *MCC*. Kazi ile ni nzuri, ni barabara pekee ya lami katika Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula Mbinga unafahamika, kwa nini wananchi hawa wanapata tabu sasa ya kusafirisha mazao, basi angalau tuanze na barabara zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais:-

(1) Mbinga – Litembo (kiwango cha lami). Majibu ya Wizara Bungeni yanaonesha kwamba fedha za upembuzi yakinifu katika bajeti ya 2012/2013, lakini halijafanyika hili. Naomba majibu juu ya utekelezaji wa ahadi hii. Hii inakwenda kwenye Hospitali kubwa ya Litembo.

(2) Unyoni (*junction*) – Maguu – Mkola. Nimeona fedha kwa ajili ya Mbinga - Mbamba Bay. Mantiki – hawa watu ni wamoja. Haipendezi waanze na hiyo lami na baada ya kufika Unyoni waanze barabara isiyo na lami. Hili ni eneo la uzalishaji mkubwa wa zao la kahawa. Fedha angalau ya upembuzi tu iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu barabara ya Kitai – Ruanda – Lituhi; pale Ntundunwaro, Kata ya Ruanda pana mradi wa makaa ya mawe na hapa patajengwa *power station*. Makaa haya yanasafirishwa kwa malori na hivyo kuna vumbi nyingi sana na kudhuru afya za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho pekee ni kuiwekea lami ili kama ni kianzio Kitai – Ruanda (kilomita 50) kwa kuanzia. Hapa hatufikirii tu uwekezaji, lakini hasa afya za watu, ni jambo la dharura. Mheshimiwa Naibu Waziri anayo barua yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa barabara; barabara ya Mbinga – Litembo – Mkili na barabara ya Paradiso – Luhangwa – Litumbandyosi mpaka Kigoli. Maeneo ya kutoka Litembo – Mkili na Litumbandyosi – Kungoli huwa siku zote hayatengenezwi. Hivyo, wananchi wa Kingoli

kuja Litumbandyosi na Mkili – Litembo wanapata tabu sana. Barabara zimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba, bajeti ya barabara hizi iongezwe ili kutengeneza pia maeneo niliyoyataja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu ya wataalam wa Wizara yake. Ikiwa ni pamoja na timu ya wataalam wa *TANROADS* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuweka *network* ya barabara nchi nzima. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuona barabara yetu ya Murugarama – Rulenge – Nyakahura bado iko kwenye hotuba zako au mipango ya Wizara yako. Mwaka huu unaoishia Juni 30 – 2012/2013, barabara hiyo ilipangwa ifanyiwe upembuzi yakinifu na zikatengwa shilingi milioni 140. Bahati mbaya hakuna kazi iliyofanyika ya kutangaza zabuni. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kazi ya kutangaza ili mpate Mkandarasi yakinifu ifanywe kati ya sasa na Juni 30 kazi hiyo ifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa mwaka ujao 2013/2014, barabara hiyo ya Murugarama – Rulenge – Nyakahura mmetenga shilingi milioni 180 kwa ajili ya *FD and DD*. Tafadhali sana naomba kazi ya *Detailed Design* ikamilike katika mwaka wa fedha 2013/2014 ili 2014/2015 ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge anayejiheshimu, sipigi kelele kwa sababu naheshimu ahadi za Serikali. Barabara hii ni ahadi ya Rais kama zilivyo barabara za Kigoma na Kilimanjaro ambazo zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inasubiriwa sana wa Warundi, ni barabara ambayo haina milima kama ilivyo ya sasa hivi – Nyakasanze – Kobero ambapo malori ya

Burundi yanashindwa kupanda milima. Barabara hii itatumiwa na malori ya mizigo ya mgodi wa Kabanga *Nickel*. Barabara hii itakuwa pia kichocheo cha maendeleo kwa Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri kama *senior citizen* kwamba, *resources* chache tulizo nazo tugawane vizuri bila upendeleo *Equitable Distribution of Resources*. Ngara ni Wilaya ambayo ni *strategically positioned*. Ngara inapakana na Rwanda na Burundi na siyo mbali na Congo – Kinshasa. Ni Wilaya muhimu kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuendelea kuwa na matumaini kwamba, Serikali yetu inatenda haki na kwamba hakuna maeneo ambayo ni *more important than others*.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza sana wote waliongozwa na wewe katika Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya. Barabara nchi nzima zinaonekana na ni kweli ifikapo 2017 nchi nzima hasa mikoa itakuwa imeunganishwa kwa lami. Hiyo ni muhimu kwa kukuza uchumi. Uchumi unaokuwa unahitaji miundombinu bora na kazi hiyo inaonekana. Nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu barabara za Wilayani; ni vyema sasa baada ya barabara za mikoa twende katika barabara za Wilaya kujengwa kwa kiwango cha lami. Ni vizuri mkaangalia barabara zinazounganisha Wilaya zaidi ya moja. Mfano wa barabara hiyo, ni barabara toka Pangani – Muheza – Amani – Maramba yaani Wilaya za Pangani – Muheza na Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu upembuzi yakinifu Tanga – Pangani – Saadani – Bagamoyo (kilomita 178); kazi hii inaendelea lakini kwa kasi ndogo sana. Kumekuwa na ucheleweshaji usio wa lazima hasa katika *design*. Mheshimiwa Rais amekwishatoa maagizo kwamba,

barabara hii ipitie Saadani *National Park*. Sasa kazi hii iende haraka na kusiwe na *delay* tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini kwamba, kama Mheshimiwa Waziri alivyoahidi kwamba ifikapo 30 Juni, 2013 kazi hiyo itakuwa imekamilika. Afisa *Development Bank* na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wanasubiri ili iweze kujengwa. Wananchi wa Pangani hawataridhishwa tena kama kazi hiyo haitaanza 2013/2014, hakuna sababu maana fedha zipo/ zitapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuhusu kivuko cha Pangani I; katika Randama sikuona Bajeti ya kununua kivuko kipya. Natumaini kwamba, Mheshimiwa Waziri atakapo-*wind up* ataeleza kwamba, Bajeti hiyo ipo na kivuko cha Pangani I kinanunuliwa mwaka huu wa fedha 2013/2014. Wananchi wa Pangani watapenda kusikia kauli yake katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kivuko kipya cha Bagamoyo – Dar es Salaam. Ni vyema Miji/Jiji yanayokuwa yakawa na usafiri wa aina nyingi *Multi-Modal Transport*". Picha ya *Boat* la *MV.* Dar es Salaam – Bagamoyo naona kama Australia vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni kuhusu barabara ya *PMMR* – Tanga – Pangani; Mheshimiwa Waziri ili kulinda heshima ya Wizara yake ondoa Mkandarasi wa barabara hii *TANROADS,* chukueni barabara hii. Mmefanya vizuri kumwondoa Mkandarasi kwa barabara ya Muheza – Boza *Junction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa 166 inaonesha *Feasibility study* of Nyamuswa – Bunda – Kisovya Nansio.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua hizi kilomita 118.5 zinaanzia Nansio- Nyamuswa au inaanzia Nyamuswa hadi Kisovya. Hii barabara inakanganya sana, naomba kufahamu.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na uongozi mzima wa Wizara hii kwa kazi nzuri kwa utekelezaji wao wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyoainisha katika ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara; nishukuru Wizara hii. Ukisoma ukurasa 47 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri unaonesha idadi ya makampuni ya wanawake Makandarasi. Pia ameeleza mkakati aliofanya kwa kuwajengea uwezo wanawake Makandarasi katika baadhi ya mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupewa ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, kutokana na Serikali kuwawezesha Makandarasi wazawa, kupewa kipaumble cha kupatiwa kazi katika miradi ya ujenzi. Je, ni makampuni mangapi ya wanawake nayo yamewezeshwa kupata fursa hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba kupatiwa ufafanuzi wa vigezo vinavyotumika kuanisha wanawake hao kwa ajili ya kupatiwa mafunzo kwa sababu, ukisoma ripoti ya mwaka jana utaona kuna baadhi ya mikoa haikufikiwa ili kuwepo na ushiriki wa wanawake wote wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa madaraja na barabara; Serikali imejitahidi kujenga na kuzipandisha hadhi kwa baadhi ya barabara za Halmashauri kwenda *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia kutokana na Halmashauri nyingi kutokuwa na wataalam wa kutosha na pesa za kutosha kuweza kujenga hasa madaraja.

Madaraja yote yangesimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Ufundi na Umeme; Wakala huu unashughulikia matengenezo ya vyombo vyote vya moto na mitambo ya aina zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tatizo gani linafanya kitengo hiki kisiimarishwe vizuri kwa kujengewa uwezo kwa kupatiwa wataalam wa kutosha na vifaa vya kisasa ili iweze kutengeneza magari ya Serikali kwa ufanisi na kupunguza gharama za Serikali hasa katika magari na mitambo, magari mengi yamekuwa yakitengenezwa katika *garage* za watu binafsi kwa gharama kubwa sana. Naomba hili liangaliwe kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano wa magari Jiji la Dar es Salaam; kutokana na tatizo hilo niungane na ushauri wa Kamati ya Miundombinu katika kitabu chao ukurasa wa tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kutokana na kukua kwa miji mingi au majiji mengi, ningeshauri ili majiji hayo yasije kupata tatizo kama hilo la Jiji la Dar es Salaam, Serikali ingefanya utaratibu wa barabara zote za majiji kuwa na fungu maalum *(special fund)* kwa ajili ya majiji hayo kuliko majiji kuwa chini ya Halmashauri ambazo hazina wataalam na pesa za kutosha kujenga barabara na madaraja. Lakini kabla hakujawa na fungu hilo maalum, basi majiji hayo kwa sasa barabara zake zishughulikiwe na *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vibali vya winchi na magari; kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya ucheleweshaji wa vibali hivyo kuchukua mpaka wiki moja mpaka mwezi huku Mamlaka ya Bandari ikitoza kodi. Pia vibali vya winchi na magari ya uokoaji vinapocheleweshwa husababisha maafa na uharibifu wa barabara. Ni vyema Mheshimiwa Waziri akalitolea ufafanuzi wa tatizo linalosababisha ucheleweshwaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wizi unaofanyika katika miradi ya barabara; kumekuwa na tatizo kubwa sana la wizi unaofanyika katika ujenzi wa miradi hii ya barabara. Kama wizi wa vifaa, mafuta ya magari, mafuta ya mitambo, nondo, *cement* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la wizi huo ni baadhi ya makampuni haya ya ujenzi kutowalipa vizuri wafanyakazi wao na vibarua wanaowatumia katika miradi hiyo na kusababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati uliopangwa, ni vyema sasa makampuni hayo yanaposaini miradi hiyo kikawepo kipengele cha malipo ya wataalam na vibarua watakaowatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali ikishakabidhiwa miradi hiyo, basi kuwepo na usimamizi maalum wa kusafisha hasa mitaro na kuondoa uchafu kupitia *TANROAD*. Leo hii ukipita barabara ya Iringa – Mikumi katika kona za Iyovi kuna uchafu mwingi yakiwemo mawe na majani ya miti inayoweza hata kusababisha ajali.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri inayofanywa ya kuboresha barabara zetu, madaraja na vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, si rahisi kukamilisha kazi hilo kwa mwaka mmoja, hivyo ni lazima tuvumiliane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache ya ushauri:-

(i) Bado baadhi ya barabara zetu nyingi zinatengenezwa *substandard* kwani zinaharibika muda mfupi baada ya matengenezo. Je, ni kwa nini? Uzito wa magari, teknolojia inayotumika au *material* zinazotumika kutengeneza barabara. Je, tunaweza kurekebisha dosari hiyo?

(ii) Baadhi ya uharibifu wa barabara tunausababisha sisi wenyewe, kwa mfano, baadhi ya wananchi wasio na

uchungu na nchi hii wanabeba nondo zilizopindwa kwenye *pick up* huku zikikwangua lami barabarani, hakuna wa kukemea, hata Polisi wanatazama tu. Baadhi wanaweka miti mikubwa, magogo na matawi barabarani wakati wanapopata uharibifu wa magari yao barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya matengenezo, uchafu ule hauondolewi, misumari na *diesel* na mafuta mengine yanatokana na matengenezo huwa yanaleta athari kwa barabara zetu. Je, ile Sheria tuliyoipitisha Bungeni ya kuwataka wanaohusika wote waondoshe matawi na miti baada ya matengenezo mbona haitumiki ipasavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu alama za zuio la kilomita 50; ni jambo jema ili kupunguza ajali, ila baadhi ya maeneo zimewekwa karibu karibu sana hata inaleta kero. Baadhi zimewekwa kwenye maeneo ambayo pengine kwa dhana yangu hata yasingepaswa. Hakuna *cross* mbele, ni tambarare, hakuna vivuko vya wanyama na binaadamu, si makazi ya watu. Je, mnaonaje kuvipitia na kutupunguzia uzito wa safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu alama mbalimbali za zuio la kupita katika njia ndogo ndogo za Mji wa Dar es Salaam, zilivyowekwa kama vile hakukufanyiwa *study* ya kutosha hivi? Hebu wasaidieni Manispaa, kwa zile zinazozuia kupita na huku ruhusa ya magari inatolewa kupita maeneo hayo huku vinguzo vya chuma vinavyoonyesha barabara kufungwa vipo pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara mipakani mwa nchi; hongereni, kazi kubwa imefanyika, ila bado yako maeneo yanahitaji kufikiriwa, kwa mfano, barabara za Kigoma na Rukwa. Barabara ya Sumbawanga kuelekea Kasanga Port na ile inayounganisha kuelekea Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo haja sasa ya kuona namna ya kusaidia ujenzi wa barabara katika visiwa vidogo vidogo Tanzania Bara, kwani mikoa na Manispaa wanapata ugumu kutokana na gharama kubwa ya kusafirisha vifaa na

zana za kutengeneza barabara hizo na upatikanaji wa *raw material* katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Kilombero lifanyiwe kazi haraka. Nawapongeza sana sana kwa kazi nzuri sana na naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Wizara kwa kuandaa Hotuba nzuri inayojitosheleza kwa vielelezo mbalimbali. Hata hivyo, nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba, kila mwaka tunaahidiwa ukamilikaji wa barabara ya Mdunda – Somanga ambapo sasa nahesabu kuwa ni hadithi za paukwa pakawa. Tatizo ni nini upatikanaji wa fedha au ukosefu wa Mkandarasi mahiri? Nashauri Serikali ihakikishe sasa kuwa hadithi hii ifikie mwisho na tuendelee na masuala mengine, ikitiliwa maana kwamba barabara hiyo ni muhimu sana kutokana na uendelezaji wa Gesi, huko Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye *TV* juzi, magari makubwa yakianza safari kuelekea Mtwara kupeleka vifaa vya Ujenzi wa bomba la gesi toka Mtwara – Dar es Salaam. Sasa kwa msingi huo kile kipande kilichobaki naamini maharibiko yatakuwa makubwa hivyo bora kinga kuliko kutibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kutotengeneza magari na kadhalika kwenye karakana za TAMISEMI jambo la manufaa kwa Taifa kwa sababu katika karakana binafsi gharama zinaweza kuwa kubwa bila sababu na ufundi wenyewe ukawa wa kulipua tu, hivyo kuwa hasara kwa Taifa. Yafaa sasa Wizara zisizotii utaratibu huu ziadhibiwe kwa kufuata taratibu zilizopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara (Serikali) kwa juhudi kubwa ya kuhakikisha kuwa barabara nyingi zinakuwa za lami ili kuharakisha maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na kadhalika. Kwa mfano, barabara ya Mtwara –

Newala – Masasi yenye kilomita 209 itarahisisha usafirishaji wa mazao kama korosho, karanga, ufuta, choroko na kadhalika kupeleka bandari ya Mtwara kutokana na ugunduzi wa gesi zitawafaidisha wananchi wa maeneo hayo kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi natoa pongezi kwa Serikali kwa jitihada za kujenga upya barabara za Mtwara – Mingoyo – Masasi (kilomita 200) ambayo itaunganisha usafiri wa barabara ya lami toka Dar es Salaam – Mbamba Bay bila kulazimika kupitia Mtwara bali Mnazi mmoja – Masasi, Tunduru, Namtumbo, Songea Mbinga – Mbamba Bay.

Hata hivyo, natoa ushauri wa jumla kuwa, katika ujenzi wa barabara zote ambazo Serikali imedhamiria kuzijenga mahitaji ya watu wenye ulemavu hasa wasioona, viziwi na wale wenye ulemavu wa viungo yazingatiwe ili huduma hii isiwe karaha kwa jamii hii ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A.L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa kuzungumzia barabara za Mkoa wa Morogoro hususani wilaya ya Ulanga na Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Hotuba cha Waziri ukurasa 163, imezungumzia ujenzi wa barabara ya Ifakara hadi *Kihansi Road* kilomita 130, ambapo haijafafanua ni ya kiwango gani? Wananchi wa Kilombero, wakulima wa mpunga, wangependa kujua ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa ili waondokane na shida ya akinamama wajawazito na watoto kufia njiani kwa kukosa usafiri wa uhakika ukizingatia Hospitali ya Wilaya na Rufaa ziko Ifakara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa 238, kinazungumzia kifungua barabara ya Ifakara – Taweta – Madeke mpakani mwa Njombe, je, hii barabara itakuwa kwa

kiwango gani? Wananchi wa Kilombero na Njombe wangependa kusikia kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara, Ifakara Mngeta – Mlimba hadi Madeke ni muhimu sana kwa kuondoa umaskini wa wananchi wa Kilombero na Njombe. Hivyo, naomba nipate majibu ya ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kumaliza mchango wangu, bila kushauri Serikali kufuatilia kwa karibu ujenzi wa daraja la Kilombero ambapo ujenzi unaendelea. Pia barabara inayounganisha Mkoa wa Morogoro kupitia Wilaya ya Ulanga hadi Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara za Manispaa ya Ilemela ni mbaya sana. Hii inatokana na mvua nyingi ambazo zimesababisha uharibifu huo mkubwa kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 na mwaka 2012/2013. Na ni ukweli usiopingika kwa uwezo wa Halmashauri ya Ilemela ni ndogo sana na kwa kutegemea *own source,* ni dhahiri kuwa barabara hizo hazitapitika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Halmashauri kuleta maombi maalum, mpaka sasa haijatolewa hata shilingi moja, jambo ambalo linakatisha tamaa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu hatma ya barabara hizo za Kata ambazo sasa zimeharibiwa kwa kiwango kikubwa cha mvua na hasa ukizingatia maombi yote maalum hayajakubalika pamoja na uharibifu ambao umekwishafanyika kutokana na mvua za muda mrefu. Sasa hili ni janga kama majanga mengine kwa sababu awali barabara hizo zilikuwa zikipitika na sasa hazipitiki tena. Hivyo naomba kupata ufafanuzi juu ya hatma ya maombi maalum

yaliyowasilishwa kwako kwa ajili kupata ufumbuzi barabara hizo ambazo zimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa kutambua upya wa Manispaa ya Ilemela na uwezo mdogo na fungu dogo *Road Fund* ambazo linapungua mwaka hadi mwaka na uharibifu mkubwa wa umma, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuagiza Halmashauri kumpa tathmini ya uharibifu ili kusaidia kupata ufumbuzi wa muda mrefu na kuondoa adha kubwa wanazopata wananchi kwa sasa.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Namtumbo – Tunduru; naomba maelezo kwa ufupi wakati wa majumuisho, licha ya uwepo wa kesi Mahakamani, Serikali inajipanga namna gani kumaliza matatizo yaliyopo na kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Tunduru – Mangaka; naomba pia maelezo wakati wa majumuisho (Hotuba ya bajeti haijafafanua) ni hatua ipi mahsusi iliyofikiwa katika mchakato wa utafutaji wa Wakandarasi? Ni nini matarajio ya Wizara (kwa makisio) kuhusu tarehe ya kuanza kazi za ujenzi wa barabara hii?

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa jitihada za kujenga barabara nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi bado ni changamoto kubwa kuhakikisha kuwa, barabara zinazounganisha Mkoa hadi Mkoa zinakamilishwa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mpanda – Kigoma barabara hii imetengewa bilioni nne na nusu (4.5 billlion) kwa kuaznia kilomita 100. Mpanda – Mishamo. Kiwango cha fedha zilizotengwa ni kidogo sana, naiomba Serikali iongeze fedha kwa barabara hii. Kwani barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mikoa ya Kigoma na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Mpanda – Sikonge – Tabora; Barabara hii ni muhimu sana kwani barabara hii inategemewa na mikoa mingi ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kuchukua chakula kutoka Mkoa wa Rukwa na Katavi. Ni vizuri Serikali ikaongeza nguvu kutafuta fedha za ndani na nje ili kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Sumbawanga – Mpanda; barabara hii ilishamaliza kujengwa na huu ni mwaka wa tatu (3) ujenzi wa barabara hii, unakwenda kwa kusuasua sana na kuifanya Serikali iingie gharama za mara mbili. Ni vizuri Wizara isimamie barabara hii ili ikamilike mapema na ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia barabara ilivyoanza kwa kasi ni tofauti kabisa na inavyojengwa kwa sasa. Kuna umuhimu mkubwa, kumaliza barabara hii ambayo itasaidia kukuza uchumi katika mikoa ambayo ilisahaulika kiuchumi. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kama mtakamilisha barabara hii itaondoa umaskini kwa Mikoa hii ya Rukwa, Katavi na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Mkoa ya Karema; naomba Serikali kufikiria barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami, kuna fursa nyingi zilizopo ukanda wa Ziwa Tanganyika kwani kwa sasa kunajengwa Bandari ya Karema. Bandari hii kama ikikamilika kujengwa haitakuwa na maana yoyote kama haitakuwa imejengwa barabara ya lami. Kuna migodi ya madini, kuna mazao yanayozalishwa ya kilimo na kuna mazao ya Ziwa Tanganyika kwa maana ya samaki na dagaa bora kushinda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Kibo - Mwese; naomba barabara hii iunganishwe na barabara ya Kigoma – Kalya, maeneo haya yakiunganishwa yatasaidia sana kukuza uchumi na ni kilomita zisizopungua hamsini kuifikia barabara ya Mwambao wa Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara za Inyonga – Ilunde; Vikonge – Bugwe na barabara – Kalilankulunkulu – Mnyaga, zipandishwe hadhi kutoka Halmashauri ya Wilaya kwenda *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi kama hazitapandishwa ni ndogo sana. Naiomba sana Serikali yangu izipandishe barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote akiwemo Meneja *TANROAD* Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa mipango mizuri ya Wizara kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara zetu nchini. Pamoja na Wilaya ya Ruangwa, Mkoani Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutengewa fedha za matengenezo ya barabara za:-

(i) Ngongo – Mandawa – Ruangwa.
(ii) Kiranjeranje – Nanjirinji – Namichiga.
(iii) Nanganga – Ruangwa.
(iv) Kipande cha lami Ruangwa Mjini *Upgrading to DSD Ruangwa township road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo hili ambalo liliahidiwa na Mheshimiwa Rais kwa kauli yake ya kuwa ataongeza kipande cha lami kutoka ilipoishia ya sasa hadi Kitandi. Napenda kukumbusha kuwa kutoka iliposhia ya sasa hadi Kitandi ni kilomita tano. Kwa kuwa tumepewa kilometa

1.7 kwa sasa, basi sio vibaya kukiwa na ziada tupate nyongeza ya hiyo tuliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wasaidizi wao wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia kazi ya ujenzi wa barabara, madaraja, vivuko na nyumba nchi nzima, hongereni sana. Pamoja na kuunga mkono, ninazo hoja zifuatazo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara za vijijini; changamoto kubwa katika sekta hii ni ubovu na barabara za vijijini, zinazohudumia asilimia sabini na tano (75%) ya wananchi wote. Barabara hizi zipo chini ya Halmashauri ambazo hazina fedha za kuzitengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ibuni utaratibu mpya wa namna ya kuzitengeneza barabara hizi. Kwanza pawe na Mfuko wa pekee wa kugharamia barabara hizi (*Rural Roads Fund*). Pili, kiundwe chombo mahsusi cha kusimamia utengenezaji barabara hizi kama ilivyo *TANROADS* kwa upande wa barabara za mikoa (*Regional Roads*). Utaratibu huu mpya utasaidia kuboresha barabara za vijijini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya mchepu ya Manyoni mjini; kwa niaba ya Wanamanyoni, niishukuru Wizara kwa kuweka barabara hii katika mpango wa utekelezaji katika mwaka 2013/2014 na kutenga shilingi bilioni 1.3. Tunaomba apatikane Mkandarasi makini ili ujenzi ufanyike kwa wakati na kwa viwango.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupandishwa daraja barabara ya Chikuyu – Mjini – Ikosi/ Chohigongo; barabara hii inapitia katika Kata nne (4) za bonde la ufa ambapo kuna shughuli za kilimo, ufugaji na viwanda vidogo vya madini ya chumvi. Aidha, barabara hii inaunganisha *Trunk Road* (kuanzia Chikuyu) na barabara mbili

za *TANROAD,* Mkoa wa Dodoma na *TANROAD* Mkoa wa Singida, eneo la Ikosi/Chohigongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imejadiliwa katika kikao cha Kamati ya Barabara ya Mkoa na ilionekana inazo sifa ya kupandishwa daraja ili iwe ya Mkoa. Aidha, Wizara imearifiwa kuhusu mapendekezo ya *Regional Board* kwamba barabara hii ipandishwe daraja. Natumia nafasi hii kuiomba Wizara ikubali ombi hili ili eneo la bonde la ufa Wilayani Manyoni ipate mawasiliano ya uhakika ya barabara.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala wa Ujenzi wa Nyumba; napongeza juhudi za *TBA* za kujenga nyumba 2,500 huko mikoani. Ushauri ni kwamba, nyumba hizi zisambazwe hadi Makao Makuu ya Wilaya zetu kwani upungufu wa nyumba ni mkubwa sana katika Wilaya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa miundombinu ya barabara ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Tukiwa na barabara kila Mkoa, Wilaya, Kata hadi Kijiji, basi tutakuwa tumepiga hatua ya kuboresha uchumi wetu kwani watu wetu watafanya biashara mbalimbali na huduma za kijamii zitakuwa zimerahisishwa. Naipongeza Wizara kwa juhudi mnazozifanya ili kuimarisha miundombinu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mufindi Kusini tuna viwanda vingi sana kwa mfano, tuna Viwanda vya Chai, Viwanda vya Mbao, Viwanda vya Nguzo za Umeme na Kiwanda cha Karatasi. Viwanda hivi vinachangia katika pato la Taifa letu. Pia wakazi wengi wa Jimbo la Mufindi Kusini ni wafanyabiashara wa mazao mbalimbali. Tatizo kubwa ni barabara ya Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango – Mgololo. Barabara hii hutumika katika usafirishaji wa bidhaa za viwandani na mazao mbalimbali ya kibiashara. Naomba Serikali kama ilivyoahidi kuwa itatengeneza kiwango cha lami, huu ndiyo uamuzi wa busara kwa kuimarisha na kuwatia moyo wenye viwanda na wafanyabiashara wa Mufindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mufindi kuna mvua nyingi sana, kwa hiyo, tunaomba barabara zitengenezwe kwa kutumia changarawe, siyo udongo hasa barabara ya:-

(1) Igowole – Kasanga – Nyigo.
(2) Mbalamaziwa – Kwatwanga.
(3) Barabara ya Mafinga – Mgololo.

Barabara hizi ni za mkoa zinamilikiwa na *TANROAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maandishi nichangie bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Awali ya yote nipongeze mafanikio yaliyotokana na utendaji wa Wizara hii kwa kufungua barabara za nchi hii. Wote wanaoijua barabara ya Dar es Salaam mpaka Mtukula umbali uliochukua siku 10-14 miaka ya 1970, leo mwendo wa masaa 18 kwa basi la abiria, ndio mashuhuda wa kweli wa kazi iliyofanyika. Pamoja na kazi kubwa, utaratibu wa kutumia fedha za ndani kupitia *fuel levy* ni darasa kuwa, tukidhamiria na kujifunga mkanda kama Taifa tunaweza kujenga sekta nyingi kwa haraka na kwa nguvu zetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ufumbuzi wa barabara kwa kilomita nyingi zipo sehemu uimara wa barabara unatia mashaka. Sehemu nyingine mfumo wa Ujenzi umeingilia mikondo asili ya maji na kupelekea maji ya mvua kuwaingilia wananchi au kusababisha mafuriko. Haikuwa dhamira ya Serikali au wajenzi, nashauri kote ilivyofanyika hivyo parekebishwe. Ushauri wa jumla katika hili ni kuwa, ukaguzi wa kina ufanyike na turekebishe kasoro kabla ya uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo katika mafuta imeleta tija hasa baada ya kutumika vizuri. Hata hivyo, nashauri ukaguzi wa kina hata ikibidi kila baada ya miezi mitatu ufanyike ili kubaini kama kila tone la *petrol* na *diesel* lililotumika

nchini limechangia lengo hili. Sambamba na ukaguzi wa wakusanyaji yapo mashaka kwa mamilioni ya lita za mafuta ziendazo migodini. Tuondoe mashaka kwa kujihakikishia kuwa mafuta yaliyopewa msamaha wa kodi na tozo kweli yalitumika ilivyokusudiwa. *TMAA* kwa kutumia kumbukumbu za mitambo inayotumika, muda iliyotumika, inaweza kutuonesha eneo lenye mashaka. Njia hii imeonesha mafanikio, lazima tuidhibiti kwa mafanikio zaidi na uendelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya barabara nikumbushie ahadi ya Rais ya Barabara ya Muhutwe kwenda Kamachumu inayowekwa lami. Natambua kazi inayofanyika na naomba basi iongezeke ili tufaidi zaidi manufaa ya barabara ya lami, kuimarisha usafiri wa barabara kwa eneo la Kamachumu – Muleba kupitia Katoke, Halmashauri imekuwa ikisota na kujenga daraja la Kishala kama njia mkato au mbadala wa daraja la Kyabakoba inapotokea dharura. Kupitia bajeti hii, naiomba Serikali kusaidia mradi huu wa daraja na barabara ya Kishala kwa kutoa fedha, wataalam na usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafanikio ya utendaji wa Wizara hii katika barabara na hususan matumizi ya *fuel levy,* nashauri taratibu barabara za Halmashauri zipelekwe *TANROADS*. Mamlaka ya barabara inayo nidhamu ya kiweledi, mfumo na njia wazi ya majukumu na uwajibikaji. Mfumo huu una watu wenye Mamlaka waliyopewa, chombo cha namna hii kinapopewa rasilimali fedha za kutosha tija na ujasiriamali unakuwa wa hali ya juu. Ushauri wangu ni kuwa, katika kundi la barabara zilizoko chini ya Halmashauri zihamishiwe *TANROADS,* hii ifanyike hata kama ni kwa kuhamisha fungu lake na kwenda nalo. Lengo ni kuona kazi inakabidhiwa chombo madhubuti tutakachohakikisha kazi inafanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa *fuel levy* iangaliwe upya na kutoza sasa shilingi 200 ya mwaka 2007 leo. Hakuna haja ya kuwa na mashaka tumeshaona utendaji wa Mfuko, lakini ikumbukwe kuwa mafanikio ya ujenzi wa barabara yanapaswa kufika sehemu nyingi nchini.

Jukumu la kujenga ni letu Watanzania na basi ili kufikisha furaha hii ya ujenzi wa barabara kwa wananchi walio wengi tuongeze tozo kwa kurekebisha kupungua nguvu kwa fedha kutokana na muda, *time value of money.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwasilishe tena maombi ya barabara mbili za Jimbo la Muleba Kaskazini ambazo kupitia ngazi zote zimependekezwa kuhamishiwa *TANROADS.* Pamoja na barabara nyingine katika kundi hili barabara inayopita Butakya, Omulunazi, Rushwa na Biija na ile ya Kaihiyo, Ngenge na Kishubo naomba mzihamishie *TANROADS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchangia Wizara hii kwa maandishi, lakini wakati wa bajeti ya Waziri Mkuu, nilichangia tena maneno haya. Mwaka wa fedha 2012/2013, katika bajeti ya Wizara hii tulipitisha hapa ndani barabara ya Mwanza *Airport by pass* - Kayenze, lakini hadi leo hakuna kilichotekelezwa, pamoja na Waziri kwenda katika barabara hii na kuitisha Mkurugenzi Mkuu wa Wilaya pamoja na Madiwani na kuikataa barabara hii na kuchukua barabara ya Mwanza - Nyanguge *by pass.* Hii siyo halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na barabara hii kuwa ni ya Jiji hapo zamani na sasa ni ya Manispaa ya Ilemela, kwa mpango ule ule ambao zinatengenezwa barabara za Dar es Salaam ambazo si za Mkoa. Mheshimiwa Waziri uliikataa barabara hii kwa kigezo gani, ambapo ilikuwa imepita hapa Bungeni ndani ya bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua barabara hii Mheshimiwa Waziri atasaidia vipi? Mcha Mungu huwa anaogopa kauli zake, nami naamini Mheshimiwa Waziri ni mmoja wao, ni vema sasa akakaa na kutafakari kuhusu barabara hiyo kwani aliitamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri, ni vema sasa akaongeza fedha za Mfuko wa Barabara katika Manispaa ya Ilemela ili barabara hii ambayo ni muhimu na wakazi ni wengi katika eneo hilo, pia ni barabara ambayo inakwenda kwa Mkuu wa Wilaya, Halmashauri ya Ilemela pia ni njia ambayo inamfanya raia au wakazi wa Halmashauri hii kufika Wilayani kwa gharama nafuu, ukilinganisha ni fupi ila mbaya. Wakazi wa Ilemela wanategemea huruma ya Mheshimiwa Waziri ili barabara hii itiwe lami kwa njia yoyote, yeye anajua kwani ni mzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Waziri kuwa, barabara ambayo aliifanya mbadala ya Mwanza *Airport* inayopita Kahama, Ilalila, Bulyankulu, Shibula, Nyamwilolelwa na Muhunze imepita katika mashamba ya watu, imeng'oa misingi ya nyumba ambazo zilikuwa zinajengwa, pia miti ya matunda na katani za wakazi wa maeneo hayo, lakini hawalipwi chochote kile ila ni uharibifu. Ni vema Mheshimiwa Waziri akatumia busara zako katika hilo, kwani maendeleo tunataka na pia ni vema kujali watu tunaowakuta katika maeneo hayo. Sasa basi busara itumike na sio mabavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Makampuni ya Uchimbaji wa Madini wakalipia, au kupima mizigo yao mara inaposhushwa baharini kwani magari yao yanabeba mizigo mizito sana na ndio ambayo yanaharibu barabara. Cha ajabu yanasamehewa na kufanya uharibifu mkubwa kwenye barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli kwa kuwasilisha Hotuba na hoja ya Wizara ya Ujenzi kwa umakini na umahiri wa hali ya juu kwake yeye, au kutoka kwake hatukutegemea, vinginevyo kufanya hivyo amesaidiwa na Mheshimiwa Lwenge, Naibu Waziri mwenye uwezo mkubwa ambaye nilibahatika kufanya naye kazi Katibu Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS,*

Wakurugenzi na Wafanyakazi wa Wizara na Idara na Mashirika wanamsaidia sana Waziri na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Katumba-Mbambo-Tukuyu imo katika orodha ya barabara zilizo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 na ahadi ya siku nyingi ya Rais ili ijengwe kwa kiwango cha lami imependekezwa na Waziri amekubali kwamba sasa ijengwe kwa awamu Mbambo – Isange – Kandete, Isonge – Kandete – Katumba, Mbambo – Tukuyu. Kwa kuwa 2015 imekaribia tumefarijika na ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwamba, pamoja na ufinyu wa bajeti ya ujenzi wa awamu ya (1) utaanza mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna shaka na ahadi ya Waziri kwani yeye ndiye aliyesimamia matayarisho yote ya kiufundi ya barabara hii mpaka usanifu wa kina, alipokuwa Waziri wa Ujenzi kabla hajakwenda Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, wanastahili pongezi siyo tu kwa kuwasilisha Bungeni Hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara, bali vile vile kwa kazi nzuri na ya viwango wanayoifanya katika kuendeleza miundombinu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kuikumbuka barabara ya Kihusya-Matema (kilomita 39.5) ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais tangu mwaka 2005, kwa kuitengea angalau Shilingi billioni 1.5 kwa ujenzi (kiwango cha lami) kwa kilometa tatu. Si haba ingawa naiomba Wizara itafute njia yoyote ile angalau kilomita tano kati ya kilomita 39.5 zijengwe mwaka ujao wa fedha ili kuondokana na adha ya kipande cha mwanzo cha barabara hiyo, kinachogeuka kuwa Mto nyakati za mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tuna miradi mingi ya barabara ambayo ujenzi wake haujakamilika, ni bora Serikali kutoanza miradi mipya ya barabara hadi hapo kumaliza miradi ilianzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi endelevu wa barabara nchini mwetu, hauwezi kutegemea wageni kila siku, ukweli usiopingika Makandarasi tulionao hawana uwezo mkubwa wa kuhimili miradi mikubwa itakayohitaji gharama kubwa, pia hawana utaalam na hawana zana za kisasa, ni bora hivi sasa Serikali iwajengee uwezo Wakandarasi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuondokana na umaskini ni lazima tulime kwa wingi na kwa maana hiyo tuweze kujenga barabara zetu ili tuweze kusafirisha mazao kwenye maeneo mengine. Naiomba Serikali ilione hili na iweze kutengeneza barabara, ni kweli bajeti ya ujenzi ni ndogo mno na isitoshe tunategemea wafadhili wa nje ambao mara nyingi hushindwa kutimiza ahadi zao kwa wakati. Naishauri Serikali kwa vile bado Tanzania tunakopesheka, Serikali iende ikope ili iweze kutengeneza barabara nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia majengo huko Dar es Salaam kuanguka na watu wengi kupoteza maisha. Naiuliza Serikali kwa yale maghorofa ambayo yalitakiwa kujengwa ghorofa 9 badala yake yamejengwa ghorofa kumi na sita je Serikali ilikuwa wapi kwa nini Serikali inakiuka wajibu wake wakufuatilia kazi zilizopangiwa. Naishauri Serikali kuwachukulia hatua kali kwa hao watendaji ambao wamezembea kazi zao na kusababisha vifo vya wananchi wengi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingi ambazo zinajengwa zinakuwa chini ya viwango, kwa nini Serikali haiwatafuti Makandarasi ambao wana uwezo wa kujenga barabara ambazo zinakuwa ni nzuri. Naipongeza Serikali kuikataa ile barabara ya Mbagala Rangi Tatu (Kilwa *road*) kuikataa kwa kuwa imejengwa chini ya kiwango na kutaka ivunjwe na ijengwe tena.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha nami nichangie bajeti hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2013/2014. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri na makini na kwa kazi nzuri ya kuendeleza sekta hii muhimu, kusimamia na kuendeleza ujenzi wa barabara, kusimamia Mfuko wa Barabara, Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo ya Serikali, Wakala wa Ufundi Umeme pamoja na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Ujenzi, Bodi za Usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi na Usimamizi wa Vifaa na Mitambo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu haya ni mazito, yanahitaji umakini mkubwa na utaalam wa hali ya juu katika utendaji wake ili kuhakikisha rasilimali zinazotumika kuendeleza sekta hii zinaleta ufanisi, tija na kutoa huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo, bajeti hii imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatoa msisitizo wa kuendeleza sekta ya ujenzi kwa maendeleo ya nchi ili iwe endelevu na yenye ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kujenga barabara mpya, madaraja na kukarabati barabara nyingine kwa kiwango cha lami, lakini changamoto bado ni nyingi katika sekta hii muhimu. Kumekuwepo kwa ujenzi wa barabara usio kidhi viwango, barabara hizo hujengwa chini ya viwango na pindi zinapoanza kutumika hazichukui muda mrefu kuharibika, kuwa na mashimo, mabonde na kufanya wananchi kuwa na maswali mengi na kuwa na wasiwasi kwamba hakukuwa na usimamizi mzuri wa Makandarasi wanaofanya kazi hizo na kutilia mashaka utendaji wa maofisa wa Wizara ama kwa kutokuwa makini, kwani Makandarasi wengi wamekuwa hawakidhi viwango vinavyohitajika katika miradi hii ya barabara na kuisababishia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwabana Wakandarasi hao pindi wakigundua barabara

hizo ziko chini ya viwango na kuwaamuru kuzirudia tena kwa gharama zao, ila zaidi nipende kuishauri Serikali kuchukua hatua madhubuti mapema wakati mchakato mzima wa kuwapata Wakandarasi hao ili kujiridhisha na utendaji wao wa kazi ili kukidhi viwango vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ukiukwaji wa Sheria. Ukiukwaji huo hufanywa na madereva wachache ambao hupitisha magari yenye uzito mkubwa katika baadhi ya barabara zilizoainisha uzito maalum unaotakiwa magari kupita katika barabara hizo. Serikali imetumia kiasi kikubwa cha fedha kuzitengeneza barabara zetu na kuzikarabati, lakini bado ukiukwaji huo wa Sheria unaendelea kufanyika na kusababisha barabara zetu kuharibika kwa muda mfupi na kuisababishia Serikali hasara kwa kuzifanyia ukarabati wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara kutilia mkazo usimamizi wa Sheria ili uzingatiwe na adhabu kali zitolewe kwa wale wote watakaobainika kuvunja Sheria hizo. Tatizo lingine ambalo limekuwa sugu ni kwenye vituo vyetu vya mizani wenye dhamana na kuyapima magari yote ya kubeba mizigo na abiria, kumekuwa na vitendo vya uvunjaji wa Sheria na rushwa kutawala kwa baadhi ya maofisa wa vituo hivyo. Kwani imegundulika magari mengi huzidisha uzito kupita kiasi kwa kubeba mizigo mizito, lakini punde wanapokamatwa huachiwa na kuendelea na safari. Hali hii inasikitisha sana kuona barabara zilizojengwa kwa gharama kubwa na Serikali lakini zinaharibiwa na watu wachache kwa kuruhusu magari hayo kuendelea na safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara kuweka mikakati endelevu ya kuwabana na kuwachukulia hatua za kisheria watumishi hao wanaokiuka sheria na utaratibu kwa kushindwa kusimamia vizuri sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita nilizungumzia sekta hii ya barabara hususani ujenzi wa barabara ya Makofia Mlandizi hadi Mzenga ambao

Mheshimiwa Rais aliahidi. Nilipouliza katika swali langu la msingi katika Bunge lililopita nilijibiwa kuwa walikuwa wanafanya upembuzi yakinifu. Baada ya mimi mwenyewe kufanya uchunguzi wangu wa kina niligundua kuwa, hakukufanyika upembuzi yakinifu na hakuna fedha zozote zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake amesema ile barabara itajengwa kuanzia Bagamoyo mpaka Mlandizi, ikizingatiwa Bandari ya Bagamoyo inayojengwa itafanya hiyo barabara kutumika kwenda Bandari ya nchi kavu Mzenga ambako kuna kituo cha Reli ya *TAZARA*. Lakini pia hakuna uhakika kama itajengwa kutoka Mlandizi mpaka Mzenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Kongowe, Soga, Kisarawe pia zingepandishwa hadhi na kuwa barabara za Mkoa. Vile vile barabara za Vigwaza, Kwala na Dutumi hadi Kisarawe pia zipandishwe hadhi kuwa barabara za Mkoa. Hata hivyo, barabara za Chalinze, Gwata, Magindu, Lukenge hadi Morogoro vijijini, barabara hizi zimeunganisha Wilaya tatu, lakini barabara hizi haziko katika kiwango cha lami. Tukiweza kuziweka barabara hizi katika kiwango cha lami tutakuwa tumefikia lile lengo la kuunganisha Wilaya hadi Wilaya na kuwafanya Wananchi wa Wilaya hizo kufanya shughuli zao za kibiashara kwa urahisi na kuleta maendeleo ikizingatiwa hivi sasa wananchi wengi wanakimbilia Kibaha na kufanya mji kukua na kuwa na mahitaji makubwa ya kimaendeleo kuanzia kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika Kata ya Mlandizi, Magindu watu waliowekewa alama x na kuambiwa wasiendeleze maeneo yao, Serikali ina mpango gani kuwalipa fidia kwani kuna watu hawajalipwa fidia zao mpaka leo na baadhi yao ni wastaafu ambao wametumia fedha zao za kustaafu ama kwa kuwekeza katika majengo na leo wamezuiliwa na hakuna fidia yoyote iliyotoka mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bajeti ya mwaka huu itilie mkazo katika changamoto hizi kwani umuhimu wa barabara hizo ni mkubwa pamoja na matatizo yanayowakabili wananchi kiujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango mizuri ya Serikali bado kuna malalamiko katika ushirikishwaji na uajiri wa Makandarasi katika miradi ya ujenzi wa barabara na nyumba za Serikali. Makandarasi wengi wanalalamikia masharti magumu yaliyowekwa ili waweze kupata kazi hizo, masharti hayo ni pamoja na kuwa na dhamana (*Security Bond*) ya fedha nyingi ambazo Makandarasi hawa hawana japokuwa wana utaalam wa kutosha wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawana dhamana za kuwapa uwezo wa kukopesheka, mitaji yao ni midogo sana, hivyo, kukosa nguvu ya kuweza kununua/kukodisha mitambo mikubwa ya kurahisisha kazi. Pia hawana uwezo wa kuajiri wafanyakazi wengi ili kazi ikamilike kwa haraka na wakati Serikali ingeweka mikakati au sheria ya kuwawezesha Makandarasi waweze kupata unafuu katika ushindani wa kupata kazi kama kuweka sheria za kuwataka Makandarasi wa kampuni za kigeni kushirikiana na Kampuni za hapa ndani ya nchi na ziwe za wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hiyo itawasaidia sana Makandarasi wetu kuwajengea uwezo wa kuongeza uzoefu wa kazi na ujuzi na pia kukuza pato la ndani ya nchi yetu kwani fedha zitabakia Nchini tofauti na Makampuni ya nje fedha hupeleka kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kuzungumzia suala zima la Jiji la Dar- es- Salaam, mfano, hivi sasa kuna huu Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi, napenda kwanza, kuipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia kwa mchakato mzima mpaka kupatikana kwa Mkandarasi wa mradi huo, lakini kuna changamoto mbalimbali ambazo hakuna njia nyingine zaidi ya kuzishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali kupitia Wizara husika kuweka utaratibu wa Mkandarasi kufanya kazi muda wa usiku ili mchana kupisha magari mengine kupita bila kusuasua, kwani kwa hivi sasa kumekuwa na msongamano mkali pale Mkandarasi anapofunga njia moja ama nyingine foleni huwa kubwa sana na kufanya safari moja kutumia masaa zaidi ya matatu mpaka manne. Tukifanya hivyo itasaidia kwani muda wa usiku watumiaji wa barabara wanakuwa ni wachache ukilinganisha na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Serikali kupitia Wizara kufanya ukarabati kipande cha barabara kuanzia Chalinze mpaka Ruvu kwani kimekuwa na mabonde mengi na miinuko ambayo husababisha magari kutokutulia barabarani, magari kuyumba na kupishana kwa shida na wakati mwingine madereva wageni inakuwa rahisi kusababisha ajali katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwashukuruni sana, jambo hili la barabara linawagusa watu wengi, mahali pengi na kwa hiyo basi, saa kumi na moja jioni tutakutana tena ili tumpe nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ataanza na Mheshimiwa Waziri atamalizia, waweze kupitia baadhi ya hoja ambozo mmezizungumza kwa siku mbili. Baada ya hapo tushirikiane kupitia mafungu mbalimballi yanayohusiana na Wizara hii. Kwa hiyo, ninawaomba sana mahudhurio yenu yawe ni mazuri jioni ya leo. Kwa jinsi hiyo, niwaombe sana, kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Omar Nundu, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Mendrad Kigola, hamkuweza kupata nafasi, kwa sababu hali ya muda haipo upande wetu.

Ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshamaliza awamu ya uchangiaji na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Lwenge aweze kuanza kupitia sehemu ya michango yetu. Mheshimiwa Engineer Lwenge karibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kabla sijaendelea, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunifikisha hapa na afya njema na kuweza kunikirimu mambo yote haya.

Naomba pia niwashukuru wapigakura wangu wa Wilaya ya Wanging'ombe kwa namna wanavyojituma katika maendeleo pamoja na kwamba muda mwingi sipo nao, lakini niwaambie tu kwamba mambo yote ambayo tumeahidi ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutayatekeleza; kero zote za maji, umeme na miundombinu tutazishughulikia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge wote, kwa kweli kwa mmetujenga sana Wizara yetu kwa namna mlivyochangia. Mawazo yenu yote yatatufanya sisi tupate nguvu mpya na tuweze kutekeleza miradi hii ambayo Waziri wa Ujenzi ameiwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijasahau, naomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Naomba sana ndugu zangu Wabunge wote tuunge mkono. Pamoja na kwamba inawezekana barabara yako haipo kwa mwaka huu, lakini kama tulivyosema, ahadi zipo nyingi na sisi tutajitahidi kuzitekeleza, kwani tunaye jemedari Rais wetu Rais Dkt. Jakaya Kikwete ambaye ameahidi na amesema kwamba atatafuta kila njia ili miradi yetu wote iweze kukamilika. Anahangaika kutafuta fedha ndani na nje ya bajeti yetu na ndiyo maana kazi nyingi zinafanyika. Pia tunaye Jemedari Dkt. Magufuli kwa kazi anayoifanya

mnaiona. Kwa hiyo, mtuunge mkono kwa kweli na tutajitahidi kuhakikisha mambo yote haya tunayatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kuchangia, hoja nyingine tutajitahidi kuzileta kwa maandishi, ikiwezekana kabla ya Mkutano huu kwisha. Kwa hiyo, hoja zote ambazo tumezipokea na tutatoa majibu na tutawasilisha.

Hoja ya Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage anasema anatoa sifa kwa Serikali kwa kujenga barabara kwa fedha zake. Nasi tunasema kwamba tutaendelea kufanya hivyo pale inapowezekana, fedha za wafadhili ziwe ni kichocheo tu kwa nguvu ya kwetu wenyewe. Kwa hiyo, miradi mingi tutaifanya kwa fedha zetu wenyewe. Anasema pia ujenzi uzingatie ubora na usiingiliwe na mikondo ya maji asili. Suala hilo tutalizingatia kwenye usanifu ambao unaendelea kufanywa nchi nzima. Huo ndiyo utaalamu, ni lazima uhakikishe kwamba barabara zile unazisanifu vizuri, kwamba maji na barabara huwa havikai pamoja. Kwa hiyo, ni lazima uhakikishe kwamba maji siku zote yanatoka nje ya barabara ili barabara hizi ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Vile vile Mheshimiwa Mwijage anashauri pia kwamba ukaguzi ufanyike kila baada ya miezi mitatu ili kubaini kama tone na petroli na dizeli linatozwa. Hii anaongelea kuhusu kuongezaMfuko wa Barabara ambayo kila mmoja anayenunua dizeli au petroli anachangia Sh. 200/= kwenye Mfuko wa Barabara. Kwa hili tutaendelea kulizingatia ili kusudi tuweze kuhakikisha kwamba wote wanalipa *fuel levy* ili kusudi tupate mfuko wa kutosha kuhudumia barabara zetu. Kama mnavyofahamu 90% ya mfuko huu inashughulikia matengenezo ya barabara na 10% tunashughulikia mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga yeye anasema barabara ya Mwanza – *Airport By pass* Kayenze ipandishwe daraja ili ihudumiwe na *TANROADS*. Tunasema kwamba, sheria namba 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake, barabara

hii itahudumiwa na Halmashauri husika na kama itakidhi vigezo vinavyotakiwa kupandisha daraja, basi suala hilo liwasilishwe kwa kupitia vikao husika kukanzia kwenye Halmashauri yake.

Mheshimiwa Profesa Mwandosya alitoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, pongezi hizo tunazipokea na pia anazungumzia habari ya barabara ya kutoka Katunda – Luangwa - Mbambo Tukuyu kwamba ipo kwenye ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nasi tunasema kwamba tumeshatenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 1,270 na barabara hiyo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kabla hujaendelea, Waheshimiwa Wabunge, naomba kumtambulisha *Chief Whip* mpya wa Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri endelea! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Harrison Mwakyembe naye anatoa shukrani kwa Wizara kwa kutenga Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ya ujenzi wa barabara kwa kilomita tatu barabara ya Kikusya – Matema. Tunasema kwamba pongezi hizo tunazipokea. Lakini anaomba fedha zaidi ili ziweze kujenga angalau kilomita tano za barabara hiyo kipande cha mwanzo. Maombi hayo yamepokelewa na tutayazingatia kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum anasema kwamba Wakandarasi wengi hawana uwezo mkubwa wa kuhimili miradi mikubwa, pia hawana utaalamu na zana bora, hivyo Serikali iwajengee uwezo. Serikali inatambua uwezo mdogo wa Wakandarasi wa kizalendo na katika kuwawezesha Wakandarasi hawa, Bodi ya Wakandarasi imebuni utaratibu na kuanzisha mfuko maalum wa kuwasaidia Wakandarasi wazalendo ili kuwawezesha hasa kwa fedha za kufanyia kazi angalau ile fedha ya kuchukua ile *advance*. Kwa hiyo, kuna mfuko uko kwenye Bodi ya Wakandarasi ili Wakandari wazalendo waweze kukopa pale. Pia Bodi inatoa mafunzo ya

kuwawezesha Wakandarasi kuengeneza miradi hata namna ya kujaza *tender;* kwa hiyo, wanafundishwa ili waweze kufika mahali waweze kushindana na Wakandarasi wakubwa.

Pia Wakandarasi wanafanya miradi mikubwa, Bodi inawahamasisha wajiunge kwenye ubia. Tayari tuna mfano, kuna Wakandarasi 13 wamejiunga pamoja, wanajenga daraja la Mbutu. Kwa hiyo, tunafikiria Wakandarasi wetu kwa namna hiyo tutawajengea uwezo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulishauriwa Serikali isianzishe miradi mipya ya barabara hadi hapo itakapomaliza miradi iliyoanzishwa na ujenzi wake. Tunasema sawa, lakini huwezi kusema kwamba utaacha mpaka mradi wa miaka mitatu; kwa hiyo, mpaka umalize miaka mitatu ndiyo uanze tena mradi mwingine. Utaratibu huo hautaweza kusaidia kujenga nchi nzima. Kwa hiyo, lazima tuendelee na miradi kama tulivyopanga. Kinachotakiwa ni kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwa kuweza kuwalipa Wakandarasi ili waweze kukamilisha kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ushauri kwamba nyumba za mazingira magumu zijengwe kwenye Wilaya zilizopo pembezoni ili kuondoa uchakachuaji unaofanywa na Halmashauri na Wakandarasi. Ushauri huo tunaupokea na tunasisitiza kwamba nyumba zote zinazojengwa na Wakandarasi wahakikishe kwamba wanajenga kwa viwango vinavyokubalika kimkataba.

Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa Mbunge wa Kibaha, anasema baadhi ya barabara zinajengwa chini ya kiwango. Majibu ni kwamba barabara zote hujengwa kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba. Baada ya zoezi la ujenzi kuwa chini ya uangalizi wa Mkandarasi kwa kwa kipindi maalum, Mkandarasi anayefanya kazi chini ya kiwango atafanya marekebisho kwa gharama zake mwenyewe. Kwa hiyo, hili tunalifuatilia na tena tuna mifano ambayo kuna miadi ambayo wamejenga chini ya kwango, tumehakikisha wanazirudia kwa gharama zao. Pia hawa Wakandarasi ambao wameshaonekana kwamba hawafanyi

kazi nzuri, natoa agizo kwamba hata Halmashauri zisiwape kazi tena, kwa sababu kama ameshaonyesha kwamba hawezi kufanya kazi nzuri, tusiwape kazi nyingine. Hilo tutalifuatilia na kuchukua hatua zinazostahili kwa wale ambao hawatazingatia agizo hili. Anasema pia pongezi kwa Serikali kukataa barabara ya Mbagala Rangi Tatu. Pongezi hizo tunazipokea.

Mheshimiwa Vincent Nyerere anasema pongezi kwa Serikali kwa kuonyesha nia ya kujenga vivuko vingi hapa nchini na hasa maeneo ambayo kumekuwa na matatizo. Pongezi hizo zimepokelewa. Lakini pia anasema Serikali imeshauriwa kutoa zabuni za kutengeneza vivuko kwa kikosi cha wanamaji *(Navy)* cha Jeshi la Wananchi Tanzania. Ushauri tunaupokea lakini tutazingatia kanuni za manunuzi katika kuwapa kazi hiyo.

Ujenzi wa barabara ya Nyanguge – Musoma umekuwa wa taratibu sana kazi ikiongezeka. Majibu ni kwamba kuchelewa kwa kazi hii kulitokana na kuhamishwa kwa miundombinu ya maji eneo la mjini yaani maji, umeme, simu na nyumba. Kwa hiyo, tatizo hilo limesharekebishwa na kazi sasa itakwenda kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Massele Bukwimba anatoa pongezi; tunazipokea. Lakini pia anasema kwamba anaomba barabara zake ambazo amezitaja nyingi kwamba zipandishwe daraja. Naomba nimshauri Mheshimiwa Bukwimba kwamba taratibu za kupandisha daraja zianze kwenye vikao vya Halmashauri. Zikishatoka kwenye Halmashauri, tupeleke kwenye Bodi za Barabara za Mikoa, hao ndio wanapeleka kwa Waziri wa Ujenzi ambaye atatuma timu kuja kuangalia barabara hizo zinazotajwa kama zinakidhi vigezo. Kwa hiyo, kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanapendekeza barabara zao zipandishwe daraja tutazishughulikia kwa utaratibu huo.

Pia Mheshimiwa Bikwimba ametaka kujua hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa barabara ya Geita – Bukhori - Kahama kwa kiwango cha lami. Mhandisi mshauri *ENV*

*Consultant* ameanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tangu tarehe 8/4/2013 kwa gharama ya Shilingi za Kitanzania milioni 406. Kwa hiyo, kazi ya upembuzi yakinifu imeanza.

Mheshimiwa Murtaza Mangungu alisema bomoabomoa kwa wananchi waliojenga kandokando ya barabara katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, siyo haki kwani wananchi walijenga nyumba zao kabla hata sheria ya hifadhi ya bomoabomoa kutungwa na Bunge.

Majibu ni kwamba kupitia tangazo la Serikali namba 242 la mwaka 1940, barabara za Mkoa za Itingi - Kipatimu – Nangurukulu Liwale katika Jimbo la Kilwa Kaskazini zilitangazwa kuwa za daraja la barabara za Mkoa zenye eneo la hifadhi ya barabara mita 22.5 kutoka katikati ya barabara. Hivyo, wananchi waliojenga katika eneo hilo baada ya mwaka 1940 wamevunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tulishauriwa Serikali kudhibiti matumizi mabaya ya madaraja kama vile kupitisha mifugo kwa daraja la Mkapa badala ya kutumia magari. Mimi nafikiri suala la matumizi mazuri ya barabara, kwa kweli barabara tunazijenga siyo ajili ya kupitisha mifugo. Hili naomba sana Watanzania tuangalie, kwani barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa. Tunaomba sana wananchi wasafirishe mifugo, kama inakwenda mbali ipakiwe kwenye magari na siyo kuswaga kwenye barabara. Lakini kwenye barabara nyingi tumejenga maeneo ya kuvukia barabara, kwa hiyo, naomba sana mifugo isiswagwe kwenye barabara.

Pia amezungumzia barabara ya Ndundu – Somanga, anauliza ni lini itakamilika? Tumeshajibu swali hili, ni kwamba barabara hii kwa namna yoyote tunategemea mwaka huu kabla ya mwezi Desemba, 2013 barabara hiyo itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Godfrey Zambi anauliza ahadi za Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa barabara ni nyingi, Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuwaelezea wananchi. Jibu

ni kwamba Serikali inatekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais kulingana na upatikanaji wa fedha. Kama nilivyosema kwenye utangulizi kwamba Mheshimiwa Rais anajitahidi kwa namna yoyote kupata fedha ndani ya bajeti na pengine hata kukopa ili tuweze kutekeleza ahadi hizi tulizokuwa tumeziahidi.

Vile vile Mheshimiwa Zambi anasema Wakandarasi waliohusika na kazi mbovu za majengo ya barabara wafutiwe usajili na Wahandisi wasiruhusiwe kuanzisha makampuni mengine. Ushauri huu tumeupokea na tutaona ni namna gani tunaweza tukawashughulikia.

Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum aliomba barabara ya Koga – Mpanda kwamba itengewe fedha ili ifanyiwe matengenezo makubwa. Katika mwaka wa fedha Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 925 kwa ajili ya kufanya matengenezo maalum katika barabara ya Mpanda – Koga. Pia aliuliza ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami? Nasema, usanifu na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa barabara ya Mpanda – Koga vilikamilika mwaka 2010/2011, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed aliiombea barabara ya Namanyere ijengwe kwa kiwango cha lami. Nasema kwa sasa hivi hatutaweza kuanza kujenga barabara hiyo, kwani tumeamua kwanza tuanze na barabara kuu halafu baadaye tutaingia kwenye barabara za Mikoa na Vijiji.

Pia aliulizia Barabara ya Sumbawanga – Kanazi kwamba imetengewa fedha za ambazo lakini hazitoshi. Labda niseme tu kwamba suala la fedha kutokutosha kwa kweli hili huwezi ku-*determine* kwenye bajeti, kwa sababu Mkandarasi analipwa kutokana na *certificate* anazoleta. Kwa mfano, kama imetengwa Shilingi bilioni sita na Mkandarasi analeta *estimate* ya Shilingi bilioni nne, kwa vyovyote utakuwa na bakaa ya Shilingi bilioni mbili ambazo zinaweza kufanya mradi mwingine. Kwa hiyo, sisi

tunachosema ni kwamba tutalipa malipo kulingana na mikataba yenyewe na Wakandarasi hawa ukiwatembelea mara nyingi wanalalamika kuhusu fedha.

Kwenye mikataba yetu tumekubaliana kwamba kazi ya mkataba huu tutakulipa kwa fedha kiasi kadhaa. Endapo mimi nakucheleweshа kukulipa, ana tozo ananitoza, lakini na yeye akichelewesha kazi na mimi namtoza tozo. Kwa hiyo, tuna mkataba ambao upo wazi na hivyo hana sababu ya kulalamika. Wakandarasi wengi ambao tumewachukua, tunaamini kabisa wana uwezo kifedha. Kwa hiyo, hawana sababu baada ya kupewa kazi, leo wanaanza kulalamika, wanapita barabarani kuwaambia watu kwamba mimi sijalipwa. Hii siyo sahihi na ni kinyume cha mkataba ambao tumekubaliana. Kwa hiyo, tutawalipa kutokana na mikataba ambayo ipo.

Mheshimiwa Profesa Msolla anaulizia kwamba ni lini barabara ya Iringa – Kilolo na Ilula – Kilolo zitajengwa? Majibu ni kwamba barabara hii tumeanza kuijenga kwa awamu na mwaka huu pia tumetenga fedha kwa ajili ya kujenga kilomita moja na nusu. Kwa hiyo, jinsi fedha zitakavyopatikana tutaendelea kuikamilisha barabara ya kutoka Iringa mpaka Kilolo.

Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya anapongeza kwa uzawa, tunashukuru kupata pongezi kutoka kwa Mbunge wa cha Upinzani, tunashukuru sana; anatambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile anaulizia barabara ya Itigi – Tabora, Tabora – Ndono na Ndono - Urambo kwamba mikataba yake ilikwisha kwa wakati. Niseme tu kwamba hii miradi kwanza ilivyosainiwa mikataba haikuanza muda ule ule ilivyosainiwa mikataba. Kwa hiyo, tarehe anazozisema yeye ndivyo walivyosaini mikataba. Lakini ni tarehe gani alianza kufanya kazi? Kwa sababu unakuta miradi mingine pengine kuna vizuizi; labda mali na nyumba hazijaondolewa barabarani. Kwa hiyo, Mkandarasi hawezi kuanza kujenga, ni lazima ku-*clear* mambo haya kulingana na ile *corridor* ya ujenzi. Kwa

hiyo, siyo kwamba mradi muda wake umekwisha, bali ni mikataba na tutauangalia na kuweza kuona ni namna gani tunaweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda wangu umekwisha, naomba niseme tena kwamba tuunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili tuweze kukamilisha barabara zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Lwenge, tunakushukuru sana kwa hotuba yako. Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli - Waziri wa Ujenzi ili aweze kupitia hotuba zetu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi karibu sana na una saa moja ya kuweza kujibu hoja. Karibu sana Mheshimiwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa ili angalau nijaribu kwa uchache kujibu hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia bajeti yetu. Sina uhakika kama nitaweza kuwajibu wote kwa sababu waliochangia kwa maandishi wapo 95 na waliochangia kwa kuzungumza wapo 50 ukiacha waliochangia kwenye Wizara nyingine zilizonitangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru sana Wabunge wote, yaani Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na hata Wabunge wa upande mwingine ule wamechangia vizuri sana na nasema kwa ukweli kabisa na kwa uwazi kwamba wametuunga mkono sana. Michango yao yote itatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba suala la miundombinu katika nchi yetu linapewa kipaumbele kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika historia ya Tanzania, wakati tulipokuwa tukipata uhuru tulikuwa na kilomita 1,130 tu za baraara za lami na wakati huo tulikuwa na magari 38,000 yaliyokuwa yamesajiliwa. Miaka 50 baadaye tumekuwa

kwenye *range* ya kilomita kati ya 6500 – 7000 za barabara za lami. Kwa sasa hivi barabara za lami zinazojengwa ni zaidi ya kilomita 11,154. Kwa hiyo, nina uhakika katika miaka michache inayokuja tutakuwa karibu kilomita 20,000 za barabara za lami katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilitaarifu Bunge lako kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi tano bora katika Afrika ambazo zinajenga barabara zake kwa kutumia fedha zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukajiuliza kwa misingi mikubwa tu ya ukweli kwamba, tunapoona nchi nyingine za Ulaya zinapata mtikisiko wa uchumi, nenda *Portugal, Spain, Italy* na hata nchi nyingine ambazo zimeendelea, zimekuwa zinapata *problem* ya *Euro zone*. Unapokuta nchi masikini kama Tanzania inaweza kuthubutu kujenga barabara zake kwa kutumia fedha zake, ni kitendo cha kupongezwa. Siyo cha kupongezwa tu kwamba, Chama cha Mapinduzi kinatimiza wajibu wake, lakini ni cha kupongezwa pia kwamba juhudi kubwa zinafanywa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema kwa dhati kabisa kwamba, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wa pande zote. Wamechangia kwa kuandika na kuzungumza, wakielezea hali halisi ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi katika kuendeleza miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango iliyotolewa na Kamati ya Miundombinu, mimi naipongeza sana. Wametoa ushauri mwingi tu, wametoa pongezi, mambo ambayo Serikali inatakiwa itekeleze, fedha zinazopangwa zipatikane, msongamano wa Jiji la Dar es Salaam utatuliwe, madeni ya Wakandarasi yazingatiwe, na mengine mengi yamezungumzwa. Lakini pia wamezungumzia juu ya msongamano wa magari katika mizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba, hatua zimeanza kuchukuliwa, lakini ni jukumu letu pia kuhakikisha kwamba ni lazima tulinde barabara zetu zinazojengwa kwa gharama kubwa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii inaongozwa na sheria, na moja ya sheria inayozingatiwa katika kulinda barabara zetu ni Sheria Na. 30 ya mwaka 1973. Katika sheria hiyo *gross weight* ya magari yanayotakiwa kupita katika nchi yetu ni tani 56. Lakini kwenye nchi zilizoendelea ambazo zinatoa misaada, hata kwa Tanzania, nikitoa mfano tu Marekani, *gross weight* yake ni tani 40, Ufaransa ni tani 40, Uingereza ni tani 44, Hungary ni tani 44, Italy ni tani 44, Armenia tani 36, Ujerumani tani 40 na kadhalika. Sasa unaweza kuona ni kwa namna gani tusiposimamia sheria katika kudhibiti uzito wa magari yanayopita kwenye barabara zetu, *investment* kubwa hii inayotumia fedha za maskini haitadumu. Ndiyo maana mizani ilianzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika nchi za wenzetu majirani, Kenya *gross weight* ni tani 54, Uganda ni tani 54, sisi ni tani 56, lakini bado watu wanazidisha uzito. Hawa wasafirishaji ni kama wafanyabiashara wengine, *they are after profit maximization*. Mwezi uliopita tumekamata magari yalikuwa na tani 100 na mwenye magari alipoomba kibali Wizarani alisema anasafirisha vipande vya *transforma* kwenda Malawi. Walipofika kwenye mzani wa Kibaha, tumekuta moja lilikuwa na tani 95, lingine tani 92 na lingine karibu tani 100. Hawajali! Kwa hiyo, tuliwakamata na wamekaa pale, kwa mujibu wa Sheria Na. 30 ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye ripoti yetu hapa, kati ya magari milioni 2.5 yaliyopita katika barabara zetu, magari zaidi ya laki 5.7 yalizidisha uzito, ambayo ni zaidi ya asilimia 25.7. Ndiyo maana barabara hizi zinajengwa kwa gharama kubwa na mikopo inahusisha hata watu masikini ili kusudi barabara zitengenezwe. Sasa kama tutakubali zitumike vibaya kwa wasafirishaji kujiunga ili kusudi wadai kwamba wawe wanapitisha mizigo mizito, barabara hizi hazitadumu. Ndiyo maana katika nchi zilizoendelea,

usafirishaji mkubwa wa mizigo mikubwa, huwa reli ndiyo inatumika. Napongeza sana juhudi za Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, katika kufufua reli ili mizigo mingi ipitie kwenye reli na barabara zetu ziweze kudumu kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge tunapochukua hatua za kuzuia mizigo mikubwa kupita kwenye barabara zetu, siyo kwamba sisi tuna mioyo mibaya, bali tunazingatia sheria mliyoipitisha ninyi na kuapa mbele ya Spika. Kwa hiyo, mtuache tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri hawa wafanyakazi wa *TANROADS* wanapata matatizo mengi na vitisho. Nilitaka nieleze tu kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani iliwa-*rank* watu wa *TANROADS* kama hawafanyi vizuri na wakati mwingine wakazungumza mpaka *zero*.

Nataka nimpe takwimu Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, na nitaziacha hapo ili kusudi apate *information* vizuri. Katika Taasisi zinazofanya kazi vizuri katika Afrika, *Executive Agency* ya kwanza inaitwa *SANRAL* ya *South Africa*, na ina-*deal* na kilomita 10,000 tu. Ya pili ni *Namibian Road Agency* nayo ina *deal* na kilomita chache. Ya tatu ni *TANROADS* ya Tanzania inayo-*deal* na kilomita 35,000 ambazo ni *trunk roads* na *regional roads*, na ina-*deal* na madaraja 4,880. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwelewa Mheshimiwa Said Arfi, angeniambia mimi Mbunge wa CCM ni *zero* ningempongeza. Lakini inasikitisha sana, unapoona *agency* kama *TANROADS* inayofanya kazi kubwa, inayosifiwa na vyombo mbalimbali; *World Bank* katika ripoti yao nayo nitakuletea hapa, inaisifu *TANROADS*. Katika maneno mafupi tu waliyozungumza katika *document ya The World Bank Report* No. ICL0001299 na iko kwenye *website* wanasema; *TANROADS did the good job. Good job* maana yake ni kazi nzuri. Hata Wasukuma wanafahamu, ukimwambia *good,* anajua ni *good*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kuzungumza ni kwamba siasa tuziweke pembeni. Kwenye vyombo hivi vya Taasisi ambavyo vinasifiwa kimataifa na hata fedha zitakazokuja sasa hivi kwa ajili ya kununua magari ya Polisi na nini, zinapitia *TANROADS* ambayo tayari wamesaini mkataba tarehe 02 Machi, 2013. Katika *document* ile inasema, "*Over site of the procurement and contract management activities of the other agencies, TANROADS have considerable experience with previous corridor project and are fully conversant with the bank procedure.*" Hii ni Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilimwelewa Mheshimiwa Arfi, hakutaka kuwasifia *TANROADS*, alifikiri labda nao ni CCM. Lakini *TANROADS* na *Chief Executive* mmeelewa mnavyosemwa kwa sababu alisema kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, pamoja na kutengeneza barabara ya Sumbawanga hadi Kasanga kilomita 112, pamoja na kutengeneza barabara zinazokwenda kwa Mheshimiwa Arfi, lakini mnaweza mkaelewa anavyoweza kuwasema. Nina uhakika amesema kwa niaba yake na siyo kwa niaba ya Wapinzani, kwa sababu wao wameunga mkono. Kwa hiyo, *TANROADS* mnaorodheshwa kama ni CCM, kwa hiyo, wafanyakazi wa *TANROADS* mji-*arrange* siku nyingine msiwe mnawapigia kura hawa watu. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, ni lazima tujisifie kutokana na *agencies* zetu zinazofanya kazi vizuri. *Agency* ya Kenya, Agency ya Uganda – *LAPF*, wamekuja kujifunza Tanzania. Kuna barua hapa ya *JICA, agency* ya Sri-Lanka, wanatumwa kuja kujifunza katika *TANROADS* ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *information* nyingi lakini kwa sababu ya muda mfupi, ukitaka hizi *information* nitakupa, ili kusudi wenzetu waweze kuelewa, kwamba tunapoanza kushambulia *agencies* ambazo kwa bahati nzuri zinatupa jina zuri katika nchi yetu, tunawavunja moyo. Hawa

watu wanafanya kazi sana, usiku na mchana. Mheshimiwa Rais amewasifu, Wabunge wengi wa Vyama vya Upinzani na CCM wamewasifu. Unaposimama hapa kwa sababu umepata nafasi na kuanza kuwasema vibaya, saa nyingine inavunja moyo. Lakini Kama Mheshimiwa Arfi angenisema mimi vibaya ningempongeza sana. Kwanza ni mtani wangu.

Kwa hiyo, wala nisingeshtuka kwa sababu ningejua anatimiza wajibu wake wa kuwasema watu vibaya, pamoja na kwamba, Mwenyekiti wake wa Chama cha CHADEMA, tarehe 31 mwezi Oktoba tukiwa Hai na kupitia *website* zao za *Jamii forums* na naweza nikazitaja, httpcolumn// www.youtube.com/watch?v=vhdateyh_kmnw, alikisifia Chama cha Mapinduzi. na *floppy* ya yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Mbowe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nampongeza sana kwa sababu ni miongoni mwa viongozi wachache wanaosifu kazi za Chama cha Mapinduzi. Kama kuna mtu atakayekuwa na ubishi, bahati nzuri nimekuja na *sound* hapa, nitaiweka halafu mumsikie alivyozungumza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za barabara ni ngumu na bahati nzuri kazi hizi zimekuwa zikishughulikiwa sana na Serikali. Michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni ya kuisaidia Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Kuna masuala ya madai ya Makandarasi, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kikamilifu. Kandarasi anapopewa kazi kwanza anapewa muda wa miezi sita kufanya *mobilization*. Lakini *tender* zote za barabara hizi zinazojengwa za urefu wa kilomita 11,159 pamoja na madaraja yake ni *international tendering*. Kwa hiyo, kandarasi anapoomba kazi ni lazima apate *guarantee.* Ndiyo maana kampuni moja ya kule Kusini baada ya kufukuzwa ilipoacha ku-*perform* kazi vizuri *progressively,* tulishika hata *guarantee money* waliyokuwa wameiweka. Walifungua kesi, tukawashinda, wamefungua kesi nyingine. Kwa hiyo, sitaki nizungumze mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mkandarasi anapoenda kwenye *site,* jukumu lake la kwanza atalipwa *mobilization amount* ya fedha, inaitwa *advance payment.* Baada ya hapo, asipo-*produce certificate*, hawezi akalipwa fedha yoyote. *No certificate, no payment!* Lakini kwa sababu Wakandarasi nao ni wafanyabiashara, *they are after profits maximization*; ukimfuata kwenye *site* atasema hatujalipwa na Serikali. Ni kisingizio na ndiyo maana kupitia Bodi ya Makandarasi, tangu ilipoanzishwa, tumeshafukuza Makandarasi 3008 katika nchi hii na tutaendelea kuwafukuza. Hata wa Tabora waelewe hivyo na Makandarasi wa maeneo mengine yote. Tunataka wafanye kazi kwa kuzingatia mkataba uliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mwaka huu fedha zote za ndani asilimia mia moja; Shilingi bilioni 296.7 zimelipwa. Asilimia mia moja! Zile fedha za wafadhili ndiyo hazikutoka kwa asilimia mia moja. Lakini kwa bahati nzuri, kwa sababu Makandarasi waliokuwa kwenye *sites* wameweza kufanya kazi nzuri na waka-*produce certificates* nyingine zaidi, leo ninapozungumza, Waziri wa Fedha ametoa fedha nyingine Shilingi bilioni 167 katika kufidia zile fedha zilizokuwa zimetolewa na wafadhili. Hizi zote nazo zitakwenda kwa Makandarasi. Kwa hiyo, ole wao Makandarasi, wafanye kazi, wasitafute visingizio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwa miradi ya Tabora, bahati nzuri iliwekewa jiwe la msingi na Mheshimiwa Rais. Katika miradi yote ya Tabora, thamani yake ni zaidi ya Shilingi bilioni 50 na fedha zote zimetolewa na Serikali kwa asilimia mia moja. Tumeshasema, Makandarasi wale ni lazima wamalize miradi ile. Kandarasi akichelewa kumaliza mradi, siyo tatizo la mlipaji kwa maana ya Serikali. Kandarasi yeyote anapochelewa kumaliza mradi kulingana na mkataba, kwenye kipengele cha mkataba cha kimataifa anakatwa *liquidation*. Tumekuwa tukifanya hivyo. Aliyekuwa anajenga daraja la Mkapa, alikatwa *liquidation*. Ni kitu cha kawaida kwa Mkandarasi kukatwa fedha kwa sababu hajamaliza kazi kulingana na wakati wake. Siyo kwamba, kila Mkandarasi

anapochelewa, maana yake ataomba *variation*; na siyo wajibu wa Mkandarasi kuchelewa kwa sababu ana *guarantee* ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makandarasi waliosajiliwa katika nchi hii wako 6691. Kwa hiyo, wanapokuja Makandarasi wa nje kufanya kazi ni lazima wapate *guarantee* kwa sababu wamewanyima nafasi Makandarasi wazalendo. Kazi hizo zingeweza kufanywa na Makandarasi wazalendo. Wasitafute visingizio kwamba wamekuja Tanzania kufanya kazi kwa sababu ni nchi tajiri ikiongozwa na Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Arfi amezungumzia juu ya kasma 4168 ya fedha Sh. 252,000,975,000/=. Kasma hii ilikuwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 na ilikuwa na *special fund* kwa ajili ya kulipia madeni ya Makandarasi. Kwenye bajeti ya mwaka 2012 nilitoa taarifa hapa nilipokuwa nikiwasilisha bajeti yangu ya mwaka 2012/2013 na leo niko kwenye bajeti ya mwaka 2013/ 2014. Mheshimiwa Arfi alinyamaza katika mwaka wa fedha 2012/2013, akasubiri mpaka ninaingia mwaka wa fedha 2013/ 2014 ndiyo anaanza kuleta kipengele hicho ambacho tayari kimeishatolewa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Bunge lilipitisha hizo fedha ambazo zilisaidia kuwalipa Makandarasi ambao waliweza ku-*speed up* kazi katika miradi mbalimbali inayotekelezwa katika nchi hii. Ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu Serikali imeongeza fedha za maendeleo. Mwaka 2012 zilikuwa Shilingi bilioni 6,700 mwaka huu ni Shilingi bilioni elfu nane na kitu. Ndiyo maana bajeti ya Wizara ya Ujenzi imepanda katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza miradi hii yote na ikamilike kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Arfi ametoa pongezi kwa Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*, ameeleza matumizi mabaya ya Mfuko wa Barabara, matumizi ya maabara, *monitoring* na kadhalika. Ningemwomba

Mheshimiwa Arfi akasome Sheria Na. 2 *Amendment Act* ya mwaka 1998 na mabadiliko yake ya mwaka 2006 ambayo yanazungumza kwamba, *ten percent of the money should be used for other development projects of the road*, *including monitoring* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama unaweza ukamwajiri Mkandarasi akaenda kwenye barabara, utakosa hata fedha za kwenda kufuatilia kule? Atakwenda kwa miguu? Utakosa hata magari ya kwenda kuangalia kule kazi zinavyofanywa? Utakosa hata fedha za ku-*test* udongo ili ujue *soil texture* ya udongo ule unaojengwa barabara ya lami ukoje? Hizi ndizo kazi za *monitoring* zilizofanywa, siyo matumizi mabaya na hiki kimepitishwa na Bunge hili.

Kwa hiyo, wakati mwingine ndugu yangu Mheshimiwa Arfi najua wewe ni mtani wangu inawezekana mambo mazuri mazuri sana yanayofanywa na Chama cha Mapinduzi huyafurahii. Lakini pongeza tu kama walivyopongeza Waheshimiwa Wabunge wengine wa Upinzani. Ukipongeza kwani hutalaanika? Utapongezwa tu, kwa sababu msemakweli wakati mwingine ni mpenzi wa Mungu. Lakini tusitafute vipengele ambavyo vingine vinaendana hata na sheria tulizozipitisha sisi Bungeni.

Mheshimiwa Arfi amekuwa hapa zaidi ya miaka saba na nusu. Mabadiliko ya mwaka 2006 alikuwepo hapa. Kama angeona hayafai, asingeyaweka humu. Sasa watu wetu wa *TANROAD* wanapotekeleza sheria kwa matakwa ya wananchi kwa matakwa ya Bunge hili, mtu unazunguka tena nyuma unasema umetumia kwa *monitoring;* wakati tunataka tujue *quality* na *quality for money.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewarudisha Makandarasi katika barabara ya Kilwa. Wangejuaje kama wasingekwenda kule? Tumewarudisha Makandarasi katika barabara ya Sekenke, ametumia zaidi ya Shilingi bilioni 15 fedha zake mwenyewe. Tukamrudisha *consultant* kutoka Ufaransa, akarudia pale na akakaa pale mwaka mzima anaangalia barabara. Angerudije kama wasingefanya

*monitoring* na ku-*test* udongo? Mambo mengine yanaumiza, lakini mimi najua maana yake. Ndugu yangu yule alitaka kunitania, alifikiri na mimi niko *TANROAD,* kumbe mimi ni Msimamizi wa *TANROAD* na *TANROAD* inasimamiwa na Serikali nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa Jiji la Dar es Salaam hatua tumeshaanza kuzichukua, tume-*include* barabara nyingi tu. Hatuwezi tukayamaliza yote kwa siku moja! Kupanga ni kuchagua. Kama msongamano huu haukwisha kwa miaka 50, mnataka mimi niumalize kwa siku moja! Msongamano upo, una mambo mengi! Watu wakitaka kujenga, wanajenga Dar es Salaam tu, hawajengi pembeni mwa Mji. Unataka niumalize msongamano leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetengeneza barabara ya Tegeta Shilingi bilioni 88 njia nne; tutaanzisha sasa usafiri wa majini kwenda baharini; tunajenga Dar es Salaam *BRT road* Shilingi bilioni 290 zinatumika pale. Pale *Fire* patakuwa na njia sita; tunatengeneza *flyover*; tume-*include* vibarabara vingine vya pembeni mpaka vya Mheshimiwa Mnyika, kingine tumekiwekea Shilingi milioni sita na hataki kushukuru; halafu atasema baadaye barabara ile ameileta yeye. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kwamba katika hali halisi tumepanua barabara ya Kilwa, kwa sasa hivi kuna fedha zimetengwa zitajenga njia nne kwa barabara inayotoka hoteli tatu pale, kuja Gerezani pamoja na lile daraja na tutatengeneza *flyover*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatengeneza lile daraja la Kigamboni, daraja la aina yake katika Afrika Mashariki na ya Kati, litakuwa *suspended* mfano wa daraja lile la Kirumi kule Musoma, lakini lenyewe litakuwa na mita 68 na litatengeneza kilomita nyingine 2.5 kila upande. Patakuwa na *flyover* sehemu ya kupisha, yote yale ni kwa ajili ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam. Tumeanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ningewaomba sana tuwe tunasikilizana kama mlivyokuwa mnaongea ninyi mlikuwa mnasikilizwa, nawaomba tusikilize majibu, ndiyo Bunge linakuwa linanoga zaidi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakyembe naye ameanza treni ya kwenda kule. Hizi ni juhudi kubwa za Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha tunapunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Hatufanyi katika Jiji la Dar es Salaam tu; Mji wa Arusha tunatengeneza *bypass;* tutatengeneza njia nne kuanzia Arusha hadi Sakia kilomita 14. Ni juhudi kubwa zinazofanywa na Chama cha Mapinduzi! Mji wa Mwanza pamoja na kwamba ni wa Wapinzani, tunatengeneza daraja pale Mabatini na Mkandarasi ameshaanza kufanya. Hapa namshukuru sana Mheshimiwa Hewa, aliomba sana na tukaamua kuweka pale kwa sababu ndio anawasemea Wabunge wa Mwanza. Kwa hiyo, tunafanya! *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika Mji wa Dodoma hapa, mnaweza mkaona *infrastructure* za barabara zinazotengenezwa. Tunataka kutengeneza *diversion* ya barabara ambayo haitapita mjini. Tunatengeneza barabara za kutoka Dodoma kwenda Iringa kwa Wahehe huko ndugu zangu na wengine hawatapata shida hata wakitaka kujiua, sasa watakuwa wanalala barabarani tu Wahehe! *(Makofi/ Kicheko)*

Tunatengeneza barabara ya kutoka hapa Dodoma kwenda Babati na tumeeleza, tuna Shilingi bilioni 56 zimetengwa kwa ajili ya barabara hii chini ya ufadhili wa *ADB*. Tunatengeneza barabara ya kutoka Masasi kwenda Mbambabay. Tumetenga fedha zote katika mradi wa Kusini kuna Shilingi bilioni 139, mpaka barabara ya kwa Mheshimiwa Komba kule inatandikwa lami mpaka kule kwenye Ziwa Nyasa. Lakini tumeweka karibu Shilingi bilioni 60 katika Mkoa wa Rukwa na Katavi. Maelezo haya yote yako kwenye kitabu na fedha zipo. Barabara ya Sumbawanga - Kasanga, barabara ya Sumbawanga – Mpanda; kutoka Tunduma

mpaka Sumbawanga kilomita 232 kuna mradi wa *MCC* wa Wamerikani, kwa sababu wanaiamini Serikali ya Tanzania. Kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda pale Kiizi Kibaoni kuna Makandarasi wawili. Kutoka Kizi Kibaoni mpaka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, napo tumeweka Makandarasi. Hizi kazi siyo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetengeneza *infrastructure* za barabara za Kigoma. Ukitoka kule Mwandiga Manyovu kule mpakani kilomita zote 60 ni lami. Barabara za Kigoma Mjini kuja Kidahwe ni lami. Ukitoka Kidahwe kwenda Uvinza kilomita 76.6 ni lami sasa hivi. Daraja la Kikwete pale limeshakamilika, magari yameshaanza kupita nje. Tumekuja mpaka Tabora, tunataka nchi nzima sasa isambae kwenye barabara za lami. Ukitoka Arusha sasa hivi kuja Babati ilikuwa ndiyo mwisho wa lami pale Minjingu. Lakini sasa utoke Minjingu, uje Babati mpaka Singida mpaka uende Chato mpaka Kagera kule ni lami. Sasa tufanyeje jamani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninataka ndugu zangu hawa wachache ambao hawataki ku-*appreciate*, wa-*appreciate* hata kama kazi zinafanywa na Chama cha Mapinduzi. Ndiyo maana Mheshimiwa Mbowe alisema "Mnyonge Mnyongeni, lakini haki yake mpeni". Kwa hiyo, nilitegemea hata wenzake walioko kule chini anaowaongoza awe anawaeleza maneno aliyoyazungumza ya kukisifia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu ni mfupi, ngoja niende sasa haraka haraka. Mheshimiwa Chenge ametoa ushauri mzuri tu, ametoa shukrani, amezungumzia kuhusu barabara zake alizoziomba ambazo kwa kweli napenda kukiri kwamba Mheshimiwa Chenge ile barua nimeshaipata kutoka kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, tutaangalia ni nini cha kufanya. Amesema anashukuru kwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya barabara ya Lamadi - Bariadi, fidia zilipwe kwa watu wa Usagara, Kisesa. Usagara, Kisesa hawatalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile barabara imeanza tangu enzi za ukoloni. Tangu enzi za Ujerumani ilijulikana kama

barabara *T8* na wale watu wamejenga kwenye *road reserve* na *ignorance of law is no defence*. Kama wanaona wanaonewa, waende Mahakamani. Bahati nzuri sisi tumeshawahi kupelekwa Mahakamani. Tulipobomoa nyumba kwa nyumba za Ubungo kwenda Kimara tulipelekwa Mahakamani na kesi hiyo ilikuwa ni kesi ya *Bounce & others,* kesi namba 39 na aliyoisimamia alikuwa Mheshimiwa *AG* hapa. Walitushitaki Maprofesa na nani na tulishinda. Naye ilikuwemo nyumba ya mjomba wake ikabomolewa. Najaribu kuzungumza ukweli kwa sababu sheria ni msumeno. Tusiwe tunapitisha sheria hapa halafu tunarudi nyuma watu tuwaangalie kulipwa fidia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu watu wamebomoa nyumba, hata mimi ukuta wa Marehemu baba yangu, nimeubomoa, ulikuwa kwenye *road reserve*. Ni lazima tuzingatie sheria ili barabara hizi tuzijenge. Lakini ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, kama mnaona hii sheria ni ya manyanyaso kwa wananchi, tukae hapa, tulete Muswada, tubadilishe, upana wa barabara uwe sentimita mbili, basi! Nasi tutaanza kutekeleza kwamba upana wa barabara kuanzia leo ni sentimita mbili. Lakini kama mmeipitisha wenyewe hiyo sheria kupitia *Cap.* Na. 167 ya mwaka 1967 na sheria ilianza mwaka 1932 mkaifanyia mabadiliko mwaka 1940, mkaifanyia mabadiliko mwaka 1942, mkaifanyia mabadiliko mwaka 1949, mkaifanyia mabadiliko mwaka 1957, mkaifanyia mabadiliko mwaka 1959, mkaifanyia mabadiliko mwaka 1967 kupitia *Cap* Na. 167 na mmeifanyia mabadiliko kupitia Sheria Na. 13 ya mwaka 2007, tutatekeleza sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siasa tuziweke pembeni, tutabomoa nyumba za wana-CCM, tutabomoa nyumba za wana-CHADEMA, tutabomoa nyumba za Wagogo, tutabomoa nyumba za Wasukuma, tutawabomolea ili mradi wako kwenye *road reserve*. Barabara ikiwafuata, watalipwa fidia kwa mujibu wa Sheria Na. 4 na 5 ya mwaka 1999 kifungu Na. 3(g). Lakini pia kwa mujibu wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi kama yalivyoainishwa kupitia Sheria Na. 6, 7, na 8 ya mwaka 2007. Lakini pia kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya

mwaka 2007. Tuzingatie sheria. *We are just servant!* Kazi hizi ni ngumu sana! Msifikiri mimi nafurahi kuona lijumba linaanguka. Kuna matatizo yake! Tulikuwa tunajaribu kubomoa mwembe mmoja kwa Mheshimiwa Mwangunga kule. Ule mwembe, *is a true story* Mheshimiwa Mangunga atawaeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, Mbunge wa Kilwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mangungu eeh, majina yale si magumu magumu ya kule! Kampuni ya Karafi wamehangaika nao siku nzima hawajauangusha. Wameleta ma-*bulldozer* na kadhalika mwembe ule haukuanguka. Tukamwomba Mheshimiwa Mangungu kwamba waombe wale wazee mti ule uondoke. Aliposema tu, kesho yake ukaondolewa na ka-*bulldozer*. Sasa kama wameshindwa kubomoa ule mwembe, mwenye mwembe yule unafikiri anasemaje kwangu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hizi ni ngumu! *Is too risk!* Lakini ni lazima tufanye kwa ajili ya Watanzania katika kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania, bila kujali *outcome* na matatizo yanayotupata. Mainjinia hawa wanapata mateso mengi! Wapo wanaowatukana, wapo wanafanya nini, lakini wanafanya kwa manufaa ya Tanzania kwamba Tanzania yetu ni lazima iwe sasa inapitika. Tumechoka mtu anatoka Bukoba aende mpaka Uganda, aende Kenya halafu anakuja Dar es Salaam. Wale Wahaya pamoja na Nshomile yao, walikuwa wanapita huko wanazunguka wanasema bwana, lakini sasa wananyoosha moja kwa moja mpaka Dar es Salaam. Ni kwa sababu tumezingatia sheria. Sasa ni vizuri mtuache kama mmetuamini kufanya kazi, tufanye kazi. Kama hamtuamini, ni vizuri pia tuwapishe wengine waje ambao watakaotekeleza sheria kwa huruma huruma hivi ili barabara zitengenezwe. Nasema kwa dhati bila unafiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia barabara za Nata Makutano, tumeshasaini zitatengenezwa kutoka

Makutano - Butiama kupitia Nyamuswa hadi Nata na tutaendelea mpaka Loliondo na kuja mpaka Mto wa Mbu. Amezungumzia kufungua barabara, hilo tunakubaliana nalo. Amezungumzia pia kupatikana kwa fedha, Serikali ya Jakaya Mrisho Kikwete inajitahidi sana katika kutafuta fedha. Anajitahidi kuzunguka kila mahali, juzi alikuwa Kuwait, anaomba fedha na amefanikiwa. Kila mahali anazunguka! Wengine wanasema anazunguka, anatembea; mwacha atembee atutafutie fedha za kutengeneza barabara. Tuwaache hao wanaokaa nyumbani kwao tu bila kutembea, wakae hivyo hivyo waangalie chakula kinavyopikwa. Yeye anazunguka ili kusudi fedha zipatikane tutengeneze barabara na ndiyo maana kuna miradi mingi. Mradi wa MCC Wamarekani wanatoa fedha. *African Development Bank*, *JICA*, Wajapan, *World Bank* ni kwa sababu Rais wetu anatembea. Ukitaka samaki, nenda ukavue. Usipomtaka, basi utaletewa hata aliyeoza. Mwache Mheshimiwa Rais atembee kusudi tupate fedha za kutengeneza barabara na miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Agripina Buyogera amesema hapa amepongeza sana. Nakupongeza sana Mama. Ni wachache, mtu wa NCCR-Mageuzi unapongeza CCM. Hata sura yako imekaa ki-CCM, CCM tu, mimi nakupongeza sana. Kwa hiyo, mwili wako ni NCCR-Mageuzi, lakini moyo wako ni wa CCM, na moyo wa CCM ni mtakatifu takatifu. Mimi nataka kukuhakikishia yale uliyotupongeza na yale uliyoyaomba tutayafanyia kazi. Kwa sababu hata watu unaowaongoza siyo wa Chama chako tu, hata CCM walikupigia kura. *(KichekoMakofi)*

Mheshimiwa Halima Mdee amezungumzia juu ya barabara ya Mwenge – Tegeta, amesema sasa hivi imeanza kuingiwa maji, tunakubaliana na hilo, tunafanya *re-designing*. Tunaangalia ili kusudi maji yasije yakaharibu, tulipata hiyo barua yake. Lakini kubwa lingine amezungumzia kuhusu nyumba ya Saruji zilizorudishwa *TBA*. Ni kweli, zile nyumba za Saruji zilirudishwa *TBA* kupitia *Government Notice* Na. 63 ya tarehe 23 Mei, 2008. Idadi ya nyumba hizo zilikuwa 226 wala siyo 150. Idadi ya wakazi wanaokaa kwenye nyumba hiyo ni

2000. Lakini mwaka 2010 walikwenda wakafungua kesi na yeye bahati nzuri ni Mwanasheria, wakafungua kesi dhidi ya *TBCC* na kesi ile ni Na. 30 ya mwaka 2010. Sasa kuanzia mwaka 2010 Wizara ya Ujenzi isingeweza kuingilia kitu chochote, wala Serikali isingeweza kuingilia kitu chochote kwa sababu kesi ilikuwa Mahakamani; na wewe ni Mwanasheria, bahati mbaya mimi sio Mwanasheria. Kesi ile imetolewa *ruling* tarehe 31 Desemba, 2012 na Mheshimiwa aliyeisikiliza ni Mheshimiwa A. F. Gwara na alitupilia mbali madai ya wakazi hawa. Baada ya hapo, hawa wakazi wameandika barua kwa Jaji Mkuu wakitaka i-*revisit* ule uamuzi, bado wamenifunga mimi kuingilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya sisi kama Wizara, *TBA* imemwandikia Jaji Mkuu kwamba wale wakazi tunawatambua na kweli zile nyumba ziko chini yetu kwa mujibu wa *Government Notice* Na. 63 ya tarehe 23 Mei, 2008. Tuyaache haya mambo ya Kimahakama yaishe, mimi sio mtaalamu wa Mahakama. Ukishaisha huo utaratibu, njoo. Bahati nzuri ile hati Serikali ipo na Mheshimiwa Tibaijuka ameshakwenda kuzungumza mpaka na maeneo hayo kwa masuala mengine mengine; sasa kwa sababu liko kwenye Mahakama, Mheshimiwa *AG* anaweza akashauri vizuri. Nimeishia hapo hapo, nimeambiwa. Kwa hiyo, kama ulikuwa mtego wa kuniingiza huko, umekwama. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Anne Kilango ninampongeza sana. Hapa ndipo naweza nikajua kwa nini mtani wangu Mheshimiwa Malecela aliweza akapanda milima yote kwenda huko kutafuta mwanamke kama wewe. Alijua ni mwanamke mwenye busara. Nampongeza sana Mheshimiwa Malecela, ndiyo maana hakuja kwa Wasukuma. Umeelezea masuala ya msingi na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais alipokwenda kwenye barabara hizo kwenda kufungua kile Kiwanda cha Tangawizi alitupa maelekezo ikiwa ni pamoja na kuitengeneza hiyo barabara. Tumekwishapokea barua yako ya kupandisha barabara hii hadhi. Bahati nzuri kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, napo tumeshapewa maelekezo. Nataka nikueleze Mheshimiwa Kilango, hii barabara tutaipandisha hadhi. Ninakushukuru

sana kwa mchango wako ulioueleza humu, ni mchango wa kitakatifu. Mengine umeshatuandikia barua, tutaendelea kuyazingatia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda haraka haraka, Mheshimiwa Shah ametoa pongezi, amezungumzia kuhusu hilo daraja. Mheshimiwa Shah nataka kukuahidi, tukimaliza hapa na bahati nzuri barabara yako ile ya kule tumeshaipangia fedha Shilingi bilioni mbili *and something*. Lile daraja lililobomoka ambalo linaunganisha na Uwanja wa Ndege nitawatuma wataalamu wangu wakaangalie namna gani ya kufanya *rehabilitation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya amezungumzia barabara za kwenda milimani. Chama cha Mapinduzi siyo kweli kwamba Watanzania wote wanachangia maendeleo. *Yes*, wanachangia maendeleo, lakini mwenye kusimamia maendeleo hayo ni CCM, kwa sababu CCM ndiyo yenye uwezo wa kuamua hii barabara itengenezwe au isitengenezwe. Ndiyo ukweli! Serikali iliyoko madarakani ni ya CCM na Ilani inayotekelezwa ni ya Chama cha Mapinduzi; na Waziri wa Barabara ni Magufuli wa CCM na Rais wa Tanzania ni Kikwete wa CCM. *That is the fact* inabaki vilevile. *(Makofi/Mayowe)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni ukweli nakubaliana na Mheshimiwa Owenya kwamba michango hii ya maendeleo inachangiwa na wananchi wote bila kujali Vyama vyao. Ndiyo maana katika kuzingatia hilo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitengeneza barabara maeneo yote bila kujali Vyama vyao. Imejenga kwa Mheshimiwa Freeman Mbowe, imejenga kwa Mheshimiwa Selasini, inajenga Kigoma kwa Mheshimiwa Zitto; hayo ndiyo maendeleo kwa sababu ni lazima tuujenge Utanzania wetu bila kuangalia itikadi zetu. Lakini msimamizi wa maendeleo haya ni CCM. Ukweli unabaki kuwa ni ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Owenya amechangia vizuri na anaomba barabara ya utalii kilomita kumi ijengwe kwa lami. Sasa kwa sababu barabara ni ya utalii,

nafikiri wenzetu wa Wizara ya Maliasili tutaongea nao na tutangalia nini cha kufanya. Lakini amesema matuta yamejengwa kwa *standard* nyingine, mengine ni makubwa na mengine ni madogo. Ushauri huu mzuri tunauzingatia na tutaangalia *standard* ya matuta yatakayokuwa yanajengwa na ikiwezekana kwenye *highway* pasiwepo na matuta kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Owenya ametoa ushauri mzuri kwa utengenezaji wa magari *TEMESA*, tumeuzingatia; amezungumzia pia msongamano wa Jiji la Dar es Salaam, Tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi ametoa pongezi kwa Wizara, amezungumzia juu ya utekelezaji wa barabara za Taifa huko juu, anaomba matengenezo ya barabara zake ambazo amezitengeneza na amezungumzia kuhusu barabara ya kwenda Amani ambapo wana-*produce* zaidi chai. Tutalizingatia Mheshimiwa Mntangi tuangalie ni namna gani tunaweza tukatengeneza baraba hiyo ambayo wana-*produce* vizuri chai. Lakini umetoa mchango mkubwa juu ya Makandarasi ambao wengine hawa-*perform* kazi vizuri, mwingine tulimtoa mwaka 2011 tutaendelea kuzingatia ushauri wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rosemary Kirigini amezungumzia juu ya barabara, na amezungumzia vizuri sana juu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchanguzi katika Ibara ya 62 hadi 77. Amezungumzia juu ya ahadi za Mheshimiwa Rais, amezungumzia juu ya barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisolya hadi Nansio na kwa sasa hivi tumeshatangaza *tender* ile barabara kwenye *section* fulani tutaimaliza ili nayo ijengwe kwa kiwango cha lami. Amezungumzia juu ya barabara za Wilaya ya Butiama kwa mfano Musoma – Bukima ijengwe kwa kiwango cha lami. Tutaanza na kilometa 1.5 nafikiri katika bajeti hii; lakini pia tutaendelea kuikarabati ile barabara iweze kutumika na kadri itakavyokuwa tunapata fedha barabara hii tutaimairisha vizuri ili iweze kupitika vizuri mpaka kule kwenye mwalo wa samaki ambao ni wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwaiposa anaunga mkono hoja, anazungumzia juu ya barabara za Ukonga. Anasema barabara nyingi ziko chini ya Halmashauri, anazungumzia juu ya barabara ya Chanika, amezungumzia barabara za kupunguza foleni. Kwa ujumla ametoa mchango wake kuhusu barabara zinazomhusu. Ushauri wake tumeuzingatia, lakini bahati mbaya muda wangu ni mfupi sana na sasa hivi nimejibu hoja chache sana. Lakini nataka kusema tu kwamba nimeyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deo Filikunjombe amezungumzia kuhusu *concern* ya barabara yake ambayo inafanyiwa *design.* Tumeanza *design* mwaka 2012 tulitenga Shilingi milioni 800 na mwaka huu tumetenga fedha nyingine. Barabara ile tunataka tuijenge kwa kiwango cha lami na alielezea *concern* yake katika Wilaya yake ndiyo Wilaya pekee ambayo haina lami. Tutaliangalia hili tuhakikishe barabara hizo tunatengeneza kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Njwayo anaunga mkono, anazungumzia juu ya barabara ya Masasi – Newala - Mtwara. Hii ni barabara ya siasa. Ni barabara ya siasa, lakini pia ni barabara ya uchumi. Amezungumzia juu ya daraja la Mwiti, amezungumzia kivuko cha Msangamkuu, amezungumza mambo mengi; amezungumza juu ya utaratibu kwenye mizani na mengine mengi. Nataka kukueleza Mheshimiwa Njwayo, ushauri wako tumeuzingatia, tutaufanyia kazi na bahati nzuri majibu yote yako hapa na baadaye tutayagawa kwa Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Malocha amepongeza Wizara, anazungumzia juu ya barabara za vijijini; amezungumzia Halmashauri zipewe fedha. Katika bajeti ya mwaka huu Mfuko wa Barabara utakusanya bilioni 504. *Percentage* fulani zitakwenda *TANROADS,* zote zilizobaki zitakwenda Halmashauri za Wilaya. Wito wangu kwenye Halmashauri za Wilaya, wazitumie fedha hizi vizuri. Kwa sababu tatizo tunalolipata kwenye Halmashauri nyingi za

Wilaya, fedha hizi hazitumiki kwenye miradi ya barabara kama Sheria inavyozungumza. Kwa hiyo, wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tujitahidi sana kuwabana kwenye Halmashauri zetu ili fedha hizi zitumike kulingana na matarajio na miradi iliyopangwa kwa ajili ya barabara.

Mfuko wa Barabara chini ya Mheshimiwa Dkt. Wanyancha umejitahidi sana kukusanya fedha. Lakini kama fedha hizi zitakuwa zinakusanywa na zinapelekwa kule kwenye Halmashauri zinaliwa, hakuna kazi zitakazofanyika. Tuzisimamie ili barabara zinazotengenezwa katika vijiji zinazopitia kwenye Halmashauri ziweze kuleta *impact* kwenye maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia fidia ya wananchi, inakuaje alama ya ‘X’ imewekwa, wanaambiwa wasiendeleze? Ile alama ya ‘X’ kwa mfano ile ya kijani ni kumtahadharisha tu kwamba asije akapata hasara yule mtu. Lakini wale wote ambao wako nje ya mita 22.5, hata kama atakuwa amewekewa ‘X’ kule, maana yake atakuja kulipwa fidia wakati barabara itakapokuwa inaendelezwa kwa sababu Sheria ya mwaka 2007 iliwakuta. Lakini wale walio ndani ya mita 22.5 maana yake Sheria ya mwaka 1932 wao ndio wameikuta. Kwa hiyo, wao lazima waondoke bila kulipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mhita amezungumzia barabara ya Dodoma - Babati ambayo pia inamhusisha mwanafunzi wangu Mheshimiwa Nkamia. Ile barabara imetengewa Shilingi bilioni 56. Ile *section* ya kutoka Mayamaya kwenda Bonga kilomita 188.8 ina fedha zote na fedha zile tumeshatangaza *tender* na zinatolewa chini ya ufadhili wa *African Development Bank*. Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mhita usiikatalie Shilingi, ukizuia Shilingi, maana yake umewanyima watu wako barabara hiyo. Ukitoa yangu, mimi nitapata mshahara wa Ubunge, kwa sababu mimi ni Mbunge wa Chato. Kwa hiyo, irudishe hiyo hela, ili fedha za *African Development Bank,* Shilingi bilioni 56 zikatengeneze ile barabara.

Ninakuomba dada yangu Mheshimiwa Mhita, fedha zile zirudi ili zikatengeneze barabara ile, tumeshaanza kwa fedha zetu za ndani kuanzia Babati hadi Bonga kilomita 19.2 na tumeanza kwa upande wa Dodoma hadi Mayamaya kilomita 43. *African Development Bank* wametoa fedha hizo. *Tender* tumeshatangaza. Kwa mwaka huu Makandarasi wataanza kufanya kazi baada ya kupata *no objection* ya *African Development Bank*.

Ninafahamu *concern* yako kwamba barabara ile imezungumzwa siku nyingi, sasa imefika wakati wake wa kujengwa kwa sababu hata lami imeshaanza kuonekana, unagusa huku lami na mwishoni unagusa lami. Sasa utagusa yote lami. Katika lami hii itatengeneza pamoja na hilo daraja kubwa kwa sababu tuliona tuweke kwenye *compact* ya fedha hizi nyingi za wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiwia ananishukuru, nami nakushukuru sana. Unajua kushukuriwa na Mbunge wa CHADEMA ni safi. Lakini amezungumza kuhusu kupandisha hadhi ya barabara. Tumepandisha ile barabara ya kutoka Nyakato, ile nyingine ya kutoka Saba Saba tunawaachia Halmashauri nao watengeneze, na bahati nzuri mna Mheshimiwa Meya mzuri sana wa CHADEMA, Mheshimiwa Matata. Ni kweli mna Mheshimiwa Meya mzuri sana wa CHADEMA anaitwa Mheshimiwa Matata. Ninachoomba tu Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza mshirikiane naye katika kutatua kero za wananchi wa Ilemela. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mbona CHADEMA wanacheka kuhusu Meya wa CHADEMA? Kuna nini? Endelea Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Henry Shekifu ametoa pongezi, amezungumzia fedha za maendeleo, amezungumzia barabara ya Amani - Muheza, amezungumzia barabara ya Tanga - Horohoro, ametoa pongezi kwa Meneja *TANROADS* amezungumzia mambo mengi; amezungumzia barabara ya Lushoto -

Magamba zimejengwa kilomita tatu tu za lami, anaomba angalau ziongezeke.

Mheshimiwa Shekifu tutaliangalia hili ili angalau ikiwezekana tuweze kuanza kumalizia kilomita tatu, tano zaidi. Lakini umezungumzia juu ya barabara ya Same - Korogwe kwamba mkandarasi aendelee, umezungumzia juu ya *TBA*, umetoa masuala ya mizani, umezungumzia juu ya hifadhi ya barabara na matuta ya barabarani. Mheshimiwa Shekifu ushauri wako wote tumeuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Nassari amesema kuliko kutenga miradi kumi ni vyema tukatenga miradi miwili tu. Halafu hapo hapo ananiomba barabara ya kwenda Nelson Mandela. Si ndiyo hiyo hiyo nimeiacha kwa sababu unataka nitenge miradi miwili badala ya kumi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo najua Mheshimiwa Nassari alitaka kuelezea *concern* yake kwa barabara hii. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshaanza kuitengeneza hii barabara. Huku mwanzoni imeshaanza kuwekwa lami, kwenye ile *section* iliyokuwa imebaki ya kwenda mpaka Nelson Mandela, Chuo pekee katika Tanzania ambacho kimeanzishwa na Serikali ya CCM na wakati wa ufunguzi Mheshimiwa Rais alitoa maagizo katika bajeti ya mwaka huu na bahati nzuri Mheshimiwa Nassari akisoma vizuri, akasome kasma namba 4132, zimetengwa Shilingi milioni 70 za kufanya *design*, ili *design* ikishamalizika, basi barabara ile ianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, usinichonganishe na Mheshimiwa Rais kwamba tumwamini nani; Mheshimiwa Rais au Mheshimiwa Waziri? Mwamini Mheshimiwa Rais na ndiyo maana tumetenga Shilingi milioni 70 kupitia kasma namba 4132 na ile barabara inajengwa. Lakini pia tutajenga barabara za Arusha - Sakina kwa njia nne. Nami nampongeza Mheshimiwa Mrema hata hakusema kitu kwa sababu amepongeza kimoyomoyo, anajua kazi nzuri zinazofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makani ametoa maelezo mazuri sana na *definition* ya bajeti. Lakini akatoa elimu nzuri sana ya namna Wakandarasi wanavyopatikana katika nchi hii. Zinapotangazwa *tender* na bahati nzuri Mheshimiwa Makani ni *Engineer*; zinapotangazwa *tender,* huwa ni *International Tendering*. Kwa hiyo, Mkandarasi anapo-*apply,* anapofanyiwa *evaluation* kupitia *TANROAD* na vyombo vingine ni lazima apate *no objection* ya *African Development Bank* kwa mradi huu.

Kwa hiyo, kama amefeli ni kitu cha kawaida Makandarasi kufukuzwa kwenye *site* kwa sababu ame-*default* mkataba, na ndicho tunachofanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Makani nakupongeza kwa kutoa maelezo haya mazuri, na kwa sasa hivi tunafanya juhudi nzuri za kuhakikisha barabara hiyo yote kutoka Masasi hadi Tunduru ikakutane na ile ya kwenda Songea, yote itengenezwe kwa kiwango cha lami mpaka Mtambaswala. Ndiyo maana kuna Shilingi bilioni 138 zimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo yote kwa kujengwa kwa kiwango cha lami na zimeshatangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makini amenisaidia pia kuhusu majengo na bahati nzuri na wewe Mheshimiwa Naibu Spika ulinisaidia. Unajua watu wakikosa neno la kukutafuta wanakubandika lolote. Ninafahamu hakuna Mbunge yeyote hapa ambaye ameshakwenda kuomba kibali cha ujenzi wa nyumba *TANROADS* au Wizara ya Ujenzi. Michoro yote inapitishwa na Halmashauri zilizopo. Bahati nzuri katika Halmashauri zetu na Manispaa zote kuna Kamati za Ujenzi, na katika kila Halmashauri ina ma-injinia, ina Maofisa Ardhi, ina Ma-*planer* na wale wote hawako chini ya Wizara ya Ujenzi. Lakini nalo lilikuwa linapindishwa, linaletwa kwa Mheshimiwa Magufuli. Bahati nzuri hili liko Mahakamani, sitaki nizungumzie zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Maige amezungumza, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza na sasa hivi nimeshapigiwa kengele. Ninachotaka kusema, michango ya Waheshimiwa Wabunge

wote ni mizuri. Ni vigumu sana kwenda kwenye michango yote ya Wabunge 50 ambayo imezungumzwa hapa.

Hata ya Mheshimiwa Keissy nayo nimeipokea. Lakini kwa taarifa ya Mheshimiwa Keissy barabara zake zimetengewa zaidi ya Shilingi bilioni 52. Ninamshauri akasome kwa mfano daraja la Mumba, barabara ya Tabora – Ipole - Mpanda Shilingi bilioni mbili, Sumbawanga – Matai – Kasanga, Sumbawanga – Mpanda, Sumbawanga – Kanazi, Kanazi – Kizi, Kizi –Starike, Mpanda – Mishamo, barabara zote hizi fedha zimetengwa. Anaweza akaangalia kwenye kitabu changu yote haya. Sasa asipounga mkono, maana yake anawakosesha watu kule watani zangu wafipa barabara hizi. Kwa hiyo nakuomba rafiki yangu Mheshimiwa Keissy. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa ujumla michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa mizuri sana. Kama nilivyotangulia kusema, michango ya Waheshimiwa Wabunge wa pande zote wa upinzani na wa CCM wametoa mawazo mazuri sana. Ni vigumu sana kujibu kila hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Waziri, angalau ungegusa barabara za Tabora na barabara ya Kongwa. Maeneo haya mawili hatujayasikia vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Barabara za wapi Mheshimiwa!

**NAIBU SPIKA:** Barabara za Tabora kwa watani zangu kule na barabara ya Kongwa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rage na Waheshimiwa Wabunge wa Tabora wamezungumza kuhusu barabara zinazowahusu. Kwa bahati nzuri barabara hizi zote zimeshawekewa jiwe la msingi na *cost* ya miradi yote hii inayotekelezwa kutoka Nzega – Ndono – Tabora – Urambo hadi Kaliua na kutoka Tabora – Chaya, fedha hizi zote zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu na kuna zaidi ya Shilingi bilioni 55.

Nataka kuwahakikishia wananchi wa Tabora na Wabunge wa Tabora, barabara hizi zitakamilika. Ni kwa bahati mbaya mwanzo, wakati wa *mobilization* Wakandarasi walichelewa kuanza. Sasa hivi fedha za *advanced payment* zote wameshalipwa na kila *certificate* wanazoleta wanalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Makandarasi waache kuweka kisingizio kwamba wanaidai Serikali kwa kusimama kwao. Kwa sababu mikataba waliyosaini haiko hivyo. Mkandarasi yeyote akichelewesha kazi anakatwa *liquidation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme ukweli pia kwamba katika kipindi cha miezi miwili mitatu kwa sababu ya mvua zilizokuwa zinanyesha, na kwa miradi mingi iliyokuwa inaendelea katika Mkoa wa Tabora na hasa kuanzia pale Tabora - Ndono hadi Urambo ambapo kazi zote za madaraja zilikuwa zimeshamalizika, kazi ya *sub base* ilikuwa imemalizika, *base* ilikuwa imemalizika, Mkandarasi alikuwa anajiandaa kufanya *stabilization*, kuchanganya lami pamoja na changarawe kusudi aanze kazi. Mvua zikaanza kunyesha, ilibidi asimame ili kusudi asipoteze lami hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia wananchi wa Tabora, barabara hizi zitatengenezwa na zitakamilika. Hata barabara ya kutoka Chaya hadi Nyaua kilomita 90 nayo tumeiwekea Shilingi bilioni 2.2 ili nayo itangazwe *tender* kwa ajili ya kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwathibitishia kwamba barabara hizi zitakamilika na ndiyo maana tulimleta Mheshimiwa Rais kuja kuweka jiwe la msingi. Bahati nzuri barabara zote zile hazitegemei wafadhili. Fedha zote zinatolewa na Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutoa maamuzi makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maamuzi makini, wengi tumezoea kusema maamuzi magumu, maamuzi magumu hata vibaka wanafanya, ni maamuzi makini ya kuhakikisha kuwa barabara za Tabora zinajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Maeneo mengine kama nilivyo...

**WABUNGE FULANI:** Kongwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Kongwa *design* tumekwishaanza kuifanya kwa kilomita zote, tunataka tumalize *design* ile na baadaye tukishamaliza kufanya *design* tutajenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda ni mfupi, lakini napenda niahidi wakati wa *clarification* kama watakuwepo Wabunge wanaouliza kuhusu maeneo yao nitakuwa radhi kutoa maelezo kikamilifu, lakini kama unaniruhusu kwa Kanuni zako niongeze hata nyingine niendelee mimi...

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana na muda hautoshi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Niendelee.

**MWENYEKITI:** Inatosha hapo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Niseme?

**MWENYEKITI:** Toa hoja Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu mfupi niliopewa, wakati mambo ni mengi sana, ambapo nafikiri nimeonewa kwa sababu ningepewa hata masaa mawili nitoe *clarification* vizuri, ili Waheshimiwa Wabunge wapitishe hoja yangu yote bila kupingwa. Kwa sababu wengi wanaikubali na kwa sababu kila mmoja anahitaji barabara na hasa kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweka trilioni 1.27 kwa ajili ya ujenzi wa

barabara hizi, ili maendeleo ya kweli ya kilomita 11,154 yakapatikane katika nchi hii, ili barabara za Tanzania ziweze kuwa *connected*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote, bila kujali Vyama vyao, bila kujali itikadi zao, waweke mbele maslahi ya Taifa, waipitishe bajeti hii ili kusudi Wahandisi hao waende wakafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Magufuli, Waziri wa Ujenzi. Tunakushukuru kwa hotuba nzuri na ufafanuzi mkubwa, Waheshimiwa Wabunge ni kweli kuwa Mheshimiwa Magufuli ni jembe. *(Makofi)*

Tuendelee, Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 98- Wizara ya Ujenzi**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resource Management*... ... Sh. 2,317,928,500/=

**MWENYEKITI:** Nawaona Waheshimiwa mmesimama; Mheshimiwa Murji, Mheshimiwa Profesa Msolla, Mheshimiwa Kikwembe, Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Kirigini tayari, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Bulaya tayari, Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Mfutakamba tayari, Mheshimiwa Blandes tayari, Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa tayari, Mheshimiwa Njwayo na Mheshimiwa Kayombo.

Pia Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Rage, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Buyogela, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Mdee, Mheshimiwa Mbassa, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Kebwe, Mheshimiwa Mhita, Mheshimiwa Machemli, Mheshimiwa Kiwia, Mheshimiwa Parreso, Mheshimiwa Sanya, Mheshimiwa Moza, Mheshimiwa Rajab Mbarouk, Mheshimiwa Mipata.

Sasa nawaomba Waheshimiwa, mtakapopata nafasi tujitahidi, kama mlivyoona ili wengi mpate nafasi nawaomba muwe wajamaa kwa kwenda moja kwa moja kwenye suala linalohusika Mheshimiwa Mkosamali tufungulie.

**MHE. FELIX. F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza juu ya barabara za Kigoma hasa Kibondo ambazo zilitengewa fedha mwaka jana zimefikia wapi, barabara ya Kibondo – Mabamba, lakini ujenzi tuthibitishiwe kama barabara ya Nyakanazi mpaka Kidahwe itaanza mwaka huu, kwa sababu imekuwa ikitengewa fedha kidogo kidogo na mwaka huu angalau imeongezeka, je, itaanza kweli? Ni hilo tu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu, Kanuni ya 101(3) Mbunge atakayeamua kutumia kifungu cha mshahara wa Waziri ataruhusiwa iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahususi la Sera na hatazungumza zaidi ya jambo moja. Naomba Kanuni hiyo ifuatwe.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mwanasheria wa Serikali na hilo linatusaidia Wabunge wote, Mheshimiwa Kikwembe!

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali kupitia Wizara hii imekuwa inatekeleza miradi mingi ya maendeleo hasa barabara ambayo hailingani na bajeti inayotolewa na miradi mingi imekuwa inachelewa na kuliongezea Taifa hasara. Miradi

mingine imekuwa ikipata fedha kidogo kidogo, kiasi cha kufanya miradi hiyo kuchukua muda mrefu na hivyo kuongeza adha kwa wananchi. Je, Serikali kupitia Wizara hii inasema nini katika miradi hiyo kwa namna ya kuweza kuitafutia pesa ili iweze kumalizika kwa haraka na kuondoa adha kwa wananchi ili kupunguza umaskini na kuleta maendeleo?

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Pudensiana kwa swali la mfano na wengine wataiga, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kikwembe kama ifuatavyo:-

Fedha zinazopangwa kwa ajili ya Wizara hii zinatutosha, kwa hiyo siyo kidogo na zimepangwa kwa ajili ya kazi zilizofanyika na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka jana zilitengwa bilioni 670 za maendeleo na mwaka huu ni bilioni mia nane themanini na kitu. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Kikwembe apitishe zinatosha.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kidogo na wala sina matatizo makubwa sana na Mheshimiwa Waziri isipokuwa nataka *clarification* tu. Unajua hawa watu wanaovunjiwa nyumba, wapo wa aina mbili; kuna watu ambao wanamiliki kiwanja, wamepata vibali vya kutengeneza *plan* za kujenga nyumba zao na wengine si hasha wana vibali kutoka katika Mamlaka husika hata Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Sheria kama alivyozitaja Mheshimiwa Waziri zimeanza zamani sana hata wengine hatujazaliwa wakati 1939/1949 mpaka zikamalizika 1957 zikaja mpaka 2007. Sasa Serikali inasemaje juu ya wale ambao wana vibali, wana hati miliki za ardhi zao na wakavunjiwa kutokana na zile barabara kupita maeneo haya? Serikali inasemaje wanaweza kupata fidia kwa namna gani angalau kwa watu wa namna hii ili kuwafikiria kutokana na hali ya maisha ilivyo na ujenzi ulivyokuwa ghali. Ahsante sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *concern* ya Mheshimiwa Sanya, lakini nataka kumjulisha kwamba, Sheria ya Ardhi Namba 4 na Namba 5 ya mwaka 1999 inatambua hifadhi ya barabara. Pia Sheria ya Mipango Miji Namba 7 na Sheria ya Matumizi ya Ardhi Namba 6 na Sheria nyingine Namba 8 ya mwaka 2007, nazo zote zinatambua hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria hizi zote zimeunganishwa pamoja na Sheria namba 13 ya mwaka 2007 na *regulations* zake. Mtu anapokwenda kujenga kwenye *road reserve* aidha, kwa kutapeliwa kwa sababu matapeli nao wapo na katika nchi hii unaweza kujenga mahali popote hata baharini na ndiyo maana mnaona hata viwanja vya wazi vinavamiwa na mtu unamkuta ana hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kusema ni kuwa, Sheria lazima ichukue Msalaba wake na *ignorance of law is no defense,* kwa hiyo, mtu ukiifuata barabara, umefuata umasikini. Ni vyema usiifuate barabara kwa sababu Tanzania ina maeneo mkubwa sana, ina kilomita za mraba 994,000 ambapo mtu unaweza kujenga mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Sheria hii haifungi yule ambaye anafikiri ameonewa, ana haki ya kwenda Mahakamani na *TANROADS* na Wizara zimekuwa zikipelekwa Mahakamani na Mahakama ndiyo wenye kujua namna ya kutafsiri Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huo ndiyo wito wangu lakini mimi kama msimamizi wa *road reserve* na kama msimamizi wa Sheria, tunawashauri watu wasijenge kwenye *road reserve,* lakini barabara ikimfuata ni lazima alipwe fidia kwa mujibu wa Sheria za ardhi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchukuaji, ulipaji wa madeni na uanzishwaji wa miradi ni suala la Kisera katika ngazi ya Wizara. Katika taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni, tulinukuu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa hesabu za Serikali ambayo inaonesha kwamba, Wizara imeshindwa kumthibitishia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 252.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maneno hayakuwa maneno ya Mheshimiwa Arfi yalikuwa ni maneno ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema: "Taarifa kutoka Wizara ya Fedha zimedhihirisha kuwepo kwa mradi wa ujenzi maalumu wa barabara hewa" siyo mimi ni *CAG* anasema barabara hewa, katika hesabu za Wizara ya Ujenzi mradi ambao ulipewa namba ya utambulisho kodi namba 4168 ambao pia ni hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anasema kuwa shilingi bilioni 152 hazikuwa na nyaraka yoyote na anasema fedha yote bilioni 252 haikwenda kulipa madeni kama namna ambavyo Waziri anasema. Tunataka Waziri atuambie fedha yetu hii imekwenda wapi? Hatuwezi kuja hapa tunasifia tu na naomba nitoe taarifa rasmi kuwa tumekuwa tukijaribu kuwa waungwana, ku-*appreciate* pale ambapo jambo limeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia leo natoa amri kwa Mbunge yoyote wa CHADEMA, mfanye jema lolote hakuna ku- *appreciate* kwa sababu mna *misuse appreciation* zetu na hii ndiyo amri Wabunge wa CHADEMA, hakuna ku-*appreciate* chochote kwa sababu mna *misuse appreciation* ambazo tunawapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utupe maelezo ya bilioni 252 ambao mliliambia Bunge hapa ni za kulipa madeni, *CAG* anasema hakuna madeni yaliyolipwa na amekagua naomba mtupe maelezo hapa hizi hela zimekwenda wapi au zimetumika namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika nitatoa shilingi mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, hiyo ni Sera kweli?

Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo:-

Kwanza nampongeza hiyo amri aliyoitoa kwa watu wake wa CHADEMA wasiwe wana- *appreciate,* hiyo ni ya upande wao, lakini katika kasma namba 4168 ambayo kwa bahati nzuri katika bajeti ya mwaka 2011/2012, kilitengewa fedha milioni mia mbili hamsini na kitu kwa ajili ya kulipia madeni, fedha zile zililipa madeni. Ndiyo maana katika bajeti yetu mwaka jana tulipokuwa tukitoa taarifa kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013, tulitoa taarifa hiyo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu, kifungu hicho hakikuwekwa kwa sababu fedha zilizotengwa kwenye bajeti hii zimeongezwa na zikagawanywa kwenye miradi kuliko kama ilivyokuwa mwaka juzi kwenye bajeti ile ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Zitto kwamba, fedha hizo zililipa madeni ya Makandarasi. Pia nataka nimweleze Mheshimiwa Zitto, katika ulipaji mzuri wa Makandarasi, Makandarasi waliweza ku-*produce* zaidi kuliko hata ilivyokuwa inategemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana zilitengwa bilioni 296.7 na kufikia Machi tarehe 30, 100% ya fedha za *development* zilikuwa zimetolewa na Makandarasi bado wanaendelea kufanya kazi hata leo na *certificate* bado zinaendelea kuwa *produced*. Ndiyo maana nilivyokuwa nikitoa taarifa, bahati mbaya labda Mheshimiwa Zitto alikuwa hajafika, leo Waziri wa Fedha ametoa fedha zingine bilioni 167 kwa ajili ya kulipa Makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimweleze Mheshimiwa Zitto aendelee ku- *appreciate* kupongeza Chama cha Mapinduzi kama alivyopongeza alipokuwa anapita kwenye daraja la Kikwete kwamba, Serikali ya

Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imefanya kazi vizuri, kwa hiyo, awashauri na wenzake wapongeze kama anavyopongeza yeye.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kisera na utaratibu, ni vizuri maeneo yale zinapopita barabara za lami Miji husika pale jirani angalau wanapata kiwango fulani cha lami. Katika kitabu hiki kimetaja tu Miji, lakini hakikutoa ufafanuzi kama kutakuwa na lami kiasi gani? Mfano mdogo, ni barabara ya Serengeti ule Mji wa Mugumu hatujui ni lami kiasi gani itawekwa. Naomba ufafanuzi, mimi sina shida na mshahara kwa sababu nikikamata mshahara barabara haitajengwa. Naomba ufafanuzi wa suala hili.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kebwe kwa kazi nzuri anayofanya katika kulitumikia Taifa hili na kwenye Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Makutano – Butiama – Nyamswa – Nata – Mugumu - Loliondo hadi Mto wa Mbu ilishamalizwa kufanyiwa *feasibility study* na ilishamalizwa kufanyiwa *detail design* kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanyika sasa hivi ni kuanza kujenga kwa vipande vipande na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, tumeweka fedha na tenda zimeshatangazwa na kandarasi zimeshasainiwa za barabara ya kilomita 50 kutoka Makutano – Butiama - Nyamswa hadi Nata kilomita 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo tutajenga tena kuelekea Mugumu mpaka Serengeti, lakini pia zimetengwa fedha zingine kwa upande ule mwingine wa kutoka Mto wa Mbu hadi Loliondo, nako zijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu itakayobakia ni ile ya kilomita 53 inayopita kwenye Hifadhi katika kulinda mazingira. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kebwe kuwa barabara hiyo iko kwenye program na tunaianza mwaka huu kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Barabara imeundwa kwa sheria ambayo ilipitishwa hapa Bungeni. Moja ya changamoto ya Bodi ya Mfuko wa Barabara ambayo waliieleza mbele ya Kamati ya Miundombinu mwaka juzi, ni suala zima la kukosa zaidi ya bilioni 26 kutokana na tozo kutoka katika makampuni ambayo yanachimba madini hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua kwa sababu mwaka jana nililiongelea suala hili na nikaomba majibu, lakini sikupata. Leo nimeliongelea, nimeomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri, sikupata. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi ni hatua gani amezichukua ili kuondoa changamoto hii inayoukabili Mfuko wa Barabara hapa nchini. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa chini ya *amendment Act* Na. 2 ya mwaka 1998 na mabadiliko yake ya mwaka 2006 na yalipitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge alete hoja binafsi ili kusudi Makampuni ya Madini nayo yaanze kuchangia kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningefurahi sana Mfuko wa Barabara, hata kama zinakusanywa bilioni elfu moja au zaidi ili kusudi nyingi ziende kwenye barabara. Lakini hili analolizungumza la mimi kwenda kuwadai au Bodi ya Barabara iende ikawadai makampuni wakati sheria haizungumzi hivyo, ni vema sheria ikafanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningemshauri Mbunge kwa sababu mawazo yale ni mazuri na ningependa

Mfuko wa Barabara unaoongozwa na Mheshimiwa James Wanyancha ukusanye fedha nyingi. Tukusanye kwenye madini na kwingineko ili fedha zipatikane nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu yeye ni Mbunge, ana mamlaka pia ya kuweka na kuleta mabadiliko humu Bungeni, alete ili kusudi yaweze kujadiliwa na Bunge na Bunge liamue ili lifanye mabadiliko kwenye Sheria ya mwaka 2006 iliyopitishwa hapa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nijue nini sheria ya *diversion*, naomba Waziri atuambie hususani kwenye zile barabara ambazo zipo kwenye *trunk road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi nikitolea mfano katika ile barabara ya Uyole hadi Mbalizi mpaka kule Songwe. Naomba ufafanuzi na nashukuru.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia Mheshimiwa Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, Serikali ina sheria gani katika suala zima la *diversion* hususani zile barabara ambazo ni *trunk road*. Nikichukulia mfano katika barabara ile ya Uyole hadi Songwe, kwa sababu hili jambo nimekuwa nikilipigia sana kelele mpaka kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nimelizungumzia sana na tumezungumzia kwenye *Road Board* bila mafanikio. Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Kwamba *diversion* zimefanyaje?

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Barabara, naomba Waziri atupe ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Barabara iko *clear,* imetoa *classification*, kuna *trunk roads*, kuna *Region roads*, kuna *District roads* na sheria hizi zote zinasimamiwa chini ya Sheria Na. 13 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, diversion *normally* huwa zinatokea kwenye barabara zinapotengenezwa. Barabara inapokuwa chini ya *construction* ndipo panakuwa na *diversion*. Inawezekana labda Mheshimiwa Mwanjelwa anataka tutengeneze *diversion* kwenye Mji wa Mbeya ambapo *congestion* imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo suala tunalipitia na tunalijadili kuangalia ni namna gani tunaweza tukapata *altenative route* ambayo itakuwa inapunguza msongamano katika Mji wa Mbeya na Mji wa Iringa baada ya barabara hii kukamilika, pia katika Mji wa Dodoma kama ambayo tumekuwa tukitengeneza *By Pass* katika sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mwanza ambapo sasa hivi inatengenezwa barabara ya *By Pass* ya kutoka Usagara kwenda Kisesa ya kilomita 17 ili magari yanayotoka Rwanda na Burundi yasipite Mjini Mwanza. Ni kama ambavyo pia tunatengeneza *diversion* nyingine ya kutoka Mwigumbi kwenda Lamadi kupitia Bariadi ya kilomita mia moja ili kusudi magari yanayokwenda Musoma yasipite Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajitahidi katika njia hiyo katika kupunguza *diversion* katika Miji yetu. Kama vile tunavyofanya Dar es Salaam na kama vile vile tunavyofanya *By Pass* kwenye Mji wa Arusha ambapo tunatengeneza *diversion* kwa barabara ya kutoka Nairobi kuja kuunganisha na hii barabara ya kwenda Minjingu, tumeongeza *diversion* ya kilomita saba.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani kupitia kwa Msemaji wake Mheshimiwa Arfi, ilihoji kuhusu usimamizi wa mikataba unaofanywa na *TANROADS* na Kambi Rasmi ilitumia ripoti ya chombo cha Serikali yenyewe, Mamlaka ya Ununuzi wa Umma ambayo ripoti hii ilisema kwamba *TANROADS* kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa upande wa kipengele cha kusimamia ubora kwa maana ya *compliance level and quality control* ilipewa alama 45 tu kati ya alama mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kipengele cha kuzingatia mikataba kwa maana ya *compliance and contract management* ilipewa alama sifuri na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma ambacho ni chombo cha Serikali. Hakikupata ushahidi wowote kwamba *TANROADS* ilisimamia mikataba ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana, Waziri katika kujibu hoja hii ya msingi sana ambayo ina-*deal* na ubovu wa mikataba, kuzuia mianya ya ufisadi kwenye ujenzi wa barabara, ameigeuza kuwa ni hoja ya Arfi, ameigeuza kwamba ni maneno ya kuokoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri kwamba, kwa hali hii mbaya ya ripoti ya Serikali yenyewe kuhusiana na *TANROADS* yupo tayari sasa kuchukua hatua za kisera za kurekebisha hali hii na kufuta maneno ya mwanzo ya kupindisha na kutumia takwimu nyingine zisizohusika katika kujibu hoja ya msingi kama hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapojibu hoja, ukiulizwa juu ya shati huwezi ukasahau kuzungumza kuhusu fulana. Kwa hiyo, alipozungumzia hii pointi, niliona nimpe kitu ambacho ni *so broad*, kwamba katika nchi zingine *TANROADS* wanaionaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *give me time please!* Ninachotaka kueleza ni kwamba, *TANROADS* ni chombo cha Serikali kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 30 ya mwaka 1997, kina-*perform* kazi nzuri, hata Wapinzani wanaelewa. Hata Mheshimiwa Mnyika anaelewa na ndiyo maana tumetangaza barabara ya kwenda Malamba Mawili, kila mmoja anafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *issue* iliyozungumzwa hapa, ilikuwa ni *issue* ambayo inahusiana na *issue* ndogo...

*(Hapa Mheshimiwa John Mnyika alikuwa anamrushia maneno Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akionesha kutokubaliana na hoja yake)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Nisikilize basi nikueleze, mbona hamnipi *time?*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana na hili huwa mara nyingi sana nalisema, Bunge ili liwe Bunge ni lazima tuwe na *culture* ya kusikilizana, kwamba Mbunge anapoongea anasikilizwa na majibu yanapotoka kuna kusikilizana. Lakini kama ni kuzomeana au kurushiana maneno haliwezi kuwa Bunge hata siku moja. Ni ngumu sana, vinginevyo kazi tunayoifanya wala haina mantiki.

Kumbukeni wapo walio wengi hapa wakiwa na tabia hizo hizo hatutasikilizana hata kidogo. Kwa hiyo, nawaomba sana tuvumiliane, tusikilizane, yatasemwa mambo ambayo yatakufurahisha utafurahi, yatasemwa baadhi ya mambo ambayo labda barabara yako labda haikupangiwa fedha au kadhalika, unaweza usifurahi, lakini tusikilizane.

Hilo ndilo jambo la msingi na nina majina mengi sana ambayo mmeomba kusema hapa. Kwa kuvutana namna hii wengine hamtapata nafasi ya kuzungumza. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa lilikuwa la kuajiri mtu aliyechukua *Material Management* katika masuala ya *procurement*. Bahati nzuri *TANROAD* wameshalitolea maelezo hata Dkt. Milinga mwenye ni Injinia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masuala haya yametolewa maelezo na nina uhakika *PPRA* baadaye watakuja kutoa majibu. Lakini *in general,* tusije tuka-*generalize* kwa vitu vidogo vidogo, tuka-*assess* vibaya, tuka-*discourage* chombo kizuri kama *TANROAD* ambacho kina heshima za Kimataifa.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni la kisera. Katika hoja nyingi ambazo Wabunge wameziulizia zaidi ilikuwa ni ucheleweshaji wa

miradi mingi hasa ya barabara. Waziri wakati akijibu alieleza kuwa Serikali inatoa pesa, lakini kwa sehemu kubwa Makandarasi ndiyo ambao wanachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekiri mwenyewe kwamba, hata hii barabara ya Dodoma Babati ni kweli imecheleweshwa. Je, sasa Waziri anatuambia nini kuhusu hao Makandarasi ambao wanapata pesa, lakini wanachelewesha miradi hii na tukizingatia barabara yetu hii ambayo umekiri ya Dodoma - Babati. Lakini shilingi imesharudishwa, naamini wananchi watakuwa wameridhika kwa majibu yako Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi inayotengeneza miradi ya kilomita 11,154 na inayofanya miradi mingine ya *design* na *feasibility study* katika nchi nzima, ni lazima pawepo na matatizo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi ambayo imekuwa ikichelewa na hatua tumekuwa tukichukua na katika maelezo yangu nimeeleza kwamba, kwa miradi yote inayochelewa, huwa tunaangalia mkataba unazungumza nini na kwa Kandarasi anayechelewesha miradi huwa anakatwa *liquidation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano kwa Mkandarasi aliyejenga daraja la Mkapa, alichelewa na akakatwa *liquidation* na miradi mingine mingi. Pia kuna miradi mingine ambayo ina sababu za msingi za kuchelewa, tumeeleza katika barabara za Tabora. Makandarasi walikuwa waanze kufanya *stabilization* kwenye barabara zinazotengenezwa, mvua zimenyesha kwa karibu miezi mitatu. Kwa hiyo, Kandarasi huyo kwa vyovyote atakuwa amechelewa miezi mitatu. *Consultant* yupo kule, ameshatuletea ripoti, maana yake ni lazima aongezwe hiyo miezi mitatu ya kufidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengine ambayo yanajitokeza katika miradi, Kandarasi anakuwa anajenga panatokea tatizo lingine. Kuna matatizo ambayo

ni *very many*, mengine ni ya *design*, mengine ni ya kufeli kwa maeneo yanayohusika. Kwa hiyo panapotokea pale mikataba ina vipengele vingi vya kuchukuliwa na vipengele hivyo vinachukuliwa *seriously*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali, Kandarasi yeyote hawezi akalipwa hela bila ku-*produce certificate*, asipo-*produce certificate* hawezi kulipwa. Kwa hiyo, Kandarasi anapo-*produce certificate* zinafanyiwa *evaluation* kwa ma-*consultant* ambao wapo kule kwa niaba ya *client*, zinaletwa *TANROAD*, zinapelekwa Hazina na fedha zinatolewa, ndiyo zinakwenda kulipwa.

**MWENYEKITI:** Twende Mtwara sasa Mheshimiwa Murji.

**MHE. HUSNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kuniona. Katika uboreshaji wa barabara zinazosimamiwa na *TANROAD* Mijini ambayo ni sera,

**MWENYEKITI:** Weka vizuri *microphone,* husikiki vizuri.

**MHE. HUSNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uboreshaji wa barabara zinazosimamiwa na *TANROAD* mijini, katika mchango wangu wa maandishi nilipeleka ombi maalum kwa Waziri, kutokana na ongezeko la watu wengi na magari mengi ndani ya Manispaa ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna barabara ambayo inaendelea kutengenezwa na *TANROAD* tulipeleka ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri kumwomba *Traffic light* katika eneo ambalo linaitwa Bima, lakini sijapata jibu. Namwomba Waziri katika uendelezaji wa utengenezaji wa barabara hiyo chini ya *TANROAD*. Tunaomba msaada wa *traffic light* pale ili iweze kutusaidia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mtamalizana na Waziri kwa sababu siyo la kisera sana, Mheshimiwa Murji kwa heshima, lakini nina hakika Mheshimiwa Waziri amekusikia. Twende Kagera kwa Mheshimiwa Blandes.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni la kisera. Sera ya Barabara ni kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara zinazounganisha nchi na majirani zetu. Kwa mfano, kule Tarime, ukienda upande wa Kenya unakuta kuna lami, ukienda kule Karagwe, upande wa Uganda unakuta kuna lami. Pia kuna barabara nyingine ambayo Mheshimiwa Waziri anaifahamu ya Nyakahanga, Nyabionza ambayo inaunganisha na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Waziri anieleze katika mifano hii michache niliyoitoa, wana utaratibu gani na mpango gani wa kisera wa barabara hizi kuhakikisha kwamba zinajengwa katika *standard* ili na wenzetu kule wa jirani waache kutukoga. Nashukuru.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Wizara ya Ujenzi na Serikali kwa ujumla ni kuunganisha barabara nyingi kwa kiwango cha lami na nchi jirani. Tumeunganisha Namanga – Arusha kwenda Kenya kwa lami, tumeunganisha Mwanza- Sirari kwenda Kenya kwa lami, tumeunganisha Burundi kwa barabara ya Mwandiga - Manyovu kilomita 60, upande wa Tanzania ni lami, upande wa Burundi hakuna lami. Tumeunganisha na Malawi lami, tumeunganisha na Tunduma lami, tumeunganisha na Mtukura kwenda Uganda kwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hatua tunazozichukua ni kutengeneza pia barabara yake ya kutoka kule Bukoba - Kyaka kupita Bugene kwenda Kasulu ikaunganishe na ile barabara ya kwenda Rwanda na Burundi kwa upande huo. Lakini hata barabara ya kwenda Mulongo nayo inafanyiwa *design* ili kusudi zitengenezwe kwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Blandes kwamba, kazi ya Serikali ni kuziunganisha nchi kwa barabara za lami kama ambavyo tumekuwa tukifanya. Ndiyo maana barabara yake ya kilomita 59.1 inajengwa kwa kiwango cha lami na tunategemea kuiweka jiwe la msingi mwezi wa Saba.

**MWENYEKITI:** Twende Katavi, Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Waziri ametolea sana mfano wa daraja la Mkapa kwamba, Mkandarasi alichelewa wakampiga tozo, lakini ninavyofahamu barabara nyingi haziishi kwa wakati katika nchi hii. Zinapangiwa miezi 36 na wananchi siku hizi ni wajanja wanasoma na kuona kwenye vibao miezi 36, miezi 30, miezi 60 lakini hakuna hata barabara mmoja iliyokwisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri haelezi Serikali inavyopata hasara kwa kupigwa tozo na Makandarasi katika nchi hii, Waziri anaeleza tu mfano daraja la Mkapa. Sasa namwomba Waziri aeleze Serikali imepata hasara kiasi gani kupigwa gharama ya tozo na Wakandarasi kwenye barabara za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano wa barabara ya Rukwa toka mwezi wa Tatu ipo asilimia 28 mpaka sasa, Wachina watapiga tozo. Alikwenda Makamu wa Rais, Mohamed Gharib Bilal akaelezwa na Wakandarasi wa Kichina kwamba, hatupati hela. Sasa wale Wakandarasi walikuwa waongo kumdanganya Makamu wa Rais?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anieleze nchi hii imepata hasara kiasi gani, Wizara yake imetutia hasara kiasi gani kwa kupigwa tozo na Wakandarasi katika nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy swali la kiasi gani haliwezi kuwa la sera, linahitaji muda ili kuleta takwimu halisi ni kiasi gani.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lijalo tuletewe takwimu.

**MWENYEKITI:** Tunakwenda Mkoa wa Mara Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza kabisa mimi ni miongoni mwa watu ambao wapo *proud* na Mheshimiwa Magufuli kwa sababu anafanya kazi na ajue watu ambao wanapenda wachapa kazi watakuwa nyuma yake siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kutenga fedha, nimeona kwenye kitabu chake kuna shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kisolya – Bunda, lakini pia naamini katika mwaka ujao wa fedha, Wizara yake pia itatangaza tenda ya barabara ya Nyamswa-Bunda ambayo ni *lot one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa barabara hizi kumegusa makazi ya watu na huu mradi umefuata makazi ya watu ambayo najua kabisa wananchi walioguswa na mradi huo hawatakuwa na ugomvi na Mheshimiwa Magufuli.

Mheshimiwa Mweyekiti, juzi tu nilikuwa huko nikifunga mashindano yangu ya *Ester Cup,* kuna wazee waliniita ambao wameguswa na huo mradi, kuna *contradiction,* hawajui ni lini watalipwa kwa sababu hata vikao vya kwenda kukaa na wananchi katika masuala mazima ya tathmini hayajafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba 'pilipili mimi namwita pilipili' hebu aniambie wale wananchi watalipwa na mchakato ukoje. Lakini nipo *proud* sana na yeye. Nashukuru.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nipo *proud* sana na Mheshimiwa Bulaya, kwanza kwa kumaliza JKT na kufanikiwa vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mradi ambao tumeutaja wa Nyamswa – Bunda - Kisolya hadi Nansio na mradi mwingine ambao umegusa katika Mkoa wa Mara wa kutoka Makutano - Butiama hadi Nata, kikubwa kitakachofanyika pale ni kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sheria zetu ambazo tumezipitisha katika Bunge hili. Wale wananchi wote watakaofuatwa na mradi ule kabla ya utekelezaji wake, barabara ikiwafuata, yaani barabara ambayo ipo sasa hivi *existing road,* ikiwafuata ni lazima watalipwa fidia kabla ya kubomoa nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wale ambao wapo kwenye *road reserve* na bahati nzuri ndiyo maana tumeanza mahali ambapo kuna migogoro michache, kule Kisolya kwenda Bunda zile kilomita 50 hakuna mtu ambaye yupo kwenye *road reserve*, watu wote wamesha-*clear*. Kwa hiyo, tunaanza kujenga kule, ile sehemu nyingine ambayo itawagusa wananchi ambao wapo kwenye *road reserve* kwa kweli hawatalipwa fidia, lakini wale ambao wapo nje ya *road reserve* na barabara imewafuata lazima tuwalipe fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndio utaratibu wa Sheria na Sheria za nchi hii ni sikivu na tumekuwa tukifanya hivyo kwa barabara inapowafuata wananchi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Bulaya na Waheshimiwa Wabunge wa Mara na wananchi wa Mara kwamba mradi huu ni kwa manufaa ya Watanzania wote. Barabara ikiwafuata watalipwa fidia, lakini na wale walio kwenye *road reserve* kwa kuvunja Sheria hawatalipwa fidia.

**MWENYEKITI:** Sasa twende Tabora, Mheshimiwa Mfutakamba!

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami pia nashukuru kwa bilioni 2.2, zimetolewa kwa ajili ya Jimbo la Igalula. Kisera najua wananchi watapata ajira, sasa pale kwa kilomita *90.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kisera linahusu ile *DARTS* ya Dar es Salaam, nataka kujua kwenye miradi ambayo ni ya *corridor* huwa *multipurpose.* Sasa huu mradi

wa mabasi yanayokwenda kasi utatumia mabasi. Nataka Mheshimiwa Waziri anieleze kisera je, uko uwezekano pia wa kuweka zile reli nyepesi *light rail?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivyo kwa sababu miji mingi mabasi yanakwenda kasi, lakini kunakuwa na zile treni zinakuwa na mabehewa matano au sita, inapeleka sehemu moja ikishafika fika kwa mfano, Jijini Dar es Salaam, baadaye inatumia kichwa kilichokuwa nyuma inakuwa ni injini inakwenda mpaka Mabibo, inakata kona, hizo *ring roads* inakata au kama ni *ring rail,* huo utaratibu upo kisera pia ili kupunguza msongamano wa Dar es Salaam? Nashukuru Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mfutakamba anafahamu, ni *engineer.* Anafahamu kazi yoyote kabla haijaanza kufanywa, kuna *feasibility study*, baada ya *feasibility study* kuna *detail design,* baada ya *detail design* ndipo wanatangaza tenda na Kandarasi anakuwa kwenye *site.* Huu mradi wa *BRT* au wa *DARTS* kabla ya kum-*engage* kandarasi *Strabag* kutoka Ujerumani kwa *cost* ya karibu bilioni 288 pakiwemo na vile vituo ilifanyika *feasibility study* na ikafanyika *detail design* na sasa hivi Mkandarasi yuko kwenye *site.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vigumu Mkandarasi yuko kwenye *site* na ameshafikia kwenye *size* hiyo, unaanza tena kumwambia sasa anza kutengeneza tena mambo mengine.

Ninachojua mimi na *TANROAD* wanachofanya, wanatengeneza barabara kwa ajili ya kupita magari yaendayo kasi. Baada ya kazi hiyo kumalizika kwa sisi *TANROAD* na Wizara tunayoisimamia, uamuzi unaweza ukafanyika hapo baadaye kwamba, badala ya kuweka mabasi yaendayo kasi waweke *taxi* zinazoenda kasi, sina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiamua waweke treni inayokwenda kasi yenye matairi wataweka. Lakini kazi yetu sisi ni kutengeneza barabara kutokana na *feasibility study* kutokana na *detail design* na kutokana na mkataba tuliosaini na *Strabag* wa kutengeneza barabara ya kutoka Kimara hadi Kivukoni na kwenda Morocco yenye kilometa 21. Kuna sehemu ina njia nne na kuna sehemu ina njia sita.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na Sera ya Wizara ya kuunganisha barabara za mikoa na mikoa chini ya usimamizi wa *TANROADS* katika Mkoa husika na kwamba barabara ya Njiapanda Mang'ola hadi makao makuu ya mkoa wa Simiyu, Bariadi iko chini ya *TANROAD*. Je, ni lini Sera hiyo ya Wizara itatekelezwa katika eneo husika?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii muhimu katika kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. Hatua zimeshaanza kwa kufanya *feasibility study* na nafikiri tutaanza kufanya *detail design,* lakini pia tumeanza kutengeneza daraja ambalo lilikuwa ni tatizo kubwa sana katika kuunganisha hiyo barabara, daraja Sibiti na kandarasi yuko kwenye *site.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Mikoa hiyo na Serikali itaendelea kuifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Twende Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbarali haiko Iringa iko Mbeya.

**MWENYEKITI:** Basi ilikuwa zamu ya Iringa, endelea Mheshimiwa Kilufi.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi ni Wizara ambayo imefanya kazi nzuri sana katika nchi hii na Watanzania leo wanafurahia sana kusikia barabara nyingi zinatengenezwa na nyingine ambazo wenyewe ni mashahidi wanashuhudia zimetengenezwa. Lakini katika utekelezaji wa jambo hili, yako maneno ya kitaalam ambayo yamekuwa yakitumika mara nyingi kwamba, kwa wale ambao pengine wanasubiria barabara zao kuna upembuzi yakinifu, upembuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya yamekuwa yakijitokeza. Sasa kwa wale ambao wamesikiliza maneno haya kwa muda mrefu, kidogo wanakuwa wanyonge. Ikiwemo wananchi wa Mbarali kwa barabara ya Rujewa – Madibira - Mafinga. Tangu Mheshimiwa Mjengwa akiwa Mbunge, maneno yalikuwa ni hayo hayo, akaja Mheshimiwa Kilasi mpaka ameondoka, ni hayo hayo na leo wanashuhudia mambo hayo hayo. Kwa kweli wanakuwa wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wanajua kazi inayofanywa na Wizara, sasa pengine Mheshimiwa Waziri angesema maneno haya yatakwisha lini kwa barabara ya Rujewa – Madibira - Mafinga ili nao waweze kusherehekea na wenzao wanapofurahia barabara nyingi ambazo zinatengenezwa.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kilufi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi wa Mbarali wafahamu tu kwamba, tukifanya upembuzi yakinifu, ni hatua mojawapo ambayo ni ya muhimu sana katika kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Barabara ya Madibira - Rujewa mpaka pale Mafinga imeshakamilika *design.* Sasa kwa sababu lazima twende kwa hatua, hatua itakayofuata sasa ni kutafuta fedha ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKKITI:** Iringa, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kujua Serikali imejipanga vipi kuhakikisha ahadi za Mheshimiwa Rais, pamoja na zile ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi zinatekelezwa kabla ya mwaka 2015?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Mheshimiwa Rais zipo na zimeainishwa vizuri na ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa na Serikali yote. Zile barabara ambazo zinahusu Wizara ya Ujenzi kwa maana nyingine yaani *TANROAD* zile za Mikoa pamoja na *Trunk Road* zitatekelezwa na Wizara yangu. Zile zinazohusika na Halmashauri nazo zitatekelezwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge, mtani wangu kwamba, barabara zinazohusika katika Jimbo lake tutazishughulikia na tutaanza na kufanya *design* na baadaye tutazijenga kadri alivyokuwa akitoa mchango wake hapa Bungeni. Sikupata muda tu wa kuweza kumjibu, lakini ningeweza nikamjibu vizuri wakati alipokuwa akichangia na amechangia vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kwamba, Serikali imejipanga vipi kuweka Sheria kali katika kudhibiti ujenzi wa majengo ambayo unaendelea katika maeneo ya miji mbalimbali nchini na hasa kuzingatia kuweka bima kwa ajili ya wajenzi wale ambao mara nyingi wanaathirika, wanapata ulemavu wa viungo na wengine wanapoteza maisha bila kulipwa *compensation* yoyote. Je, katika hili Serikali imejipanga vipi?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la majenzi liko Wizara ya Ardhi na habari nzuri kuna Sheria ya Matumizi ya Ardhi na Sheria ya Mipango Miji na ndiyo maana tulipitisha hapa, nafikiri ni kati ya Sheria Na. 7 au Na. 8 ya Mipango Miji ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ile pameainishwa vizuri, wajibu wa Halmashauri katika kudhibiti ujenzi holela, pameainishwa *Master Plan* ambazo zinatolewa na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jukumu kubwa pia linahusisha Halmashauri zetu, ni namna gani tunaweza tukafanya katika kudhibiti haya mambo. Kazi ya Wizara ya Ujenzi ni kutengeneza miundombinu katika barabara zinazokwenda kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, Sheria ya Ujenzi ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nafikiri Serikali ipo kwenye mchakato wa kuleta Sheria ya *Building Act* ambayo nina uhakika itakapoletwa humu Bungeni, Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mangungu wataichangia ili itengeneze makali zaidi kwa kuweza kudhibiti majengo ambayo yanakwenda hovyo hovyo katika miji yetu.

**MWENYEKITI:** Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimpongeze ndugu yangu Magufuli pamoja na Wizara yake. Lakini vile vile nisisahau kumpongeza Meneja wa *TANROAD,* Mkoa wa Tanga. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua barabara ya kutoka Korogwe, Old Korogwe kwenda Kwashemshi, Bumbuli mpaka Soni imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi. Je, itajengwa lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa atakujibu kwa wakati wake, tulisisitiza suala la Sera. Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kazi nzuri sana zinazofanywa na Wizara hii ya Ujenzi kwa ujumla wake. Napenda tu nipate ufafanuzi kwa sababu barabara nyingi, karibu nchi nzima sasa hivi zina lami ikiwemo Miji ya Dar es Salaam, Mwanza na kadhalika. Lakini kama hatutazingatia magari mazito haya ambayo yanapita katikati ya barabara hizi na yakaingia katikati ya miji yetu ni kwamba lami itatoweka.

Je, sasa Wizara au Serikali inatoa ufafanuzi wa namna gani ambapo tunaweza kunusuru lami hii kwa maana ya kujali sasa barabara zinazochomoza kabla ya kuingia kwenye miji yetu ili lami ibaki salama na watu waweze kupita kwa urahisi kama hivi zinavyotengenezwa *flyover* na mambo mengine. Nitolee mfano tu, barabara ya kutoka Usagara kwenda Kisesa na barabara zingine katika Tanzania hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Watu wanasema maendeleo Tanzania hakuna, mpaka Wasukuma wanajua *flyover* ni nini bwana. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa ujumla imekuwa ikiweka mipango maalum ya kuhakikisha kwamba, barabara kuu hazipiti katikati ya miji yetu. Nikitoa mfano tu na mimi kwenye barabara za Mwanza, ili kuhakikisha kwamba barabara magari yanayotoka nje ya nchi yasipite katikati ya Jiji la Mwanza, tumeshatangaza tenda na tumesaini mkataba wa *by-pass* wa barabara ya kutoka Usagara kwenda Kisesa kilometa 17 na Kandarasi ameshaanza kufanya *mobilization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba magari yasipite katika Jiji la Mwanza. Tunafanya hivyo hivyo pia katika maeneo mengine kama ambavyo nilitoa maelezo wakati nilivyokuwa nikitoa maelezo yangu. Tunafanya *design* kwa barabara ya Dodoma, tunafanya hivyo Arusha, tutafanya hivyo Iringa, tunafanya hivyo Dar es Salaam. Lengo kubwa ni kwamba yale magari makubwa yasiwe yanapita katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivyo Manyoni. Hatukupitisha kwenye mji wa Manyoni, tukahama lakini baadaye tulikohamia kule wananchi wakatufuata, tukaenda kuwabomolea ili kusudi wajue ile ni *Trunk Road* na wakae nje ya *road reserve.*

**MWENYEKITI:** Twende Mkoa wa Ruvuma, Mheshimiwa Kayombo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri, nilizungumzia juu ya kuangalia uwiano wa hizi barabara Mkoa kwa Mkoa. Nashukuru katika Mkoa wa Ruvuma tumepata ile barabara sasa kutoka pale *junction* ya Peramiho kwenda Mbinga na imekamilika vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa yako matatizo ya barabara ambazo zinatakiwa ku-*feed* hii barabara kutoka katika vijiji na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais alipofika aliahidi barabara ya Mbinga – Litembo, Mbinga - Maguu lakini pia kuna mradi wa makaa ya mawe katika Kijiji cha Mtunduwalo kule. Yale mavumbi wanaposafirisha makaa yale yanawaathiri sana wananchi na tulipendekeza ile barabara ijengwe kwa lami. Kwa hiyo, katika uwiano huu Mheshimiwa Waziri anatoa ufafanuzi gani?

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninafahamu *concern* ya Mheshimiwa Kayombo. Lakini napenda kusema kwamba, kupanga ni kuchagua na masuala ni mengi. Ndiyo maana tumeanza na barabara ya kutoka Masasi-Tunduru-Peramiho-Songea-Mbinga hadi Mbamba Bay na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, kutoka Mbinga hadi Songea kuna Kandarasi chini ya mradi wa *MCC* na unaendelea vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Mbinga kwenda Mbamba Bay kilomita zile 64, napo mwaka huu tumeweka

fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami baada ya kumaliza yale madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya hapo tutaangalia tena barabara zingine ambazo zinaweza kuunganisha. Kama ni barabara ya Halmashauri wenzetu wa Halmashauri wanaweza kuziunganisha zile barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kama ziko chini ya Wizara ya Ujenzi tutaendelea kuziungansha kama ambavyo zimepangwa Mkoa kwa Mkoa kulingana na Kiambatanisho Na. 3 hadi 5 ambacho kiko kwenye hotuba yangu.

**MWENYEKITI:** Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nashukuru. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu kuhusiana na suala la *TBA* alisema kwamba, imewaandikia barua na inawatambua wapangaji. Lakini nina nyaraka inayoonesha kwamba Kiwanda cha *Twiga Cement* ambao mkataba ninao wa mauziano mwaka 1997, inaonesha kwamba, kuna eneo ambalo lilibaki Serikalini ambalo linajumuisha na nyumba hizo 226.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Twiga wamei-*task* kampuni ya Majembe ikiwaambia, wakawaondoe wananchi ambao ni wapangaji wa nyumba za *TBA* ambazo baadhi ya nyumba ziko kwenye kiwanja namba moja, nne na saba ambavyo kwa mujibu wa Mkataba hizo nyumba zote ni za Serikali kwa maelezo kwamba wao ni wamiliki wa eneo lote.

Sasa nataka tu kauli kutoka kwa Serikali na nataka kauli kwa kuzingatia kwamba, kuna nyaraka mbalimbali ambazo zinaonesha zimetoka Kiwanda cha Twiga kwenda kwa Katibu Mkuu ikikiri kwamba Hati yao Na. 42336 ya kiwanja namba moja, nne na saba inatakiwa igawanywe mara mbili. Hali kadhalika kutoka kwa *Imma Advocate* na *City Bank* ikienda kwa Kamishna wa Ardhi, ikitoa taarifa ya uwasilishaji wa Hati igawanywe mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kauli na hasa kwa kuwa Waziri wa Ardhi yupo, kwamba hii Hati ambayo umesema kuna vitu unavishughulikia. Lakini unavishughulikia kwa sababu ulikuwa huna hizi taarifa. Hii Hati ya viwanja namba moja, nne na saba, ambavyo ndani yake kulikuwa kuna Kiwanda cha Twiga ambacho kiligawanywa mara mbili baada ya mauziano, imeshagawanywa mara mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nipate kauli thabiti kutoka kwa Waziri ambayo *TBA* iko chini yako. Je, hizi nyumba 226 bado ziko Serikalini na kama ziko Serikalini, hii barua ya *Twiga Cement* kwenda kwa Majembe kuwafukuza wale wananchi ili-*base* katika misingi gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu na nafikiri Mheshimiwa Mdee amenisikia vizuri. Nimeeleza kwamba, nyumba za Saruji kule zilipewa *TBA* chini ya *Government Notice No. 63* ya tarehe 23 Mei, 2008. Idadi ya nyumba ziko 226 na idadi ya wakazi wako 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 wakazi hao walifungua kesi dhidi ya *TBC*, kesi namba 30 ya mwaka 2010. Tarehe 31 Desemba, 2012, ile kesi ikatupiliwa mbali. Wale wahusika wameamua kumwandikia Mheshimiwa Jaji Mkuu wakiomba uamuzi ule upitiwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina mahali zaidi pa kuzungumza kwa sababu, nina uhakika kama mwaka 2010 hawa wakazi wasingekwenda Mahakamani, Wizara yangu ingeweza kushughulikia chini ya *TBA.* Lakini kwa sababu, walikwenda Mahakamani na inawezekana kuna mtu aliwashauri kwenda Mahakamani, inawezekana ndio tumefikia hapa, lakini ngoja masuala ya Mahakama yaishe, halafu Wizara yangu iweze kuhusika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mdee, ni Mwanasheria, anafahamu Mahakama huwa haziingiliwi.

Nami sitaki kuiingilia Mahakama, ngoja haya mambo yaishe vizuri Mahakamani, halafu tuweze kuya-*solve* vizuri *administratively.*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa ridhaa yako, niseme kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Makele, Nyarugusu, Herushingo, Kigadye na Kitanga kwamba, hoja yao imekubalika na Serikali. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la bilioni 10. Nikaomba ufafanuzi, Serikali au Wizara, kwa kuwa imekuwa na mpango wa kutafuta fedha za nje kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri. Je, kuna mpango wowote ambao unafanyika kwa ajili ya kupata fedha za nje, kuongezea kwenye bilioni 10, ili kuwa na uhakika wa kukamilisha mradi wa barabara ya Kidahwe – Nyakanazi? Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa *concern* yake ya maeneo hayo anayoyazungumza. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba, eneo hilo tumelitengea shilingi bilioni 10. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tutaanza ujenzi, tumeshatangaza upande mmoja, lakini pia tutatangaza upande ule mwingine wa kutoka Nyakanazi kuja kukutana, ili kusudi Mkandarasi mwingine aanzie Nyakanazi na Mkandarasi mwingine aanzie Kidahwe, ili kusudi barabara ile iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeshapeleka maombi kwa *African Development Bank* na Wafadhili wengine mbalimbali, ili waweze kutusaidia katika kujenga barabara hizo. Vile vile, hata katika ziara ya Mheshimiwa Rais, ingawaje sio vizuri kuzungumza, kuna baadhi ya miradi ya barabara ambayo imepelekwa kule, ili kusudi tuweze kupata ufadhili wa *Kuwait Fund.* Kazi zinafanyika ili kupata fedha nyingi za kutosha katika kuhakikisha barabara zetu zinatengenezwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ugomvi wa Mheshimiwa Mkosamali, kwamba, inaanzia wapi, naamini kabisa umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tumalizie na Mkoa ule wa kilometa tano. Mheshimiwa Susan Lyimo?

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, nini Sera ya Wizara yake kuhusiana na suala zima la ujenzi wa matuta?

Mheshimkiwa Mwenyekiti, naliuliza hili kwa sababu, kumekuwa na kero kubwa sana na ajali nyingi sana zinazosababishwa na matuta kwa sababu, matuta hayo, mengine ni makubwa kupita kiasi. Lakini suala hili nililiuliza toka enzi ya Waziri Kawambwa na akasema analifanyia utafiti na kulishughulikia, lakini mpaka leo kwa kweli, matuta yamekuwa ni kero kubwa sana. Sasa ni nini Sera yake?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria Namba 13 ya mwaka 2007, *Highway* yoyote haitakiwi kuwa na matuta, lakini pia ni Sera hata katika dunia nyingine, huwezi ukakuta matuta kwenye *Highway*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matuta tumeyaleta sisi Wanasiasa; mtoto akigongwa au mtu akigongwa mahali Fulani, tunawahamasisha watu, wanakwenda kuandamana mle kwamba, lazima matuta yawekwe na wanaimba *"Matuta, Matuta",* kesho yake tunaambiwa wekeni matuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima sasa tushirikiane Watanzania wote, Sera ya matuta kuweka kila mahali panapotokea ajali, tuzingatie Sheria. Kwa sababu, saa nyingine Watendaji wangu wanapata ugumu kweli, panatokea ajali mahali wanasema lazima pawe na matuta. Kwa hiyo, barabara zetu zimekuwa ni za matuta tu, tukiweka alama barabarani, zinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu, tumeweka fedha makusudi kwa kuanza kuweka alama za

barabarani. Kila alama ya barabarani itakapoibiwa, tutamshika Mwenyekiti wa Kijiji wa eneo lile, ili kusudi ajue ni kwa namna gani ile alama ya barabarani imeibiwa. Nina uhakika kwa njia hii Watanzania wote tutashiriki katika kulinda alama za barabarani za maeneo yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katika kundi hili Waheshimiwa, sio rahisi kuwapata wote kwa sababu ya muda; nimejaribu angalau kupata Mikoa kidogo, naomba tuvumiliane; katika kundi hili Mheshimiwa Zitto, peke yako ndiyo ulionesha...

Mheshimiwa Zitto Kabwe?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza hapo awali, nilimsomea Mheshimiwa Waziri, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusiana na jumla ya shilingi bilioni 252 ambazo Wizara yake, ilishindwa kutoa uthibitisho kwa *CAG* kwamba, zilitumika kwa ajili ya kulipia Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yake pia, hayakuweza kutosheleza kwa sababu, *CAG* pia katika Ripoti hii anasema kwamba, katika Taarifa ya Madeni ya Serikali, hapakuwa na orodha ya Wakandarasi wowote ambao walikuwa wanaidai Serikali, kwa hiyo, hapakuwa uthibitisho...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto?

**MHE. KABWE. Z. ZITTO:** Naam.

**MWENYEKITI:** Utaruhusiwa tu kuendelea endapo unaelekea kwenye kutoa shilingi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio natoa hoja ya kuweza kutoa shilingi ya Mshahara wa Waziri kwa sababu, maelezo yake hayajathibitisha namna ambavyo shilingi bilioni 252, ambapo hapa Bungeni tuliambiwa kwamba, ni kwa ajili ya kulipia madeni, Wizara ya Fedha, ikatoa hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* alipokwenda kuwakagua, hawakutoa uthibitisho wowote kwamba, madeni yale yamelipwa na katika maelezo ya Waziri hapa, anatoa maelezo yaleyale ya mwaka 2011 ya kwamba, walikwenda kulipia madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Waziri, aweze na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, waweze kukubaliana nami kwamba, tuondoe shilingi katika mshahara wake kwa sababu, ameshindwa kulithibitishia Bunge, matumizi ya shilingi bilioni 252 kama jinsi ambavyo haikuthibitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ni kwa sababu, hiyo ndio maana barabara nyingi sana zimesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumza kwamba, barabara za Tabora 30%, yeye anasema zimetengenezwa, lakini tukipita Tabora hakuna hiyo 30% na mama Margreth Sitta, amezungumza mchana hapa kwamba, barabara ile ya Urambo - Tabora, ilitakiwa ikabidhiwe mwezi Machi mwaka huu, lakini Waziri anasema kwamba, 30% imejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela za kulipa madeni zilitengwa, lakini *CAG* anasema watu hawajalipwa na kwa mazingira kama haya na kazi yetu sisi ni usimamizi, kazi yetu sisi ni kuisimamia Serikali, kuhakikisha kila senti ya umma inatumika vizuri, sasa Wizara yake imeshindwa kumthibitishia *CAG* kwamba, ametumia fedha zile vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitoe hoja kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, tuchomoe shilingi yake katika mshahara, ili aweze kwenda kusimamia vizuri na kupata majibu muafaka ya fedha za umma ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anasema kwamba, zimetumika vibaya; shilingi bilioni 252 ambazo zinaweza zikajenga barabara kuanzia Itigi mpaka Tabora, hazionekani matumizi yake na tulimtengea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nitawapa nafasi mnaotaka kuchangia; kaeni kidogo, halafu nitawaruhusu wale wanaotaka kuchangia hoja. Hoja ya Mheshimiwa Zitto, imenipa tabu kidogo kwa sababu, moja tu kwamba, yeye ni Mwenyekiti wa *PAC,* kwa maana kwamba, hoja kama hiyo ya uzito huo, matarajio yangu ni kwamba, Kamati ya *PAC* ingeichukua. Kwa hiyo, ambacho tungeletewa hapa ni maoni ya Kamati ya *PAC* chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Zitto, kuhusu jambo zito kama hili. *(Makofi)*

Sasa anapoileta hapa katika mazingira haya, inatufanya Bunge zima, sasa sijui tunafanya mazingira gani ili tuweze kufikia maamuzi. Wakati jambo hili kwa kweli, liko mikononi mwake Mheshimiwa Zitto.

**MBUNGE FULANI:** Sifa tu.

**MWENYEKITI:** Mnaonaje Waheshimiwa Wabunge, tukikubaliana kwamba, jambo hili liende kwenye Kamati ya *PAC,* walijadili, kwa wakati muafaka watatushauri Bunge, namna gani ya matumizi ya fedha hizo? *(Makofi)*

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MBUNGE FULANI:** Hatujaafiki.

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit... ...* Sh. 771,350,160/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division... ...* Sh. 203,951,100/=
Kif. 1004 – Government Communication Unit... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 315,560,300/=
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit... ... ... ... ... ... ... ... ...* Sh. 314,064,200/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit... ... ... ... ...* Sh. 249,160,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 – *Legal Services Unit… … … … …*Sh. 203,951,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kif. 1008 – *Information, Communication Technology… … … … … … …* Sh. 190,600,500/=
Kif. 2002 – *Technical Services Division… … … … … … … …* Sh. 9,895,785,405/=
Kif. 2005 – *Roads Development Division… … … … … … …* Sh. 365,582,705,835/=
Kif. 5002 – *Safety and Environment Division… … … … … … … …* Sh. 589,669,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division… … … … … … … …* Sh. 500,131,000/=
Kif. 2002 – *Technical Services Division… ..*Sh. 14,821,700,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 – *Roads Development Division… … … … … … …* Sh. 825,425,167,000/=

**MWENYEKITI:** Nimewaona Waheshimiwa wangapi? Nitajieni, Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Mangungu.

Tuanze na Mheshimiwa Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Fungu dogo la 4127, hii *New Bagamoyo Road (Kawawa Junction – Tegeta),* nataka kupata ufafanuzi kutoka

kwa Waziri; barabara ya Mwenge – Tegeta, ambayo ni *phase* ya kwanza, inakwenda kwa kusuasua sana. Kimkataba inatakiwa imalizike mwaka huu wa 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafahamu pia kwamba, kwa Mwaka huu wa Fedha, kuna matayarisho yanaanza kuanzia Mwenge kuelekea Morocco. Sasa nataka nijue hizi bilioni 20 ambazo zimetengwa hapa ni kwa ajili ya Mwenge kwenda Tegeta, kuendeleza ujenzi ambao unaonekana unakwenda kwa *pace* ndogo sana? Ama ni kwa ajili ya maandalizi ya Mwenge kwenda Morocco?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kwa ajili, ya maandalizi ya Mwenge kwenda Morocco, Fungu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Mwenge – Tegeta liko wapi? Kwa sababu, kwa kweli, hali haitii matumaini sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa kilometa 17 unafadhiliwa na Serikali ya Japan kwa asilimia mia moja. Mradi huu ulianza na *Phase I* ya kuanzia Mwenge hadi Tegeta, *Phase Number II* itaanzia Mwenge kwenda Morocco. Kazi ambazo zimeshaanza kufanyika kwa sasa hivi pale Morocco, tumeshaweka *X* na Serikali, imeshaanza kulipa *compensation* kwa wale wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha hizi zote ambazo zina-*cost* mradi wote wa bilioni 88 ni kwa *compact* ya mradi wote *Phase I* na *Phase II,* ambapo barabara yake iliwekewa Jiwe la Msingi na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, fedha hizi ni fedha za kutoka Serikali ya Japan na ni *grant.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mdee kwamba, mradi huu hauendi kwa suasua, mradi huu unakwenda vizuri na bahati nzuri una madaraja makubwa makubwa sana ambayo, ni lazima yatengenezwe, ili barabara iweze kupitika, ili wananchi wa Jimbo lake na Watanzania wengine waweze kufaidika na ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile itakwenda kuunganisha na barabara nyingine inayokwenda Tanga, kwa

kuunganisha ile barabara ya Bagamoyo. Kwa hiyo, hizi zote ni kwa ajili ya mradi huo pamoja na ile *Section* ya kilomita 4.1. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 4138, ukurasa wa 266, *De-Congestion of Dar-es-Salaam Road.* Kifungu kinachohusiana na kupunguza msongamano kupitia barabara za pembezoni. Mwaka huu kimetengewa shilingi bilioni 28.6 ambazo naamini ni kwa ajili ya hizi barabara zilizotangazwa kwenye Tangazo lililotoka kwenye gazeti jana, kwa maana ya Malamba Mawili, Goba na barabara nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni 10.5 na nina Kumbukumbu Rasmi za Bunge hapa za Mheshimiwa Waziri, kwa sababu, niliulizia tena Kasma hii mwaka jana. Mheshimiwa Waziri, mwaka jana alisema kwamba, bilioni 10.5 ilikuwa ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kimara – Kilungule – *External* bilioni moja, barabara ya Kimara – Baruti ya ahadi ya Rais vile vile ya Mavurunzwa – Bonyokwa na barabara nyingine kama ambavyo zilioneshwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na maelezo ambayo aliyatoa Mheshimiwa Waziri, katika Mwaka huu wa Fedha, hizi barabara hazikufanyiwa matengenezo kabisa, kinyume na kauli ya Mheshimiwa Waziri, ikiwemo barabara ile ambayo ni ya ahadi ya Rais ya Kimara – Mavurunzwa – Bonyokwa mpaka Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ukiondoa hizi barabara zilizotangazwa za bilioni 28.6, kwa kuwa, Mwaka wa Fedha utekelezaji unaendelea, je, hizi bilioni 10.5 ambazo zilikuwa zimekwishatengwa tayari, Waziri ataelekeza kwamba *TANROADS* iendelee na matengenezo ambayo Waziri, alishaahidi hapa Bungeni, yatafanyika?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu na kumpa ufafanuzi ndugu yangu Mheshimiwa Mnyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hiki, barabara yoyote kabla ya kujengwa huwa kuna maandalizi yake na kila maandalizi yana pesa. Kuna *feasibility study* inachukua fedha, *detail design* inachukua fedha na ndipo inakuja kufikia wakati wa kutangazwa *tender.* Barabara hiyo kwa fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka jana ambazo zingine bado zipo, tulifanya *feasibility study,* tukafanya *detail design* na sasa tumetangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tumetangaza katika mwaka huu, hatukusubiri hizi hela kama zitakataliwa. Kwa sababu, tungeweza leo hii bajeti ikakataliwa na Mheshimiwa Mnyika tusitangaze, lakini tulitangaza kutokana na fedha za mwaka jana. Kwa hiyo, kwa mwaka jana ukizijumlisha fedha na za mwaka huu tulizozipanga, ndio maana barabara hii inaweza kutengenezwa vizuri kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana pia katika barabara, kwa ufafanuzi wake na Wapiga Kura wake, ili kusudi akawaeleze jinsi Serikali ya CCM inavyofanya kazi, barabara ya Kimara – Kilungule – *External* imetengezwa kwa bilioni tano, Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi bilioni sita na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mnyika, kwamba, barabara hizi zitatengenezwa kwa kiwango cha lami, zitapunguza msongamano; hata sisi tunapokuja Dodoma, tutakuwa tunapita hizo, tunasalimu kule, tunawaambia kazi ya CCM, halafu tunakuja Dodoma. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimekwishaongeza nusu saa. Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Kasma ndogo ya 4143, zimetengwa shilingi bilioni 5.28. Nataka kufahamu katika pesa hizi ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga, zinaweka pia ujenzi au usimamizi wa zile *diversions?* Kwa sababu, matatizo makubwa ya wananchi wa Mikoa hiyo, hii barabara inajengwa, lakini *diversions* hazitengenezwi kabisa, hasa *TANROADS* Mkoa wa Pwani, huwa hawafanyi *maintenance* ya hizo *diversions.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu na alikuwepo pale; nashukuru ametembelea mara mbili katika eneo lile na Mheshimiwa Waziri aliwahi kutembelea mara moja. *Diversions* hazijengwi na hazisimamiwi, mvua zinanyesha, wananchi wana-*stuck* pale zaidi ya saa 10, siku mbili. Sasa hata wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri, sasa hivi umekuwa kama Joka la Kibisa tu, hawakuogopi tena, wanakuchezea; naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizotengwa ni kwa ajili ya kumalizia na kutengeneza kazi ya sehemu ya Ndundu – Somanga iliyobaki. Barabara ya Ndundu – Somanga ina kilomita 60. Mpaka sasa hivi zimeshamalizika karibu kilomita thelathini na kitu, zimebaki kilomita 22.6 ambazo zinaendelea kujengwa. Tuta limeshajengwa, madaraja yote yameshamalizika, *sub base* imeshamalizika, kwa hiyo, tumetenga hizi fedha ambazo Mkandarasi atalazimika amalize kabla ya Mwezi Disemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mangungu kwamba, fedha hizi ni kwa ajili ya kumaliza barabara hiyo, kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Lakini pia, kwa mujibu wa Mkataba wa Sheria ambazo zipo, Kandarasi yeyote anapokuwa kwenye *site* na hii si kwa barabara ya Ndundu – Somanga tu kwa barabara zote Tanzania, panapotokea mkwamo, *diversion* na kitu kingine chochote huwa ni jukumu la Mkandarasi kufanya hiyo kazi kwa sababu liko ndani ya Mkataba.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 5002 – *Safety and Environment Division... ... ... ... ... ... ... ...* Sh. 4,478,981,000/=

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Fungu hili, Kifungu Namba 4136, kinazungumzia *Road Safety Activities*. Katika mchango wangu wa maandishi na mwaka jana Mheshimiwa Waziri, alikuwa anajibu huku akisikitika na mara nyingine alikuwa akilia kuhusiana na alama za barabarani ambazo zinang'olewa na zinakwenda kuuzwa kama chuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua, kwa ahadi aliyoitoa katika Bunge la mwaka jana, pesa hizi zitahusika pia katika kufanya usimamizi mzuri wa Sheria kwa wale ambao wanang'oa alama za barabarani na kusababisha ajali na uharibifu mkubwa wa barabara?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu ni ndiyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kasma hiyo, imeshaulizwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati na kupitia Makadirio ya Wizara ya Ujenzi Kifungu kwa Kifungu na

kuyapitisha bila mabadiliko na bila marekebisho. Hivyo, naomba Makadirio hayo sasa yakubaliwe rasmi na Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana katika kuyapitia, kuyachambua na kuyajadili makadirio haya ya Wizara ya Ujenzi.

Kwa niaba yenu, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Dokta John Pombe Magufuli; Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Lwenge; Katibu Mkuu na Wataalam wengine wote. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa shughuli yenu kubwa ya ujenzi wa barabara kwa mwaka huu 2013/2014 na matarajio ya Watanzania kwa sehemu kubwa yako kwenu, kuhakikisha kwamba, barabara zetu zinakuwa bora zaidi kuliko zilivyo sasa.

Kwa kufikia hapo, yale yaliyopangwa kwenye *Order Paper,* yote yamekamilika. Kwa hiyo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge, hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 15 Mei, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*